**12 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 12 Mei, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya

Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Tunanza Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 302

**Posho kwa vijana wanaofanya kazi na Kampuni za Kichina**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itahakikisha Watanzania wanaofanya kazi kwenye Kampuni za Kichina wanalipwa vizuri kwa mujibu wa sheria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ili kulinda haki za wafanyakazi. Aidha, katika kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa sekta binafsi, Serikali kupitia Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara cha Sekta Binafsi imefanya utafiti na kuboresha

kima cha chini cha mishahara ya sekta binafsi, viwango hivyo vipya vya mishahara vilitangazwa kupitia Gazeti la Serikali Namba 687 la tarehe 25 Novemba, 2022 na utekelezaji wake umeanza rasmi tarehe 01 Januari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika na masuala ya kazi itaendelea kuhakikisha kuwa waajiri wanatekeleza ipasavyo viwango vya mishahara vilivyotangazwa kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara katika maeneo ya kazi na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi ili uelewa wao katika kutekeleza Sheria za Kazi unafanyika. Aidha, ofisi imeendelea kuchukua hatua dhidi ya waajiri wanaobainika kukiuka Sheria za Kazi hususan ulipaji wa mishahara kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri kuna viwanda katika Mkoa wa Pwani sehemu za Mbagala na sehemu za Mkuranga wanawapa wafanyakazi shilingi 4,000 kwa siku. Mfanyakazi anaingia saa mbili asubuhi anatoka saa 11 jioni anapata ujira wa shilingi 4,000; je, hii ni sawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali mnasimamia vipi matajiri na waajiri wakubwa ambao wanadaiwa madeni na wafanyakazi kwa muda mrefu. Makampuni ya Chai ya Rungwe, Kampuni ya Kiwira *Coal Mine* na Kampuni ya *TANESCO* waliokuwa vibarua takribani sasa ni miaka mitano hawajapata fedha zao.

Je, Serikali mnasimamiaje suala hilo kuhakikisha watu hawa wanapata haki ambayo wanastahili waliyoitendea kazi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge ni kweli tumeendelea kufanya kaguzi, kwa mujibu wa sheria ipo namna na mikataba ya kazi ambayo inatambua aina ya ajira mtu anayoifanya. Wapo wanaofanya kazi kwa maana ya *permanent and pensionable* kwa maana ya mkataba unavyoeleza lakini pia wapo wanaolipwa kwa mpango wa wiki moja, kila baada ya wiki, wapo wanaolipwa kila baada ya mwisho wa mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo hayo, imebainika ndiyo moja ya tatizo ambalo tumelibaini Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, wapo waajiri ambao wamekuwa wakikwepa kuwapa mikataba ya kazi wafanyakazi hawa ili kuendelea kuwaita vibarua na wakafanya kazi kwa muda mrefu. Huo ni unyonyaji mkubwa na Ofisi ya Waziri Mkuu tayari tumekwishaanza kuchukua hatua na tunafanya kaguzi, tunaenda kuangalia historia wafanyakazi wamefanya kwa kipindi gani na ni aina gani ya kazi anayoifanya ili kuweza kuhakikisha tunawaingiza kwenye mfumo wa kuwa na mikataba ya kazi ili haki zao ziweze kulindwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni lile linalohusiana na udhulumaji ambao unafanyika au kutokulipa maslahi ya wafanyakazi. Vivyo hivyo katika Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini inaeleza moja ya mambo ni kukubaliana katika mkataba, yaandikwe na yaainishwe wazi. Kitendo cha waajiri kutokuwalipa mishahara au maslahi yao ni kuvunja Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini lakini sambamba na hilo, ndani ya

mkataba kuna masuala ya *Pay As You Earn* kwa maana ya kodi ya Serikali. Maana yake asipolipwa maana yake anakwepa pia kodi ya Serikali, pia kuna kipengele ambacho ni cha lazima cha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, asipolipwa mshahara maana yake anakwepa pia kupeleka fedha kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu kipo kipengele cha *WCF* kwa maana ya *workers compensation*. Kama halipwi mshahara maana yake hiyo pia ni eneo ambalo anakosa haki hiyo ya kuweza kulipwa, sambamba na hilo sheria nyingine tumeendelea kuzichukua na tunawapeleka mahakamani kwa *summary suits* maana yake hana muda wa kujitetea na hatua tunazichukua na sasa yapo mashauri ambayo tunaendelea nayo, hivyo kwenye maeneo hayo mahsusi nitaomba pia aniambie ni wapi ili tuweze kushirikiana naye kuweza kuchukua hatua. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mufindi Kampuni ya *Ekaterra* imeinunua Kampuni ya *UNILEVER* jambo ambalo limeacha malalamiko makubwa ya wananchi kukosa stahiki zao. Je, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu haioni umuhimu wa kuwasaidia wananchi hawa kumaliza malalamiko yao, ikiwa ni pamoja na kufika pale ili waendelee kunufaika na Taifa lao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kihenzile kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwamba suala hili Mheshimiwa Kihenzile amekuwa analifuatilia kwa muda mrefu la kampuni hiyo ya *UNILEVER* baada ya kuingia mkataba wa kwamba sasa kampuni inakuwa *winded up* na kuchukuliwa na kampuni nyingine. Utaratibu uliopo kampuni inaponunuliwa au inapoenda kufilisika wajibu wa kwanza ni kuhakikisha wametambua madeni lakini pia kwa maana ya *liabilities* pamoja na *assets* zilizopo. Kwa wafanyakazai hatua ya pili itakuwa sasa ni kulipa madeni ikiwemo madeni ya wafanyakazi kwenye kampuni husika, hata kama kuna *transfer* ya umiliki, jambo la kulipa madeni ambayo ni *liabilities* ni la msingi na ni la kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kwenye eneo hili la kesi ya *UNILEVER* Mheshimiwa Mbunge nimueleze tu kwamba kuna hatua mbili ambazo Ofisi ya Waziri Mkuu ilichukua. Hatua ya kwanza Kamishna wa Kazi alikutana na wafanyakazi hao na kuchukua malalamiko yao. Wapo ambao walifukuzwa kazi wakati huo bila kufuata utaratibu wa *retrenchment* tuliagiza warudishwe kazini. Pia lipo kundi la pili la wafanyakazi ambao walilipwa walikuwa zaidi ya 500 na hatua ya tatu kundi la tatu kwenye wafanyakazi hao ni wale ambao bado maslahi yao yalikuwa hayajaelezeka vizuri, wapo ambao walikuwa wana mikataba na wasiokuwa na mikataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ambayo tumeichukua tuliwaelekeza waende *CMA* ambapo shauri linaendelea mpaka sasa katika Mahakama ya Kazi na hatua ya tatu ambayo tunaenda kuichukua ni kuhakikisha baada ya maamuzi ya *CMA* na wale ambao walikuwa bado hawajaainishwa kwamba wako kwenye eneo gani la vipengele vya mikataba, wakutane na Kamishna wa Kazi ili haki zao ziweze kulindwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Neema Gelard.

Na. 303

**Posho Maalumu kwa Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanza kutoa Posho kwa Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Wenyeviti wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji katika kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kila Halmashauri inatakiwa kuweka utaratibu wa kuwalipa posho, Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kubuni na kuimarisha vyanzo vya mapato pamoja na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ya kukusanya na kutumia fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na matumizi mengineyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya maswali ya nyongeza. Nitakuwa na maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali haina utaratibu maalum wa ulipaji wa posho kwa hawa Wenyeviti wa Mitaa, Vitongoji na Vijiji na wamejitengenezea utaratibu wa kujipatia fedha kupitia mihuri yao na uuzaji wa viwanja kitu ambacho kinaleta migogoro mingi sana kwenye jamii na kaadhia kubwa kwenye jamii na urasimu mkubwa.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na utaratibu maalum wa kuwa na posho ya madaraka kwa viongozi hawa wa ngazi ya mitaa, vijiji na vitongoji? *(Makofi)*

Swali la pili, Wenyeviti hawa wa Mitaa, Vijiji na Vitongoji pamoja na Madiwani wamekuwa na dhamana kubwa sana ya usimamizi wa miradi ya Serikali kwenye maeneo yao, lakini mpaka leo hawana posho ya usimamizi wa miradi.

Je, nini kauli ya Serikali kuhakikisha kunakuwa na posho ya usimamizi wa miradi kwenye maeneo yao? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwandabila.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza la Serikali haina utaratibu maalum na ni nini kauli ya Serikali kuweka utaratibu huo. Kama nilivyokwishasema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba kwa mujibu wa Sheria ile ya

Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura Namba 290, posho hizi zinatakiwa zilipwe kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri husika na ndiyo maana Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuziimarisha hizi Halmashauri zetu kwa kuwapa miradi ya kimkakati kuwajengea vyanzo vya mapato mbalimbali ambavyo vitaongezea nguvu kuweza kulipa posho hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili ya usimamizi wa miradi. Ni kweli Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji, Mitaa wanafanya kazi nzuri katika kusimamia miradi, hasa miradi mingi ambayo kwa sasa tumeona Taifa letu Mheshimiwa Rais amemwaga miradi katika Sekta mbalimbali. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kulileta hili hapa na tunalichukua kama Serikali kwa sababu lina *budget implication* na pale ambapo tutaona Serikali ina uwezo wa kuweka kwenye bajeti zake tutaweka lakini kwa sasa bado tutaendelea na utaratibu ule kama sheria inavyotaka ile ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura Namba 290.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, jiandae Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa, Serikali imezipokea halmashauri kulipa ile posho iliyokuwa ya Madiwani.

Je, sasa Wizara haioni kwa nini isielekeze zile posho zilizokuwa zinalipwa kwa Madiwani na Halmashauri ziende zikawalipe Wenyeviti wa Serikali za Vijiji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalipokea kwa niaba ya Serikali

na tutakwenda kuliangalia na kulifanyia kazi na kama tutaona liko *viable* basi tutachukua hatua.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali katika Bajeti yake ilipitisha posho ya Watendaji wa Kata ya kila mwezi, lakini posho hii imeonekana ni hisani. Baadhi ya Halmashauri zinalipa zingine hazilipi.

Je, Serikali mna tamko gani kuhusu posho hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, posho hizi zilipitishwa kwenye bajeti na Bunge hili Tukufu na tutaenda kuhakikisha kwamba linatekelezwa kwa sababu tayari zilitengwa ili Watendaji hawa waweze kupata posho hizi za madaraka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 304

**Hitaji la Vituo vya Afya Kata za Mnongodi na Nyundo – Nanyamba**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa Fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata za Mnongodi na Nyundo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilitenga Shilingi Bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya kimkakati kwenye Kata 234 nchini. Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ilitengewa kiasi cha Shilingi Milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kitaya. Ujenzi wa Kituo hicho upo hatua za ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye Kata za Kimkakati nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye Kata za Mnongodi na Nyundo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili.

Mosi, kwa kuwa ujenzi wa Kituo cha Afya Kitaya umeshakamilika, je, ni lini Serikali sasa itapeleka vifaatiba na wataalam ili huduma ziweze kutolewa?

Swali langu la pili, katika Bajeti ya TAMISEMI ambayo tumepitisha hivi karibuni zimetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vipya vya afya. Je, Serikali inatoa tamko gani sasa kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Nyundo au Mnongodi au Kata za kimkakati katika Jimbo letu la Nanyamba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Chikota la Kituo cha Afya Kitaya. Serikali imetenga katika mwaka wa fedha huu 2023/2024 shilingi milioni 400 kwa ajili ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba kwa ununuzi wa vifaatiba kwa ajili ya zahanati na vituo vya afya. Sasa ni maamuzi ya kwao wao kwamba shilingi milioni 400 hizi wazi-*allocate* wapi kwenye zahanati zipi, vituo vya afya vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la kupata vituo vya afya. Tutaangalia katika bajeti iliyotengewa kwa mwaka wa fedha huu 2023/2024 tuone Nanyamba imetengewa vituo vya afya vingapi lakini kama haijatengewa katika mwaka wa fedha huu Serikali itahakikisha inatenga fedha kwa ajili ya vituo vya afya vya Nanyamba katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Chomete.

Na. 305

**Hitaji la walimu wa sayansi - Mara**

**MHE. GHATI Z. CHOMETE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo la upungufu wa walimu wa sayansi Mkoani Mara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Mkoa wa Mara ulipata walimu 531 kwa shule za Msingi na Sekondari. Kati yao walimu wa masomo ya sayansi walikuwa 197. Ni dhamira ya Serikali kuendelea kuajiri na kuongeza idadi ya walimu wa sayansi ili kuendana na malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tayari imetenga nafasi za ajira za walimu na watumishi wa kada ya afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo jumla ya nafasi 13,130 ni za kada ya elimu na kipaumbele ni masomo ya sayansi. Waombaji watapangiwa vituo vya kazi kwa kuzingatia maeneo yenye upungufu mkubwa ukiwemo Mkoa wa Mara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Naishukuru Serikali kwa kutuletea walimu wa sayansi 197, lakini bado tuna upungufu mkubwa sana wa walimu wa masomo ya sayansi 889; je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mkoa wa Mara ili waweze kutatua changamoto hii iliyowakabili na watoto wao waweze kufaulu vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa walimu wengi wa masomo ya sayansi ni walimu wa jinsia ya kiume: Je, Serikali haioni haja ya kuwa na *program* maalum ya kuwawezesha watoto wa kike kufundisha masomo ya sayansi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya

Mheshimiwa Chomete, la kwanza la upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi katika Mkoa wa Mara; kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba tunaajiri walimu 13,130 na tutazingatia maeneo yenye upungufu mkubwa hapa nchini ikiwemo Mkoa wa Mara. Hivyo nimtoe shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba Mkoa wa Mara nao upo katika mikoa ya kipaumbele kupata walimu hawa wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali la pili, nitoe rai kwa watoto wa kike waweze kwenda kwenye vyuo hivi vya ualimu na kusomea kufundisha masomo ya sayansi, ili tuweze kupata *pool* kubwa ya maombi ya watoto wa kike wanaoenda kufundisha masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tena kwamba katika ajira hizi mpya, tutahakikisha wale walimu ambao wanakidhi vigezo na ni walimu wa sayansi wanaajiriwa katika mwaka huu wa fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa tunakubaliana kwamba tuna tatizo kubwa la walimu wa sayansi nchini na pia tunatambua kuna maendeleo ya sayansi na teknolojia: Ni kwa nini Serikali isione namna ambavyo inaweza kutumia TEHAMA kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inatatua tatizo la walimu kwa mwalimu mmoja kuweza kufundisha shule nyingi kwa wakati mmoja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa TEHAMA, na ndiyo maana Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitoa vishikwambi kwa walimu wote

kama kianzio cha kwenda kwenye TEHAMA kwa walimu hawa. Kadiri siku zinavyokwenda, kuna shule ambazo zinajengwa za kimkakati kama shule ya mfano iliyokuwepo hapa Iyumbu Jijini Dodoma ambazo zitakuwa ni shule za TEHAMA kuweza kufundisha wanafunzi wetu wengi zaidi, na miaka inavyokwenda, tutazidi kuongeza kama Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Francis Mtega.

Na. 306

**Kituo cha Afya Igurusi**

**MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuboresha Kituo cha Afya Igurusi ili upasuaji uweze kufanyika katika kituo hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Jimbo la Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Igurusi kilijengwa mwaka 1966 na kuanza kutoa huduma katika ngazi ya zahanati hadi ilipofika mwaka 2010 kilipopandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya. Aidha, miundombinu ya kituo hiki ni michache na iliyopo ni chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imefanya uchambuzi na kupata vituo vya afya

vikongwe 193 nchini kote ambavyo vinahitaji kufanyiwa ukarabati na kuongezewa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki umefanyika kutambua vituo vya afya vikongwe na Serikali iko kwenye mchakato wa kutafuta fedha ili kuvikarabati vituo hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtega.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na uchambuzi mzuri uliofanyika na Serikali, wananchi wa Igurusi wanapata shida hasa wazazi wanapokuwa na uzazi pingamizi: Je, ni lini sasa maboresho yataanza kufanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, kuna mpango gani wa kupeleka vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Chimala ili waweze kusaidiwa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali lake la kwanza la lini maboresho yatafanyika, kama nilivyoshasema kwenye majibu yangu ya msingi, ni kwamba tumefanya tathmini na kugundua kuna vituo vikongwe hapa nchini 193, na hivi sasa tuko katika mchakato wa kutafuta fedha na kuhakikisha tunavikarabati na kuviongezea majengo vituo hivi vya afya ambavyo ni vikongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili tutapeleka fedha kadiri ya upatikanaji wa fedha hizo na tutaangalia katika mwaka wa fedha huu ambao bajeti imepitishwa, kama kuna vituo ambavyo viko *allocated* Mkoa

wa Mbeya, basi tutakaa na Mheshimiwa Mbunge kuona ni namna gani Mbarali nao wanaweza kupata. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi halafu jiandae Mheshimiwa Samweli.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa ni zaidi ya miezi mitano sasa tokea Serikali imepeleka *x-ray machines* kwa kwenye Vituo vya Afya vya Muriti, Bwisya na Hospitali ya Wilaya ya Nansio, lakini mpaka sasa vifaa hivi havijaanza kutoa huduma kwa wananchi; nini kauli ya Serikali? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada za Serikali zimekuwa ni kubwa sana kupeleka vifaa tiba maeneo mbalimbali hapa nchini ikiwemo Muriti na Bwisya kule Ukerewe. Nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kuagiza timu yetu ambayo inazunguka mikoani kutoa mafunzo kwa wataalam wetu kutumia vifaa hivi vya kisasa, wahakakikishe wanafika Ukerewe mara moja na kutoa mafunzo kwa watumishi hawa wa Muriti na kule Bwisya.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kituo cha Afya cha Endasaki miundombinu yake ni chakavu sana; je, ni lini Serikali itatoa fedha zote zinazohitajika ili kukarabati miundombinu ya kituo hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Endasaki pale ambapo upatikanaji wa fedha hizo utakuwepo. Tutaangalia katika mwaka wa fedha huu 2023/2024 kama kituo hiki kimetengewa, ili fedha hizo ziweze kwenda mara moja. Kama hakijatengwa katika mwaka huu wa 2023/2024, tutahakikisha mwaka 2024/2025 kituo hichi kinatengewa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi.

Na. 307

**Ukarabati na kujenga nyumba za Makambi ya JWTZ**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga upya na kufanyia ukarabati nyumba zilizo katika Makambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na kuboresha miundombinu mbalimbali kwenye vikosi vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, ikiwemo ukarabati wa makambi na nyumba za makazi kwa Maafisa na Askari. Ukarabati wa makambi

ulianza kutekelezwa tangu mwaka 2020, na unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha na vipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya kwanza ya ukarabati inahusu nyumba zilizonunuliwa kimakundi nje ya makambi ya Jeshi, ikiwemo magorofa ya Mwenge, Keko, Nyumba za makazi za Masaki, Kitangili, Nyegezi, Nyamanolo, Tabora, Tanga, Shinyanga na Mtwara. Aidha, ukarabati huu umeanza kutekelezwa katika magorofa ya Mwenge Dar es Salaam na Tanga. Inategemewa ifikapo Desemba, 2023, ukarabati wa awamu hii utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati awamu ya pili utahusisha nyumba zilizopo makambini kwa kuzingatia kanda mbalimbali kwa kuanza na Kanda ya Mashariki, Zanzibar, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kusini, Kanda ya Ziwa na kumalizia ukarabati Kanda ya Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa jeshi letu limekuwa mstari wa mbele katika kuimarisha ulinzi wa nchi na mipaka yake; je, ni maeneo gani kwa Zanzibar ambayo yatapewa kipaumbele katika ujenzi huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mahanga katika kambi hapa nchini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Maryam Mwinyi kwa kufuatilia mambo haya ya msingi kwa ustawi wa majeshi yetu. Nimhakikishie, kwenye majibu yangu ya msingi nimeeleza kwamba kwenye ukarabati wa makambi ya awamu ya pili, Zanzibar imo katika vipaumbele. Ninapozungumzia Zanzibar, ni Unguja na Pemba. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwenye awamu ya pili upande wa Zanzibar pia ni kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili kuhusu mahanga, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali hili. Wizara itafanya tathmini ya mahitaji ya mahanga kote nchini na kuhakikisha katika utekelezaji wa ujenzi wa mahanga pia upande wa Zanzibar wanapewa kipaumbele, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Nashon Bidyanguze.

Na. 308

**Ujenzi wa barabara ya Simbo - Kalya kwa Iwango cha Lami**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Simbo - Kalya yenye urefu wa km 234?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Simbo – Kalya yenye urefu wa kilometa 234 kwa kuanza na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa daraja la *Lower Malagarasi* ambalo lipo katika barabara hii. Kazi za usanifu zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Novemba, 2023. Baada ya usanifu kukamilika, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja na kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Simbo hadi Kalya, yenye urefu wa kilometa 234, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hiyo barabara ya Simbo – Kalya, hiyo barabara inaendelea mpaka Wilaya ya Tanganyika ambayo ni Kalya -Lugalaba, Bujombe yenye urefu wa kilometa 37 ambayo inaenda kwenye Wilaya ya Tanganyika katika Mkoa wa Katavi. Ni lini nayo itawekewa fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha changarawe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika barabara hiyo hiyo, iko barabara ambayo ni ya Lukoma hadi Mwese, yenye urefu wa kilometa 47 ambayo nayo inakwenda nayo kwenye Mkoa wa Katavi. Naomba nijue, ni lini nayo itawekewa fedha kwa ajili ya ujenzi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo tunazihudumia sisi zinaishia Kalya, lakini ni kweli pia kwamba, kwa sababu tumeshawekeza eneo la Sibosye, tuna bandari yetu pale, kwa hiyo, tumefungua barabara mpaka Sibosye kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hiyo bandari inafanya kazi, na tutaendelea kwa barabara ambayo inaenda Katavi. Pia kwa upande wa Kigoma tumeshaifungua mpaka mpakani mwa Katavi, na wenzetu wa Katavi pia wameshaanza kutenga fedha kuifungua ili hizo barabara ziweze kuunganishwa ambapo itatumika pia kama barabara ya ulinzi kwa mikoa hiyo miwili ya Katavi na Mkoa wa Kigoma, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Issaay, jiandae Mheshimiwa Mrimi.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kipande cha barabara ya lami kutoka Mbulu Garbabi, kazi ya Mkandarasi imesimama kwa miezi minne; je, ni lini mkandarasi yule ataanza kazi ile rasmi ili barabara hiyo iweze kutekelezwa kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara anayoisema hii, ni kweli kulikuwa kuna changamoto ya mvua na pia mkandarasi alikuwa hajalipwa fedha zake alizokuwa anadai. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tunavyoongea sasa hivi mkandarasi ameshaanza kazi ya Mbulu kwenda Garbabi na tunategemea muda wowote kuanzia sasa tutasaini mkataba wa Labay kwenda Haydom, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrimi, jiandae Mheshimiwa Mwesongole.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Tunaishukuru sana Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kusukuma sana ujenzi wa barabara ya Sanzate – Nata; je, ni lini kipande cha Nata mpaka Mugumu ujenzi wake utaanza? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nata kwenda Mugumu ni barabara ambayo tutakuwa tunakamilisha barabara ya makutano Nata hadi Mugumu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ambayo tunaiendea, tumeipanga ili iweze kukamilika na hivyo kukamilisha mzunguko wa Nata – Mugumu; Mugumu hadi Tarinya kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa George.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mlowo – Utambalila mpaka Kamsamba, nyaraka za tenda, usanifu wa kina, kila kitu kipo

tayari, na ipo ndani ya mpango wa bajeti: Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili ujenzi wa kiwango wa cha lami uanze kwenye hiyo barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mlowo - Utambalila hadi Kamsamba, barabara ambayo Mheshimiwa Mbunge amekuwa anaiulizia mara kwa mara, tumemhakikishia kwamba hiyo barabara ambayo inaunga Mkoa wa Songwe na Rukwa, tumeiweka kwenye mapendekezo, na tuliagizwa pia na viongozi kwamba barabara hiyo sasa tuanze kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tusubiri bajeti kama itapitishwa, barabara hiyo tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Minza Simon Mjika. *(Makofi)*

Na. 309

**Kujenga Daraja la Lyusa na Itembe – Mto Sibiti**

**MHE. MINZA S. MJIKA** aliuliza:-

Je, lini Daraja la Lyusa na Itembe na kalavati la Nkoma, Lyusa na Mwanjolo vitajengwa ili Daraja la Sibiti lipitike mwaka mzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Minza Simon Mjika, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Lyusa na makalavati ya Nkoma, Lyusa na Mwanjolo yamejumuishwa katika mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa yenye urefu wa kilometa 389 ambapo Mkandarasi ameshapatikana na mkataba wa ujenzi unatarajiwa kuwa umesainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa daraja la Itembe lenye urefu wa mita 150 lililopo katika Mkoa wa Simiyu, kazi za ujenzi zinaendelea na zimepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2023; ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Minza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Majibu aliyoyatoa yako sahihi na kama yatatekelezeka, Meatu tutafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mpango huu wa kujenga madaraja haya kwa kupitia barabara hiyo ya lami itakuwa ni mwezi Oktoba: Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga madaraja haya kwa muda mfupi, Lyusa pamoja na Chobe ili wananchi wa Meatu waendelee kutumia ile barabara kwa mwaka mzima? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Minza yote kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi, haya madaraja ni madaraja aina ya *drift,* na katika mpango ambao tutaujenga sasa kwa mpango mkubwa wa *EPC+F,* kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, tunategemea mradi huu usainiwe kabla ya mwisho wa mwezi Juni. Kwa hiyo, tumejumuisha hayo madaraja, yatajengwa wakati huo mradi mkubwa unatekelezwa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ndaisaba.

Na. 310

**Mradi wa Bwawa la Umeme wa Rusumo**

**MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza:-

Je, lini Mradi wa Bwawa la kufua umeme wa RUSUMO utazinduliwa ili kuondoa tatizo la kukatika kwa umeme Ngara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swala la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kufua umeme wa Rusumo wa Megawati 80 wa nchi tatu za Tanzania, Burundi

na Rwanda ambazo zitagawanywa sawa, umefikia asilimia 99 na utaanza kufanya kazi mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashine tatu za kuzalisha umeme zitawashwa kwa mashine moja kila mwezi kuanzia mwezi wa Juni na hivyo tunatarajia kuuzindua baada ya mwezi wa saba baada ya kuwashwa kwa mashine zote tatu kukamilika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimefurahishwa na majibu ya Serikali nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa eneo lile la Rusumo limewahi kukumbwa na majanga ya moto hasa eneo lile ambalo bwawa lenyewe limejengwa. Na kwa kuwa ulipotokea moto tulilazima kuomba ndege ya kuzima moto kutoka Taifa Jirani. Ni upi mkakati wa Wizara wa kuhakikisha tunakuwa na gari la zimamoto ili kulinda miundombinu yetu tuliyowekeza pale, pale itakapotea majanga ya moto kama ilivyotea huko nyuma? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa niaba ya Serikali kwa kufurahishwa na majibu haya na ukamilikaji wa mradi. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufatilia mradi wote lakini hasa suala la kuzima moto. Nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalichukua tunaamini mradi utakapo kamilika kuna *serving* ambayo itatafanyika. Tutahakikisha basi tunawashawishi ili waombe katika mahitaji yao muhimu ya matumizi ya ile pesa itakayobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Miradi ya *CSR* ambayo itaanza kufanyika baada ya mradi kukamilika tutawashauri pia walilete kama moja wapo ya hitaji lao ili

tuweze kulifanyia kazi na Serikali itahakikisha kwamba linafanyika kwa ajili ya ku–*safe guard* maisha ya watu wanayo tumia maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere jiandae, Mheshimiwa Salome jiandae, Mheshimiwa Sanga jiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri nawashukuru sana Wizara ya Nishati, mmeleta pale vijiji 33 kutengeneza umeme kilometa mbili mpaka kilomita tatu na sasa Mkamburo Mkandarasi atengeneze kilometa moja tu na ameleta mzozo mkubwa kwa wananchi wale waliyopimiwa mara ya kwanza kuwaonyesha kwamba ni kilomita mbili. Ni lini sasa mtaongeza hizo kilomita mbili au tatu zilizokuwa zimepungua kutoka kilometa tatu mlizokuwa mmeongeza zamani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tunaendelea kukamilisha mikataba ya kuongeza kilomita mbili kwa kila kijiji kutoka kwenye ile kilomita moja ambayo ilikuwa inafanyika katika ya awamu ya tatu mzunguko wa pili wa *REA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku siyo nyingi wakandarasi wale ambao wameonekana wakikidhi kufanya vizuri miradi hii ya *REA three round two* watakuja *site* kuonyeshwa hizo kazi za nyongeza. Wale ambao wameonekana wakilegalega tutahakikisha tunapata wengine ili waje wafanye hiyo kazi na kuikamilisha yote kwa pamoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Salome.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi Kata ya Mamboya katika Jimbo la Kilosa maeneo mengi hakuna umeme. Nini mpango wa Serikali kuweka umeme katika maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeeleza mara kwa mara hapa Bungeni ni azima ya Serikali wa Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha kwamba kabla kabla ya Desemba, 2023 vijiji vyote vimepata umeme. Naamini katika kata hiyo waliyoitaja vijiji vilivyomo ambavyo havijapata umeme vinakuwa vimepata umeme kabla ya mwezi Desemba kuisha mwaka huu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Wilaya ya Makete mmetupatia mradi wa ujenzi wa Bwawa la Umeme la Rumakali mmeishafanya *demarcation*, mmeifanya tathimini ni takribani miezi mitano toka mmefanya hivyo amjaanza kulipa kwa maana kuwalipa wafanyakazi wale. Muda huu wananchi wa Makete wanawasikiliza ni lini Serikali itawalipa wananchi wanaozunguka bwawa hilo ili waachane na shughuli za kilimo na za kiuchumi zilizoko pale waanze kufanya shughuli zingine? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikweli Serikali ya Awamu ya Sita inayo dhamira ya kujenga Mradi wa Rumakali wa kuzalisha megawati 222 kwa kutumia nguvu ya maji. Kama alivyosema Mheshimiwa Festo tayari tumeishafanya upembuzi yakinifu na tathimini ya *site* imeishafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotarajiwa sasa ni mwezi unaofuata wa sita wananchi wataenda kuonyweshwa nani atalipwa shilingi ngapi, ili kwenye mwaka wa fedha unaokuja kuanzia Julai fidia hiyo iweze kufanyika. Kwa hiyo, wananchi wawe na subiri kidogo ndani ya miezi miwili, mitatu fidia yao itaanza kulipwa kwa ajili ya kupisha maeneo ya mradi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Habari, Mawasiliano. Mheshimiwa Sangu kwa niaba ya Mheshimiwa Bupe.

Na. 311

**Changamoto ya Mawasiliano Kata za Kwela**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA K.n.y. MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto za mawasiliano ya simu Kata za Milepa, Zimba, Kaengesa na Lusaka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI,** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Kwela kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilibaini kuwepo kwa changamoto katika Kata za Lusaka, Milepa, Kaengesa pamoja na Zimba. Hata hivyo, Kata ya Lusaka imepata mtoa huduma wa kufikisha huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata za Milepa, Zimba pamoja na Kaengesa zitafikishiwa huduma za mawasiliano kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Bupe.

**MHE BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; Kata ya Mpui, Ikozi na Lusaka hayana kabisa minara ya simu. Ni lini sasa Serikali itajenga minara ya simu kwenye kata hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; minara iliyopo Kata ya Milepa, Zimba, Mfinga na Lusaka minara hiyo haina kabisa *internet.* Ni lini sasa Serikali itaweza kuweka *internet* kwenye minara hiyo hili wananchi wasiweze tena kupanda kwenye miti kutafuta *internet?* Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kuhusu kata ya Mpui pamoja na Ikoze Serikali iko katika utaratibu wa kufanya tathimini na tathimini hiyo itakapokamilika Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika kata hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili maeneo ya Milepa pamoja na Zimba ni azima ya Serikali kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuhakikisha kwamba tunapanua wigo wa matumizi ya *internet* kutoka asilimia 45 mpaka 80 Serikali imeshaanza na minara 488 katika awamu ya kwanza na katika awamu ya pili tutajumuisha Kata ya Milepa na Zimba ili wananchi wa maeneo hayo wapata huduma ya *internet*, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lemburis, jiandae Mheshimiwa Nyamoga.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Jimbo la Arumeru Magharibi kuna kata kama tano ambazo hazina mawasiliano Kata ya Bwawani yenye vijiji vinne, Olonyowase yenye vijiji vinne, Oljoro yenye vijiji vitatu, Laroi vijiji vitatu na Mwande vijiji vitatu.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka minara na kuhakikisha kwamba wananchi wale ambao wanateseka kupanda juu ya miti na juu ya milima na vigongo kwa ajili ya kupata mawasiliano ya kuwasiliana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupokea changamoto ya mawasiliano katika kata ambao Mheshimiwa Mbunge, amezitaja. Tutazifanyia kazi na baadae tutamrejea kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma ya mawasiliano.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Nyamoga, jiandae Mheshimiwa Iddi Kassim, jiandae Mheshimiwa Shonza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru napenda kujua ni lini wananchi wa Kata ya Masisile, Udekwa, Ilole na Nyanzwa katika Wilaya ya Kilolo watapata mawasilino ya simu na kuacha kupanda miti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZARI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya

Masisiwe, Udekwa, Mahenge, Kimara, Kilolo pamoja na Ebomu tayari Serikali inaenda kuingia mikataba na watoa huduma kesho tarehe 13 kwa ajili ya kufikisha huduma ya mawasiliano katika Jimbo la Kilolo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim, jiandae Mheshimiwa Shonza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya mawasiliano kwenye Kata ya Jana, Mwalugulu, Kashishi, Chela na maeneo mengine je, ni lini sasa Serikali itaanza rasmi ujenzi wa minara hii katika maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshmiwa Naibu Spika, kwa Kata ya Jana tayari tumepata mtoa huduma *Vodacom,* Kata ya Mwalugulu tumepa mtoa huduma tigo na kata zingine na uhakika kwamba Mheshimiwa Mbunge akishatoka hapa tutawasiliana ili ajue watoa huduma gani wanaenda kutoa huduma katika maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mshimiwa Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Kata ya Kapele pamoja na Kata ya Mkomba katika Jimbo la Momba ni miongoni mwa kata ambazo zenye shida kubwa sana ya mawasiliano. Naomba kufahamu ni lini Serikali itapeleka mawasilino katika kata hizo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kata

ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge zipo katika vijiji 2,116 ambavyo tunasubiri Serikali ipate fedha ili tuweze kufikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Mheshimiwa Zaytun Seif Swai.

Na. 312

**Kukomesha vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto**

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza: -

Je, kuna mkakati gani wa kukomesha vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Ambapo, kamati za ulinzi wa wanawake na watoto zimeundwa kuanzia vijijini, mitaa hadi Taifa. Madawati ya jinsia na watoto sasa yako vituo vyote vya polisi. Madawati ya ulinzi na usalama wa watoto yanaendelea kuundwa ndani na nje ya shule zote za msingi na sekondari. Vyuo vyote vimeundwa madawati ya jinsia na mabaraza ya watoto 560 yameanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha utekelezaji wa MTAKUWWA, Serikali imeelekeza halmashauri zote kuhakikisha, ajenda ya kutokomeza ukatili kwa wanawake na watoto ni ya kudumu kwenye vikao ngazi zote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Swai.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Hali ya ukatili nchini hapa ni mbaya bado hususani kwa wanawake na watoto. Kwanza niwapongeze umoja wa wanawake Tanzania kwa kuweza kufatilia ufanisi wa madawati ya kijinsia nchi nzima. Lakini vilevile madawati haya bado yanachangamoto kubwa sana ikiwemo ukosefu ya miundombinu rafiki ya kuhudumia wahanga hawa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka mazingira rafiki ya kuboresha miundombinu hii ili kuulinda usiri wa wahanga hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni juzi tu kuna kesi ya ulawiti mzazi kamlawiti mtoto wake Mkoani Shinyanga na kesi hii imepelekwa Mahakani juzi. Tukio hili limetokea Januari lakini kesi imepekwa juzi, mtuhumiwa huyu amepewa dhamani.

Je, Serikali haioni licha ya ushahidi wote uliyopelekwa Mahakani lakini mtuhumiwa huyu kapewa dhamani; je, Serikali haioni kwamba kwenye kulegeza mazingira haya ya kesi hizi inachochea mazingara haya kwenye jamii zetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, madawati mengi yalianzishwa kwa kutumia majengo ya zamani ndani ya vituo vya polisi. Hata hivyo

Serikali itaendelea kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jensi la Polisi ili kuboresha madawati hayo lakini hata hivyo hadi sasa madawati 79 yenye viwango yameisha jengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili; kosa la ubakaji na ulawiti ni makosa ambayo yanadhaminika kisheria hivyo watuhumiwa kuachiwa huru na kupewa dhamana haimanishi Serikali ina halalisha na kuchochea ongezeko na vitendo vya ukatili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kama kuna vifungu vya sheria ambavyo mnahisi vinaleta msongamano kwa wananchi ama vinaleta tatizo basi Waheshimiwa Wabunge mlete maoni yenu ili Wizara ya Katiba na Sheria iweze Kutunga Sheria na kutafuta……

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri, ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mheshimiwa Kakunda. *(Makofi)*

Na. 313

**Kuweka alama za mipaka kutenganisha hifadhi na vijiji**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaweka alama za mipaka kutenganisha maeneo ya hifadhi na vijiji 975 vilivyotolewa kwenye Hifadhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya kuweka alama za mipaka kutenganisha maeneo ya Hifadhi na Vijiji 975 vilivyotolewa kwenye hifadhi imefanyika katika baadhi ya hifadhi na bado kazi hiyo inaendelea. Hifadhi zilizowekewa alama za mipaka mpaka sasa ni pamoja na eneo la kilomita za mraba 1,500 za Hifadhi ya Pori Tengefu Loliondo vigingi 422 vya alama vilishawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Pori la Akiba la Wamimbiki alama 277 na kilomita 156 za mkuza zimetengenezwa. Hifadhi ya Pori la Akiba Swagaswaga alama 226 kati ya 250 na kilomita 27 za mkuza zimetengezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Pori la Akiba Mkungunero alama 99 kati ya 157 na kilomita 35.8 za mkuza zimetengenezwa. Hifadhi ya Taifa ya Ruaha alama 650 na kilomita 177 za mkuza zimeishatengenezwa pamoja na Bonde la Usangu, alama 632 zimewekwa kwenye eneo lenye urefu wa kilomita 316 kati ya 350 na mkuza wenye kilomita za mraba 177 umechongwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoani Tabora, alama za mipaka zimeshawekwa kwenye vijiji vitano vya Mwendakumila, Mwaharaja, Chemkeni, Uhindi na Nsimbo vya Wilaya ya Kaliua vilivyokua kwenye hifadhi ya Ulyankulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika na usimamizi wa hifadhi, kuendelea na utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri ikiwemo kazi ya kuweka mipaka kwa kutumia alama za kudumu zinazoonekana ili kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza la kwanza baada ya ziara ya mawaziri nane kwenye maeneo yetu ya Wilaya Sikonge. Serikali ilituma timu ya watalamu ambao ilifanya kazi na viongozi wa vitongoji, vijiji na kata na mimi kazi hiyo waliyoifanya narizika. Kwa sababu waliweka mipaka na rangi kwenye hiyo mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo nitayataja Luseseko, Isenga na Manzagata, Misulu, Simbaudenga, Ngakaro, Kawemimbi na Manyanya ya 2,567 zina wakazi 25,000. Sasa swali la kwanza je, ni lini hasa kwenye maeneo haya yenye wakazi wengi watakuja kuweka bikoni ili kuwaondolea wasiwasi wananchi wangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kwa kuwa uamuzi wa Serikali wa mwaka 2019 uliondoa zile mita 500 za bafa *zone* ambazo zilikuwa chini ya hifadhi kipindi kile sasa zikawa chini ya halmashauri ili waweze wananchi kuzitumia je, hizo mita 500 kuzunguka maeneo yote ya hifadhi wananchi watakabidhiwa lini kwenye halmashauri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza suala la lini hasa bikoni zile zinaenda kuwekwa, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika eneo lako watalamu wanakwenda kuendelea na shughuli hizi. Kwa sababu mpaka sasa watu wako uwandani wanaendelea na kazi. Kitu cha msingi kikubwa kuweka msukumo mkubwa ambao watawezesha sasa alama zote katika maeneo husika ziweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote katika maeneo yenu yanayopitiwa na hii miradi tuwaombe wananchi wawe watulivu sana katika zoezi hili kwa sababu wakati mwingine linapotoshwa katika ile tafsiri halisi wakati utekelezaji umesimama imara kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; hii bafa *zone* ambayo tumeiyondoa katika maeneo yetu, wakati zoezi la upimaji wa vijiji unao endelea ndiyo wakati ambao utabainisha hizi mita 500 za eneo ambalo zinatakiwa zirudishwe kwenye halmashauri, naomba tu tuwe watulivu wakati zoezi hili likiendelea, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii Mheshimiwa Mzeru.

Na. 314

**Hitaji la miundombinu katika kivutio cha utalii *Uluguru Waterfalls***

**MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaweka miundombinu katika kivutio cha utalii cha *Mount Uluguru Waterfall?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nora Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kujenga miundombinu mbalimbali ikiwemo ngazi kuelekea kwenye Maporomoko ya Hululu, ujenzi wa choo, kuweka

miundombinu ya maji, mfumo wa umeme wa jua na mashine ya kusukumia maji na kujenga daraja la mbao kuvuka mto Mgeta. Aidha, Serikali kupitia mradi wa kupunguza athari za UVIKO -19 ilikarabati barabara ya kuelekea kwenye msitu huo wenye urefu wa Kilometa nane kutoka Kijiji cha Kibaoni hadi Bunduki kwenye kivutio cha Maporomoko ya Hululu. Ukarabati huo umewezesha kufikika kwa urahisi kwenye kivutio hicho kwa shughuli za utalii na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea kuhamasisha wawekezaji kuwekeza miundombinu ya utalii katika msitu huo. Miundombinu ya utalii inayoweza kuwekezwa na sekta binafsi ni pamoja na makambi *(camp sites)*, *lodge*, *hotel* na maeneo ya burudani, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mzeru.

**MHE. NORAH W. MZERU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini Serikali itawekeza fedha kwenye kuutangaza Mlima Uluguru kama kivutio kizuri cha utalii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa maporomoko haya yanaleta mvutio mkubwa kwa utalii.

Je, ni lini Serikali ina mpango wa kuyatunza na kuhifandhi mazingira yaliyozunguka maporomoko hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutapita vizuri kwenye Jibu la msingi tulisema kwamba Serikali kupitia mfuko wa UVIKO tayari tulishawekeza pale takribani shilingi 214.3 ilikuwa lengo na madhumuni ni kujenga ile miundombinu ya barabara ya kilomita nane kutoka barabara kuu kuelekea kwenye kivutio hichi. Lakini kiubwa nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti yetu ambayo tunategemea kusoma hivi karibuni tutahakikisha kwamba tutatenga fungu maalumu la kutengeneza miundombinu rafiki katika kituo ama katika kivutio hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili nimwambie tu kwamba ipo mikakati kabambe ambayo Serikali na Wizara tumeshaichukua kuhakikisha kwamba tunatunza mazingira katika eneo hili. Tumeshakaa sisi ndani ya Wizara ya Maliasili na Utalii, lakini pia tumeshakaa na watu wa Halmashauri pamoja na *TFS* kuhakikisha kwamba, la kwanza tunakwenda kupanda miti ya kutosha, lakini tulishatoa maelekezo kwa kuwaambia wananchi waliozunguka maeneo yale kwamba wasifanye shughuli zozote za kibinadamu katika meneo yale, ikiwemo za ufugaji, kilimo na nyingine. Lengo na madhumuni ni ili tutunze kivutio, tuvute watalii lakini pia tuongeze pato, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Mpembenwe.

Na. 315

**Kugawa maeneo ya Bonde la Mto Rufiji kwa njia ya mnada**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza kugawa maeneo ya kilimo kwa njia ya mnada katika Bonde la Mto Rufiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Bonde la Mto Rufiji ni miongoni mwa mabonde 22 ya kimkakati na linakadiriwa kuwa na eneo lenye ukubwa wa hekta 64,896 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde hilo ili kujua ukubwa wa eneo na gharama halisi za kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji katika bonde hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baada ya upembuzi yakinifu kukamilika, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mkoa wa Pwani, zitaandaa Mpango shirikishi wa namna bora ya ugawaji wa maeneo ya kilimo katika bonde hilo ili kuongeza uzalishaji na tija.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza;

Je, ni lini sasa mchakato huu wa Serikali utakwenda kukamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa maeneo haya ni maeneo ya asili ya makazi ya wananchi, kwa mfano, maeneo ya Mtunda, Moyoyo, Nyafeja Pamoja na Nguwalo.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa kuweza kuhakikisha wakati wa kugawa maeneo haya wananchi hawa wanakwenda kupewa kipaumbele, kupata maeneo ya kulima ili waweze kuendesha maisha yao na vilevile kuchangia Pato la Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni lini mchakato huu unakamilika? Tarehe 23 Mei, 2023 tunategemea taratibu zote za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziwe zimekamilika na tutaanza ujenzi katika mwaka wa fedha unaoanza 2023/2024, kwa maana kuanzia tarehe 1 Julai mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili la kuhusu maeneo haya kugaiwa kwa wakazi wa maeneo hayo. Ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba wanufaika wa kwanza wanakuwa ni wakazi wa maeneo hayo. Kwa hiyo nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wake watapata maeneo katika mashamba haya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendela, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Nyalusi.

Na. 316

**Hitaji la Chuo cha VETA – Kilolo**

**MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Wilaya ya Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge Viti Maalum kutoka Iringa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kujenga chuo cha ufundi stadi katika kila mkoa na wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 64 ambazo zilikuwa hazijajengewa vyuo hivyo. Tayari Serikali imeshakamilisha kuandaa michoro na upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kilolo eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha ufundi stadi ni katika Kijiji cha Luhindo Kata ya Mtitu. Aidha, pamoja na kiasi cha shilingi milioni 45 kilichotolewa awali kwa ajili ya shughuli za maandalizi, tayari Serikali imetuma kiasi cha shilingi milioni 228 kwa kila chuo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nancy.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Serikali kwa utekelezaji ambao unaendelea. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa vyuo vingi vya *VETA* vina uhaba wa walimu na vifaa vya kujifunzia;

a) Je, Serikali ina mpamngo gani wa haraka wa kutatua changamoto hiyo?

b) Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mitaala ya *VETA* inaendana na shughuli za kiuchumi katika maeneo husika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nancy, Mbunge Viti Maalum kutoka Iringa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali lake la kwanza, anataka kufahamu kuhusu mkakati wa Serikali kwa upande wa walimu na vifaa. Naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshapata kibali kwa ajili ya kuajiri waalimu 514; na mpaka hivi sasa walimu 151 tayari wameshaajiriwa na kuripoti kwenye vile vyuo ambavyo vilikuwa vinaendesha mafunzo na hivi vyuo vipya; na tutaendelea na mkakati na mchakato huo wa kuajiri walimu kwa kadri fedha zitakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika swali lake la pili kuhusiana na suala la vifaa vya kufundishia na kujifunzia, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu, kwamba Serikali tayari ilishatoa jumla ya shilingi bilioni 8.6 kwa ajili ya ununuzi wa samani kwenye vyuo vile 25 pamoja na vile vya mikoa na vifaa hivyo tayari vimeshanunuliwa na kupelekwa kwenye maeneo hayo. Lakini kwa upande wa vifaa vya kufundishia naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, tarehe 22 mwezi wa nne mpaka tarehe 30 mwezi wa nne, timu yetu ya wataalamu kutoka Wizara ya Elimu ikiongozwa na mimi mwenyewe pamoja na watu wa *NACTVET* pamoja na *VETA* tulifanya ziara katika nchi ya China kwa ajili ya kufanya *venting* ya vifaa vya kujifunzia na kufundishia, na Serikali tayari imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili kuhusiana na suala la mitaala, naomba nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge tunaendelea na mchakato wa mapitio ya mitaala pamoja na sera yetu ya elimu katika ngazi zote ikiwemo na hii ya *VETA*. Basi ushauri wake huu wa kuona namna gani tunaweza kuhusisha shughuli za kiuchumi na mitaala yetu tutakwenda kulizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha, ni kipindi sasa cha wageni. Wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Wageni waliopo Jukwaa la Spika; wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni Ndugu Nsolo Mlozi, Mkuu wa Idara ya Kilimo NMB*;* Ndugu Janeth Shango, Meneja Kanda ya Kati NMB; na Ndugu Grace Matemu, Meneja wa Tawi la Bunge. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya ambao ni viongozi kutoka Wizara ya Afya, Dkt. Seif Shekalaghe - Katibu Mkuu; Dkt. Grace Magembe - Naibu Katibu Mkuu; na Profesa Tumaini Nagu - Mganga Mkuu wa Serikali, karibuni. *(Makofi)*

Viongozi hawa wameambatana na Kamati ya Uratibu wa Kuifanya Tanzania Kuwa kitovu cha utalii wa tiba, wakiongozwa na Profesa Mohamed Janabi. *(Makofi)*

Pia yupo mtoto aliyekuwa na ugonjwa wa selimundu *(sickle cell)* na kutibiwa kwa kupandikizwa uloto Hospitali ya Benjamin Mkapa. Pia yupo na ndugu yake aliyemtolea uloto pamoja na wazazi wao, ambao pia ameambatana na timu

ya wataalam waliompatia huduma, karibuni na hongereni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo mambo ya kuitangaza Tanzania. Waziri wa Afya haya uyaseme ili tupate wagonjwa kutoka nchi zingine na wagonjwa wa ndani ya nchi, hongereni sana madaktari. *(Makofi)*

Wapo pia viongozi na madaktari wa ngazi zote kutoka Wizara ya Afya, Wakurugenzi wa taasisi, timu za madaktari, wasajili wa maabara wote simameni, mliokuja hapa. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, ni familia yake wakiongozwa na dada yake Ndugu Mwanahawa Mwalimu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni sita wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati kutoka Bukoba Mjini wakiongozwa na Twaibu Juma ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Siasa Bukoba Mjini. *(Makofi)*

Ukishaona Mjumbe wa Kamati ya siasa anaingia humu ndani ujue biashara imeanza huko. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Doto Biteko, Waziri wa Madini kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Oran Njeza kutoka Mbalizi Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Innocent Kalogeris kutoka nchi ya Australia, karibu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Joseph Tadayo kutoka Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wageni 31 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga kutoka Vwawa, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Wageni 30 wa Mheshimiwa Justin Nyamoga kutoka Kilolo, Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Neema Mwandabila kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Kenneth Nollo kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Mlaghila wanaotoka Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Mkoa wa Mbeya na hawa ni Madiwani. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Nusrat Hanje kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wakitokea Mkoani Kilimanjaro, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi kutoka Malinyi, Mkoa wa Morogoro**.** *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo makatibu saba wa vijana wa UVCCM kutoka Wilaya za Mkoa wa Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wafanyakazi 27 kutoka Chuo cha Sila cha Jijini Arusha, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Jackline Mtaita na Ndugu Naomi Mtaita. Huyu Jackline mmeona amekaa pale yeye ni mlemavu, ni msichana mdogo sana kwa bahati mbaya alipata changamoto, alipata ajali na hali yake kama vile mnavyomuona. Kaamua kuja Bungeni kutembea, kujifunza lakini na kuonana na baadhi ya Wabunge na kusalimiana. *(Makofi)*

Wageni wawili kutoka Kijiji cha Kafujo Kiregete Kata ya Kamagambo Wilaya ya Karagwe ambao ni Ndugu Method Karoly na Ndugu Bundala Charles. *(Makofi)*

Wanakikundi 22 cha kinamama kiitwacho *Apple* kutoka Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni 11 wa kipindi cha Malumbano ya Hoja cha *ITV* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rashid Shangazi Katibu wa *caucus* anaomba kuwatangazia kikao cha *party caucus* leo Ijumaa tarehe 12 Mei, 2023, saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa leo.

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa tarehe 15 Mei, 2023 itakuwa ni siku ya Kimataifa ya Familia Duniani. Itaadhimishwa nchi nzima katika ngazi ya Mikoa na Wilaya. Kauli mbiu ya mwaka huu itakuwa ni Imarisha Maadili na Upendo kwa Familia Imara.

Kufuatia maadhimisho hayo Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum anawaomba Wabunge wote kushiriki na kuhamasisha wanachi washiriki na kuketi na familia zao ili kujadili mustakabali wa familia kwenye

kudumisha upendo na mshikamano hasa kwenye malezi na makuzi ya watoto na hivyo kuwalinda dhidi ya ukatili.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnaombwa kushiriki kikamilifu katika maadhimisho tajwa katika maeneo yenu ya uwakilishi. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2024

**NAIBU SPIKA:** Waziri wa Afya. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Afya na masuala ya UKIMWI ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya. Ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/2023 na Vipaumbele vya Wizara ya Afya kwa mwaka 2023/2024. Aidha, ninaliomba Bunge lako tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida pamoja na miradi ya maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu, kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo.

Aidha kwa heshima na unyenyekevu mkubwa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia sekta ya afya. Sekta inayogusa maisha ya kila siku ya kila mtu, mwanamke au mwanaume, kijana au mzee, tajiri au masikini, kwani mtu ni afya na afya ni mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua jukumu kubwa nililonalo mimi pamoja na Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel la kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya. Namuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitaendelea kuifanya kazi hii kwa weledi, uaminifu na ubunifu mkubwa ili kuhakikisha Watanzania wanakuwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kutupatia rasilimali fedha nyingi, ikiwemo kuimarisha miundombinu ya afya katika ngazi ya halmashauri na mikoa yote nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba, kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ametimiza wajibu wake. Deni limebaki kwetu sisi watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuhakikisha tunatoa huduma bora za afya kwa wananchi wetu kwa kuzingatia weledi, maadili, miiko ya kitaaluma ya watoa huduma za afya sambamba na kuzingatia kutoa huduma nzuri kwa wateja, matumizi ya lugha ya staha na lugha ya faraja kwa wateja wetu. Tunakuhakikishia Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kwamba mimi na Naibu Waziri na wasaidizi wetu hatutalala, tutafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya, huduma za kinga na tiba ili kupambana na adui maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali inatimiza wajibu wake wa kuboresha huduma za afya. Nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na maelekezo yake ya mara kwa mara kwetu ya kuhakikisha tunaimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 5 Aprili, 2023 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yanayotekelezwa na Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa weledi, ubunifu na uadilifu mkubwa, lakini pia kwa kuzingatia na kusimamia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge letu. Aidha, nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kazi kubwa na nzuri unayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge katika kusimamia mijadala ndani ya Bunge. Tunapenda kuwahakikishia kwamba, uongozi na watumishi wa Wizara ya Afya tutatekeleza wajibu wetu wa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia sheria na kanuni mbalimbali zinazopitishwa na Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ambao umeiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za afya. Kipekee niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ikiongozwa na Mwenyekiti mahiri, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni kwa ushauri na maelekezo mbalimbali

wanayoyatoa katika kuboresha utendaji wa Wizara, hususani kwa kipindi cha maandalizi ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru sana Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia, lakini kipekee tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa jitihada zao binafsi wanazozifanya za kutatua changamoto za afya katika majimbo yao kwa kutumia fedha zao za mishahara yao ikiwemo kuchangia ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, kununua mashuka, vifaa tiba na kuwagharamia wagonjwa wanaoshindwa kulipa huduma za afya katika majimbo yao. Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Waheshimiwa Wabunge, kama si hivyo, mambo yasingeenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pole kwa Watanzania wote waliopoteza ndugu zao, jamaa na marafiki. Kwa namna ya pekee natoa pole kwa familia na jumuiya ya wataalam wa afya nchini kwa kupoteza wataalam mbalimbali wa afya wakati wakitimiza wajibu wao wa kuwahudumia wananchi. Kitendo kilichotusikitisha sana ni mtumishi wetu wa tarime kuuliwa wakati akitimiza wajibu wake wa kuokoa maisha ya Watanzania. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupoteza wataalam wa afya wakati wa kutoa huduma, natoa pongezi na shukrani za pekee kwa wataalam wote wa afya nchini waliokuwa mstari wa mbele katika kuhudumia wahisiwa na wagonjwa wa *marburg* Mkoani Kagera, tumempoteza mtumishi mmoja wa afya lakini nashukuru wote ambao walijitoa usiku na mchana kuwahudumia wagonjwa, lakini tunawashukuru pia, wataalam wote wa afya ambao wanafanya kazi usiku na mchana bila kuchoka katika kuwahudumia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali, sasa naomba nitoe maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2022/2023, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na vipaumbele vya mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nitakwenda harakaharaka, lakini kwa upande wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 tulikadiriwa kukusanya Shilingi bilioni 622.9 na hadi kufikia Machi, 2023 tumekusanya bilioni 435, sawa na asilimia 70 ya lengo. Kwa upande wa bajeti Bunge lako Tukufu lilituidhinishia Sh.1,109,421,722,000 ili kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Machi, tumepokea jumla ya shilingi bilioni 742.9, sawa na asilimia 67 ya fedha. Kati ya hizi, fedha za maendeleo tulizopokea ni bilioni 284.4, sawa na asilimia 51. Taarifa ya kina iko katika ukurasa wa 7-10 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara imepokea kiasi cha Shilingi bilioni 77.2 kutoka kwa wadau wa maendeleo kupitia mfumo wa *D-Fund*. Fedha tumepokea bilioni 68.6 kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, *Global Fund*, bilioni 5.8 kutoka *Susan Thompson Buffet Foundation*, bilioni 2.0 kutoka *BADEA-COVID-19 Response grant* na Shilingi milioni 192 kutoka *Global Alliance for Vaccine (GAVI)* kwa ajili ya chanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kazi zilizotekelezwa; kwa upande wa huduma za kinga tumeendelea kutoa chanjo, hususan chanjo za watoto na kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, tunapima kiwango cha uchanjaji kwa kuangalia chanjo ya *Penta3* ambayo inazuia magonjwa ya donda koo, kifaduro, kupooza, homa ya ini na homa ya uti wa mgongo. Kwa hiyo, kwa mujibu wa takwimu zetu tumewafikia watoto 1,596,951 sawa na asilimia 98.6 tukilinganisha na asilimia 94 mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa pia chanjo kwa ajili ya kuwakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi. Kwa sababu ya chanjo hizi hazipatikani tumejikita katika wasichana wenye umri wa miaka 14, tumewachanja wasichana 535,708. Lengo letu ni kutoa chanjo hizi kuanzia miaka tisa hadi miaka 14.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuimarisha huduma mbalimbali za lishe, ikiwemo kutoa matone ya *Vitamin A* kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano. Takwimu nimezionesha katika hotuba yangu, tumewafikia takribani watoto milioni 9.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa katika masuala ya chanjo ni utashi, utayari na uongozi wa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan wa kusimamia masuala ya lishe ambapo kwa mara ya pili amewasainisha mikataba ya lishe Wakuu wote wa Mikoa Tanzania Bara kupima utekelezaji wa masuala ya lishe. Tumebainisha viashiria 15, tunaamini kabisa endapo kila Mkuu wa Mkoa atasimamia viashiria hivi, basi tutaweza kuboresha hali ya lishe, hususan kwa watoto wa umri wa chini ya umri wa miaka mitano, vijana balehe na wanawake wa umri wa kuzaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya ya uzazi, mama na mtoto. Tumeendelea kutoa huduma kabla ya kujifungua, kabla ya ujauzito, ambazo ni huduma za uzazi wa mpango. Tumenunua bidhaa mbalimbali na katika kipindi hiki tumepata au tumewahudumia wateja milioni 4.5 wa uzazi wa mpango wanaotumia njia za kisasa kulinganisha na wateja milioni 4.9 mwaka jana. Maana yake kiwango cha matumizi ya njia za kisasa za uzazi wa mpango zimepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za afya wakati wa ujauzito. Tumeendelea kuhakikisha tunatoa elimu, lakini pia kuhakikisha wanawake wajawazito wanahudhuria kliniki. Kwa mujibu wa takwimu zetu jumla ya wajawazito 2,028,151 sawa

na asilimia 98 walihudhuria kliniki kwa mara ya kwanza, ikilinganishwa na wajawazito milioni 1.5 mwaka jana. Maana yake wanawake wajawazito wana imani na huduma zinazotolewa katika vituo vyetu vya kutoa huduma za afya. Niendelee kuwasisitiza kuwahi kuanza kliniki mapema ili kutambua mimba zilizo salama na zile zenye matatizo kama kutunga nje ya kizazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma wakati na baada ya kujifungua; takwimu zinaonesha kwamba, wajawazito 1,500,404 walijifungulia katika vituo vya kutoa huduma za afya ukilinganisha na wajawazito 1,400,003 katika kipindi kama hicho. Vilevile tumepata vifo vinavyotokana na uzazi, kwa mujibu wa takwimu, vifo 943 kulinganisha na vifo 982. Takiwimu rasmi ya vifo vitokanavyo na uzazi zitatolewa ndani ya miezi michache mwaka huu baada ya Taasisi ya Takwimu ya Taifa *(NBS)* kukamilisha kufanya uchambuzi na kuchakata taarifa zilizokusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea kuimarisha huduma kwa watoto wachanga ambapo pia tumenunua vifaa tiba, tutavisambaza katika vituo 120. Waheshimiwa Wabunge wakiangalia kiambatisho namba 4 na namba 5 vya hotuba yangu, wataona ni vituo gani na majimbo gani tutapeleka vifaa tiba hivyo. Niwaahidi wote, majimbo yote watapata vifaa tiba kwa ajili ya kuhudumia watoto wachanga, ikiwemo watoto wachanga mahututi na watoto njiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeimarisha pia huduma kwa vijana, kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 43 hadi vifo 33 katika vizazi hai mwaka jana. Vifo vya watoto wa umri wa chini ya miaka mitano vimepungua kutoka vifo 67 hadi vifo 43 kama mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kuboresha huduma kwa ajili ya akinamama wajawazito. Katika jukwaa lako tumewatambua Madaktari Bingwa, Wauguzi, Wafamasia 100, naomba wasimame. Hawa watakwenda kujenga uwezo kwenye hospitali za wilaya, hospitali za mikoa na vituo vya afya. Wataifanya kazi hii kwa mwezi mzima na watapita kila mkoa, kwa hiyo, watafanya kile kitu kinaitwa *couching* na *mentorship,* kwamba, hii ndio unafanya kufanya upasuaji, hii ndio unamhudumia mtoto mchanga. Tunawashukuru sana wataalam wetu kwa hiyo, tuna Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Uzazi na Wanawake, tuna Madaktari Bingwa wa Watoto, tuna Wauguzi Bingwa, tuna Wafamasia, tuna watu wa usingizi 100, tutaanza kufanya shughuli hii. Hii ni kuonesha dhamira ya dhati ya Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwamba, linapokuja suala la afya ya mama na mtoto na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi atafanya kila linalowezekana kuboresha huduma kwa wajawazito. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, hawa wataalam hii ni *program* maalum aliyoianzisha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo, tuendelee kumpongeza Rais kwa namna anavyojali afya za Watanzania na tunawapongeza Madaktari wetu wote kwa namna mnavyofanya kazi vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pia tumeendelea kununua dawa kwa ajili ya watoto wachanga kwa sababu, watoto hawa wanakufa kwa magonjwa ya homa ya mapafu *(pneumonia)* pamoja na kuharisha. Nataka kusisitiza jambo moja, kidonge myeyuko cha *amoxicillin*, zinc na *ORS* kwa ajili ya kutibu kuhara kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, dawa hizi zinanunuliwa na Serikali na zinapaswa kutolewa bure kwa watoto wote nchini. Naomba kulisisitiza hili. Waganga Wakuu na Waganga Wakuu wa

Mikoa kusimamia suala hili. Amoxicillin, ORS na *zinc* zinapaswa kutolewa bure kwa watoto wote wenye umri wa chini ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuboresha huduma za afya ya uzazi kwa kundi la vijana, tumeongeza vituo kutoka 215 hadi 905. Kukamilisha suala la afya ya mama na mtoto tumebadilisha ile kadi ya kliniki, tumetengeneza vitabu vipya ili tuweze ku-*capture* masuala yote muhimu kuhusu maendeleo ya watoto. Kwa hiyo, tumetengeneza kitabu kwa ajili ya watoto wa kike, tumetengeneza kitabu kwa ajili ya watoto wa kiume. Vitabu hivi haviuzwi ni bure, vinapaswa kutolewa bure kwa watoto wote wanaohudhuria kliniki.

Mheshimiwa Spika, katika mapambano dhidi ya UKIMWI, kifua kikuu, malaria na homa ya ini, tumeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kudhibiti UKIMWI, homa ya ini, kifua kikuu pamoja na malaria. Niseme jambo moja tu kuhusu UKIMWI kwamba, watu milioni 1.6 wanatambua hali zao kuhusu maambukizi ya UKIMWI. Haya ni mafanikio makubwa sana kwetu ni asilimia 95, lakini pia watu 1,612,520 wanaotambua hali zao kuhusu UKIMWI wanatumia dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeangalia ufanisi wa dawa. Tumefanya vipimo kwa wagonjwa 309,263 na asilimia 96.6 ya waliofanyiwa vipimo *viral load suppression* wameonekana kwamba, UKIMWI au virusi vimefubazwa. Haya ni mafanikio makubwa sana, lakini katika mapambano dhidi ya UKIMWI naomba nisione aibu, nitumie Bunge lako Tukufu kueleza tunaona ongezeko la magonjwa ya ngono. Idadi ya magonjwa ya ngono mwaka jana ilikuwa 458,614, sasa hivi imepanda ni 480,448. Nitoe wito kwa Watanzania, hasa vijana, kutumia kinga ili kujikinga na magonjwa ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za tiba, upande wa vituo vya kutoa huduma vimeongezeka

kutoka 8,549 hadi vituo 11,000 takwimu nimeonesha zahanati ni ngapi, hospitali ni ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeimarisha upatikanaji wa dawa, tunafuatilia dawa 2,976 pamoja na vifaatiba, tumebainisha dawa 290 kama za kipaumbele. Tunashukuru sana kutokana na maboresho ambayo tumeyafanya ndani ya *MSD* hali ya upatikanaji wa dawa 290 inaendelea kuimarika kutoka asilimia 52 hadi asilimia 73. Kwenye zahanati bado hali ya upatikanaji wa dawa siyo nzuri. Tunamshukuru Rais kwa kutupatia shilingi bilioni 159.9 sawa na asilimia 80 ya bajeti kwa ajili ya dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za uchunguzi nitaongelea mambo makubwa matatu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, tumenunua mashine za kisasa za *MRI* Sita zenye thamani ya shilingi bilioni 14.5. Lakini kipekee alichokifanya Rais Samia Suluhu Hassan Mtwara Kuchele, Mtwara sasa hivi wana kipimo cha *MRI.* Ndugu zangu Wasukuma, Chato wanaweza kutoa huduma za kipimo cha *MRI. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba Mheshimiwa Spika amekuwa akizungumzia *MRI* katika Hospitali ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya. Tunakuahidi kabla ya Tarehe 30, Juni *MRI* Mbeya itakuwa imefungwa na imekamilika na watu wa Nyanda za Juu Kusini watapata huduma, hawatakuja Dar es Salaam au Dodoma. Tumefunga pia *CT-Scan* mpya 32, 24 zimeanza kufanya kazi. Haya ni mapinduzi makubwa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo watu wa Kigoma wanapata huduma za *CT-Scan,* watu wa Iringa wanapata huduma za *CT-Scan,* Kagera, Shinyanga, Morogoro, Singida, *Mt. Meru,* kwetu Bombo - Tanga, Sekou Toure, Kilimanjaro, Manyara, Kitete, Tabora, Geita, Ruvuma, Rukwa, Mbeya,

Njombe na Simiyu. *CT-Scans* Nane zinaendelea kufungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, mnyonge mnyongeni, Rais Samia ameacha alama kubwa katika kuboresha huduma za uchunguzi, huduma za uchunguzi ndipo inapotofautisha waganga wa kienyeji na huduma za kitaalamu kwa sababu tiba ni uchunguzi, uchunguze kujua kuna nini ndiyo utatoa matibabu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumenunua *x-ray machines* 346, tumenunua *ultrasound* na vifaa vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda nizungumze kuhusu huduma za matibabu. Katika kipindi hiki tumewahudumia wagonjwa milioni 35.8 kulinganisha na wagonjwa milioni 33.6 mwaka jana.

Waheshimiwa Wabunge, hapa pia naomba kuna jambo moja nilisisitize, katika wagonjwa wote waliohudumiwa hawa milioni 35.8, wagonjwa milioni 31 wamepata huduma katika ngazi ya msingi, maana yake wamepata huduma kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku ndiko tunapaswa kuweka nguvu kwa sababu asilimia 86 ya Watanzania wanapata huduma katika ngazi hii ya msingi. Kwa hiyo, ndiyo maana moja ya mipango tuliyokuja nayo chini ya Rais Samia ni kutumia Wataalam Bingwa wale washuke chini ili kuwajengea uwezo wataalamu wetu katika ngazi za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeonesha magonjwa yanayowaathiri zaidi wananchi, yakiwemo mfumo wa hewa, maambukizi ya njia ya mkojo na Malaria. Taarifa yangu katika ukurasa wa 66 hadi 68 inaonesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita pia imewekeza katika huduma za dharura na huduma za wagonjwa mahtuti. Majengo ya dharura yameongezeka kutoka nane hadi 38 kipindi hiki, pia TAMISEMI kuna majengo ya huduma za dharura 80 kwa hiyo kwa ujumla ndani ya miaka miwili ya Rais Samia majengo ya huduma za dharura yameongezeka kutoka Nane hadi kufikia 118. Nani kama mama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za wagonjwa mahututi tumeongeza wodi za wagonjwa mahututi kufikia 45, vitanda vitatoka 258 hadi 1,000. Nchi yetu sasa hivi ina uwezo wa kulaza wagonjwa wa dharura 1,000 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya uchambuzi wa magari ya wagonjwa ambapo kuna magari 761, kati ya hayo magari 595 yanafanya kazi, 221 yapo katika hatua mbalimbali za matengenezo. Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tumekamilisha ununuzi wa magari ya kubebea wagonjwa 727 na magari 77 yameshawasili, lakini tukapata kigugumizi kidogo aanze nani asubiri nani, tukasema bora kwanza yafike angalau nusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za matibabu ya Ubingwa, hospitali zetu za Muhimbili, Jakaya Kikwete, *MOI, Ocean Road,* Benkamin Mkapa, Mbeya, *KCMC,* Bugando, Mtwara, Kibong'oto na Mirembe zimehudumia wagonjwa takribani milioni 4.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja naomba niliseme, hospitali zimetoa misamaha ya takribani shilingi bilioni 88.5 kwa wagonjwa, na hospitali hizi zimeendelea kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ikiwemo kupandikiza figo, kupandikiza uloto na kupandikiza vifaa vya usikivu, pamoja na kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kwa upande wa huduma mpya, Hospitali ya Benjamin Mkapa imeanzisha huduma ya upandikizaji uloto *(bone marrow transplant)* kwa watoto wenye *sickle cell,* na wameshawafanyia watoto watatu kuanzia Januari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, nimsimamishe mtoto wangu Elisha John. Ana miaka 11 amezaliwa na ugonjwa wa *sickle cell* na mama yake ametueleza badala ya kwenda shule anahudhuria miezi mitatu tu, mtoto mwenye *sickle cell* anaishiwa damu, mara anaumwa viungo, mara hivi. Madaktari wetu hawa wamejiongeza, mwanangu Esther John ana miaka Sita amemchangia Kaka yake uloto. Uloto ni sawasawa na kwenye nyama kuna ule kama uteute tunaouvuta, nadhani mnaujua! *bone marrow,* kwa hiyo Esther ametolewa *bone marrow* akamuingizia Kaka yake, Madaktari wetu wamepima mara tatu wamemuona Elisha hana tena ugonjwa wa *sickle cell. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika tano, nitumie fursa hii kwanza kuwapongeza baba na mama Elisha kwa maamuzi waliyoyafanya. Wangesema mwanangu Esther namtoa kidude labda wataenda kumchokonoa, lakini wamewaamini Madaktari wetu. Kipekee nipongeze jopo la wataalam Bingwa wa Kitengo cha Kupandikiza Uloto wakiongozwa na Dkt. Stella. Dkt. Stella naomba usimame, Mwanamama wa Kitanzania, Dkt. Shakilu Jumanne pamoja na Wauguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, hawa ni vijana wetu wa Kitanzania, wamejiongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimsimamishe Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dkt. Chandika. Kwa nini namsimamisha Dkt. Chandika. Serikali

tumewapa vifaatiba, gharama ya kumfanyia mtoto mmoja ni takribani bilioni 58, hospitali wamejichanga wenyewe wakawalipia wagonjwa hawa. Kwenye vipaumbele vyangu tutaonesha nini tunafanya kama Serikali kuwaunga mkono Madaktari Bingwa wetu waliojiongeza na kufanya kazi kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mloganzila nao wamefanya kazi nzuri ya kuanzisha huduma ya kupunguza uzito kwa kuwekewa puto, wametoa matibabu ya kuondoa mawe, matibabu ya njia ya mirija, kuchepusha damu, mambo ni mengi Mloganzila wamefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja kuhusu tiba utalii. Hospitali zetu zimeanza kuaminika, kutoa huduma kwa wagonjwa nje ya nchi kama huduma za tiba utalii *(medical tourism)*. Katika kipindi hiki wagonjwa 812 wamehudumiwa na hospitali zetu kulinganisha na wagonjwa 364 mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wagonjwa hao wametoka Kenya, Uganda, Congo, Comoro, Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi, Msumbiji na *South Sudan*. Kipekee nimsimamishe tena Prof. Janabi na Kamati yake. Wizara tumeunda Kamati ya kuhakikisha tunafanya utalii tiba katika nchi yetu, inaongozwa na Prof. Janabi, tumechukua wataalamu kutoka sekta mbalimbali. Tunataka huduma hizi watu wa Congo, Zambia na kwingine waje Tanzania. Prof. Janabi, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za hospitali zipo, niruke eneo moja la kukabiliana na magonjwa…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri yuko na *CEO* wa *JKCI* pale, Dkt. Kisenge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa, tunatambua Madaktari wetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, tumeweza kudhibiti Ebola haijaingia nchini, lakini tumeweza kudhibiti Ugonjwa wa *Marburg*. Tulikuwa na wagonjwa tisa, wagonjwa sita walifariki, habari njema wagonjwa watatu wamepona na wanaendelea na shughuli zao. Kwenye hili niwashukuru sana wataalam wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa uwazi wake na uongozi wake. Tungeficha labda tungepata wagonjwa wengi zaidi, lakini hatua za haraka zimetufanya kuokoa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali watu katika sekta ya afya tumeendelea kuajiri. Lakini kubwa tena, Rais Samia ameanzisha mpango maalum wa kusomesha Madaktari Bingwa unaoitwa *Samia Health Super Specialization Programme*. Madaktari Bingwa 981 tunawasomesha ndani na nje ya nchi. Madaktari Bingwa 802 ni vyuo vya ndani, Madaktari Bingwa 179 ni nje ya nchi; tunamshukuru sana Rais Samia.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo nimeeleza kwenye kiambatisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya taasisi nimeeleza ukurasa wa 134 mpaka 163.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nizungumze tu kuhusu *NHIF*. Tunao wajibu kama Serikali kulinda uhai na uendelevu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Wataalam wamefanya tathmini, bima ni sayansi, kuna *actuarial studies.* Kwa hiyo kati ya jambo moja walifanya vifurushi vyote na kubaini kifurushi cha *Toto Afya Card* watu wanachangia shilingi bilioni nne

lakini matumizi ni shilingi bilioni 40. Waheshimiwa Wabunge, hiyo siyo bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukaenda mbali, hawa watoto wanakwenda kutibiwa wapi, asilimia 58 ya fedha hizi zinakwenda kwenye *private hospitals,* asilimia 20 zinakwenda kwenye *public hospitals,* asilimia 22 zinakwenda kwenye *faith-based organizations.* Ukiwa Waziri wa Afya huwezi kuendeleza mfumo wa bima huu katika kila shilingi 100 mgonjwa anatumia shilingi 677.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusu *NHIF* ni udanganyifu. Tumechukulia hatua watumishi wetu wa Mfuko wa Bima ya Afya, tumewapeleka mahakamani na kuna wengine tumewafukuza kazi. Watumishi 131 tumewapeleka kwenye mabaraza. Tumesitisha vituo vya afya 38 kwa sababu wao wamekiri wenyewe kwamba hizi hela wanadai, mtu amefanya upasuaji wa 100,000 anakwambia 1,000,000 au 10,000,000, hatuwezi kuwa na Mfuko wa Bima ya Afya wa aina hii! Kwa hiyo tumewasitishia mikataba, tutaendelea kuwasikiliza tuone jinsi gani tutaliweka sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema mbele ya Bunge lako Tukufu, Serikali haitamvumilia mtumishi yeyote wa *NHIF* anayesababisha udanganyifu, mtoa huduma za afya yeyote anayefanya udanganyifu au mwananchi yeyote anayefanya udanganyifu. Tunawajua wananchi wanatumia kadi za bima za afya zisizo za kwao, kadi za ndugu na jamaa zao. Hatuwezi kuwa na Mfuko wa Bima ya Afya wa aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ni mengi, nimeonesha pia *MSD,* Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye vipaumbele: -

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa;

ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya;

iii. Kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa;

iv. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto;

v. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi;

vi. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao na tiba shufaa;

vii. Kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatari;

viii. Kudhibiti Magonjwa ya UKIMWI, *TB,* Malaria na Homa ya ini;

ix. Kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza, hususan tumebainisha Magonjwa matatu; Kisukari, Shinikizo la Juu la Damu na Magonjwa ya Moyo;

x. Kuimarisha upatikaji wa wataalamu wa afya;

xi. Kuendeleza na kusimamia tiba asili na tiba mbadala nchini;

xii. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu; na

xiii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipaumbele hivi kwenye kinga, chanjo tumetenga shilingi bilioni 114, ikiwemo kununua majokofu 1,600 na magari 102 ya kusambaza chanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye lishe tutanunua vinu 300 vya kuongeza virutubisho na kutoa matone ya *Vitamin A* kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kinga – hili nalo ni jipya – tuna watu wanaitwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii *(Community Health Workers)*. Hawa mtu wa UKIMWI ana-*train* siku moja, mtu wa *TB* ana-*train* siku moja, mtu wa Malaria vivyo hivyo, kila mtu ana wahudumu wake wa afya ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunakwenda kwenye mfumo unaita *Coordinated and Integrated Community Health Workers' Programme*. Tutawasomesha kwa miezi sita, watachaguliwa na Serikali zao za vijiji, tutawapa vitendea kazi na tutawapa motisha ya kila mwezi. Hawa ndio watakuwa jeshi la afya, watakuwa ndiyo *Afya Commandos* katika ngazi ya jamii, ngazi ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutaanza na watumishi wa afya ngazi ya jamii 5,000. Tutakapotangaza kwenye vijiji vyenu tunaomba tusichomeke watoto, hakikisheni wasichomekwe watoto wa wakubwa. tunachukua *form four* kwa sababu *form four* wengi wamemaliza wako vijijini, wako mitaani hawana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ubora wa huduma, tumeona vifaatiba vipo, majengo yapo, dawa zipo, shida ni uongozi. Kwa hiyo tunaanzisha programu ya mabadiliko ya kiutendaji kwa wasimamizi na watoa huduma za afya *(Leadership for Health Transformation Programme)* ili kuwaongezea uwajibikaji, ufanisi na tija na mambo mengine tumeyaeleza, pamoja na miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema jambo moja; katika kuunga mkono huduma za matibabu ya kibingwa

na ubingwa bobezi, imempendeza Rais Samia, tumetenga kwenye bajeti yetu, Kamati yetu ya Bunge ni shahidi, shilingi bilioni tano haikuwepo, juzi tumepata shilingi bilioni tano, itagharamia huduma za ubingwa bobezi bure kwa Watanzania. Kwa hiyo, angalau tunaweza tukawatibu watoto wenye *sickle cell* 100 au tukasema *sickle cell* 20 mwaka huu, wanaotakiwa kupandikizwa figo 30, tutaweka na vigezo nani atapaswa kupata huduma hii. Tutaendeleza pia huduma za UKIMWI, *TB* na Malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa dawa tuna bilioni 205, tumezionesha pale. Kwenye dawa kubwa tumeona tuwasimamie kikamilifu wafamasia wa Mikoa na Halmashauri. Kwa mujibu wa Sheria ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za 2013, wanapaswa kuleta maoteo yao kabla ya tarehe 31, Januari ya kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za afya ya mama na mtoto, nimesema tutafanya kazi kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma. Tumewanyanyua madaktari, tunataka huduma zote hizi zitolewe pamoja na dawa. Pia tumetenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika hospitali zetu. Tumetenga Shilingi bilioni nane kwa ajili pia ya kununua vifaa tiba vya *MOI* pamoja na Muhimbili, *JKCI*, Bungando na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya ya akili, tumeliona hili jambo. Kubwa, hatuna wataalam. Kwa hiyo, tutahakikisha upatikanaji wa wataalam wa afya ya akili kwa kushirikiana na vyuo vikuu. Tumeongea na wenzetu wa Chuo Kikuuu cha *MUHAS,* mwaka huu wataanza Shahada ya Kwanza ya Sayansi ya Saikolijia tiba *(Clinical Psychology)*. Pia tumewaomba waanzishe *Bachelor of Science in Occupational Therapy, Bachelor of Science in Speech Therapy* na mambo mengine. Tumeona, sasa mpaka hawa wamalize, hatuwezi kukaa hivi hivi, kwa hiyo,

tutaanzisha kozi za muda mfupi za wataalam wa afya ya akili na huduma tengamao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutajikita kwenye huduma za utengamao kwa Watoto. Nimeshuhudia watoto wenye *autism* hawezi kuongea, hawezi kuvaa nguo, hawezi kupiga mswaki, hawezi kula chakula. Akipewa huduma za tiba za *physiotherapy,* akipewa huduma za *occupational therapy, speech therapy,* miaka miwili mitatu, mtoto anaweza akaanza kuvaa nguo mwenyewe, akapiga mswaki, akala chakula, akaonesha wapi anataka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nimeliona kama Waziri na kama mama. Asilimia 99 ya watoto wenye ulemavu wanalelewa na akina mama. Tumeona wanawake wenzetu wakiacha kazi zao nzuri, wakiacha biashara zao nzuri, wakiacha shughuli zao ili kulea watoto wenye ulemavu. Hatutawaacha, Rais Samia ni Rais wa huruma, ametuelekeza tulifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ni mengi. Tumesema magonjwa ya mlipuko, tumetenga shilingi bilioni 20 pamoja na kujenga kituo. Kaka yangu Mheshimiwa Mwijage, najua na Mheshimiwa Mushashu wamezungumza sana kule Kagera. Vile vile tumetenga shilingi bilioni 101 kwa ajili ya UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu. Pia tuna shilingi bilioni 22 kwa ajili ya huduma za dharura pamoja na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Kwa wataalam, tuna Shilingi bilioni 83.1 ambapo tutafanya pia mafunzo kwa wataalam wapya na kulipia mafunzo kwa watarajali *intense,* ambao ni madaktari, wauguzi, na wafamasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yangu yote iingie katika Hansard kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani kwanza, kwa ushirikiano tunaoupata kutoka nchi rafiki, mashirika ya

Kimataifa na sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za afya na ustawi wa jamii. Napenda kuzishukuru nchi za Canada, Denmark, Ireland, Uswisi, Korea Kusini na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ya Benki ya Dunia na *UNICEF*, kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja *(Health Basket Fund)*. Hawa kwa kweli ndio wadau wetu wakubwa. Fedha hizi za *basket fund* zinakwenda moja kwa moja mpaka kwenye zahanati, ndiyo zinatumika kulipia umeme, maji, kununua dawa na vifaa tiba. Waheshimiwa Wabunge tutawapa taarifa ya kila robo mwaka, kiasi gani kimekwenda ili mweze kuzisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunashukuru nchi nyingine zinazotusaidia ikiwemo China, Cuba, India, Italy, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na nchi nyingine. Sekta ya Afya inapata mchango mkubwa kutoka Shirika la Afya Duniani, Benki ya Dunia, *GAVI, Global Vaccine Alliance*, Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na *UKIMWI*, *PEPFAR*, Kituo cha Kutokomeza Magonjwa cha Marekani*, (USDC, USAID, DSID, Global Fund for HIV, TB na Malaria); Bill and Melinda Gates Foundation; Suzan Buffett Foundation* na wengine wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru watu binafsi, vyama vya kiraia pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali. Katika hotuba yangu nimeyataja mashirika yote yasiyo ya Kiserikali, yako mengi, lakini navishukuru Vyuo Vikuu vyote, kikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, *CUHAS, St. Augustine*, Dodoma kwa kutoa kozi mbalimbali za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Vyuo vyetu Vikuu ni kutoa kozi ambazo zinakidhi matarajio ya sasa ya sekta ya afya. Kwa hiyo, juzi tumekaa na *MUHAS,* Profesa Pembe na timu yake tutakubaliana kozi gani zinahitajika katika mazingira ya sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Godwin Mollel. Naibu Waziri wangu ananipa msaada mkubwa sana. Ni mwepesi sana kukimbia. Ukimwambia kuna tatizo kimbia, hata saa nane za usiku ataenda. Ni mtu msikilizaji, *very loyal, very committed* kwa Waziri wake. Kwenye hili kwa kweli namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nimepata Naibu Waziri *very loyal, very committed.* Nakushukuru sana Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Katibu Mkuu, Dkt. Seif Shekalaghe na Naibu Katibu Mkuu, Grace Maghembe, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanafanya katika kunisaidia, vile vile namshukuru Mganga Mkuu wa Serikali, Profesa Tumaini Nagu. Siyo kwamba napendelea wanawake, toka nimempata, Mheshimiwa Rais kuridhia maombi yangu ya kutupa Profesa Tumaini Nagu kuwa Mganga Mkuu wa Seikali, mambo ya kitaaluma Wizarani yanakwenda vizuri sana. Kwa kweli siyo kwamba namsifu kwa sababu ni mwanamke, lakini anafanya kazi kubwa na nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nawashukuru Wakuu wa Vitengo vya Wizara, nawashukuru Wakurugenzi wa Hospitali zetu za Taifa na Kanda nikianza na Profesa Mohamed Janabi wa Muhimbili. Waheshimiwa Wabunge nyie ni mashahidi, Muhimbili kulianza kulegalega. Janabi alikuwa anafanya vizuri sana *JKCI,* anapaswa kustaafu, tumeangalia Wizarani, nani wa kwenda kuinyoosha Muhimbili? Hatukumwona mtu zaidi ya Profesa Janabi. Sasa kazi zinakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam saa moja na nusu Madaktari Bingwa wako kwenye *clinic* zao; saa mbili kamili *clinic* zinaanza. Upasuaji Muhimbili unaweza ukapigwa

foleni mpaka wiki nane, wiki kumi na mbili; chini ya Janabi unaambiwa jamani leteni wagonjwa kumeisha huku. Kwa hiyo, ni suala la usimamizi na uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Dkt. Respicious Boniface wa Taasisi ya *MOI*, anafanya kazi nzuri pia. Mkisikia hiyo huduma ya kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu, ameianzisha yeye. Dkt. Kisengi wa Jakaya Kikwete tunakushukuru sana. Tunaamini utaendeleza mazuri ya Janabi, ulikuwa pale, kwa hiyo, sio mgeni, utafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Dkt. Julius Mwaisalage wa *Ocean Road,* anafanya kazi nzuri. Malalamiko ya *Ocean Road* yamepungua kwa kiasi kikubwa. Nawashukuru Dkt. Leonard Subi wa Hospitali ya Taifa Kibong'oto, anafanya kazi nzuri; Dkt. Paul S. Lawala wa Mirembe, naye ndio maana tunataka kuipandisha hadhi Mirembe isiwe hospitali, iwe ni taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia watu wa Nyanda za Juu Kusini nadhani ni mashahidi, Dkt. Mbwanji Mkurugenzi wetu wa Hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda anafanya kazi nzuri sana. Watu wa hapa, Wabunge, Dkt. Chandika wa Benjamin Mkapa, anafanya kazi nzuri. Kidogo kulilegalega, lakini amerudi, mambo yanakwenda vizuri. Dkt. Brian Mawala Chato, Fabiani Masanga, Profesa Masanga pia wa *KCMC* na Bugando tunawashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara; *MSD, NHIF, TMDA, NIMR*, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, *TFNC,* Mabaraza ya Kitaaluma; nawashukuru Wakuu wa Idara wote Wizarani, Waganga wakuu wa Mikoa na Wilaya, *Medical Officer In charge* wa Zahanati, Vituo vya Afya Wakuu wa Mafunzo, na Mashirika ya Dini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho niwashukuru Watanzania. Tukitoa maelekezo kuhusu afya wanayazingatia. Kwa hiyo, nawaomba sana Watanzania kujali na kulinda afya zao ikiwemo kwa kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa, kufanya mazoezi ya viungo mara kwa mara na kujiepusha na unywaji wa pombe kupita kiasi. Ni muhimu Watanzania wakatambua kwamba mtu ni afya, na afya ni mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kuishukuru sana familia yangu, kwa upendo wao mkubwa kwangu, kwa uvumilivu wao, kwa kunitia moyo na kuniombea dua mara kwa mara katika kutekeleza majukumu yangu. Kipekee ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Tanga Mjini kwa kuniheshimisha, kuniamini kuwa Mbunge wao. Nawaahidi kwamba, sambamba na majukumu ya kitaifa niliyonayo, nitaendelea kutekeleza wajibu wangu wa kuwatumikia, wa kuifanya Tanga yetu kuwa Jiji la mahaba, ukarimu na maendeleo zaidi. Nawapenda sana wakazi wa Tanga Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niombe fedha. Kwa kuwa naomba fedha, basi nipunguze *speed*. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 nimetaja vipaumbele 14. Katika vipaumbele hivi kwanza tunatarajia kukusanya shilingi 677,621,168,390.95. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 88,414,775,177.00 zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara. Shilingi 111,585,224,823.00 zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali, shilingi 477,621,168,390.95 zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika mashirika yaliyo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa matumizi ya kawaida, Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi 502,951,909,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 41 ya bajeti tengwa, ambapo kiasi cha shilingi 354,342,486,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na

Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha shilingi 148,609,423,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo, Wizara inakadiria kutumia shilingi 732,364,607,000.00 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 59 ya bajeti iliyotengwa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi 430,298,000,000.00 na fedha za nje ni shilingi 302,066,607,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya fedha zote zinazoombwa Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge lako Tukufu wanipitishie ili Wizara iweze kutekeleza vipaumbele tulivyovipanga ni shilingi 1,235,316,516,000.00. Kwa bajeti yetu, matumizi ya kawaida ni asilimia 41 na matumizi ya maendeleo ni asilimia 59.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu inapatikana katika tovuti za Wizara ya Afya lakini pia katika kishikwambi cha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua bajeti ya Wizara ya Afya, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya kwa

mwaka 2022/23 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/24. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida pamoja na miradi ya maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2023/24.

**2. Mheshimiwa Spika,** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kipekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Sekta ya Afya, sekta ambayo inayogusa maisha ya kila siku ya kila mtu, mwanawake au mwanaume, kijana au mzee, tajiri au masikini kwani Mtu ni Afya na Afya ni Mtaji. Ninatambua jukumu kubwa nililonalo mimi pamoja na Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel la kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema. Ninamuahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa nitaendelea kuifanya kazi hii kwa weledi, uaminifu na ubunifu mkubwa ili kuhakikisha watanzania wanapata huduma bora za Afya. Vilevile, nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kutupatia rasilimali fedha ili kuimarishaji utoaji wa huduma bora za afya nchini ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya afya katika Halmashauri na Mikoa yote nchini, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa Bobezi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa. Deni sasa limebaki kwetu Sekta ya Afya kwa kuhakikisha tunatoa huduma bora za afya kwa wananchi wetu kwa kuzingatia weledi, maadili na miiko ya kitaaluma ya watoa huduma za afya sambamba na kuzingatia kutoa huduma nzuri kwa mteja (good customer care), matumizi ya lugha ya staha na ya Faraja kwa wateja wetu. Tumuhakikishie

Mheshimiwa Rais, waheshimiwa wabunge na watanzania kuwa nasi hatutalala, tutatanya kazi usiku na mchana katika kupambana na adui maradhi ili kuhahakikisha wananchi wanapata huduma bora za kinga na tiba na kwa gharama nafuu.

3. **Mheshimiwa Spika,** ninapenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali inatimiza wajibu wake wa kuboresha huduma za afya nchini hususani kwa wananchi wa maeneo ya Vijijini. Nitumie fursa hii pia kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na maelekezo yake ya mara kwa mara ya kuhakikisha tunaimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya nchini kuanzia ngazi ya Msingi hadi Taifa. Aidha, ninampongeza kwa Hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 5 Aprili, 2023 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2023/24.

4. **Mheshimiwa Spika,** ninapenda kukupongeza wewe binafsi **Mheshimiwa Spika** kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa weledi, ubunifu na kwa uadilifu mkubwa, lakini pia kwa kuzingatia na kusimamia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge lako tukufu katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Aidha nampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu**, **Naibu Spika** na **Wenyeviti wa Bunge** kwa kazi nzuri ya kukusaidia kuliongoza Bunge letu pamoja na kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge. Tunapenda kukuhakikishia kuwa uongozi na watumishi wa Wizara ya Afya tutakeleza wajibu wetu wa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia Sheria na Kanuni mbalimbali zinazopitishwa na Bunge lako tukufu.

**5. Mheshimiwa Spika,** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao umeiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za afya. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha kuwa watanzania wana afya bora ili washiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo, kujenga uchumi wa viwanda, na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati.

**6. Mheshimiwa Spika,** kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na masuala ya UKIMWI, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki** na Makamu wake, **Mheshimiwa Dr. Faustine Ndugulile**, **Mbunge wa Kigamboni** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa katika kuboresha utendaji wa Wizara hususani katika kipindi cha maandalizi ya bajeti hii. Aidha, ninawashukuru waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wenu katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa wananchi. Kipekee ninawashukuru sana waheshimiwa wabunge kwa kujitihada binafsi mnazofanya ili kutatua chhangamoto za upatikanaji wa huduma za afya katika majimbo yenu ikiwemo kuchangia ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Wizara yangu itaendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zenu za kuwatumikia Wananchi ndani na nje ya Bunge.

**7. Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa pongezi kwa **Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa **Jimbo la Amani – Zanzibar**. Aidha, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa Familia na Wananchi wa Jimbo la Amani - Zanzibar kwa kifo cha

**Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani Zanzibar**.** Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wote, waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali.

**8. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee natoa pole kwa familia na jumuiya ya wataalam wa afya nchini kwa kupoteza wataalam mbalimbali wakati wakitimiza wajibu wao wa kuhudumia wananchi. MUNGU azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Pamoja na kupoteza baadhi ya wataalam wa afya wakati wa kutoa huduma, natoa pongezi na shukrani za pekee kwa wataalam wote wa afya nchini hususan waliokuwa mstari wa mbele kutoa huduma kwa wahisiwa na wagonjwa wa Marburg mkoani Kagera, kuhudumia wagonjwa mahututi na wagonjwa wengine kwa ujumla usiku na mchana bila kuchoka.

**9. Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/23, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2023/24.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2022/23

**10. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya (Health Sector Strategic Plan (HSSP V)) 2021/22 – 2025/26, pamoja na makubaliano

ya Kimataifa na kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

**11. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2022/23, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala wa Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano;

ii. Kusimamia viwango vya ubora wa huduma za kinga na tiba katika ngazi zote za utoaji huduma za afya nchini;

iii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, vifo vya watoto wachanga pamoja na mimba za utotoni;

iv. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya;

v. Kuimarisha huduma za lishe hususani kwa watoto wa umri wa chini ya miaka 5, vijana balehe na wanawake wa umri wa kuzaa;

vi. Kuimarisha huduma za afya na usafi wa mazingira ili kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na hivyo kupunguza idadi ya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini;

vii. Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa;

viii. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi;

ix. Kudhibiti magonjwa ya mlipuko, magonjwa ya kuambukiza na magonjwa yasiyo ya kuambukiza;

x. Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalamu katika Sekta ya Afya;

xi. Kuimarisha mifumo ya kugharamia huduma za afya nchini;

**xii.** Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za afya; na

**xiii.** Kuimarisha mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu katika utoaji wa huduma za afya nchini.

**MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA**

**12. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Fungu 52, ina jukumu la kusimamia upatikanaji na utoaji wa Huduma za Afya nchini. Wizara hukusanya mapato kutokana na huduma za tiba zitolewazo katika Hospitali zilizo chini yake, tozo na uchangiaji wa huduma katika Taasisi mbalimbali, ada za Vyuo na uuzaji wa zabuni.

**43. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 622,986,024,980.00** ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi **144,260,351,186.00** ni kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara (ikiwemo Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma), Shilingi **85,739,648,814.00** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na Shilingi **392,986,024,980.00** kutoka Hospitali za Kanda, Maalum, Taifa pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**13. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2023, Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekusanya jumla ya kiasi cha Shilingi **435,074,652,838.23** sawa na **asilimia 70** ya makadirio yote ya maduhuli ya Shilingi **622,986,024,980.00**. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi **44,715,733,505,** sawa na **asilimia 31** ya makadirio, kimekusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, kiasi cha Shilingi **73,185,916,466.87** sawa na **asilimia 85** kimekusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha Shilingi **317,173,002,867** sawa na **asilimia 81** kimekusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara, kama ilivyoanishwa katika **Kiambatisho Na. 1 hadi Na. 3.**

**14. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu kiasi cha **Shilingi 1,109,421,722,000.00** ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi **554,289,666,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **555,132,056,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya Shilingi **554,289,666,000.00** zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi cha Shilingi **222,723,260,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi **331,566,406,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara Makao Makuu, Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa.

**15. Mheshimiwa Spika,** kati ya kiasi cha Shilingi **555,132,056,000.00** zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Shilingi **410,298,000,000.00** ni fedha kutoka vyanzo vya ndani na Shilingi **144,834,056,000.00** ni fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo wanaochangia katika Sekta ya Afya.

**16. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Mwezi Machi, 2023, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha Shilingi **742,905,741,100.11** sawa na **asilimia 67** ya fedha zilizoidhinishwa (Shilingi **1,109,421,722,000.00**). Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi **458,486,800,216.86** sawa na **asilimia 83**

ya Shilingi **554,289,666,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **284,418,940,883.25** sawa na **asilimia 51** ya Shilingi **555,132,056,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**17. Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi cha **Shilingi 205,559,069,433.78** sawa na **asilimia 92** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 252,927,730,783.08** sawa na **asilimia 76** ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara makao Makuu, Hospitali ya Taifa, Hospitali maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa. Aidha, kati ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa **Miradi ya Maendeleo**, **Shilingi 266,493,496,368.12** sawa na **asilimia 65** ni kutoka vyanzo vya ndani na **Shilingi 17,925,444,515.13** sawa na **asilimia 12** kutoka vyanzo vya nje.

**18. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepokea kiasi cha **Shilingi 77,209,210,120.00** kwa ajili ya **utekelezaji wa miradi mbalimbali** kupitia mfumo wa D-Fund. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi **68,649,108,849.81** kutoka Mfuko wa Dunia "Global Fund", Shilingi **5,815,168,586.50** kutoka Susan Thompson Buffet Foundation, Shilingi **2,011,072,788.00** kutoka BADEA-COVID 19 Response grant na Shilingi **192,627,600.00** kutoka Global Alliance of Vaccine kwa ajili ya huduma za Chanjo.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA
## HUDUMA ZA KINGA

**20. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha huduma za kinga ikiwemo kuhakikisha **huduma za chanjo** na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana kulingana na mahitaji ya Mikoa yote nchini. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, wajawazito na wasichana wenye umri wa miaka 14

ambao ni walengwa wa huduma za chanjo wanapata huduma hizo kwa wakati. Aidha, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa chanjo na vifaa vya kutolea chanjo dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 vinapatikana.

**21. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha chanjo za watoto wadogo za kuwakinga na magonjwa ikiwemo Pepopunda, Kifaduro, Kupooza, Surua, Homa ya Uti wa Mgongo, Kifua Kikuu, Dondakoo, Nimonia, Homa ya Ini, Rubella na Kuharisha zinapatikana bure kulingana na mahitaji. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilinunua dozi 2,186,800 za IPV (Inactivated Polio Vaccine) kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa Kupooza kwa watoto; Chanjo ya Pentavalent dozi 1,763,500 kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya Kifaduro, Dondakoo, Kupooza, Homa ya Ini na Homa ya Uti wa Mgongo; Chanjo ya Pneumococal Conjugate Vaccine (PCV) dozi 4,290,800 kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya Homa ya Mapafu (Nimonia) na Homa ya Uti wa Mgongo; Chanjo ya Bivalent Oral Polio Vaccine (BOPV) dozi 7,263,000 kwa ajili ya kuzuia virusi mbalimbali vinavyosababisha ugonjwa wa Kupooza kwa watoto; Chanjo ya Rotarix (Rota) dozi 3,656,000 kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya kuhara kukali; Chanjo ya Surua na Rubella (MR) dozi 3,195,000 kwa ajili ya kukinga watoto na ugonjwa wa Surua na Rubella; Chanjo ya Bacillus Calmette Geurin (BCG) dozi 5,900,000 kwa ajili ya kuwakinga watoto wachanga na ugonjwa wa Kifua Kikuu; na Chanjo za kampeni ya Polio dozi 17,761,880. Chanjo hizi ni nyongeza ya dozi za chanjo ambazo zilikuwepo tayari katika maghala ya dawa, ambazo zilikuwa ni IPV dozi 2,186,800; Pentavalent dozi 1,763,500; PCV dozi 1,376,000; bOPV dozi 7,263,000; Rota dozi 3,576,000; MR dozi 1,960,000; BCG dozi 3,978,980; na HPV dozi 1,084,540. Chanjo zote zilizoagizwa zilipokelewa na kusambazwa kwenye mikoa yote kulingana na idadi ya walengwa na uhitaji.

**22. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha wa kuanzia Julai 2022 mpaka Machi 2023, Wizara ilikuwa na lengo la kuchanja jumla ya watoto 1,618,737. Hadi kufikia mwezi Machi 2023 jumla ya **watoto 1,596,951** sawa na **asilimia 98.6** walikuwa wamechanjwa chanjo ya Penta3 ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha chanjo. Hili ni ongezeko la asilimia 4 ukilinganisha na uchanjaji wa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, uchanjaji wa chanjo ya Surua na Rubella dozi ya kwanza ulifikia asilimia 98.1 ikilinganishwa na asilimia 95 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22; Surua na Rubella dozi ya pili ilifikia asilimia 96.7 ikilinganishwa na asilimia 84 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22; huduma za chanjo ya kuwakinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Polio, kwa kutumia chanjo ya matone (OPV3) ulifikia asilimia 99.2 ikilinganishwa na asilimia 98 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22, uchanjaji kwa kutumia sindano (IPV) ulifikia asilimia 100 ikilinganishwa na asilimia 98 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Juhudi hizi zinalenga kuhakikisha kuwa tunazuia ugonjwa wa Polio hapa nchini.

**23. Mheshimiwa Spika,** pamoja na utekelezaji wa utoaji wa chanjo kulingana na miongozo, Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya afya, imetekeleza kampeni mbalimbali za utoaji wa chanjo kwa watoto. Kampeni hizo ni; **kampeni za kudhibiti Polio** na **kampeni ya chanjo ya Surua.** Kwa upande wa chanjo ya Polio, awamu ya kwanza ilifanyika katika mikoa minne inayopakana na nchi ya Malawi ambayo ni Mbeya, Njombe, Ruvuma na Songwe ambapo ililenga kuwafikia watoto 975,839. Katika awamu hiyo watoto 1,130,261 walifikiwa sawa na asilimia 115.8. Awamu ya pili ilifanyika katika mikoa yote nchini ikilenga kuwafikia watoto 10,576,805 ambapo watoto 12,436,361 sawa na asilimia 117.58 walifikiwa. Awamu ya tatu ililenga kuwafikia watoto 12,692,166 ambapo watoto 15,052,442 sawa na asilimia 118.6 walifikiwa, na awamu ya nne ililenga kuwafikia watoto 15,052,442 ambapo watoto 17,816,933

sawa na asilimia 118.8 walifikiwa. Wizara iliweza kuvuka lengo la kufikia watoto kutokana na mwitikio chanya wa Jamii kupeleka watoto katika vituo kupata huduma za chanjo.

**24. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kukabiliana na ugonjwa wa Surua, tathmini ya kiwango cha uchanjaji wa chanjo ya Surua hapa nchini kwa kipindi cha miaka mitatu ilifanyika. Matokeo ya tathmini hiyo yalionyesha kuwa Watoto **541,153** wenye umri wa chini ya miaka 5 hawakupata kabisa chanjo ya MR kwa kipindi cha mwaka 2019-2023 na Watoto **1,430,871** wenye umri wa chini ya miaka 5 hawakukamilisha ratiba ya chanjo ya MR kwa kipindi cha mwaka 2019-2023, hali ambayo imesababisha uwepo wa mlipuko wa Surua katika halmashauri 49 kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi April,2023. Katika kukabiliana na hili, Wizara kwa kushirikiana na ORTAMISEMI na Wadau iliendesha **kampeni ya nyumba kwa nyumba ya chanjo ya Surua,** katika maeneo yote ambayo yaliyobainika kuwa yana watoto wengi ambao bado hawajapata chanjo ya Surua kwa ukamilifu. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuwapatia watoto huduma ya chanjo kwa wakati na kwa kuzingatia ratiba ya chanjo. Kutokana na jitihada hizi mlipuko wa Surua umeweza kudhibitiwa na hadi kufikia mwezi Aprili 2023 Halmashauri zenye mlipuko wa Surua zimepungua hadi kufikia saba.

**25. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuwalinda wasichana wenye umri wa miaka 14 dhidi ya Saratani ya mlango wa kizazi kwa kununua na kusambaza chanjo ya Human Papilloma Virusi (HPV) dozi **763,500.** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, **Wasichana 535,708** wenye umri wa miaka 14 ambao ni walengwa wa huduma za **chanjo ya kuzuia Saratani ya mlango wa kizazi** walipatiwa chanjo.

**26. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu upatikanaji wa **chanjo dhidi ya UVIKO-19** kupitia mpango wa kidunia kuhakikisha nchi zinapata chanjo ya UVIKO-19 (COVAX facility) na misaada kutoka nchi rafiki. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 jumla ya dozi 46,848,520 zilikuwa zimepokelewa na kusambazwa ambapo dozi 39,187,358 (sawa na asilimia 84) zimetumika hadi sasa. Wizara inaendelea kuratibu utoaji wa chanjo ya UVIKO -19 kupitia vituo vya kutolea huduma za Afya vya umma na binafsi, huduma za mkoba na kampeni. Jumla ya vituo vya kutolea huduma 7,200 vinatoa huduma ya chanjo ya UVIKO-19 hapa nchini. Hadi kufikia mwezi Machi 2023 jumla ya watu 32,735,546 ambao ni sawa na asilimia 53.4 ya watanzania wote walikuwa wamekamilisha chanjo dhidi ya ugonjwa huu. Chanjo hii imeweza kujenga kinga kwenye jamii hivyo kupunguza hatari ya kuugua ugonjwa huu na hata waliougua kutopata madhara makubwa. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, kumekuwa na wastani wa visa 302 kwa mwezi bila kifo ikilinganishwa na kipindi kama hiki 2021/22 ambapo kulikuwa na wastani wa visa 1,557 na vifo 43 kwa mwezi.

**Huduma za Lishe**

**27. Mheshimiwa Spika,** Lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo huchangia katika kuongeza tija katika uzalishaji mali kwa kaya na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara ya Afya imekuwa ikitekeleza Mpango Jumuishi wa pili wa Kitaifa wa Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan 2021/22 – 2025/26). Kupitia Mpango huo Wizara imekuwa ikitekeleza afua za lishe zilizothibitishwa kuwa na matokeo makubwa ili kukabiliana na matatizo ya utapiamlo wa lishe duni na lishe ya kuzidi.

**28. Mheshimiwa Spika,** afua zinazotekelezwa na Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI ni pamoja na; utoaji wa matone ya vitamin A na dawa za kutibu minyoo ya tumbo,

matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto, utoaji wa vidonge vya madini chuma na Folic Acid kwa wajawazito, uongezwaji wa virutubishi vya madini na vitamini kwenye vyakula vinavyoliwa kwa wingi na wananchi ikiwemo unga wa ngano, unga wa mahindi, chumvi, mafuta ya kula na elimu kuhusu lishe na ulaji bora.

**29.** katika kuhakikisha afua za lishe zinatekelezwa na kusimamiwa vizuri katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata na Vijiji, kwa mara nyingine **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **ametia saini Mikataba ya Lishe na Wakuu wa Mikoa** yote Tanzania Bara tarehe 30 Septemba, 2022. Utekelezaji wa mikataba hiyo hupimwa kwa kuangalia viashiria 15 vinavyopima ufanisi wa mkoa husika. Hadi tarehe 30 Novemba, 2022, Mikoa yote ilikuwa imeshakamilisha utiaji saini baina ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wa Kata, Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji.

**30. Mheshimiwa Spika,** tathmini ya utekelezaji wa viashiria hivyo hufanyika kwenye ngazi ya Taifa mara moja kwa mwaka na inategemewa kufanyika mwezi Agosti 2023. Katika ngazi ya Mikoa hufanyika mara mbili kwa mwaka, na kila robo mwaka katika ngazi ya Halmashauri. Tathmini ya utekelezaji ngazi ya Mkoa imefanyika tarehe 30/01/2023 na matokeo yanaonyesha katika kiashiria cha kutenga Shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya utekelezaji wa afua lishe kwa watoto, wajawazito na akina mama wanaonyonyesha, mikoa imetenga fedha, lakini bado kuna changamoto katika kutolewa fedha hizo. Mikoa ambayo ipo nyuma zaidi ni Rukwa asilimia **24.51**, Manyara asilimia **34.23** na Simiyu asilimia **34.26,** ingawa kitaifa kiashiria hiki kimefanikiwa kwa asilimia **63.05**. Viashiria vingine **14** vimefanikiwa kwa kati ya asilimia **70 – 100**.

**31.** katika kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto, Wizara imeendelea kuimarisha afya na lishe ya watoto chini ya miaka 5 kwa kuendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya **utoaji wa matone ya Vitamini A kwa watoto walio chini ya miaka mitano.** Jumla ya **watoto 9,456,436** walipatiwa matone ya vitamin A ambayo ni sawa na **asilimia 99** ya lengo la kutoa matone ya Vitamin A kwa **watoto 9,460,369** wenye umri wa kati ya miezi 6 mpaka 59 nchi nzima. Kiwango cha utekelezaji kimeongezeka ikilinganishwa na asilimia 97.2 iliyofikiwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

**32. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhamasisha wazalishaji wa vyakula **kuongeza virutubishi kwenye vyakula** vinavyoliwa kwa wingi nchini, ambapo virutubishi vya madini na vitamini (Iron, Folic Acid, Zinc, Vitamin B12, Iodine na Vitamin A) huongezwa kwenye unga wa ngano, unga wa mahindi, chumvi na mafuta ya kula. Katika kipindi cha Julai 2022 - Machi, 2023 jumla ya mashine **116** za kunyunyizia virutubishi (dosifiers) kwenye vyakula zimefungwa katika mikoa yote nchini na hivyo kufikia jumla ya mashine **837** ukilinganisha na mashine **721** zilizokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Lengo ni kufikia mashine 1000 kwa mwaka huu wa fedha. Pia katika kipindi hicho kiasi cha tani **105,617** za unga wa mahindi ziliongezwa virutubishi ikilinganishwa na tani **81,185** zilizoongezewa virutubishi mwaka 2021/22.

**33.** Wizara imeendelea kuboresha **huduma za matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto** kwa kuimarisha upatikanaji wa chakula dawa, kutengeneza mazingira wezeshi ya upatikanaji wa vifaa vya kufanyia tathmini ya hali ya lishe, pamoja na kuwajengea uwezo wataalam. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imewajengea uwezo watumishi **180** kuhusu matibabu ya utapiamlo mkali katika Mikoa ya **Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Mara, Manyara, Dodoma, Mtwara na Katavi**. Katika kufanikisha

upatikanaji wa chakula dawa kwa ajili ya matibabu ya utapiamlo mkali nchini na pia kupunguza gharama za uagizaji wa chakula dawa nje ya nchi, Wizara imeanza utaratibu wa kuhamasisha Viwanda vya ndani kuanza utengenezaji wa maziwa (F75 na F100) na chakula dawa (Plumpynuts) ikiwemo kutoa mwongozo wa utaratibu na viwango vya kuzingatia. Aidha, Wizara ilifanya kikao na wazalishaji wa maziwa kwa kushirikiana na Bodi ya maziwa Tanzania na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa lengo la kupanga namna ya kuanza uzalishaji mwaka 2023/24.

**34. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wananchi wanaelewa umuhimu wa kula lishe bora na mtindo bora wa maisha, Wizara imeendelea **kuelimisha** na **kuhamasisha jamii** kupitia njia mbalimbali ikiwemo Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji inayofanyika kila robo mwaka kwenye vijiji na mitaa na pia kwa kupitia katika majukwaa na mitandao ya kijamii ambapo jumla ya vipindi vya redio na runinga **93** vya masuala ya lishe vilirushwa, Makala **18** zilirushwa kwenye magazeti, na jumbe za lishe **123** kwenye mitandao ya kijamii (social media). Jumla ya waandishi wa habari **60** walijengewa uwezo katika masuala ya lishe kupitia semina maalumu ya wanahabari.

**35. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifanya uzinduzi wa **mwongozo** wa **Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji/Mtaa** tarehe 29 Oktoba, 2022 katika Kijiji cha Mikese Mkoani Morogoro na kuwajengea uwezo Wakufunzi **78** ngazi ya Mikoa na Wakufunzi **306** ngazi ya Halmashauri namna ya kutekeleza Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji. Aidha, utekelezaji wa Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji/Mtaa unaendelea kufanyika kila robo mwaka ambapo hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya vijiji na mitaa **14,750** sawa na asilimia **88.6** ya vijiji na mitaa **16,648** vimetekeleza zoezi hili.

**Usafi na Afya Mazingira**

**36. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya inatambua kuwa usafi na afya mazingira ni nguzo muhimu katika ustawi wa afya ya jamii. Magonjwa mengi haswa yale yanayoambukiza na yasiyoambukiza yanaweza kuepukika kwa kula chakula ambacho ni salama, kutumia maji safi na salama, lakini pia kwa kuhakikisha mazingira yanayotuzunguka ni salama na safi ili yasiwe mazalia ya wadudu wanaoweza kusababisha magonjwa kwa jamii.

**37. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara imeratibu utekelezaji wa mradi wa **Huduma Endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira** Vijijini katika Sekta ya Afya (Sustainable Rural Water Supply and Sanitation - SRWSS) kwenye Halmashauri za Wilaya 86 zilizopo kwenye Mikoa 17 ya Ruvuma, Lindi, Mtwara, Manyara, Mara, Simiyu, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Kigoma, Tabora, Singida, Iringa, Songwe, Rukwa na Katavi, ambapo jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 370 vinaendelea na maboresho ya miundombinu ya maji safi, vyoo, bafu, vifaa vya kunawia mikono, viteketezi taka (incinerators) na maboresho ya vyumba vya kujifungulia akina mama wajawazito. Tangu kuanza kwa mradi huu mwaka 2019/20 hadi sasa jumla ya Vituo 1,904 vimefikiwa sawa na asilimia 72.2 ya lengo la mradi ambapo vituo 2,636 vimekusudiwa ifikapo Juni, 2025. Kutokana na mafanikio ya mradi huu, Serikali imeongeza wigo wa utekelezaji ambapo katika mwaka huu wa fedha zimeongezwa Halmashauri 51 na kufanya Halmashauri zinazotekeleza mradi huu kufikia Halmashauri za Wilaya 137 nchini.

**38. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza afua za **kudhibiti magonjwa yatokanayo na kinyesi** kwa kuratibu shughuli za uhamasishaji wa ujenzi na matumizi ya vyoo bora pamoja na vifaa vya kunawia mikono ngazi ya kaya ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023

kaya zenye vyoo bora zimeongezeka kutoka kaya 7,192, 981 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 hadi 7,236,188 ikiwa ni ongezeko la kaya 43, 157 sawa asilimia 73.2 ya kaya zenye vyoo bora nchini. Lengo ni kufikia asilimia 75% ifikapo mwaka 2025. Aidha, kaya zenye vifaa vya kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni zimeongezeka kutoka asilimia 41.4 mwaka 2021/22 hadi asilimia 42.7 katika kipindi hiki cha Julai 2022 hadi Machi 2023.

**39. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na ORTAMISEMI imekuwa ikiratibu shughuli za kuimarisha ubora wa huduma za afya mazingira ili kudhibiti mazalia ya vimelea vya magonjwa na kuzingatia kanuni za afya. Katika kipindi hiki jumla ya kaya 1,663,540, masoko 8,465, migahawa 72,757, viwanda 6,985, nyumba za ibada 47,134, Ofisi za umma 38,117, nyumba za kulala wageni 256,927 zilikaguliwa. Katika maeneo haya yaliyokaguliwa ilani za marekebisho 95,754 zilitolewa. Lengo la kaguzi hizi ni kuhakikisha wahusika kwenye makazi na maeneo ya kutolea huduma za kijamii wanafuata kanuni za afya ili kuikinga jamii dhidi ya maradhi.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara iliweza kutekeleza huduma mbalimbali za jamii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha **udhibiti salama wa taka zitokanazo na huduma za afya** ambapo jumla ya Hospitali za Mikoa 26 na Kanda 5 zilizalisha taka zaidi ya tani 44.8 ambapo asilimia 80 ya taka hizi ziliweza kuteketezwa kwa kutumia viteketezi taka (Incinerators) zilizopo ndani ya Hospitali. Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa viteketezi taka ambapo jumla ya viteketezi vipya katika Hospitali 8 za Mikoa, Hospitali 15 za Wilaya, Vituo vya afya 25 na Zahanati 10 vilijengwa na hivyo kuongeza asilimia ya uwepo wa viteketezi taka ikilinganishwa na ile ya mwaka 2021 kutoka asilimia 75 hadi 85 kwa Hospitali za Mikoa, asilimia 38 hadi 40 kwa Hospitali za Wilaya, na asilimia 34

hadi 37 kwa vituo vya Afya na Zahanati. Aidha, kutokana na baadhi ya Hospitali za Mikoa na Wilaya kutokuwa na viteketezi taka, Wizara imeendelea kuchukua hatua na kupata fedha kwa ajili ya viteketezi taka 298 ambavyo vitapelekwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Wilaya zenye changamoto hiyo.

**Huduma za Afya Mipakani (Port Health Service)**

**41. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kudhibiti kuingia kwa magonjwa yanayoambukiza kupitia maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu kwa kufanya uchunguzi wa afya kwa wasafiri wanaotoka katika nchi zenye maambukizi ya magonjwa hayo ikiwemo Ebola, Homa ya Manjano na UVIKO-19. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wasafiri 8,189,248 walikaguliwa ambapo 1,902,837 sawa na asilimia 23.2 ni wasafiri wa nje (International travelers) na 6,286,411 sawa na asilimia 76.8 ni wasafiri wa ndani (domestic travelers). Kati ya wasafiri walioingia nchini, wasafiri 35,604 walichunguzwa uwepo wa maambukizi ya UVIKO 19 kwa kutumia kipimo cha haraka (rapid antigen test) na kati yao, 106 sawa na asilimia 0.29 walibainika kuwa na maambukizi na walishauriwa kujitenga katika maeneo waliyofikia ili kuzuia kueneza kwa ugonjwa huo. Aidha, katika kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Manjano, wasafiri 4,889,591 walikaguliwa kama wamepata chanjo dhidi ya ugonjwa wa homa ya manjano na wasafiri 10,583 walichanjwa chanjo ya ugonjwa huo.

**42. Mheshimiwa Spika;** Wizara iliendelea kuchukua **tahadhari ya Ugonjwa wa Ebola** tangu mlipuko wa Ebola uliporipotiwa nchini Uganda tarehe 20 Septemba 2022, ambapo jumla ya wasafiri **19,561** waliotoka nchini Uganda walichunguzwa afya zao na hakuna msafiri aliyebainika kuwa na ugonjwa wa Ebola. Wizara ilifanya mikutano ya ujirani mwema na nchi ya Uganda, kusambaza vifaa kinga,

dawa na kuweka miundombinu ya tahadhari ya tishio la kuingia kwa ugonjwa wa Ebola nchini. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo kwa Maafisa Afya 336 kutoka katika ofisi za afya mipakani na katika Mkoa wa Kagera kuhusu udhibiti wa maambukizi, ufuatiliaji wa afya za wasafiri, usibuaji (Decontamination) na maziko salama (safe and dignified burial) endapo kungetokea kifo kutokana na ugonjwa wa Ebola. Aidha, katika kuongeza uwezo wa uchunguzi na uwasilishaji wa taarifa kwa wakati Wizara ilisambaza vitendea kazi katika ofisi za Afya mipakani, ambapo ofisi 42 zilipatiwa Laptops 40, Vishikwambi 80, printers 35 pamoja na vifaa 14 vya kisasa vya kupimia joto la mwili (thermoscanners). Pia vifaa vya kudumu vya kunawia mikono (Mass Hand Washing Facilities) vimejengwa katika mipaka ya Tunduma na Kasumulu ili kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza katika maeneo ya mipakani.

**Ufuatiliaji na Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko (Disease Survaillance)**

**44. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa ya mlipuko kwa kuanzisha mfumo wa Kielektroniki wa utoaji wa taarifa za tetesi zinazoweza kuwa na athari za kiafya kabla ya kuleta madhara kwenye jamii (Electronic Event Based Survaillance - eEBS). Tetesi hizi zinatoka katika ngazi ya jamii, vituo vya kutolea huduma za afya, mipakani pamoja na mitandao ya kijamii. Tetesi zinazotolewa huingizwa kwenye mfumo na kupokelewa ngazi ya Taifa mara moja kwa ajili ya kuchujwa na kuhakikiwa. Ngazi ya wilaya na mikoa wanaweza kuona tetesi hizo kulingana na mahali tetesi ilipotoka. Vile vile, mwananchi yeyote anaweza kutoa taarifa za tetesi kwa kutuma ujumbe kwenda namba 199 bila malipo kwa kuanza na neno TETESI- Jina la Wilaya - Ujumbe. Tetesi hizi pia huingia katika mfumo wa eEBS.

**45. Mheshimiwa Spika,** Mpaka sasa jumla ya tetesi **5,151** tayari zimetolewa taarifa kupitia mfumo huu na kuchunguzwa ambapo kati ya hizo, magonjwa ya mlipuko kama vile **Kipindupindu, Surua, na Kimeta** yaliweza kubainika. Kupitia mfumo huu Wizara imeweza kuongeza utambuzi wa magonjwa ya milipuko mapema na kuweka mikakati ya haraka ya udhibiti. Sambamba na hilo Wizara imeanzisha dawati la kuchakata tetesi lenye lengo la kufatilia tetesi zote zinazopokelewa na kuzitolea taarifa kwa ufuatiliaji. Aidha, jumla ya watoa huduma wa vituo vya kutolea huduma **1,301**, wahudumu wa afya ngazi ya jamii (CHWs) **1,325** na wenyeviti wa vijiji **480** wamejengewa uwezo na wanatoa taarifa za tetesi kwa kutumia mfumo huo.

**Kudhibiti Magonjwa yaliyokuwa hayapewi Kipaumbele (NTDs)**

**45. Mheshimiwa Spika,** Wizara imetoa kipaumbele cha kudhibiti na kutokomeza magonjwa matano yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ambayo ni Matende na Mabusha,Trakoma, Usubi, Kichocho na Minyoo ya Tumbo. Shughuli za udhibiti wa magonjwa haya zimegawanyika katika maeneo makuu matatu ambayo ni shughuli za kinga kwa ugawaji wa kingatiba kwa magonjwa yote matano, shughuli za tiba kwa kufanya upasuaji wa mabusha na usawazishaji wa vikope na shughuli za utengamao kwa kutoa matunzo ya wagonjwa wa matende.

**46. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023. Wizara iliendelea kufanya zoezi la umezeshaji kingatiba dhidi ya ugonjwa wa matende na mabusha, kichocho, minyoo ya tumbo na usubi. Katika kipindi hiki Wizara iligawa dawa kinga za Ivermectine na Albendazole katika Halmashauri tisa **(9)** zenye maambukizi ya juu zenye kuhitaji kingatiba kati ya Halmashauri **119** zilizokutwa na kiwango cha juu cha maambukizi mwaka 2008

(halmashauri 110 tayari zimefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo). Halmashauri hizo ni Mafia, Pangani, Kilwa, Lindi MC, Lindi DC, Mtwara – Mikindani, Temeke, Jiji la Dar es Salaam na Kinondoni. Lengo ilikuwa ni kuwafikia walengwa **6,314,482.** Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya walengwa **4,339,013** sawa na asilimia **69** ya lengo walimezeshwa kingatiba.

**47. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliweza kutoa dawa kinga ya Praziquantel ya kudhibiti **ugonjwa wa Kichocho** katika Halmashauri **134** kati ya Halmashauri **179** zilizotarajiwa kupata huduma hii katika kipindi hiki. Halmashauri hizo zinatoka katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Iringa, Katavi, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora na Tanga, ambapo walengwa (Watoto wenye umri wa kwenda shule miaka 5 - 14) walikuwa **3,973,550** na waliomezeshwa kingatiba ni watoto **3,447,752** sawa na **asilimia 75** ya lengo.

**48. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeweza kutoa dawa kinga ya albendazole ya kudhibiti **ugonjwa wa Minyoo ya tumbo** kwa Halmashauri **137** kati ya **183** zilizotarajiwa kupata huduma hii katika kipindi hiki. Halmashauri zilizopata huduma hiyo ni kutoka katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Geita, Iringa, Katavi, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora na Tanga, ambapo walengwa (Watoto wenye umri wa kwenda shule miaka 5 - 14) walikuwa **8,098,082** na waliomezeshwa dawa ni **7,039,974** sawa na **asilimia 75** ya lengo.

**49. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifanya zoezi la umezeshaji wa dawa kinga ya Ivermectin ya kudhibiti **ugonjwa wa Usubi** katika Halmashauri 15 zilizokuwa zimelengwa katika kipindi hiki kati ya halmashauri 29 zenye kiwango cha juu cha maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa

usubi.Halmashauri hizo ni Mufindi DC, Njombe DC, Gairo DC, Kilosa DC, Morogoro DC, Mvomero DC, Ludewa DC, Madaba DC, Mbinga DC, Mbinga TC, Namtumbo DC, Nyasa DC, Songea DC, Songea MC na Tunduru DC. Idadi ya walengwa katika Halmashauri hizo walikuwa ni **3,763,834** na waliomezeshwa kingatiba walikuwa ni **3,194,245** ambao ni sawa na asilimia **84.9** ya lengo.

**50. Mheshimiwa Spika;**. Katika Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara iliendelea kutoa huduma za tiba kwa kufanya **upasuaji wa mabusha na usawazishaji wa vikope.** Huduma za upasuaji wa mabusha zilitolewa kwa njia ya kambi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi ambapo jumla ya wagonjwa **212** walipata huduma hiyo, na jumla ya wagonjwa **25** walipata huduma katika vituo vingine vilivyojengewa uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa mabusha.

**51. Mheshimiwa Spika,** Katika kusogeza huduma kwa **wagonjwa wa Matende na Mabusha**, Wizara imewajengea uwezo watumishi wa afya **69** jinsi ya kutoa huduma na matibabu ya Matende na Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii **93** ili kuibua wagonjwa wa Mabusha katika Halmashauri ya Mtama iliyoko mkoani Lindi. Aidha, hadi kufikia Machi, 2023 wataalam hao wameweza kubaini wagonjwa **2,202** na kati ya hao **704** ni walioathirika na Matende na **1,498** walioathirika na Mabusha. Wizara inaendelea kutoa huduma ya upasuaji wa mabusha na kutoa elimu ya jinsi ya kusafisha na kujihudumia viungo vilivyoathirika na Matende.

**52. Mheshimiwa Spika,** Wizara ililenga kufanya **usawazishaji wa Vikope kwa wagonjwa 1,967** waliopangwa katika kipindi hicho kati ya wagonjwa wa vikope **12,774** nchini kutoka Halmashauri za Wilaya za Mbarali (Mbeya), Iringa (Iringa DC), Songwe (Songwe DC), Wanging'ombe na Makete (Njombe), Karatu, Longido na Monduli (Arusha),

Mpwapwa, Chamwino na Bahi (Dodoma), Nkasi (Rukwa), Magu (Mwanza), Kyerwa (Kagera), Babati, Mbulu, Kiteto na Simanjiro (Manyara). Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya wagonjwa **2,106** walifanyiwa usawazishaji wa vikope ikiwa ni asilimi ya lengo.

**Elimu ya Afya kwa Umma**

**53. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa Elimu ya Afya kwa Umma ili kuelimisha na kuhamasisha jamii masuala mbalimbali ya afya hususani kujikinga dhidi ya magonjwa. Mbinu mbalimbali zilitumika ikiwemo radio, TV, mitandao ya kijamii, majarida, midahalo na vipeperushi. Vilevile, Wizara imeanzisha Dawati la Uratibu ndani ya Idara ya Kinga linalosimamia Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (Community Health Workers) ambao jukumu lao kubwa ni kutoa Elimu na taaarifa za masuala mbalimbali ya afya katika ngazi ya msingi. Katika kipindi hiki jumla ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii wapatao 5,760 wametambuliwa, kupatiwa mafunzo ya angalau wiki mbili na wanatumika katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Kati yao, wahudumu 1,322 wamejengewa uwezo, kupewa vitendea kazi na kuajiriwa ili kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kukabiliana na ugonjwa wa Marburg mkoani Kagera katika Halmashauri za Bukoba DC na Bukoba MC kwenye Mitaa 66, vijiji 94 na Vitongoji vyote 515 katika Halmashauri hizi mbili (2).

**54. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma za afya ngazi ya jamii, Wizara imeandaa **Mpango wa Uzalishaji, Uratibu na kuwatumia Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii katika utekelezaji wa Afua Jumuishi ngazi ya jamii nchini** (Integrated and Coordinated Community Health Workers Program). Wizara itashirikiana na Wadau mbalimbali katika kuwasajili Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (Community Health Workers) kutoka katika maeneo yao wanayoishi,

kuwapatia mafunzo maalum kupitia Vyuo vya Afya vya Kada ya Kati, kuwapatia vitendea kazi na hatimaye kuwaajiri. Afua zitakazotekelezwa zinahusu masuala mbalimbali ya afya ikiwa ni pamoja na Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto; Lishe; Afya na Usafi wa Mazingira; Magonjwa ya Kuambukiza (mfano Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI); Magonjwa Yasiyoambukiza na Magonjwa ya Mlipuko. Vilevile, Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii chini ya utaratibu mpya watachanguliwa na Serikali za Vijiji/Mitaa yao, watapewa mafunzo na vyeti ili kutambuliwa rasmi na kufanya kazi kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO**

**55. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ili kupunguza au kumaliza kabisa vifo vinavyozuilika vinavyotokana na uzazi. Huduma zilizoimarishwa ni pamoja na huduma kabla ya kujifungua, wakati wa kujifungua, baada ya kujifungua, na huduma kwa watoto, afya ya uzazi kwa vijana wa rika balehe na huduma dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia. Katika kuimarisha usimamizi wa huduma hizo mwezi Julai, 2022 Serikali iliamua **kuanzisha Idara ya Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto**. Hatua hii itasaidia kuimarisha uongozi, usimamizi, uwajibikaji na msukumo chanya wa matumizi ya rasilimali mbalimbali katika kuboresha huduma za afya ya uzazi, mama, mtoto na vijana wa rika balehe ili kufikia lengo endelevu la tatu la dunia la 2030 la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto.

**56. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma kabla ya kujifungua** ambapo, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Serikali ilinunua na kusambaza vidonge vya uzazi wa mpango 2,538,247 sawa na asilimia 89 ya lengo, sindano za uzazi wa mpango aina ya Depo-

provera dozi 2,564,691 sawa na asilimia 94 ya lengo na vipandikizi 552,494 sawa na asilimia 81 ya lengo. Aidha, katika kipindi cha taarifa hii jumla ya wateja 4,509,605 walitumia njia mbalimbali za kisasa za uzazi wa mpango ikilinganishwa na wateja 4,905,854 kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Huduma mkoba za uzazi wa mpango zinaendelea kutolewa sehemu mbalimbali nchini ambapo asilimia 18 ya wateja wa njia za uzazi wa mpango walipata huduma kupitia njia hii (outreach services)

**57. Mheshimiwa Spika,** takwimu za Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA) zinaonyesha kuwa njia za uzazi wa mpango ambazo zilitumika katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ni pamoja na vipandikizi (asilimia 45.7); Sindano (asilimia 22.8); vidonge (asilimia 12.6); kondomu (asilimia 11.6), vitanzi (asilimia 5.9); kufunga kizazi (asilimia 0.6); na njia nyingine (asilimia 0.9). Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya wateja wapya 3,491,989 sawa na asilimia 60.7 ya wanawake walio wa umri wa kupata ujauzito waliotumia njia za kisasa za uzazi wa mpango ikilinganishwa na wateja 3,049,011 sawa na asilimia 62.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, mikoa iliyoongoza kwa kuwa na asilimia kubwa ya wateja wapya wanaotumia njia za uzazi wa mpango kati ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 ni Katavi (asilimia 38.2), Kigoma (asilimia 38.2), Kilimanjaro (asilimia 31.1), Mara (asilimia 29.9) na Iringa (asilimia 28.8). Katika kipindi hicho, jumla ya **wanawake 570,211 walipatiwa huduma za uzazi wa mpango mara baada ya kujifungua** ikiwa ni asilimia 42 ya akinamama wote waliojifungua katika kipindi hicho.

**58. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza mikakati ya kupunguza vifo vya wakinamama wajawazito. Katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti iliyopita vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 943 ukilinganisha na vifo 982 katika kipindi kama hicho mwaka wa 2021/22 hii ni sawa na kupungua kwa asilimia 4 ya vifo hivi. Mikakati hii ni pamoja

na kuimarisha miundo mbinu ya kutolea huduma, kusogeza upatikanaji wa **huduma za afya wakati wa ujauzito** kwa kuhakikisha wajawazito wanawahi kliniki ili kupatiwa huduma stahiki kwa wakati, kuhakikisha uwepo wa dawa muhimu kwa wajawazito pamoja na upatikanaji damu salama kwa akina mama wanaohitaji kuongezewa damu, kutoa mafunzo kazini kwa mwisho kushirikiana na vyama vya kitaaluma.

**59.** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa **huduma za afya wakati wa ujauzito** kwa kuhakikisha elimu inatolewa kuanzia ngazi ya jamii kuhusiana na umuhimu wa mama mjamzito kuhudhuria kliniki kama inavyoainishwa katika Mwongozo wa Huduma za Kliniki kwa Wajawazito wa Mwaka 2018. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, takwimu za MTUHA zinaonyesha kuwa, jumla ya wajawazito 2,028,151 sawa na asilimia 98 walihudhuria kliniki kwa mara ya kwanza, ikilinganishwa na wajawazito 1,572,778 sawa na asilimia 86 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Mikoa iliyoongoza kwa kuwa na asilimia kubwa ya wajawazito waliohudhuria kliniki hudhurio la kwanza ni Katavi (asilimia 105.9), Tabora (asilimia 88.3), Geita (asilimia 78.3), Shinyanga (asilimia 77.6) na Rukwa (asilimia 76.3). Mikoa iliyokuwa na asilimia ndogo ya wajawazito waliohudhuria kliniki hudhurio la kwanza ni Mtwara, (asilimia 43.9); Njombe, (asilimia 44.6); na Kilimanjaro, (asilimia 45.8).

**60. Mheshimiwa Spika,** Wajawazito waliohudhuria **mahudhurio manne** na zaidi walikuwa 1,897,773 sawa na **asilimia 83 ya waliotarajiwa** ikilinganishwa na idadi ya wajawazito 1,788,591 sawa na asilimia 79 katika kipindi hicho cha mwaka 2021/22. Hata hivyo pamoja na mafanikio ya mahudhurio ya wajawazito kliniki mara nne kufikia asilimia 83, bado mahudhurio ya kliniki ya wajawazito wenye umri wa mimba chini ya wiki 12 katika kipindi cha 2022/23 imeendelea kuwa katika kiwango cha chini kwa asilimia 37.8, sawa na wajawazito 632,930 ikilinganishwa na

asilimia **36.6** katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ikumbukwe kwamba kuanza kliniki katika umri chini ya wiki 12 ni wakati muafaka kwa matokeo chanya ya ujauzito kwani wahudumu wa afya watatumia fursa hii kutambua na kutibu changamoto mbalimbali zitokanazo na ujauzito au hata zile ambazo hazitokani na ujauzito lakini zinaweza kuhatarisha maisha ya mama au mtoto aliyeko tumboni.Changamoto hizi ni kama vile upungufu wa damu, malaria, mimba kutunga nje ya kizazi; au hata magonjwa ya moyo au changamoto zitokanazo na makundi madogo ya damu yasiyoendana baina ya wenza (Rh incompactibility). **Nitumie fursa hii kuwahimiza akinamama wajawazito pamoja na wenzi wao kuwahi kuanza kliniki mapema ili wataalamu waweze kuwa na muda muafaka wa kutambua changamoto hizi na kuchukuwa hatua stahiki kwa wakati.**

**61. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia Sera ya Afya kwa kuhakikisha vituo vinatoa huduma bora za kliniki wakati wa ujauzito ambazo ni; kuwapatia elimu ya afya kuhusu vidokezo vya hatari na lishe, kuwafanyia vipimo vya msingi kama shinikizo la damu (BP), kundi la damu, wingi wa damu, kuangalia protini kwenye mkojo, maambukizi ya Malaria, VVU na kaswende. Aidha, wakati wa kliniki mama mjamzito anapewa kadi maalumu ya kliniki ya ujauzito, huduma za dawa kinga za minyoo, dawa za kuongeza wingi wa damu na dawa za kinga ya malaria (SP). Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, asilimia 87 ya wajawazito wote walipatiwa dawa za kukinga na kuzuia Malaria (IPT2+) ikilinganishwa na asilimia 84 ya wajawazito mwaka 2021/2022 katika kipindi kama hicho. Aidha, wajawazito waliopata dawa ya kuzuia upungufu wa damu (FEFO) katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 walikuwa ni asilimia 86 ya wajawazito wote ukilinganisha na asilimia 78 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Wajawazito waliopewa dawa za kutibu minyoo walikuwa ni

asilimia 83.4 ikilinganishwa na asilimia 68.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

**62. Mheshimiwa Spika,** Upande wa **huduma za wakati na baada ya kujifungua** kwa kutumia takwimu za MTUHA zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wajawazito 1,500,404 sawa na asilimia 98 ya akina mama wote 1,555,738 waliojifungua, walijifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na wajawazito 1,403,761 sawa na asilimia 97 ya 1,444,947 waliotarajiwa katika kipindi cha mwaka 2021/22. Aidha, wajawazito waliohudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi wameendelea kuwa asilimia 94 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 kama ilivyokua katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Wizara, kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma; Chama Wakunga Tanzania (TAMA), Chama cha Wauguzi (TANNA), Chama cha Madaktari Bingwa wa Watoto Tanzania (PAT), Chama cha Madaktari Bingwa wa Magonjwa ya Akinamama na Uzazi (AGOTA), Chama cha Wataalamu wa Dawa za Ganzi na Usingizi (SATA) imeendelea kufuatilia na kufanya mapitio ya **vifo vitokanavyo na uzazi kwa njia ya mtandao katika kila siku ya kazi** ili kubaini mapungufu ya mifumo ya afya na kufanya maboresho yanayowezesha kufikia lengo la kutokomeza vifo vitokanavyo na uzazi. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, **jumla ya vifo 943** vitokanavyo na uzazi vilitolewa taarifa ikilinganishwa na vifo 982 kipindi cha mwaka 2021/22. Hata hivyo napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, uchambuzi wa matokeo ya utafiti wa hali ya afya na demografia nchini ya mwaka 2022 (Tanzania Demographic and Health Survey, TDHS 2022) uliofanywa na Taasisi ya Takwimu ya Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya Bara na Zanzibar utakapokamilika tutapata takwimu rasmi za kitaifa kuhusu idadi ya vifo vya wajawazito.

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma kwa Watoto wachanga** ambapo matokeo ya

utafiti wa TDHS 2022 inaonesha uwepo wa kiwango kidogo cha kupungua kwa vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 25 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi 24 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2021/2022. Matokeo haya yanatuonesha umuhimu wa Serikali kuongeza nguvu zaidi katika kupunguza vifo vya watoto wachanga ili kufikia lengo la Kimataifa la kupunguza vifo vya watoto wachanga kufikia 12 kwa vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2030. Moja ya mikakati iliyotekelezwa ni kuziwezesha hospitali kuanzisha Wodi maalum za watoto wachanga mahututi (Neonatal Intensive Care Unit-NICU) ambapo wodi hizo zimeongezeka kutoka 165 mwaka 2021/22 hadi 248 mwaka 2022/23.

**64. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua kuwa baadhi ya NICU zilikuwa na upungufu wa vifaa muhimu vya kutolea huduma, Wizara imenunua vifaa tiba vya huduma za watoto wachanga wagonjwa wakiwemo mahututi na njiti vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 6.3** ambavyo katika awamu ya kwanza vitasambazwa kwenye vituo **120** vya kutoa huduma za afya. **Kiambatisho na. 4 na 5.** Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imefanya ukarabati na ununuzi wa vifaa vyenye thamani ya Shilingi Milioni **264** kwa ajili ya NICUs kwa Hospitali tano za Halmashauri za Kasulu mji, Kibondo, Urambo, Nzega na Igunga ili kuongeza ukubwa na uwezo wa kutoa huduma kwa watoto wachanga. Kwa kuzingatia vifo vya watoto wachanga husababishwa na kuzaliwa na uzito mdogo na kabla ya muda, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za mama kangaroo (KMC) kwa ajili ya watoto wenye uzito mdogo na njiti ambapo vituo vya afya na hospitali za Halmashauri zinazotoa huduma hii vimeongezeka kufikia 559 katika kipindi cha Julai 2022 mpaka Machi 2023 ukilinganisha na vituo 453 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Hatua hii imeongeza idadi ya vitanda vya mama kangaroo kufikia 1,174 kutoka 1,017 katika kipindi hicho.

**65. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia **huduma za afya kwa watoto walio chini ya miaka mitano**. Kwa mujibu wa Takwimu za TDHS 2022 vifo vya watoto umri chini ya mwaka mmoja vimepungua kwa asilimia 23 kutoka vifo 43 kwa vizazi hai 1,000 vya mwaka 2016 hadi vifo 33 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022. Aidha, vifo vya watoto umri chini ya miaka mitano vimepungua kwa asilimia 36 kutoka vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 43 kwa vizazi hai 1000 mwaka 2022. Mafanikio haya ni matokeo ya kuimarika kwa huduma za chanjo, udhibiti na Matibabu ya Magonjwa ya Watoto kwa uwiano (Integrated Management of Childhood illness - IMCI) hasa homa ya mapafu (Nimonia), Malaria na Kuharisha, ambayo huchangia kwa kiwango kikubwa vifo kwa Watoto wa umri chini ya miaka mitano.

**66. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilinunua na kusambaza dawa kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa homa ya mapafu (Nimonia) ya kidonge myeyuko cha **Amoxicillin** vidonge milioni 30.1 sawa na asilimia 95.5 ya lengo, na dozi 94,300 za **Zinc** na **ORS** kwa ajili ya matibabu ya kuharisha sawa na asilimia 67 ya lengo. Ununuzi wa dawa hizi uliwezesha kuimarika kwa upatikanaji wa dawa za watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika vituo vya kutolea huduma kwa asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 85.3 katika kipindi hicho mwaka 2022. **Naomba kutumia fursa hii kusisitiza kwamba dawa za kidonge myeyuko cha Amoxicillin, Zinc na ORS kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, zinanunuliwa na Serikali kwa kushirikiana na wadau na dawa hizi hazipaswi kuuzwa. Hivyo, nawaelekeza Waganga wakuu wa Mikoa na Halmashauri wasimamie suala hili kwa ukamilifu**. Aidha, katika kuimarisha ujuzi wa watoa huduma za Matibabu ya Magonjwa ya Watoto kwa uwiano (IMCI), Wizara iliwajengea uwezo watoa huduma 611 wa Mikoa 8 ya Mwanza, Tabora, Kigoma, Mara, Geita, Shinyanga, Manyara na Simiyu.

**67. Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha huduma hii za afya ya uzazi na mtoto, Wizara imetengeneza Kitabu cha Afya ya Mama kitakachotumika kufuatilia afya ya mama wakati wa ujauzito. Kitabu hiki ni mbadala wa kadi ya kliniki ya wajawazito (RCH4). Aidha, imetengeneza kitabu kipya cha kufuatilia makuzi na huduma za watoto walio chini ya miaka mitano. Katika kuhakikisha upatikanaji kwa akinamama na watoto kwa vitabu hivi, Wizara imeipa jukumu Bohari ya Dawa MSD kuchapisha kitabu cha mama na vitabu vya afya ya mtoto jumla ya milioni 2.6 (Kiume 1,300,000 na Kike 1,300,000) kwa ajili ya ufuatiliaji wa makuzi, malezi na maendeleo ya mtoto. **Wizara inasisitiza kuwa vitabu hivi vitatolewa bila Malipo kwa mama mjamzito au mtoto wa chini chini ya miaka mitano** kwani tayari vimelipiwa na Serikali.

**68. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma kwa wahanga wa matukio ya **ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.** Aidha, Wizara imeendelea kusisitiza wahanga kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya ndani ya saa 72 baada ya tukio kutokea ili kuhakikisha wanapatiwa huduma jumuishi ikiwemo ushauri nasaha, uchunguzi na vipimo, tiba-kinga za kuzuia magonjwa ya ngono na ujauzito, mwendelezo wa huduma ikiwemo huduma za kisaikolojia na msaada wa kisheria. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya wateja 194,368 walifika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na wateja 164,209 mwaka 2021/ 2022. Aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, asilimia 7 ya wahanga wa ukatili walikua ni watoto, kati yao, 13,130 wa jinsi ya kike na 836 jinsi ya kiume. Mikoa 10 iliyoongoza ni pamoja na; Dar es salaam (17,774), Shinyanga (11,986), Geita (11,210), Tabora (10,205), Mara (10,020), Mwanza (9,730), Kagera (8,627), Kilimanjaro (7,006), Kigoma (6,951) na Arusha (6,066). Aidha, jumla ya watoa huduma za afya 650 kutoka mikoa ya Singida, Shinyanga, Dar es Salaam Kagera, Arusha, Manyara, na

Dodoma walijengewa uwezo juu ya utoaji huduma kwa manusura wa vitendo vya Ukatili wa Kijinsia

**69. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kuboresha **huduma za afya ya uzazi kwa kundi la vijana 15-24** kwa kutoa elimu ya afya uzazi kwa vijana kuhusu namna ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU, mimba za utotoni, ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya watoto na lishe. Wizara imeendelea kuongeza na kuimarisha **vituo vya huduma rafiki** za Afya ya uzazi kwa vijana kutoka **215** mwaka 2021 hadi **901** Machi 2023. Katika Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Serikali iliweza kutoa elimu kwa watoa huduma 750 kutoka Mikoa ya Mara, Shinyanga, Dar es Salaam, Katavi, Arusha, Manyara, Geita, Tabora na Dodoma namna ya kutoa huduma rafiki kwa vijana kwa masuala ya afya ya uzazi.

**70. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kujenga mfumo wa huduma za kuzuia na kukinga **Saratani za mfumo wa uzazi (Reproductive cancers)** zikiwemo Saratani ya Mlango wa kizazi na Saratani ya matiti. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 wanawake wapatao 426,774 walifanyiwa uchunguzi wa Saratani ya mlango wa kizazi na kati yao wanawake 13,721 sawa na **asilimia 3.2** waligundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya Saratani ya mlango wa kizazi, ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2021/22. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Wizara imefanikiwa kuanzisha vituo vipya 122 vya kutoa huduma za uchunguzi wa Saratani ya Mlango wa Kizazi na hivyo kufikia jumla ya vituo 923 ikilinganishwa na vituo 801 mwaka 2021/22.

**71. Mheshimiwa Spika,** katika kuvijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya kutoa huduma za uchunguzi na tiba ya **mabadiliko ya awali ya Saratani ya mlango wa kizazi**, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imenunua mashine tiba (**thermocoagulators**) 50 zinazotibu mabadiliko

ya awali ya Saratani ya mlango wa kizazi na kusambazwa katika vituo 50 vya kutolea huduma za afya nchini na watoa huduma wameshajengewa uwezo namna ya kuzitumia. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeagiza mashine Tiba (thermocoagulators) 100 zaidi ambazo zinatarajiwa kusambazwa kwenye vituo vya kabla ya mwezi Disemba 2023. Upatikanaji wa vifaa tiba hivi utaenda kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya matibabu ya Saratani ya mlango wa kizazi katika vituo 100 zaidi vya ngazi ya msingi ikiwemo hospitali ya wilaya, vituo vya afya na zahanati katika mikoa 13 inayoongoza kwa tatizo la saratani ya mlango wa kizazi.

**MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI, HOMA YA INI, NA MAGONJWA YA NGONO**

**72. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuboresha afua mbalimbali za **kudhibiti maambukizi ya VVU/UKIMWI** ikiwemo kuhamasisha wananchi kupima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU/UKIMWI, kutoa huduma za ushauri, upimaji, matunzo na huduma za dawa kwa wenye maambukizi ya VVU/UKIMWI.

**73. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya **wateja 1,632,328** sawa na **asilimia 94.4** ya watu 1,729,408 wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI nchini walikuwa **wanatambua hali zao za maambukizi** (95 ya kwanza). Kati yao wateja 1,612,520 walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI, ambapo watoto walikuwa ni 58,760. Idadi hii ya wagonjwa walio katika **matumizi ya dawa** za kufubaza Virusi vya UKIMWI ni **asilimia 98.8** ya watu wanaotambua hali zao za maambukizi (95 ya pili). Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya vipimo 309,263 vya kujua wingi wa Virusi vya UKIMWI kwa wagonjwa walioanza kutumia dawa vilifanyika na kati ya vipimo hivyo, vipimo 298,657 ambavyo ni sawa na **asilimia 96.6** vilikuwa **vimefubazwa** na

kuwa na wingi wa Virusi vya UKIMWI chini ya nakala 1,000. (95 ya tatu) kama inavyoonekna kama **Jedwali Na. 1**.

**Jedwali Na. 1: Mafanikio kuelekea kufikisha malengo ya 95-95-95**

| **Na.** | **KIASHIRIA** | **Machi, 2022** | **Machi, 2023** | **Hatua iliyofikiwa 95-95-95** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wanaokadiriwa kuwa na maambukizi | 1,795,905 | 1,729,408 | |
| | Wanaotambua hali zao za Maambukizi | 1,530,058 | 1,632,328 | |
| | Asilimia ya wanaotambua hali zao | **85.2** | **94.4** | **95 ya kwanza** |
| 2 | Wenye maambukizi na wameanza dawa | 1,520,589 | 1,612,520 | |
| | Asilimia ya walioanza dawa (on ART) | **99.4** | **98.8** | **95 ya pili** |
| 3 | Idadi ya waliopimwa makali ya VVU (VL test) | 244,056 | 309,263 | |
| | Idadi makali yaliyofubazwa | 233,800 | 298,657 | |
| | Asilimia ya walifubazwa makali (VL<1000) | **95.8** | **96.6** | **95 ya tatu** |

**74. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza kutekeleza Huduma ya afua ya kujipima VVU kuanzia Januari 2020 kwa lengo la kupanua wigo na kuboresha upatikanaji wa huduma za upimaji wa VVU hasa kwa makundi ambayo hayafikiwi kirahisi na huduma za afya na kuongeza kasi ya kutambua wenye maambukizi. Katika kipindi cha Januari 2020 hadi Machi 2023 jumla ya vitepe vya kujipima (HIVST) **805,682** sawa na asilimia 33 ya malengo viligawiwa kwa

wateja na jumla ya wateja **729,703** sawa na asilimia 91 walirudisha majibu. Kati wateja waliorudisha majibu, **21,449** sawa na asilimia 3 walipata majibu yanayoonesha dalili za maambukizi. Kati yao wateja 17,874 sawa na asilimia 83 walifanyiwa uhakiki na kukutwa na maambukizi. Wizara inahimiza kutumia huduma hii ya kujipima mwenyewe VVU kwani inawezesha kuibua watu ambao walikuwa hawafahamu hali zao za maambukizi.

**75. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa huduma kwa WAVIU zinasogezwa karibu zaidi na jamii, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali wa maendeleo imekuwa ikifanya jitihada za makusudi za kuhakikisha kila kituo cha afya nchini kinakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Hadi kufikia mwezi Machi 2023, Idadi ya vituo vinavyotoa huduma ya Tiba na Matunzo (CTC) vimefikia **vituo 7,072** kutoka **vituo 6,919** mwaka 2020/21, hii ni sawa na **asilimia 82** ya ya vituo vyote (8,529) vinavyotoa huduma za afya nchini. Lengo ni kufikia asilimia 95 ya vituo vyote vya afya viwe vinatoa huduma ya tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (WAVIU) ifikapo mwaka 2025. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau inatekeleza afua ya kuwajengea uwezo Wauguzi na Wakunga nchini kuwahudumia watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na UKIMWI ikiwa ni pamoja na kuwaanzishia WAVIU dawa za kufubaza makali ya VVU na UKIMWI (Nurse Initiated Management of Anti Retroviral Therapy -NIMART). Afua hii imekuwa na mchango mkubwa katika kufikia katika malengo ya 95-95-95.

**76. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za kupunguza maambukzi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ikiwemo kuhakikisha **Watoto wachanga waliozaliwa na akina mama wenye VVU** wanapimwa maambukizi ya VVU kwa kutumia vinasaba katika mahali zitolewapo huduma (Early infant Diagnosis

(EID) Point of Care). Idadi ya vituo vinavyotoa huduma za EID point of care iliongezeka kutoka 54 mwaka 2020 hadi vituo 130 mwezi Machi 2023, lengo ni kufikia vituo 340. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya watoto 33,814 walizaliwa na akinamama wanaoishi na VVU, kati yao watoto 24,659 waliingizwa katika ufuatiliaji na kupewa tiba kinga (ARVProphylaxis). Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya watoto 27,785 sawa na 78.7% walipimwa kipimo cha wiki sita (6) ambapo watoto 181 sawa na **asilimia 0.65**, walithibitika kuwa na maambukizi ya VVU. Aidha, matokeo ya upimaji katika umri wa miezi 18 yanaonyesha kuwa, **watoto 14,720** sawa na asilimia **44.8%** ya watoto 32,876 waliostahili kupimwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ambapo katika kipindi hichohicho jumla ya watoto **340** sawa na **2.3%** ya watoto wote waliopimwa kipimo cha uthibitisho waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU. Wizara kwa kushirikiana OR-TAMISEMI na wadau itaendelea kuimarisha mikakati ya ufuatiliaji wa wajawazito na wanaojifungua wakiwa na maambukizi ya VVU ili kuhakikisha wanaendelea kuhudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma na kupata huduma stahiki za kuzuia maambukizi kwenda kwa mtoto.

**77. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na jitihada za kudhibiti maambukizi ya **homa ya Ini** ambapo kwa mujibu wa tafiti kinaonesha kiwango cha maambukizi ya Homa ya Ini B katika jamii ni asilimia 4.1, Homa ya Ini C ni asilimia 1. Aidha, asilimia 6.3 ya wajidunga wameonekana kuwa maambukizi ya Homa ya Ini C. Wizara inaendelea kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya Homa ya Ini, ambayo ni mojawapo ya magonjwa ya kuambukiza hapa nchini. Katika utafiti uliofanyika wa mwaka 2017 (THIS 2017) ulionyesha kuwa maambukizi ya B yapo kwa asilimia 4.1 na ya aina C asilimia 1.

**78. Mheshimiwa Spika,** ili kudhibiti maambukizi ya homa ya ini Serikali imeendelea kutoa chanjo ya homa ya ini B kwa

watumishi wa afya ambapo hadi Machi 2023 watumishi 10,966 walikuwa wamepatiwa chanjo hii na asilimia 70 kati yao walikuwa wamemaliza chanjo zote tatu zinazohitajika. Wizara pia inatoa huduma ya uchunguzi wa Homa ya ini (Hepatitis B na C) kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa VVU wakiwemo waraibu wa dawa za kulevya. Idadi ya waraibu wanaopata huduma ya kuchunguza Homa ya ini (Hepatitis B na C) imekuwa ikiongezeka katika kila robo mwaka ambapo hadi kufikia Machi 2023, jumla ya waraibu 138,064 walichunguzwa Homa ya ini aina Hepatitis B na waraibu 102,394 walichunguzwa Homa ya ini aina ya Hepatitis C. Aidha, hadi kufikia Machi 2022, jumla ya wanaume na wanawake walio katika makundi hatarishi 49,559 walichunguzwa Homa ya Ini B na 41,475 walichunguzwa Homa ya Ini C.

**79. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha 2022/23, Wizara imeanza utekelezaji wa afua za kuzuia maambukizi ya virusi vya **homa ya ini** aina 'B' kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto ambapo huduma za vipimo na chanjo za homa ya ini B zinatolewa katika vituo 100 vilivyopo katika mikoa ya Njombe, Geita, Mbeya na Dar es Salaam ili kupata takwimu za kufanyia maoteo na kueneza huduma hizi katika vituo vyote nchini. Aidha, kuanzia mwaka 2000 Wizara imekuwa inatoa chanjo ya Pentavalent kwa watoto wenye umri wa chini ya mwaka mmoja na hivyo kuwakinga dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini B. Ili kudhibiti maambukizi ya homa ya ini, kipaumbele cha Wizara ni kupima na kutoa chanjo ya maambukizi dhidi ya homa ya ini ni kwa watu waliozaliwa kabla ya mwaka 2000 na pia imeimarisha uratibu wa magonjwa haya kwa kuyaweka chini ya usimamizi wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI.

**80. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza afua za kudhibiti **magonjwa ya ngono (STIs)** kwa kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya magonjwa haya, huduma za uchunguzi na tiba. Katika

kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya watu 480,448 waligundulika kuwa na magonjwa ya ngono kulinganisha na watu 458,614 katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2021/22. Aidha, magonjwa ya ngono yaliyoongoza ni Klamidia (Chlamydia), Kaswende (Syphilis) Kisonono (Gonorrhea) na Herpes. Aidha, ili kuwakinga watoto wachanga kuzaliwa na maambukizi ya magonjwa ya ngono jumla ya wajawazito 1,095,506 sawa na asilimia 65 walipimwa **maambukizi ya Kaswende** ikilinganishwa na wajawazito 1,042,921 sawa na asilimia 66 katika mwaka 2021/2022. Wajawazito 11,068 sawa na asilimia moja (1) ya wajawazito wote waliopimwa walibainika kuwa na maambukizi ya kaswende na walianzishiwa tiba ikilinganishwa na wajawazito 10,535 sawa na asilimia moja (1) kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/2022.

**81. Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwaelewa Wananchi kuwa magonjwa ya ngono bado yapo hivyo wanapaswa kuchukua hatua za kujikinga na endapo watapata maambukizi kuwahi kwenda kwenye vituo vya kutoa huduma ili wapate tiba sahihi na mapema.

**Mapambano Dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma**

**82. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za Kifua Kikuu na Ukoma sanjari na Mpango Mkakati wa Sita wa mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma. Lengo kuu katika mpango huu ni kupunguza maambukizi mapya ya Kifua Kikuu kwa asilimia 50, kupunguza vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu kwa asilimia 75 na kutokomeza Ukoma katika Halmashauri zenye wagonjwa wa Ukoma ifikapo mwaka 2025.

**83. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilipanga kuibua wagonjwa wa Kifua Kikuu **74,418** ambapo **74,513 waliibuliwa ikiwa ni sawa na**

**asilimia 100.1** ya lengo. Kwa kipindi cha 2021/2022, jumla ya wagonjwa 70,382 (sawa na asilimia 104) waliibuliwa ikilinganishwa na lengo la kuibua wagonjwa 67,489 kwa kipindi hicho. Mafanikio haya yametokana na kuwashirikisha waliougua kifua kikuu na kupona (MKUTA), waganga wa tiba asili na wahudumu wa afya ngazi ya jamii. Aidha, asilimia 92 ya wagonjwa wa Kifua Kikuu **walioanza matibabu** kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 walitibiwa na kupona ikilinganishwa na asilimia 95 ya wagonjwa wa Kifua Kikuu walioanza matibabu kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2020/2021. Mpango unaendelea na ufuatiliaji wa kimkakati wa karibu kwa wagonjwa vituoni na ushirikishwaji wa watoa huduma katika ngazi ya jamii ili kufikia lengo la Shirika la Afya Duniani (WHO) la kuponyesha asilimia 90 ya wagonjwa wanaoanza matibabu. Vilevile, katika kipindi hicho jumla ya wagonjwa 266 wa **Kifua Kikuu Sugu** waligundulika na kuanzishiwa matibabu ambao ni sawa na asilimia 40 ya lengo la kugundua wagonjwa 664 ikilinganishwa na wagonjwa 381 waliogundulika katika kipindi kama hicho mwaka 2021/2022 sawa na asilimia 62 ya lengo la kuibua wagonjwa 619 wa Kifua Kikuu Sugu. Bado hatujafanya vizuri katika eneo hili kutokana na kutowafikia na kuwabaini wagonjwa wote walioko kwenye jamii.

**84. Mheshimiwa Spika,** katika **kuimarisha huduma za upimaji wa Kifua Kikuu**, Serikali kupitia Wizara ya Afya imenunua **mashine 30** za kisasa aina ya **Truenat** ambazo zimesimikwa kwenye vituo vya kutolea huduma za Kifua Kikuu visivyohitaji uboreshwaji wa miundombinu kama vile chumba cha upimaji (Point of Care Test). Wizara imeendelea kutoa **huduma mkoba za kliniki tembezi** zenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi na ugunduzi kwa magonjwa ya Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa katika maeneo yenye makundi hatarishi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya watu 8,298 walichunguzwa na

kupimwa Kifua Kikuu. Kati ya wagonjwa 8,298 waliopimwa, wagonjwa 2,368 sawa na asilimia 29 waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu na kuanzishiwa matibabu.

**85. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kutokomeza **Ukoma** nchini, Wizara inaendelea kusimamia huduma za uchunguzi. Kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya **wagonjwa 1,019** waligundulika na ugonjwa wa Ukoma ikilinganishwa na wagonjwa 1,290 waliongundulika katika kipindi kama hicho mwaka 2021/2022. Sambamba na uibuaji huu, Kaya 300 zilifikiwa na kufanyiwa uchunguzi ambapo jumla ya wagonjwa 20 waliibuliwa na kuanzishiwa matibabu. Sanjari na hilo, Wizara imeendelea na **utoaji wa tiba kinga ya Ugonjwa wa Ukoma kwa makundi hatarishi** ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya watu 1,344 waliokuwa katika makundi hatarishi walipewa tiba kinga na watu 802 waligundulika kuwa na magonjwa mengine ya ngozi na kuanzishiwa matibabu. Wizara imeendelea kutoa vifaa tiba kwa kugawa jozi za viatu 165 ili kupunguza athari za ulemavu kwa waathirika wa Ukoma.

**Mapambano dhidi ya Malaria**

**86. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Mpango Mkakati wa Miaka mitano wa kipindi cha 2021-2025 wenye lengo la kupunguza maambukizi ya malaria kutoka asilimia 7.5 mwaka 2017 hadi chini ya asilimia 3.5 mwaka 2025. Pamoja na hilo, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwepo ugawaji wa vyandarua kwa makundi maalum, upuliziaji wa viuatilifu ukoko na kuhakikisha dawa za kutibu malaria zinapatikana kwa kipindi chote bila malipo katika vituo vya kutolea huduma, ili kuwakinga Wajawazito, Watoto chini ya miaka mitano na jamii kwa ujumla dhidi ya ugonjwa wa Malaria.

**87. Mheshimiwa Spika,** Serikali iliendelea kuhakikisha vipimo, dawa, vyandarua na bidhaa nyingine za kudhibiti malaria zinapatikana bila malipo katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuendelea kudhibiti ugonjwa wa malaria. Katika kipindi hicho, vipimo **22,578,350** vya malaria (mRDT); dozi **6,817,260** za dawa ya mseto na vichupa **2,890,242** vya dawa ya malaria ya sindano vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na vipimo **23,182,375** vya malaria (mRDTs), dozi **18,899,880** za dawa ya mseto na vichupa **3,290,650** vya dawa ya malaria ya sindano mwaka 2021/22. Dawa na vitendanishi hivi vimeendelea kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kupitia Bohari ya Dawa (MSD) kulingana na mahitaji ya vituo. Kwa kipindi hiki, utoshelevu wa dawa za malaria ilikuwa ni **asilimia 98** ikilinganishwa na asilimia 97.8 kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

**88. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi husika, **vyandarua** 6,119,732 vyenye dawa vilinunuliwa ikilinganishwa na vyandarua 7,508,122 vilivyonunuliwa mwaka 2021. Vyandarua hivyo vilisambazwa kwa watoto wa shule za msingi, wanawake wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja katika vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima pamoja na kaya zote katika Halmashauri sita (6) za mikoa ya Mtwara na Lindi. Wizara ilifanya **upuliziaji wa viuatilifu ukoko** katika Mkoa wa Kigoma kwenye Halmashauri mbili (2) za Kasulu DC, Kibondo DC ikijumuishwa kambi za wakimbizi za Nduta na Nyarugusu ambapo jumla ya kaya 254,858 sawa na asilimia 94.7 zimepuliziwa viuatilifu ukoko na kukinga jumla ya watu 1,035,998 dhidi ya maambukizi ya Malaria, ikilinganishwa na kaya 592,444 zilizopuliziwa viuatilifu ukoko mwaka 2021 na kukinga jumla ya Watu 2,665,998.

**89. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutekeleza **mradi wa kuelekea utokomezaji wa malaria** (Towards Elimination of Malaria in Tanzania-TEMT) unaotekelezwa

kwenye Mkoa wa Tanga. Halmashauri tatu (3) za Mkoa wa Tanga ambazo ni Handeni DC, Lushoto DC na Tanga CC tayari zimepatiwa mafunzo. Jumla ya washiriki 969 kutoka katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri, Kata na vijiji wamepatiwa mafunzo, pampu za kupulizia 532 na lita 490 za viuadudu zimenunuliwa na kusambazwa katika Halmashauri hizo za Mkoa wa Tanga.

**90. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Afua ya kutokomeza malaria katika maeneo yenye kiwango cha chini cha maambukizi, ambapo **Ufuatiliaji wa Ugonjwa wa Malaria hufanyika hadi katika Ngazi ya Kaya (Malaria Case Based Surveillance-MCBS)** na kufanya Tathmini katika Halmashauri 29 za mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Njombe na Iringa. Katika utekelezaji wa Afua hii wagonjwa wanaogundulika kuwa na maambukizi ya malaria katika vituo vya kutolea huduma za Afya hufuatiliwa mpaka katika kaya zao ambapo wanakaya hupimwa na kutibiwa pale wanapokutwa na maambukizi ya malaria. Mpaka kufikia Machi 2023 jumla ya wagonjwa 1,401 walifuatiliwa na wanakaya 1,518 walipimwa malaria ambapo watu 54 sawa na asilimia 3.6 walikutwa na maambukizi ya malaria na kupatiwa matibabu.

**91. Mheshimiwa Spika,** Wizara imewajengea uwezo **Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (CHWs) 2,500,** juu ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kudhibiti Malaria katika Halmashauri zote za mikoa nane (8) ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Geita, Kigoma, Tabora, Katavi na Rukwa. Aidha, matangazo 487 ya Redio juu ya elimu na ujumbe wa kinga, matibabu sahihi ya malaria yamerushwa katika vituo vitatu vya Kitaifa na radio za kijamii katika Mikoa tisa (9) ya Tanga, Lindi, Shinyanga, Katavi, Tabora, Kigoma, Ruvuma, Mwanza na Rukwa. Matangazo 292 ya Television yamerushwa katika vituo vitatu vya TBC 1, ITV na Clouds. Jumla ya mabango (posters) 524,000 yenye ujumbe wa Malaria

yamechapishwa na kugawiwa katika mikoa yote na Halmashauri zote za Tanzania Bara.

**92. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na afua mbalimbali zilizotekelezwa katika kupambana na Malaria, **idadi ya wagonjwa wa malaria** imepungua hadi kufika milioni 3.5 mwaka 2022/23 kutoka milioni 4.4 mwaka 2021/22. Aidha, **idadi ya visa vipya vya malaria** kwa kila watu 1,000 imepungua hadi visa 58 kwa mwaka 2022/23 kutoka visa 76 mwaka 2021/22 na **idadi ya vifo vitokanavyo na malaria** ilipungua hadi vifo 1430 mwaka 2022/23 kutoka vifo 1,811 mwaka 2021/22.

**93. Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza upatikanaji wa rasilimali fedha za ndani na kuongeza kasi ya kutokomeza malaria, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliteua wajumbe 19 kutoka Wizara na Taasisi za Serikali, taasisi za dini, sekta binafsi na taasisi za kiraia wa Baraza la Kutokomeza Malaria. Baraza hili lilizinduliwa na Mhe. Kasim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani Jijini Dar es Salaam tarehe 25.04.2023. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuunda Baraza hili muhimu. Nitoe wito kwa Bunge lako tukufu na wananchi wote kwa ujumla kutoa ushirikiano kwa Baraza hili ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa lengo la kuhakikisha raslimali za kutekeleza afua muhimu za malaria zinapatikana.

**94. Mheshimiwa Spika,** ili kuweza kufikia lengo la kutokomeza malaria mwaka 2030 kupitia kauli mbiu ya Ziro Malaria Inaanza na Mimi, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria itaendelea kuwekeza na kuimarisha ushirikishwaji wa Jamii katika kupambana na ugonjwa wa Malaria. Maeneo muhimu yatakayopewa kipaumbele ni ushirikishwaji wa Jamii katika kudhibiti mbu waenezao

malaria kwa kushiriki katika afua za unyunyiziaji wa dawa za kuuwa viluilui wa mbu kwenye mazalia, usafi wa mazingira na kutiririsha maji yaliyotuama ili kuzuia mazalia ya mbu

**HUDUMA ZA TIBA**

**95. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za Afya nchini, Wizara imeendelea **kuratibu ujenzi wa miundombinu** na utoaji wa huduma mbalimbali za tiba. Hadi kufikia Machi, 2023, kulikuwa na **jumla ya vituo 11,040** vya kutolea huduma za afya, ambapo Hospitali zilikuwa 430, Vituo vya afya vilikuwa 1,030, Zahanati zilikuwa 7,458, Kliniki zilikuwa 906 na Maabara Binafsi 1,216 ikilinganishwa na **vituo 8,549** vilivyokuwepo Machi 2022. Aidha, vituo vilivyokuwa vinamilikiwa na Serikali vilikuwa 6,682 sawa na asilimia 60 ya vituo vyote, Mashirika ya dini vilikuwa 1,040 sawa na asilimia 9.4 ya vituo vyote na Sekta binafsi vilikuwa 3,318 sawa na asilimia 30 ya vituo vyote nchini. Kwa upande wa vitanda vya hospitali, hadi kufikia mwezi Machi 2023 kulikuwa na jumla ya vitanda 95,868 ikilinganishwa na vitanda 93,356 vilivyokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, kati ya vitanda hivyo 95,868 vitanda 49,143 vipo katika ngazi ya Hospitali, vitanda 24,957 vipo katika Vituo vya Afya, vitanda 20,582 vipo katika Zahanati na vitanda 1,186 vinapatikana katika kliniki na vituo vinginevyo kama inavyoonkena katika **Jedwali Na 2**.

**Jedwali Na 2; Mchanganuo wa idadi ya vitanda katika vituo vya kutolea huduma za Afya**

| Aina ya Kituo | Vinavyohitajika | Vilivyopo Wodini | Upungufu |
|---|---|---|---|
| **Hospitali** | 67,367 | 49,143 | 18,224 |
| **Vituo vya Afya** | 35,735 | 24,957 | 10,778 |
| **Zahanati** | 42,743 | 20,582 | 22,161 |
| **Kliniki** | 1,475 | 865 | 610 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Nyinginezo** | 742 | 321 | 421 |
| **JUMLA** | **148,062** | **95,868** | **52,194** |

**Huduma za Dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi**

**96. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa **upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara** katika vituo vya kutolea huduma za afya unakuwa wa kuridhisha. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) hununua, hutunza na husambaza zaidi ya aina 1,500 za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara. Kati ya hizo, aina 290 zimeainishwa kuwa ni bidhaa za afya muhimu na za kipaumbele hivyo Wizara ya Afya ina lengo la kuhakikisha kuwa bidhaa hizi zinapatikana wakati wote katika Bohari ya Dawa (MSD). Aidha, hadi sasa, Wizara ya Afya imeshapokea na kupeleka MSD kiasi cha Shilingi bilioni 159.9 sawa na asilimia 80 ya bajeti ya Shilingi Bilioni 200 iliyoidhinishwa na Bunge lako kwa ajili ya ugharamiaji wa mnyororo mzima wa upatikanaji wa bidhaa za afya. Aidha, vituo vya kutolea huduma za afya kupitia fedha za uchangiaji vimepeleka MSD kiasi cha Shilingi bilioni 33.8 na kufanya jumla ya fedha zilizopelekwa MSD kwa ajili ya ugharamiaji wa bidhaa za afya kufikia Shilingi bilioni 193.8.

**97. Mheshimiwa Spika**, kupatikana kwa fedha hizi kumewezesha upatikanaji wa bidhaa za afya za kipaumbele **aina 290** kuongezeka kutoka wastani wa **asilimia 52.4** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi kufikia wastani wa **asilimia 73** katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya (Zahanati asilimia 52, Vituo vya Afya asilimia 57), Hospitali za Wilaya asilimia 67, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 98 na Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa ni asilimia 94. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya bidhaa muhimu za kipaumbele 290 kwa lengo la kuendelea kuboresha upimaji wa bidhaa hizo vituoni. Kufuatia mapitio hayo, kwa sasa Zahanati zitapimwa kwa aina 100 ya bidhaa za afya; Vituo vya Afya aina 178 Hospitali za Halmashauri aina 203;

Hospitali za Rufaa za Mikoa aina 245 na Hospitali za Kanda na Taifa ni aina 290. Upimaji huu pia umezingatia mahitaji ya Hospitali Maalumu kama JKCI, ORCI, Mirembe na Kibong`oto.

**98. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha upatikanaji wa dawa za wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara imefanya maboresho kwenye mwongozo wa matibabu (STG) kwa kuongeza dawa aina tano za magonjwa ya NCD ziweze kupatikana ngazi ya Zahanati na Vituo vya Afya. Wizara itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha maoteo ya bidhaa za afya kwa mfumo wa bottom-up quantification, kufanya ufuatiliaji wa bidhaa za afya vituoni, kuongeza matumizi ya kielektroniki katika kusimamia na kutoa taarifa za bidhaa za afya.

**99. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za afya nchini, na kutekeleza Sera ya Viwanda; Serikali imeendelea kutengeneza **mazingira bora ya uwekezaji** katika eneo la uanzishaji wa viwanda vya bidhaa za dawa kwa wawekezaji wa ndani na wale wa nje, ili kupunguza utegemezi na uchelewaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Ambapo hadi kufikia Machi, 2023 tayari kuna jumla ya viwanda 36 vya kuzalisha bidhaa za afya nchini. Kati ya viwanda hivyo, viwanda 11 vinazalisha dawa ambapo kimoja kina ubia na Serikali na vingine 10 ni vya sekta binafsi. Aidha, viwanda vingine 25 vinajihusisha na uzalishaji wa vifaa tiba ambapo Serikali inamiliki viwanda viwili na sekta binafsi viwanda 23. **Uwekezaji huu wa Serikali unaohusisha pia uzalishaji wa barakoa umewezesha Serikali kujitosheleza kwa mahitaji ya barakoa nchini na hivyo kuachana za uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.**

**100. Mheshimiwa Spika,** naomba pia kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa sasa Tanzania ina viwanda viwili (02) (Kairuki Pharmaceuticals Industry Ltd na na Alfa

Pharmaceuticals Limited) vyenye uwezo wa kuzalisha majitiba jumla ya chupa milioni 98 zaidi ya mahitaji ya nchi ambayo ni chupa milioni 24. Kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa majitiba 'infusion' baada ya viwanda hivi viwili kuanza kuzalisha na kuuza kwa Bohari ya Dawa, **Serikali inakusudia kuacha kuagiza kabisa majitiba "infusions" kutoka nje ya nchi**. Aidha, Serikali inakusudia kutumia zaidi ya **Shilingi bilioni 60** kufanya ununuzi wa bidhaa za afya kwa viwanda vilivyopo nchini. Hadi sasa kuna jumla ya **aina 120** za bidhaa muhimu za afya zinazozalishwa na viwanda vya ndani, wazalishaji wa bidhaa hizi tayari wanamikataba na MSD. Lengo la Serikali ni kushusha uagizaji wa bidhaa za afya nje ya nchi kutoka **asilimia 80** ya sasa na kuwa chini ya **asilimia 50** ifikapo **mwaka 2030.** Haya ni mafanikio makubwa sana katika sekta ya uzalishaji wa bidhaa za afya hapa nchini.

**101. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza makubaliano ya Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kutoa kipaumbele kwenye **mapambano ya Usugu wa Vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa**. Wizara imezijengea uwezo **maabara 25 za Hospitali za Rufaa** ili ziweze kufanya utambuzi na ufuatilaji wa usugu wa vimelea dhidi ya dawa (culture and susceptibility test for AntiMicrobial Resistance and Survaillance-AMR). Kufuatia kujengewa uwezo kwa Hospitali hizo kumeiwezesha Tanzania kuwasilisha taarifa katika mfumo wa Global AntiMicrobial Resistance and Use Survaillance SystemGLASS unaotumiwa na WHO. Tathmini kupitia mfumo huo imeonesha kuna matumizi makubwa ya dawa za antibiotiki nchini na baadhi zimefikia usugu wa asilimia 59.8 hivyo juhudi za pamoja kukabiliana na janga hili zinahitajika. Wizara imefanya mapitio ya utekelezaji mpango mkakati wa kwanza (NAP AMR 2017 – 2022) na sasa imeandaa mpango mkakati wa pili (NAP AMR 2023 - 2028) unaotekelezwa katika utaratibu wa Afya Moja.

**Huduma za Damu Salama**

**102. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu ya kuhakikisha **damu salama** inapatikana kwa wakati na ya kutosha ili kuokoa maisha ya wagonjwa wenye uhitaji mkubwa wa damu wakiwemo **wakina mama wajawazito haswa wakati wa kujifungua**, watoto walio chini ya miaka mitano, wagonjwa wa upasuaji pamoja na wagonjwa wa dharura wanaopata ajali na kuhitaji damu. Wizara inahakikisha upatikanaji wa damu salama unakuwa wa kuridhisha kwa kukusanya damu kutoka kwa wachangiaji damu wa hiari wenye afya njema na wasio kwenye makundi hatarishi. Aidha, Wizara hupima sampuli za damu zilizokusanywa kwa kutumia vipimo vya maabara vyenye viwango vya kimataifa vyenye uwezo wa kugundua maambukizi kwa muda mfupi tangu mtu ameambukizwa pamoja na kupima makundi ya damu.

**103. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya chupa za damu 550,000. Hadi kufikia Machi 2023, Wizara ilifanikiwa kukusanya **chupa za damu 344,936** sawa na **asilimia 84** ya lengo. Idadi hii ni sawa na ongezeko la chupa **125,497** ikilinganishwa na chupa za damu zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. **Ongezeko la chupa hizi limetokana na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Wizara ya Afya ya kutaka Serikali kuchukua jukumu la kununua na kusambaza bure mifuko ya kukusanyia damu nchi nzima na kuhakikisha hakuna upungufu wa mifuko ya kukusanyia damu katika vituo vyote kwa wakati wote.**

**104. Mheshimiwa Spika,** Serikali **imeongeza vituo 7** vya kutengenezea Mazao ya Damu kama vile majimaji ya damu (Fresh Frozen Plasma-FFP), chembe sahani za damu (Platelets), na kufanya kuwa na jumla ya **vituo 15** nchi nzima. Kwa kufanya hivyo, Wizara kupitia Mpango wa Taifa

wa Damu Salama, umeweza kutengeneza chupa 25,658 za mazao ya damu aina ya Plasma (FFP) ambazo zilitumika kusaidia akina mama wanaopata matatizo ya kutokwa na damu nyingi wakati wakijifungua, na chupa 6,625 za chembe sahani (Platelets) zilizotumika kutibu wagonjwa wa saratani, seli mundu pamoja na wagonjwa waliokuwa na matatizo mengine.

**105. Mheshimiwa Spika,** wananchi waliojitokeza na wanaoendelea kujitokeza kuchangia damu kwa hiari, wanapata faida na fursa mbalimbali zinazotokana na uchangiaji wa damu, kama vile **kujua makundi yao ya damu, kupata ushauri nasaha** jinsi ya kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya damu, kujua hali ya afya zao kwa kupimwa magonjwa ya kuambukiza kama vile **Homa ya ini B & C, VVU na Kaswende** pamoja na yasiyokuwa ya kuambukiza ikiwemo **shinikizo la damu** (Blood Pressure.)

**106. Mheshimiwa Spika,** Serikali imekamilisha ujenzi wa kituo cha Damu Salama **kanda ya kati Dodoma** ambacho kimeimarisha upatikanaji wa huduma za Damu salama katika Mikoa Dodoma, Iringa na Singida. Ujenzi wa majengo ya vituo vya Damu Salama unaendelea katika Mikoa **minne (4)** na upo katika hatua mbalimbali; **Rukwa** (asilimia 78), **Manyara** (asilimia 70), **Kigoma** (asilimia 55). Aidha, ujenzi katika kituo cha mkoa wa **Njombe** umekamilika kwa **asilimia 100** na ufungaji wa vifaa unaendelea. Mara baada ya kukamilika kwa uwekezaji huu, huduma za Damu salama nchini zitaimarika maradufu.

**Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa**

**107. Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua umuhimu wa huduma za uchunguzi katika tiba, Serikali imeendelea kuimarisha **huduma za uchunguzi wa Magonjwa** katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwekeza kwenye

maeneo makuu mawili ambayo ni **huduma za maabara** na **huduma za radiolojia**. Kwa upande wa huduma za maabara, hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya maabara zilizopo ni takribani 10,551. Kati ya hizi, Bodi ya Maabara binafsi imesajili maabara 4,026 ambapo maabara za kujitegemea (Autonomous) ni 1,266 na zilizojishikiliza kwenye vituo vya afya, Zahanati,kliniki na hospitali (Attached ) ni 2,760. Mwelekeo wa Wizara ni kuhakikisha maabara zote za binafsi na umma zinatambuliwa, kusajiliwa na kuingizwa mchakato wa kuimarisha ubora wa huduma za maabara kwa njia ya ithibati. Hadi sasa kuna jumla ya maabara 53 ambazo zimeshapata ithibatiya kimataifa, maabara zote za serikali katika ngazi ya Mkoa, Kanda, Maalum na Taifa zimepata ithibati ya kimataifa ambapo vipimo vinavyofanyika katika maabara hizi zinaaminika na kukubalika duniani kote. Wizara itaendelea kuzijengea uwezo maabara zilizobakia ngazi ya wilaya zile za binafsi na za umma kufikia viwango hivi vya Kimatafa. Katika kipindi hiki tayari tuna maabara 40 zimekidhi vigezo na ziko katika hatua mbalimbali za mchakato wa kupata ithibati kwa mwaka 2023 ili kutimiza viwango vya Kimataifa vya Ubora wa huduma na vipimo vya maabara. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa maabara ya Kibong'oto iliyozinduliwa na Mhe. Makamu wa Rais, tarehe 16 Julai, 2022. Umuhimu wa maabara hii ni kupima magonjwa ya kuambukiza yanayoathiri afya ya jamii ikiwemo ugonjwa wa Kifua Kikuu (TB).

**108. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Radiolojia nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, ambapo imefanikisha ununuzi na usimikaji wa vifaa vya Radiografia katika ngazi tofauti na kuboresha utoaji huduma kuanzia ngazi ya taifa mpaka ngazi za msingi. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wizara imenunua na kusimika **vifaa vya Radiolojia** katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini ambapo mashine za **MRI sita (6) zimenunuliwa** zenye gharama ya **Shilingi 14,534,624,000**. Kati ya hizo nne (4) zimeshasimikwa katika

Hospitali ya Taifa-MNH, Hospitali ya Taifa ya Saratani-Ocean Road, Hospitali ya kanda-CHATO na Hospitali ya kanda-MTWARA, usimikaji wa mashine moja (2) za MRI unatarajiwa kukamilika mwezi 30 June 2023.

**109. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha ununuzi wa **mashine za CT scan 32** zenye gharama ya **Shilingi 56,465,145,570,** ambapo CT Scan 24 tayari zimeanza kufanya kazi katika Hospitali za Taifa, Kanda, Maaalumu Rufaa za Mikoa na CT Scan 8 taratibu za usimikaji zinaendelea. Ununuzi wa mashine hizi umewezesha kuimarika kwa huduma za Radiolojia kwa kuwa na mashine za CT Scan 45 nchi nzima. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI iliratibu ununuzi wa **Digital XRay 199** zenye gharama **ya Shilingi 44,680,031,171** ambapo Digital X-Ray 168 zimeshasimikwa katika vituo mbalimbali zinaendelea kutoa huduma, usimikaji wa Digital X-Ray 31 bado unaendelea. Aidha, usimikaji utakapokamilika utawezesha Sekta ya afya kuwa na jumla ya **Digital X-Ray 346**

**110. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hichi, Wizara **imenunua Mini-Angio Suite moja (1)** yenye gharama ya **Shilingi 1,900,000,000** ambayo imefungwa katika Hospital ya Taifa ya Muhimbili – Upanga, na **echocardiography saba (7)** zenye gharama **ya Shilingi 805,000,000** ambazo zimefungwa katika Hospitali za Jakaya Kikwete Cardiac Institute (JKCI), Benjamini Mkapa Hospital, Hospitali ya kanda ya Ziwa – Bugando, Hospitali ya kanda kaskazini - KCMC, Hospitali ya kanda Mbeya, Hospitali ya Kanda ya Chato na Hospitali ya kanda Mtwara. Pamoja na mashine hizo, Wizara imenunua **Fluoroscopy mashine moja (1)** yenye gharama ya **Shilingi 725,000,000**, ambayo ipo kwenye taratibu za usimikaji, itafanya kuwe na jumla ya flourocopy mashine kumi (10) hapa nchini. Aidha, mashine za **Ultrasound 76** zenye gharama ya **Shilingi 4,695,000,000** zimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya

nchini. Ongezeko hili la ultrasound machine 76 linafanya sekta ya afya iwe na jumla ya **mashine za Ultrasound 552. Jedwali Na. 3** limeainisha idadi ya mashine zilizokuwepo zilizonunuliwa na jumla ya mashine zilipo hadi sasa.

**Jedwali Na. 3: Idadi ya mashine zilizokuwepo, mpya na jumla ya mashine**

| AINA YA MASHINE | ZILIZOKUWEPO | MPYA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| MRI | 7 | 6 | 13 |
| CT SCAN | 13 | 32 | 45 |
| MINI ANGIO SUIT | 4 | 1 | 5 |
| FLUOROSCOPY | 9 | 1 | 10 |
| DIGITAL X-RAY | 147 | 199 | 346 |
| ULTRASOUND | 476 | 76 | 552 |
| ECHOCARDIOGRAM | 95 | 7 | 102 |

**111. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa kwenye vifa, na vifaa tiba kama Mitambo ya huzalisha hewa tiba ya oksijeni, Mashine za CT scan, MRI, Digital X ray, huduma za dharura (EMD) na uangalizi maalumu (ICU). Katika kulinda uwekezaji huu, Wizara inaendelea **kuimarisha kitengo cha Wahandisi na Mafundi Sanifu wa Vifaa, Vifaa Tiba na Mitambo** ndani ya vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuajiri mafundi sanifu na wahandisi wapatao 150 katika ngazi mbalimbali. Wataalamu hawa wanapatikana katika ngazi za hospitali ya taifa, maalumu, kanda, rufaa za mikoa, halmashauri na taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Afya kama vile TMDA, MSD, Mkemia Mkuu,Maabara ya Taifa na Damu Salama kwa lengo la kusimamia ubora wa vifaa na miundombinu mingine yote. Aidha, Wizara imeanzisha Karakana katika kikanda 6 ambavyo vinaendelea na mafunzo mbalimbali kwa wataalamu hawa kuhakikisha pindi mashine zinapopata hitilafu wanaweza kushughulikia

kwa wakati na kupunguza adha kwa wagonjwa na watoa huduma.

**112. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa Mafunzo kwa wataalamu hawa kulingana na vifaa vilivyopo katika vituo wanavyo hudumu ikiwa ni Pamoja na CT scan, MRI na vifaa vya ICU na EMD vilivyonunuliwa ili kuhakikisha kunakuwa na uendelevu wa kuvidhumia vifaa hivi pale muda wa matazamio (warranty period) unapomalizika sambamba na mkataba wa manunuzi. Katika eneo la kusimamia ubora wa vifaa na vifaa tiba, tumeweza kuanzisha **mfumo wa kielekroniki wa menejimenti ya vifaa na vifaa tiba** (Medical Equipment and Infrastructure Management Information System – MEIMIS) ambao tunategemea utazinduliwa hivi karibuni ili uanze kutumika katika ngazi zote za vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Kupitia mfumo huu tunaweza kupata taarifa za vifaa vyote vilivyopo kituoni. Lengo la kuboresha huduma za uchunguzi na utambuzi wa magonjwa kuanzia ngazi ya msingi hadi Taifa ni kuimarisha huduma za matibabu sahihi kwa wagonjwa.

**UTOAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU**

**113. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia **utoaji wa huduma za matibabu** kwa wananchi ambapo, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya Wagonjwa 35,873,466 walipatiwa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ambapo wagonjwa 34,298,339 ni wa nje na wagonjwa 1,575,127 ni waliolazwa, ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2021/22 ambapo wagonjwa 33,688,803 walipatiwa huduma. Kati yao, wagonjwa 2,268,017 walipata huduma katika ngazi ya Taifa, Kanda na Maalum ikilinganishwa na wagonjwa 1,769,252 waliopata huduma katika ngazi hiyo kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, walioonwa katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa walikuwa Wagonjwa 2,529,971. Vilevile, Wagonjwa 31,075,478

sawa na asilimia 86.6 ya wagonjwa wote waliohudumiwa katika kipindi hiki walipata huduma katika ngazi ya Msingi (Primary health Care) kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 4**. Hii inamaanisha huduma zimesogezwa karibu zaidi na wananchi ambapo ndipo tunapopaswa kuweka nguvu kubwa.

**Jedwali Na. 4; Idadi ya wagonjwa katika vituo vya huduma za afya**

| Aina ya Kituo | Julai 2021 - Machi 2022 | | | | Julai 2022 - Machi 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **OPD** | **IPD** | **Total** | **%** | **OPD** | **IPD** | **Total** | **%** |
| Hospitali za Taifa, Kanda, Maalum | 1,596,778 | 172,474 | 1,769,252 | 5.3 | 1,899,417 | 368,600 | 2,268,017 | 6.3 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRH) | 3,734,847 | 250,322 | 3,985,169 | 11.8 | 2,253,991 | 275,980 | 2,529,971 | 7.1 |
| Hospitali ngazi ya Halmashauri | 5,458,779 | 578,851 | 6,037,630 | 17.9 | 7,819,361 | 544,794 | 8,364,155 | 23.3 |
| Vituo vya Afya | 6,424,102 | 378,111 | 6,802,213 | 20.2 | 6,591,701 | 377,022 | 6,968,723 | 19.4 |
| Zahanati | 13,766,427 | 10,125 | 13,776,552 | 40.9 | 13,549,308 | 8,696 | 13,558,004 | 37.8 |
| Kliniki | 1,317,987 | - | 1,317,987 | 3.9 | 2,184,561 | 35 | 2,184,596 | 6.1 |
| **Jumla** | **32,298,920** | **1,389,883** | **33,688,803** | | **34,298,339** | **1,575,127** | **35,873,466** | |

**114. Mheshimiwa Spika** Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Magonjwa ya nje (OPD) yameendelea kuchangia idadi kubwa katika magonjwa yote katika kwenye ngazi zote za vituo vya kutolea huduma. Aidha, huduma katika ngazi ya Afya msingi hususan Hospitali za Halmashauri zimezidi kuimarika ambapo asilimia 22.8 ya wagonjwa wa nje walihudumiwa katika Hospitali hizo ikilinganishwa na asilimia 16.9 ya wagonjwa wa nje waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 5**

**Jedwali Na. 5; Mchango wa idadi ya wagonjwa wa nje (OPD) kwa magonjwa yote katika ngazi za zote za huduma za afya**

| **Aina ya Kituo** | **Julai 2021 - Machi 2022** | | **Julai 2022 - Machi 2023** | |
|---|---|---|---|---|
| | **OPD** | **% OPD** | **OPD** | **% OPD** |
| Hospitali za Taifa, Kanda, Maalum | 1,596,778 | 4.9 | 1,899,417 | 5.5 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa (RRH) | 3,734,847 | 11.6 | 2,253,991 | 6.6 |
| Hospitali ngazi ya Halmashauri | 5,458,779 | 16.9 | 7,819,361 | 22.8 |
| Vituo vya Afya | 6,424,102 | 19.9 | 6,591,701 | 19.2 |
| Zahanati | 13,766,427 | 42.6 | 13,549,308 | 39.5 |
| Kliniki | 1,317,987 | 4.1 | 2,184,561 | 6.4 |
| **Jumla** | **32,298,920** | | **34,298,339** | |

**115. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 **magonjwa yaliyoongoza katika kuwaathiri zaidi wananchi (Top ten OPD)** na kuwasababishia kwenda katika vituo vya huduma kupata matibabu ni maambukizi katika mfumo wa hewa (asilimia 24), Maambukizi ya njia ya mkojo (asilimia 13), na Malaria (asilimia 7) ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2021/22 ambapo pia magonjwa yaliyoongoza yalikuwa; maambukizi ya mfumo wa hewa (asilimia 23), maambukizi ya njia ya mkojo yalikuwa (asilimia 13) na Malaria ilikuwa (asilimia 8). Aidha, **magonjwa yaliyoongoza Kulazwa (Top ten IPD)** ni Malaria (asilimia 11), Homa ya Mapafu (asilimia 10) na Anemia (asilimia 6.2) ikilinganishwa na na kipindi kama hicho mwaka 2021/22 ambapo Homa ya mapafu (asilimia 11.6), Malaria (asilimia 11.5) na Anemia (asilimia 6.4) kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 6** na **Na.7.**

**116. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje (OPD) wenye **umri chini ya miaka mitano** yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa (asilimia 37.3), Malaria (asilimia 10.69) na kuharisha pasipo kupungukiwa maji mwilini (asilimia 8.39). **Kwa umri wa miaka mitano na zaidi** magonjwa yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa (asilimia 18.8), Maambukizi katika njia ya mkojo (asilimia 16.1) na Malaria (asilimia 6.5). Magonjwa yasiyoambukiza yanaongezeka kwa kasi hadi kufikia kuwemo katika orodha ya magonjwa kumi yanayoongoza kusababisha watu kuhudhuria katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 8.**

**117. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, **magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa kulazwa (IPD)** kwa wenye **umri chini ya miaka mitano** yalikuwa ni homa ya mapafu (asilimia 25.5), Malaria (asilimia 19.18) na kuharisha sana (asilimia 13.8). Kwa upande wa wagonjwa walio na **umri wa miaka mitano na zaidi**, magonjwa yaliyoongoza yalikuwa ni Malaria (asilimia 13.8), Maambukizi katika njia ya mkojo (asilimia 9.77) na Shinikizo la juu la damu (asilimia 8.92), Kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 9** Katika kundi hili la wagonjwa, magonjwa yasiyoambukiza (NCD) yalikuwa ni chanzo cha watu kwenda kulazwa katika vituo vya kutolea huduma hali inayoashiria kukua kwa kiwango cha tatizo la magonjwa ya aina hiyo.

**118. Mheshimiwa Spika,** idadi ya **vifo vilivyotokea katika vituo vya huduma** vimeendelea kushuka ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya wagonjwa 40,878 walifariki dunia, ikilinganishwa na wagonjwa 45,895 waliofariki kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Katika kipindi hicho zaidi ya vifo 23,292 sawa na asilimia 57 ya vifo vyote vilitokea katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za mikoa na Hospitali za Wilaya na vifo 13,404 sawa na (asilimia 32.8) vilitokea katika ngazi ya Kanda, Maalum na Taifa kama

inavyoonekana katika **Jedwali Na 6**. Aidha, magonjwa yaliyoongoza kwa kusababisha vifo zaidi ni Homa ya Mapafu (asilimia 9.3), Neonatal Asphyxia (asilimia 6.6) na Shinikizo la juu la damu (asilimia 6.0) kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 10.**

**Jedwali Na. 6; Idadi ya vifo vilivyotokea katika vituo vya kutolea Huduma**

| AINA YA KITUO | Julai 2021 - Machi 2022 | % | Julai 2022 - Machi 2023 | % |
|---|---|---|---|---|
| Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Kanda | 15,369 | 33.5 | 13,404 | 32.8 |
| Hospitali RRH | 9,142 | 19.9 | 10,465 | 25.6 |
| Hospitali za Wilaya | 16,479 | 35.9 | 12,827 | 31.4 |
| Vituo vya Afya | 4,213 | 9.2 | 3,630 | 8.9 |
| Zahanati | 692 | 1.5 | 552 | 1.4 |
| Jumla | 45,895 | 100 | 40,878 | 100 |

**Huduma za Wagonjwa wa Dharura na Ajali**

**119. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukamilisha ujenzi wa **majengo 23** ya kutoa **huduma za dharura (EMD)** katika Hospitali Maalum, Kanda na Mikoa na kuziwekea vifaa na vifaa tiba. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya EMD 15 zilikuwa zimekamilika na zimeanza kutoa huduma. Kukamilika kwa ujenzi wa EMD kumeongeza idadi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, maalumu, na kanda zinazotoa huduma hiyo kutoka saba **(7)** mwaka 2020, nane **(8)** mwaka 2021 na kufikia **38** kipindi cha mwezi Machi 2023. Aidha naomba kutumia fursa hii kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Serikali ya awamu ya sita

imewezesha ujenzi wa majengo ya **EMD 80 katika ngazi ya Halmashauri.** Haya ni mapinduzi makubwa katika Sekta ya Afya hapa Tanzania tangu uhuru kwa Serikali kuweka mfumo madhubuti wa huduma za dharura kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya. Matokeo ya uwezekaji huu yatapunguza vifo ndani ya Hospitali kwa asilimia **40** na kuokoa maisha ya wananchi wanaohitaji huduma za dharura.

**120. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kukamilisha ujenzi wa **wodi 45** kwa ajili ya **wagonjwa mahututi na wanaohitaji uangalizi maalum (ICU)** katika Hospitali ngazi ya Taifa, Maalum, Kanda na Mkoa na kuziwekea vifaa na vifaa tiba, ambapo hadi kufikia Machi 2023 jumla ya **ICU 33** zilikuwa zimekamilika na zimeanza kutoa huduma. Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya ICU kutaongeza idadi ya vitanda vya ICU kutoka **vitanda 258** vilivyokuwepo na kufikia jumla ya **Vitanda 1,000** na uwekezaji huu utaokoa maisha ya wananchi wengi zaidi ndani ya Hospitali kwa asilimia 20 hadi 30.

**121. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya tathmini ya **magari ya wagonjwa (Ambulance)** nchini ambapo jumla ya **magari 595** kati ya **magari 761** yaliyopo yanafanya kazi na **221** yapo katika hatua mbalimbali za matengenezo. Serikali kupitia Wizara ya Afya na OR TAMISEMI imekamilisha ununuzi wa magari ya kubebea **wagonjwa 727** ambapo hadi sasa jumla ya **magari 77** yamewasili nchini. Uwepo wa magari ya wagonjwa (ambulance) utasaidia kusafirisha wagonjwa mbalimbali wakiwemo akinamama wajawazito kwa wakati kutoka Hospitali moja na nyingine. Magari haya yatasaidia huduma za uokoaji na huduma kwa wahanga wa ajali katika barabara kuu na kuwasafirisha kwa wakati huku wakipatiwa huduma wakati wakiwa njiani. Aidha, tathmini imefanyika kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi la maeneo korofi/tete kwa ajali katika Miko ayote nchini. Taarifa na utambuzi wa maeneo haya zitatumika kuboresha huduma za dharura na uokoaji kwa wahanga wa ajali.

**Udhibiti wa Magonjwa yasiyo ya Kuambukiza (Non Comunicable Desease-NCDs)**

**122. Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ulimwenguni kote ikiwemo Afrika na Tanzania kwa ujumla. Magonjwa haya ni pamoja na Magonjwa ya Moyo, Figo, Shinikizo la juu la damu, Saratani, Kisukari, matatizo sugu ya mfumo wa upumuaji, ajali (injuries), afya ya akili na madawa ya kulevya. Magonjwa haya yanabakia kuwa ndio sababu kuu ya madhara na vifo. Miongoni mwa vyanzo vikuu vinavyohusishwa na ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni pamoja na, **ulaji usiofaa, matumizi ya tumbaku, kutoshughulisha mwili (kazi zinazotumia nguvu) na matumizi ya pombe kupita kiasi.**

**123. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, magonjwa yasiyoambukiza ambayo yamesababisha wagonjwa wengi kuhudhuria vituo vya kutolea huduma za afya ni pamoja na **shinikizo la juu la damu wagonjwa 890,788** sawa na asilimia 3.8 ikilinganishwa na asilimia 3.6 kipindi kama hicho mwaka 2021/22 na **kisukari wagonjwa 436,232** sawa na asilimia 1.8 Aidha, takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi hicho, ugonjwa uliongoza katika kusababisha vifo vingi kati ya magonjwa yasiyoambukiza ulikuwa ni ugonjwa wa moyo ambao ulisababisha vifo 1,388 sawa na asilimia 6.0 ya vifo vyote, ikilinganishwa na asilimia 5.4 ya vifo vilivyosababishwa na ugonjwa huo kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hali hii inaonesha magonjwa yasiyoambukiza yasipodhibitiwa yanaweza kusababisha ongezeko kubwa la vifo nchini,

**124. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea **kutoa elimu kwa jamii** kuhusu namna bora ya kujikinga na Magonjwa yasiyoambukiza ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya **watumishi 1,690** katika vituo vya afya 497 vilivyopo katika halmashauri 120 wamepatiwa **mafunzo** kuhusu kugundua na kutibu magonjwa haya kwa ufanisi.

Lengo likiwa ni kuzifikia Halmashauri zote hapa nchini kufikia Desemba, 2023. Wizara imenunua na kusambaza mashine maalum ikiwemo Mashine 700 za Kupima shinikizo la damu, vifaa 700 vya kupima mapigo ya moyo, mashine 2,000 za kupima sukari, vifaa 700 vya uchunguzi wa saratani, mizani 700 za kupima uzito na urefu na vifaa vingine vya uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza kwenye ngazi ya msingi.

**125. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuwekeza na kuruhusu uwekezekaji binafsi katika huduma za kusafisha damu (hemodialysis) kwa wagonjwa wa figo. Hadi kufikia Machi,2023 idadi ya vituo vilivyosajiliwa vimeongezeka kutoka 44 hadi 62 ambapo kati ya vituo hivyo Hospitali zinazomilikiwa na Serikali ni 27, idadi ya mashine za kusafisha damu imeongezeka toka 633 hadi 742 na idadi ya wagonjwa wanaonufaika na huduma hii imeongezeka toka 2245 hadi kufikia 3252. Serikali inaendelea kutafuta namna za kupunguza gharama za huduma hii muhimu sambamba na kupanua huduma za upandikizaji wa figo ili kupunguza muda wa kusubiria upandikizaji na utegemezi wa kusafishishwa damu kwa wagonjwa hawa.

**126. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za macho** nchini ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya waalimu 158 wa shule za msingi wamepatiwa mafunzo ya kutambua Watoto wenye matatizo ya macho. Aidha, Waalimu hao wamefanya utambuzi wa awali kwa jumla ya Watoto 20,000 kati yao Watoto 3,000 walikutwa na matatizo ya macho yanayohitaji kutibiwa na wataalamu wa macho. Vilevile Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kuimarisha huduma za macho ikiwa ni pamoja na kununua vifaa na vifaa tiba, kusomesha wataalamu, kuimarisha miundombinu ili iwe rafiki kwa watu wenye ulemavu, uelimishaji wa jamii na kuendesha huduma za mkoba maeneo yasiyo na wataalamu. Wizara kwa kushirikiana na wadau wa macho imeendesha kambi kubwa 6 za huduma za kibingwa bobezi za macho kwenye

mikoa ya Lindi, Ruvuma, Tabora, Kigoma, Mwanza na Mbeya. Hadi kufikia Machi 2023 jumla ya wagonjwa 20,000 wamefanyiwa uchunguzi wa afya ya macho na 1,500 wamefanyiwa huduma ya upasuaji wa macho

**127. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha **huduma za Afya ya Kinywa na Meno** nchini. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Wizara imenunua na kusimika viti vya kutolea huduma za kinywa na meno 80 katika vituo vya kutolea huduma za Afya. Aidha, Serikali imeanzisha mafunzo ya Shahada ya Udaktari wa Kinywa na Meno (DDS) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Ndaki ya Mbeya ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa wataalamu waliobobea katika huduma za kinywa na meno. Vilevile, Serikali iliajiri watumishi 186 wa Afya ya Kinywa na Meno.

**Huduma za Afya Akili**

**128. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za afya ya akili** kwa kuendelea kujenga uelewa kwa jamii juu ya Afya ya Akili. Kazi kubwa iliyotekelezwa ni kuandaa Kongamano na Mdahalo wa Kitaifa wa Afya ya Akili mwezi Octoba 2022 wenye lengo la kuleta wataalamu mbalimbali na jamii kujadiliana juu ya masuala ya Afya ya Akili kwa jamii, watoto, vijana na makundi mengineyo. Jumla ya wananchi 1,155 walishiriki kwenye Kongamano na mdahalo, na washiriki 8,150 walishiriki kwa njia ya mtandao. Baada ya mdahalo huo, majukwaa huru matatu ya Afya ya Akili yameanzishwa kwa ajili ya kuendelea kutoa elimu kwenye jamii kuhusu Afya ya Akili na Dawa za Kulevya ambapo zaidi ya watu 10,000 wanashiriki kwenye kutatua changamoto za afya ya akili, ukatili na dawa za kulevya kupitia majukwaa hayo.

**129. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea **kuiwezesha Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe** ili kuendelea kutoa huduma bora za afya ya akili ikiwemo huduma za

uchunguzo na tiba ambapo katika kipindi hiki kiasi cha shilingi biioni mbili zimetolewa. Katika kipindi hiki jumla ya **wagonjwa 138,625 wa Afya ya Akili** walihudumiwa. Mwelekeo wa Wizara ni kukusanya takwimu za wagonjwa wa afya ya akili wanaohudumiwa katika vituo vingine vya kutoa huduma za afya vya umma na binafsi. Aidha katika kuongeza wataalam wa afya ya akili nchini, **Wizara inafadhili wataalam 10 katika ngazi ya ubingwa wa magonjwa ya afya ya akili wanaosoma MUHAS**. Vilevile Wizara inashirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kuanzisha Programu ya Sayansi ya Saikolojia (BSc. Psychology) ngazi ya shahada. Uzalishaji wa waatalamu hawa utatoa mchango mkubwa katika kuimarisha utolewaji wa afua mbalimbali za huduma ya Afya ya Akili hapa nchini. Wizara itaendelea kushirikiana na MUHAS ikiwemo kutafuta rasilimali fedha ya kufadhili wataalam zaidi.

**Huduma za Utengamao, Wazee na Tiba Shufaa**

**130. Mheshimiwa Spika,** katika kutambua uwepo wa watu wenye ulemavu hususan watoto, ongezeko la umri wa kuishi na kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Serikali imeanzisha sehemu mahsusi ndani ya Idara ya Tiba ambayo inaratibu utoaji wa huduma za utengamao, huduma shufaa na huduma kwa Wazee. Kwa upande wa **huduma za utengamao** kipaumbele kimewekwa katika utoaji wa huduma 5 za utengamao ambazo ni Tiba mazoezi (Physiotherapy), Tiba kwa njia ya kazi, Viungo saidizi, Tiba lugha na matamshi, na Tiba saikolojia). Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 huduma ya utengamao inayoongoza kutolewa ni Tiba mazoezi ambayo inatolewa katika Hospitali 33 ikifuatiwa na Tiba kwa njia ya kazi hospitali 12 na viungo saidizi hospitali 10. Hadi kufikia Machi 2023 kulikuwa na jumla ya watalaam 143 ambao wanafanya kazi katika hospitali za Kanda, Maalum na Taifa ambapo idadi kubwa ni kada ya Tiba mazoezi (92) ikifuatiwa na tiba kwa njia ya kazi (29). Serikali itaendelea

kuimarisha huduma hizi ili ziweze kuwafikia wananchi wengi zaidi kwa kuhakikisha uwepo wa wataalam, miundombinu (Rehabilitation Centres) na vifaa saidizi kwa ajili ya huduma za utengamao kwa kuanza na Hospitali za Rufaa za Mikoa 10. Ili kuendelea kuimarisha upatikanaji wa viungo saidizi, Wizara itaanza utengenezaji wa karakana tano (5) kwa ajili ya viungo saidizi katika hospitali za Rufaa za mikoa.

**131. Mheshimiwa Spika,** ili kutambua mapema watoto wanaozaliwa na ulemavu Wizara itaendelea kuhakikisha watoto wanakaguliwa ili kubaini aina yoyote ya ulemavu mara baada ya kuzaliwa kabla ya kupewa na kuweka viashiria mahususi vya ulemavu kwenye kadi ya mtoto kwa lengo la kubaini mapema. Aidha, katika mwaka wa 2023/24 Wizara itakamilisha kuandaa nyenzo za kukusanyia takwimu (MTUHA) za huduma za utengamao hususan kwa watoto na kujumuishwa katika mfumo wa DHIS2 pamoja na kuwafundisha namna ya kutumia nyenzo hizo watoa huduma katika hospitali zote zinazotoa huduma za utengamao.

**132. Mheshimiwa Spika,** katika kuendelea kuimarisha huduma za Utengamao na Huduma za shufaa nchini, Serikali kupitia Wizara imedhamiria kujikita zaidi katika kuhakikisha tunapata watalaam wenye sifa stahiki na hivyo mkakati wetu kwa mwaka huu ni kuongeza idadi ya watalaam wenye sifa stahiki katika maeneo hayo. Wizara yangu imewasilisha maombi rasmi kwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) ili Chuo hicho kianze rasmi programu maalum za mafunzo ya Shahada ya Kwanza ya Huduma za Tiba Mazoezi (BSc. Physiotherapy) na Mafunzo ya Shahada ya Kwanza ya Huduma za Tiba kwa njia ya Kazi (BSc. Occupational Therapy) na Shahada ya Kwanza ya Mafunzo ya Matibabu ya Usikivu matamshi na Lugha (BSc. Audiology, Speech and Language Pathology).

**133. Mheshimiwa Spika,** awali mafunzo tajwa hapo juu yalikuwa yanatolewa na chuo kimoja nchini ambacho ni Chuo Kikuu cha KCMC na hivyo kutokidhi uhaba mkubwa wa watalaam hao ambao wanahitajika. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa tayari MUHAS imefanikiwa kupata ridhaa ya Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kwa ajili ya kuanzisha programu hizo. Kwa sasa kuna wanafunzi 45 ambao tayari wanaendelea na mafunzo ya Shahada ya kwanza ya Tiba Mazoezi (BSc Physiotherapy) na katika mwaka huu wa fedha Wizara yangu imedhamiria kusomesha wanafunzi 10 kwa kila kozi na imetenga fedha hizo za masomo katika bajeti ya mwaka huu. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Afya pia inaendelea kushawishi wadau wengine kuunga mkono jitihada za Serikali za kusomesha wataalam wa huduma za utengamao hususan watoto.

**Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**

**134. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za tiba asili na tiba mbadala** ambapo awali kiwango kikubwa cha dawa hizi kilikuwa kinatumika bila ya kufanyiwa utafiti wa awali wa kisayansi. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) imeratibu utafiti wa usalama wa awali wa dawa 42 za tiba asili kwa ngazi ya Wanyama (pre-clinical study) kutoka kwa watengeneza dawa za asili 19 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2923. Matokeo ya utafiti huo yameonesha dawa aina 39 sawa na asilimia 92.3 zimekidhi vigezo vya awali vya kuwa salama kwa matumizi ya binadamu. Aidha, Wizara imeendelea kufanya tafiti mbalimbali za tiba asili kwa kushirikiana na vyuo vikuu vya ndani vikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kikuu cha tiba na sayansi Muhimbili, Chuo kikuu cha kilimo cha Sokoine na Chuo kikuu cha Nelson Mandela. Vilevile, Wizara imeboresha kiwanda cha kimkakati na maabara ya utafiti kilichopo NIMR-Mabibo Dar es Salaam kwa kununua mashine za kutengenezea dawa na vifaa vya maabara.

Kiwanda hiki kimeanza kufanya kazi na kitaboresha tafiti na uzalishaji wa dawa za asili zilizo bora.

**135. Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kuimarisha huduma za Tiba asili nchini, Wizara inaanzisha **Huduma Jumuishi za Tiba Asili** katika hospitali saba za Rufaa za Mikoa ya Rufaa za Mikoa ya Mwanza, Arusha, Tanga, Dar es salaam, Morogoro, Mbeya na Dodoma. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 watoa huduma 21 kutoka katika hospitali 7 za Rufaa za Mikoa wamepatiwa mafunzo ya jinsi ya kutoa huduma hizo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara kwa kushirikiana na watengeneza dawa 22; Taasisi za Utafiti, vyuo vikuu vya ndani vikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo kikuu cha kilimo cha Sokoine na Chuo kikuu cha Nelson Mandela; na Hospitali saba za Rufaa za Mikoa ya Mwanza, Arusha, Tanga, Dar es salaam, Morogoro, Mbeya na Dodoma imeendaa miongozo kuanzishwa kwa **Huduma Jumiushi za Tiba Asili** katika hospitali saba za Rufaa za Mikoa. Uanzishwaji wa huduma jumuishi za tiba asili katika hospitali za rufaa za mikoa utaboresha na kuimarisha huduma za tiba asili nchini ikiwa ni pamoja na tiba utalii. Wizara kwa kushirikiana na Vyuo vya Afya vya Kati vinne na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilitoa **mafunzo kwa waganga na watengeneza dawa** za asili 229 ya jinsi ya utoaji huduma, salama, utengenezaji wa dawa na umuhimu wa kusajili dawa husika ili kuweza kumlinda mtumiaji wa huduma za tiba asili.

## UIMARISHAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU YA KIBINGWA NA UBINGWA BOBEZI

**136. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya Kibingwa na Ubingwa bobezi nchini kwa kusogeza huduma hizi karibu na wananchi. Huduma hizi hutolewa na Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za kanda, Hospitali maalum na Hospitali za Rufaa za Mikoa. Katika Kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya

**wagonjwa 4,797,988** walihudumiwa katika hospitali hizi ikilinganishwa na **wagonjwa 5,754,421** waliohudumiwa katika hospitali hizi katika kipindi kama hiki mwaka 2021/22, idadi ya wagonjwa imepungua hali inayoashiria kuimarika kwa huduma za afya ngazi ya msingi hususani Hospitali za halmashauri. **Kiambatisho Na. 11** kimeainisha. Aidha katika kutekeleza sera ya matibabu sawa kwa wote, matibabu ya misamaha yenye thamani ya **shilingi 88,565,989,835** yalitolewa katika kipindi hicho, ikilinganishwa na misamaha yenye thamani ya **shilingi 38,942,930,007.19** iliyotolewa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na. 12.**

**137. Mheshimiwa Spika,** huduma za **utalii tiba** (Medical Tourism) zimeendelea kuimarika baada ya uamuzi wa Serikali wa kuendelea kuimarisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi hapa nchini na hivyo kuvutia wagonjwa kutoka nchi mbalimbali kufuata huduma hizo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya **wagonjwa 812** wamehudumiwa na Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda ukilinganisha na **wagonjwa 368** kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Wagonjwa hao walikuwa wanatoka katika nchi za Kenya, Uganda, Congo, Zambia, Comoro, Burundi, Rwanda, Zambia, Malawi, Msumbiji, DRC, South Sudani. Serikali itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma hizo na kuanzisha nyingine kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha utalii tiba katika nchi za Afrika.

**138. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusogeza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchi kwa kuendesha kambi mbalimbali za matibabu ya mkoba huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ikiwa ni pamoja na huduma za Ushauri, Upasuaji wa Matatizo mbalimbali, Macho, figo, kisukari, kinywa na meno, pua, na koo, mfumo wa mkojo, mifupa na meno, huduma za Moyo, Uchunguzi wa saratani ya matiti, tezi dume, mlango wa kizazi, chanjo ya homa ya Ini, huduma za TB, magonjwa ya watoto, magonjwa ya ndani,

afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya ubongo na mishipa ya fahamu na magonjwa ya masikio, pua na koo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya **wagonjwa 80,018** walihudumiwa kupitia mpango huo. Mpango huo umewezesha wananchi kupata huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kwa gharama nafuu. Serikali itaendelea kuimarisha huduma hizi ili ziweze kuwafikia wananchi wengi zaidi hasa wale wasiokuwa na uwezo wa kugharamia huduma husika.

**Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)- Upanga**

**139. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imetoa huduma kwa **wagonjwa 375,057** ikilinganishwa na **Wagonjwa 367,213** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Kati ya hao wagonjwa wa ndani (IPD) ni **35,745** na wa nje (OPD) ni **339,312.** Huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambazo zimetolewa na Hospitali katika kipindi hicho ni pamoja na Upandikizaji wa figo, Kusafisha damu na Upandikizaji wa vifaa vya usikivu. Katika kutekeleza Sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Hospitali ya Taifa Muhimbili imetoa **huduma za msamaha** zenye gharama ya **shilingi 12,804,756,748.34** kwa wagonjwa 47,390 kuanzia Julai 2022 hadi Machi, 2023 ikilinganishwa na gharama ya shilingi bilioni 14.1 kwa wagonjwa 46,591 kwa kipindi kama hicho Julai 2021 hadi Machi 2022. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha na uchangiaji wa gharama ni pamoja na usafishaji wa damu (Renal Dialysis), Huduma za ICU, Huduma za vipimo vya CT Scan na MRI pamoja na huduma za dawa. Aidha, katika kipindi hicho, Hospitali ilihudumia wagonjwa 333 ambao walitoka nchi mbalimbali ikilinganishwa na wagonjwa 353 katika kipindi kama hichi mwaka 2021/22.

**140. Mheshimiwa Spika,** hali ya upatikanaji wa dawa ilikuwa wastani wa asilimia 90. Hali ya upatikanaji wa damu katika Hospitali ilifikia wastani wa asilimia 82.9 ya mahitaji ikilinganishwa na wastani wa asilimia 74.6 kwa kipindi kama hiki mwaka 2021, Hospitali imetumia jumla ya shilingi bilioni 10.16 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 zilizotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vitendanishi.

**141. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeanzisha **Huduma mpya** ambazo ni pamoja na matibabu ya njia ya mirija kwenye kansa mbalimbali kwa mfano ya ini (trans arterial chemo embolization of liver tumor, TACE), kuchepusha damu iliyoshindwa kupita kwenye ini lenye unyafuzi (Trans jugular trans-hepatic portal systemic shunt, TIPS, in liver cirrhosis). Huduma nyingine ni ufunguaji wa mishipa iliyobana au kuziba iliyokua inatanuka kwenye usafirishaji wa damu (percutaneous transluminal angioplasty). Huduma hizi za tiba radiolojia zimeendelea kupunguza gharama za kusafirisha nje ya nchi kwa wagonjwa wanaozihitaji, ambapo kiasi cha shilingi Bilioni 19.9 ziliokolewa.

**142. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa huduma ya kibingwa bobezi **ya upandikizaji figo** (Renal Transplant) kwa wagonjwa wanne (4) kwa mwezi September na Oktoba 2022, na hivyo kufikia jumla ya **wagonjwa 72** tangu huduma hii ilipoanzishwa mwezi Novemba, 2017 kwa gharama ya shilingi 2,220,000,000 ambayo ni wastani wa shilingi milioni 30 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na huduma ya upandikizaji figo kwa mgonjwa mmoja nje ya nchi (India) kwa wastani wa shilingi 120,000,000. Hivyo wagonjwa 72 waliopata huduma hii katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wangegharimu shilingi 8,880,000,000 Kama wangetibiwa nje ya nchi. Kwa kuanzisha huduma hii hapa nchini Serikali imeokoa jumla ya shilingi 6,660,000,000 katika kipindi husika.

**143. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea na utoaji wa huduma ya **upandikizaji vifaa vya usikivu (Cochlear implant surgery)** kwa watoto tisa (9) ikilinganishwa na watoto watano (5) kwa kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Gharama ya huduma hiyo ni shilingi milioni 36 kwa mgonjwa mmoja nchini na nje ya nchi (India) huduma hii hugharimu shilingi milioni 100. Hadi sasa jumla ya wagonjwa 58 wamefanyiwa upasuaji kwa gharama ya shilingi bilioni 2.1 toka kuanza kwa huduma hii kutolewa hapa nchini. Kwa kuanzisha huduma hii hapa nchini Serikali imeokoa jumla ya shilingi bilioni 3.7 ambazo zingetumika kugharimia upandikizaji wa vifaa vya usikivu nje ya nchi.

**144. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Hospitali iliendelea kutoa huduma za maabara ambapo jumla ya vipimo 713,561 vimefanyika. Hospitali imeendelea kufanya maboresho ya kuongeza aina mpya ya vipimo vya damu vinavyohusiana na uchunguzi wa ugandaji wa damu. Vipimo vingine vilivyoongezeka katika kipindi hiki ni vile vinavyohusiana na uchunguzi wa saratani ya damu na uchunguzi kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo. Aidha, huduma za radiolojia zimeendelea kuimarishwa ambapo idadi ya huduma 49,222 zilifanyika katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023. Hili ni ongezeko kwa asilimia 32.5 ikilinganishwa na huduma 33,229 zilizofanyika katika mwaka 2021/22. Hospitali imeongeza wigo wa kutoa huduma za kichunguzi ambapo, huduma za kichunguzi bobezi kwa Mfumo wa fahamu, moyo na mishipa ya damu na huduma za kichunguzi kwa kina mama zilianza kutolewa kibobezi. Huduma ya kibingwa bobezi ya tiba radiolojia (Interventional Radiology) imendelea pia kuimarishwa ambapo aina ya huduma zitolewazo zimeongezeka kutoka 5 mpaka 12. Aidha, Hospitali iliendelea kutoa **huduma za mkoba** (outreach Program) katika hospitali za Rufaa za Mikoa za Hospitali ya Mwananyamala ambapo jumla ya wagonjwa 710 walihudumiwa na katika Hospitali ya Rufaa ya Tumbi walihudumiwa wagonjwa 863, huduma katika maeneo hayo

zilihusisha ushauri na upasuaji kama tiba ya matatizo mbalimbali.

**145. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **mafunzo ya kibingwa na kibingwa bobezi** kwa kushirikiana na wataalamu wabobezi kutoka nchi mbalimbali duniani ambao walishirikiana na wataalamu wetu wa ndani kufanya mafunzo kwa vitendo wa utoaji huduma za kiuchunguzi na matibabu katika kambi mbalimbali. Mafunzo hayo yaligharamiwa kwa ushirikiano kati ya hospitali ya Taifa Muhumbili na taasisi marafiki. Utaratibu huu wa kushirikiana na wataalamu bobezi umepanua wigo kwa wataalamu wa ndani ya nchi kujifunza na hivyo kupelekea wagonjwa wengi kutibiwa. Hii imezidi kuokoa fedha za kigeni ambazo zingetumika kupeleka wataalamu takribani 17 wa Muhimbili nje ya nchi kupata mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Aidha, hii imeifanya hospitali ya Taifa ya Muhimbili kuwa kituo cha ubora (Centre of excellence) kwenye tiba radiolojia ambapo mpaka sasa tumeweza kupokea jumla ya wataalamu 16, kumi na moja (11) kutoka ndani ya nchi (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Bugando, Benjamin Mkapa hospital) na watano (5) nje ya nchi (Uganda hospitali za Mulago na Makerere) kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi.

**146. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinakuwa endelevu, Serikali imeendelea kuhakikisha Hospitali inakuwa na wataalam mabingwa wa kutosha, ambapo katika kipindi hiki jumla ya wataalam wa ubingwa na ubingwa bobezi 8 wa fani za magonjwa ya afya ya watoto, magonjwa ya afya ya akili, magonjwa ya kinywa na meno, magonjwa ya ndani na wataalamu wa maabara waliajiriwa, na kufanya jumla ya wataalam hao kufikia 288, ambayo ni sawa na asilimia 71 ya mahitaji halisi kulingana na IKAMA. Hata hivyo, jumla ya wataalam 36 wanaosomea ubingwa na ubingwa bobezi wapo kwenye mafunzo ndani na nje ya nchi.

**Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila**

**147. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Hospitali imetoa huduma kwa jumla ya **wagonjwa 123,981** ikilinganishwa na **wagonjwa 91,744** waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kati ya wagonjwa hao, wa kulazwa (IPD) ni **9,875** na wagonjwa wa nje (OPD) ni **114,106**. katika kutekeleza sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Hospitali imetoa **huduma za msamaha** zenye gharama ya **shilingi 2,424,239,320** kwa wagonjwa 16,887 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.9 kwa wagonjwa 2,928 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha na uchangiaji wa gharama ni pamoja na usafishaji wa damu (Renal Dialysis), Huduma za ICU, Huduma za vipimo vya CT Scan na MRI pamoja na huduma za kulazwa. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 hali ya upatikanaji wa dawa ilikua wastani wa asilimia 90 ambapo Hospitali imetumia jumla ya shilingi bilioni 5.1 zilizotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na hali ya upatikanaji wa Damu katika Hospitali ilifikia wastani wa asilimia 71 ya mahitaji.

**148. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imetoa **Huduma mpya** za kibingwa na bingwa bobezi ambazo ni pamoja na kupunguza uzito kwa kuwekewa Puto (Intragastric balloon), ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Hospitali ilifanikiwa kutoa huduma hii kwa wagonjwa 87. Gharama ya kumpeleka mgonjwa mmoja nje ya nchi ni kati ya USD 6,000 hadi USD 15,000 ambapo Hospitali inatoa huduma hiyo kwa gharama ya shilingi milioni 4.2 tu. Aidha, Hospitali imeanza kutoa huduma ya matibabu ya kuondoa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mawimbi mshtuko (Extracorporeal Shock Wave Lithotripsy) ambapo hadi Machi 2023 jumla ya wagonjwa 380 walipatiwa

matibabu hayo. Hapo awali huduma hii ilikuwa ikipatikana nje ya nchi. Huduma zingine za kibingwa zilizoanzishwa ni upasuaji kwa njia ya tundu dogo.

**149. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ilifanikiwa kutoa **huduma ya upandikizaji wa uloto** (bone marrow transplant) kwa wagonjwa 11. Huduma hii ni mara ya kwanza kufanyika nchini na katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Gharama za kumpeleka mgonjwa mmoja nje ya nchi ni shilingi milioni 250 wakati katika Hospitali hii ni shilingi milioni 70 tu. Hivyo Hospitali imetumia shillingi milioni 770 na kama wangeenda nje ya nchi, Serikali ingetumia shilingi bilioni 2.75, hivyo jumla ya shilingi bilioni 1.98 zimeweza kuokolewa.

**150. Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha huduma kwa wagonjwa wenye matatizo ya ubongo na mishipa ya fahamu, Hospitali ya Taifa Muhimbili iliamua kuwahudumia wagonjwa hawa chini ya Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila na kuwapangia kazi madaktari bingwa na wabobezi wa fani hii. Utaratibu huu wa kutoa huduma mahsusi chini ya hospitali mahsusi na mabingwa/ wabobezi mahsusi ni msingi wa dhana ya Vituo vya Umahiri (Centres of Excellence) ambayo ndio dhana tunayoijenga kwa sasa katika utoaji wa huduma za kibingwa na kibobezi hapa nchini. Vituo hivi kwa mfano vya kutoa matibabu kwa wagonjwa wa kiharusi (Stroke Units) vitakuwa chachu ya kuboresha huduma za afya nchini kwa kuchochea matibabu bora, mafunzo mahiri na Utafiti utakaotoa majawabu yatakayoboresha huduma za afya nchini.

**151. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa huduma mbalimbali za uchunguzi za kibingwa ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya vipimo vya maabara 172,072 vilifanyika. Aidha, Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wagonjwa 84 kutoka nchi za Comoro, Kenya, Uganda, Korea, Canada, Misri na China walipatiwa huduma. Vilevile, Katika kipindi cha Julai 2022 hadi

Machi 2023, Hospitali ilitoa **huduma bobevu za mkoba** za upasuaji, macho, figo, kisukari, moyo, kinywa pua na koo (ENT), Mfumo wa mkojo (Urology), mifupa pamoja na meno. Huduma hizi zilitolewa katika hospitali za Parokia ya Kibamba, Hospitali ya Ndanda, Hospitali ya wilaya ya Mkuranga, Hospitali ya rufaa ya Mwananyamala, Tumbi na Temeke ambapo jumla ya wagonjwa **4,368** walipatiwa huduma hizi (Ndanda 1,302, Tumbi 863, Mwanayamala 710, Temeke 478, Mkuranga 615 na Kibamba 400).

**Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)**

**152. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Taasisi ilihudumia jumla ya **wagonjwa 93,017** ikilinganishwa na **wagonjwa 87,332** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) ni **89,725** na wagonjwa wa kulazwa ni (IPD) **3,292**. Huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambazo zimetolewa na Taasisi katika kipindi hicho ni pamoja na uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo, kufunga vifaa visaidizi vya moyo, kuzibua mishipa ya damu ya moyo na kutibu hitilafu ya mfumo wa umeme wa moyo.

Katika kutekeleza sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Taasisi imetoa **huduma za msamaha** zenye gharama ya **shilingi 521,962,007.69** kwa wagonjwa 1,167 ikilinganishwa na shilingi milioni 814.8 kwa wagonjwa 2,135 waliopewa msamaha katika kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha na uchangiaji wa gharama ni pamoja na ada ya kumuona daktari, vipimo vya maabara, upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo pamoja na malazi kwa upande wa wagonjwa mahututi. Hali ya upatikanaji wa damu katika Taasisi, imefikia wastani wa asilimia 100 ya mahitaji na hali ya upatikanaji wa dawa ilikuwa wastani wa asilimia 96.

**153. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeweza kufanya **upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua** na mishipa ya damu kwa wagonjwa 502, kati ya hao wagonjwa 397 walikuwa watu wazima na wagonjwa 105 walikuwa watoto. Watu wazima 170 wenye matatizo kwenye mishipa ya damu walifanyiwa upasuaji wa mishipa ya damu. Taasisi ilifanikiwa kufanya upasuaji mgumu ikiwa ni ishara ya kuimarika kwa uwezo wa waatalamu wetu katika utoaji huduma kwa magonjwa ya moyo. Taasisi ilifanya **upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo** kwa kutumia mtambo maalum "Catheterization Laboratory" ambapo **wagonjwa 1,069** walipatiwa matibabu ya moyo, kati ya hao 884 sawa na asilimia 82.6 walikuwa ni watu wazima na 165 walikuwa ni watoto sawa na asilimia 17.4.

**154. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imetoa huduma kwa wagonjwa 14 wenye shida ya mfumo wa umeme wa moyo kwa kutumia mtambo wa Carto 3 ambapo jumla ya shilingi bilioni 26 zimeweza kuokolewa kama wagonjwa husika wangepelekwa nje ya nchi kupata matibabu hayo ya moyo. Aidha, Taasisi imetoa **huduma za mkoba** ambapo jumla ya wagonjwa 5,101 katika mikoa ya Arusha (1,259), Dar es Salaam (1,969), Geita (513), Mtwara na Lindi (584) na Zanzibar (776) walifikiwa. Vilevile, Taasisi imetoa ufadhili wa masomo ya muda mrefu kwa watumishi 57, na masomo ya muda mfupi kwa watumishi 49, kati ya hao waliopewa ufadhili wa masomo ya muda mrefu wataalamu 20 wapo kwenye kozi za kibingwa na ubingwa bobezi.

**155. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki, Hospitali ilifanya **Utalii Tiba** ambapo ilihudumia wagonjwa 92, kutoka nje ya nchi, ikilinganishwa na wagonjwa 58 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2021/22, wagonjwa hao walikuwa wanatoka katika nchi za Burundi, Comoro, Rwanda, Uganda, Kenya, Cameroon na Zambia. Maboresho makubwa yanayoendelea kufanywa katika Taasisi hii umewezesha Serikali kupata ffedha za kigeni kwa kuhudumia wagonjwa

kutoka nje ya nchi. Aidha uhitaji wa matibabu ya Moyo umeongezeka na hivyo Serikali inaendelea na maandalizi ya upanuzi wa huduma hizo katika Hospitali ya Dar Group. Vilevile Taasisi ya Moyo inaendelea kuimarishwa ili iwe kituo cha mafunzo ya wataalamu wa upasuaji wa moyo kwa nchi jirani za Afrika.

**Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

**156. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Taasisi imehudumia jumla ya **wagonjwa 171,711** ikilinganishwa na **wagonjwa 154,260** waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kati yao, wagonjwa wa nje (OPD) ni **165,185** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni **6,526**. Aidha, katika kutekeleza sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Taasisi imetoa **huduma za msamaha** zenye gharama ya **shilingi 5,244,248,518** Kwa wagonjwa 2,869 ikilinganishwa na shilingi 7,102,362,612 zilitolewa kwa wagonjwa 2,156 mwaka 2021/22. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha na uchangiaji wa gharama ni Upasuaji, Mionzi (Radioloy), Malazi (Admission), Vipimo vya Maabara pamoja na Dawa. Hali ya upatikanaji wa dawa imefikia asilimia 96 ikilinganishwa na upatikanaji wa asilimia 87 kipindi kama hicho mwaka 2021/22, na hali ya upatikanaji wa damu salama ni asilimia 90.

**157. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Taasisi ilifanya upasuaji kwa wagonjwa 5,477 ambapo upasuaji wa mifupa mbalimbali ni wagonjwa 2,313, kubadilisha nyonga wagonjwa 145; upasuaji wa goti wagonjwa 124; upasuaji wa goti kwa kutumia matundu wagonjwa 228; upasuaji wa mfupa wa kiuno wagonjwa 77; upasuaji wa uti wa mgongo wagonjwa 277; upasuaji wa ubongo wagonjwa 160; watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi 364; upasuaji wa dharura 1,679. Vilevile, Taasisi imefanya upasuaji wa kunyoosha vibyongo (Scoliosis Surgery)

kwa watoto 23 na upasuaji wa kuondoa uvimbe ulio kwenye sakafu ya ubongo kupitia tundu la pua (trans-sphenoidal hypophysectomy) wagonjwa kumi na moja (11) na upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye mshipa wa damu kwenye ubongo (Aneurysm clipping) wagonjwa watano (5). Aidha, Taasisi imeendelea kutumia **Mtambo maalum wa kuchunguza na kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu (Angio – Suite),** ambapo katika kipindi hiki, jumla ya wagonjwa **94** walihudumiwa kwenye maabara hii na kuendelea kutoa matibabu ya kifafa (Epilepsy) kwa njia ya upasuaji. Uwepo wa mitambo huu umeimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi.

**158. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imetoa **huduma za mkoba** ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wateja 4,528 walipatiwa huduma hiyo katika Hospitali za Mikoa ya Mtwara, Lindi na Dar es Salaam. Aidha, Taasisi imefanya **Utalii Tiba** wagonjwa kutoka nchi za nje ikiwa ni pamoja na nchi za ukanda wa Bara la Afrika, ambapo kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Taasisi ilipokea jumla ya wagonjwa 176 ikilinganishwa na wagonjwa 162 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za
Kenya, Uganda, Congo, Zambia, na Comoro

**Taasisi ya Saratani Ocean Road**

**159. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Taasisi ilihudumia jumla ya **wagonjwa 43,922** ikilinganishwa na **wagonjwa 37,882** waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) ni **41,542** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni **2,380**. Huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambazo zimetolewa katika kipindi hicho ni pamoja na tiba mionzi (2D radiotherapy, 3D) conformal radiotherapy (3DCRT), Intensity Modulated Radiation Therapy (IMRT), brachetherapy, Tiba kemia (cytoxic targeted), na tiba nyuklia (radioactive Iodine). Katika kutekeleza sera ya kutoa huduma kwa njia ya

msamaha kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama za matibabu ya saratani, Taasisi imetoa **misamaha ya shilingi 37,293,822,470** kwa wagonjwa 13,740 ikilinganishwa na misamaha ya shilingi bilioni 13.9 kwa wagonjwa 2,792 iliyotolewa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni tiba mionzi, dawa za tiba ya saratani, uchunguzi wa maabara na radiolojia na huduma za kulaza wagonjwa Hali ya upatikanaji wa dawa za saratani ilikuwa wastani wa asilimia 100 ikilinganishwa na asilimia 98 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 na upatikanaji wa damu salama ni asilimia 72.

**160. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Taasisi imeanzisha **Huduma mpya** za wodi za wagonjwa mahututi (ICU) yenye vitanda 24, uchunguzi wa mashine ya MRI na digital x-ray; na huduma za tiba mtandao (Telemedicine). Aidha, Taasisi imeendelea kuimarisha huduma za maabara ambapo imepata ithibati ya Kimataifa ya SADCAS. Vipimo vya kawaida 162,665 na vipimo vya patholojia 1,002 vilifanyika, huduma za radiolojia zimeimarishwa ambapo vipimo 24,520 vya radiolojia vilifanyika, kati ya vipimo hivyo, vipimo 11,486 ni vya digital X-ray, 10,153 vya ultrasound, 2,390 vya CT Scan, 167 vya MRI na 324 vya mammograph. Vilevile, Huduma bobezi za uchunguzi na tiba nyuklia zimefanyika kwa wagonjwa 398 ambao walifanyiwa uchunguzi (diagnostic scans) katika mifupa, figo, ubongo, na tezi ya shingoni; na wagonjwa 37 walipatiwa tiba ya nyuklia. Taasisi ilitoa huduma ya tiba kemia kwa mizunguko 48,016 ikilinganishwa na mizunguko 46,443 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Taasisi ilitoa huduma ya tiba mionzi kwa wagonjwa 179,766.

**161. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imetoa **huduma za mkoba** katika eneo la huduma za uchunguzi wa Saratani ya matiti, Saratani ya mlango wa kizazi, ngozi, utumbo mpana na tezi dume; utoaji wa elimu juu ya umuhimu wa kupima Afya; utoaji

wa chanjo; na matibabu kwa waliogundulika kuwa na matatizo ya Saratani. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 mpango huu ulitekelezwa katika mikoa 8 ya Dar es Salaam, Dodoma, Tanga-Handeni, Katavi, Rukwa, Pemba, Unguja, na Kigoma ambapo wateja 12,732 walihudumiwa. Aidha, upande wa **Tiba Utalii** wagonjwa 152 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ukilinganisha na wagonjwa 148 waliopata huduma hiyo kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za Malawi, Kenya, Komoro, DRC, Msumbiji, Sudani ya Kusini, Zambia, pamoja na Uganda.

**162. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili iliendelea kutoa **mafunzo** kwa wanafunzi 46 wa Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Mionzi (Bachelor of Science in Radiation Therapy Technology), watumishi 36 wa Shahada ya Uzamili ya Onkolojia (Masters of Medicine in Clinical Oncology) na watumishi 12 wa Shahada ya Uzamili ya Uuguzi katika Onkolojia (Masters of Science in Nursing Oncology). Mafunzo haya yameongeza uwepo wa wataalamu wa huduma za saratani hapa nchini, kwa sasa Taasisi ina madaktari bingwa 37. Aidha, Taasisi iliwezesha mafunzo ya muda mrefu katika kozi za kibingwa na ubingwa bobezi kwa watumishi 23 katika program za uzamili na watumishi 2 katika program za uzamivu; kwa ufadhili wa Taasisi, Wizara na washirika wa maendeleo.

**Hospitali ya Benjamin Mkapa**

**163. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2023, Hospitali imeendelea kutoa huduma ambapo jumla ya **wagonjwa 178,299** wamehudumiwa na kupata matibabu ikilinganishwa na **wagonjwa 168,479** kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) ni **169,555** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni **8,744**. Wagonjwa wa **msamaha** walikuwa 2,200 ambao kiasi cha gharama zao

za msamaha ni **shilingi 244,555,860** ikilinganishwa na wagonjwa 2,228 waliotibiwa kwa msamaha wa shilingi 281,797,150 kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha na uchangiaji wa gharama ni Vipimo, Upasuaji, kumuona Daktari na Dawa. Aidha, Hospitali imeendelea kuboresha huduma zinazotolewa kwa kuongeza vifaa vya kisasa na wataalam wenye ujuzi, ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya vipimo vya maabara 141,957 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa. Jumla ya huduma za upasuaji 5,203 zilifanyika, sawa na ongezeko la asilimia 6.7 ikilinganishwa na huduma ya upasuaji kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Vilevile, Hospitali imetoa huduma ya upasuaji kwa kutumia tundu dogo kwa wagonjwa 723.

**164. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wagonjwa sita (6) walipata huduma ya upandikizaji wa Figo na kufikisha jumla ya wagonjwa 35 waliopata huduma hii toka Hospitali ilipoanza kutoa huduma za kupandikiza figo mwaka 2018. Gharama ya upandikizaji figo katika Hospitali ni kati ya shilingi milioni 22 hadi 35 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na shilingi milioni 75 hadi 100 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Pia, Hospitali iliweza kutoa huduma za ubingwa wa juu wa kutumia maabara maalumu (CathLab) kuchunguza na kutibu magonjwa ya moyo ambapo jumla ya wagonjwa 170 walinufaika na huduma hii, hivyo kufanya jumla ya wagonjwa 894 waliohudumiwa toka huduma hii ilipoanza kutolewa. Gharama ya huduma hii kwa wastani wa shilingi milioni 4.5 hadi shilingi milioni 6 hapa nchini ikilinganishwa na zaidi ya shilingi milioni 30 hadi milioni 40 nje ya nchi, hivyo uanzishwaji wa huduma hii umeokoa fedha za Serikali na kusaidia wananchi.

**165. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeanzisha **huduma ya uwekaji wa betri kwenye moyo** (Pace Maker) ambapo hadi kufikia Machi 2023, jumla ya wagonjwa **12** wamepatiwa

huduma hiyo. Huduma za upasuaji wa moyo (open heart surgery) zilianzishwa ambapo hadi sasa jumla ya watoto **18** wamefanyiwa upasuaji huo. Aidha, Hospitali imeanzisha huduma ya **Upandikizaji wa Uloto (Bone marrow Transplant)** iliyoanza mwezi Januari 2023 na hadi sasa wagonjwa watatu **(3)** wamepandikizwa. Huduma hii ya upandikizaji wa uloto inamwezesha mtoto mwenye ugonjwa wa sikoseli kutopata madhara yatokanayo na ugonjwa huu na hivyo kumwezesha kuishi maisha ya kawaida na kushiriki shughuli za kijamii.

**Hopitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

**166. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMH) inatoa huduma za matibabu ya kibingwa kwa magonjwa ya Akili, magonjwa ya mwili, pamoja na huduma za matibabu kwa waathirika wa dawa za kulevya. Hospitali ya Mirembe ina sehemu kuu nne (4) za kutolea huduma; Mirembe hospitali Kuu inayotoa huduma kwa magonjwa ya akili na huduma za matibabu ya magonjwa ya mwili; Sehemu ya Isanga inayohudumia wagonjwa wa akili wahalifu; na Sehemu ya Itega ambayo inatoa huduma kwa waathirika wa dawa za kulevya na Hombolo ambako wagonjwa waliokataliwa na jamii huendelea kupewa wanaendelea kujengewa uwezo wa kujitegemea na kuchangamana na jamii kwa kupitia tiba ya utengamao na tiba kwa njia kazi.

**167. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Hospitali ilihudumia jumla ya **wagonjwa 212,065,** kati yao **wagonjwa 138,625** sawa na **asilimia 65.3** walikuwa **wagonjwa wa Afya ya Akili** ikilinganishwa na **wagonjwa 131,711** ambapo kati yao wagonjwa **79,619** sawa na **asilimia 60.4** walikuwa wagonjwa wa afya ya akili waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021. Katika kipindi hichi, wagonjwa **104,400** walikuwa wagonjwa wa nje (OPD) na wagonjwa **107,665** walikuwa ni wagonjwa wa kulaza (IPD). Huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambazo

zimetolewa na Hospitali ni Magonjwa ya Mfumo wa Fahamu, Magonjwa ya kumbukumbu, Saikolojia, Magonjwa ya Afya ya Akili, Huduma za Afya ya Akili kwa Watoto na vijana, Magonjwa ya wanawake, Mifupa na Watoto.

**168. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Hospitali imetoa **huduma za msamaha** zenye gharama ya **shilingi 77,925,540** kwa wagonjwa 10,867. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha na uchangiaji wa gharama ni chakula kwa wagonjwa, Huduma za kulaza Wagonjwa, kumuona Daktari, Dawa, na Vipimo. Hali ya upatikanaji wa dawa muhimu na maalumu umeendelea kuimarika, ambapo, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 upatikanaji wa dawa muhimu umefikia asilimia 93 ukilinganisha na asilimia 65 iliyokuwepo kipindi kama hiki mwaka 2021/22.

**169. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Hospitali imeendelea kutekeleza **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wanafunzi 18,154 walipatiwa elimu kuhusu magonjwa ya afya ya akili katika shule mbalimbali za sekondari mkoani Dodoma. Aidha, Hospitali imeendelea kuboresha huduma za Afya ya Akili kwa kutoa elimu kwa jamii na matembezi na kufanikiwa kuwafikia Watanzania 25,564 katika Mkoa wa Dodoma. Vilevile, Hospitali imeendelea kuratibu **huduma za mafunzo** ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake kwa wizara kuendelea kudhamini watumishi katika fani mbalimbali za kibingwa katika vyuo vya ndani na nje ya nchi, ambapo jumla ya watumishi 14 wapo katika ngazi mbalimbali za masomo.

**Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto**

**170. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa huduma za tiba kwa wagonjwa ambapo jumla ya wagonjwa waliohudumiwa kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 ni

**wagonjwa 20,749** ikilinganishwa na **wagonjwa 26,884** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Kati yao, wagonjwa wa nje (OPD) ni **20,159** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni **590**. Aidha, Hospitali ilihudumia kwa **msamaha** jumla ya wagonjwa 4,544 kwa gharama ya **shilingi 38,096,276** ikilinganishwa na jumla ya wagonjwa 497 waliotibiwa kwa msamaha wa gharama ya shilingi 114,541,967 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni dawa, kumuona Daktari, huduma za maabara pamoja na huduma za mionzi. Hali ya upatikanaji wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI ni asilimia 100, dawa za matibabu ya Kifua Kikuu ni asilimia 100 kwa dawa za mstari wa kwanza na wa pili na dawa nyingine muhimu (essential medicine) ni asilimia 82 ikilinganishwa na asilimia 75 kwa mwaka 2021/22.

**171. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wenye Kifua kikuu ambapo, hadi kufikia Machi, 2023, jumla ya watu 932 waliokuwa wanahisiwa kuwa na TB walipimwa, kati yao 444 waligundulika kuwa na TB na 46 waligundulika kuwa na TB pamoja na HIV. Aidha, Hospitali imetoa **huduma za mkoba** kwa wagonjwa 1,198 ambapo kati yao, wagonjwa 106 waligundulika kuwa na TB, wagonjwa 6 waligundulika kuwa na HIV na wagonjwa 9 waligundulika kuwa na TB pamoja na HIV. Maeneo yaliyohudumiwa ni pamoja na jamii za wachimbaji wa madini katika Mkoa wa Manyara (Mererani na Simanjiro) na Simiyu (Simiyu, Shinyanga DC na Bariadi). Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mafunzo** ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake, ambapo jumla ya watumishi 9 (PhD 5, Masters 2 na Diploma 2) wamedhaminiwa na Hospitali katika Mafunzo hayo ndani na nje ya nchi.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya nyanda za juu kusini Mbeya**

**172. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Hospitali ilihudumia jumla ya **wagonjwa 262,496**

ikilinganishwa na **wagonjwa 237,186** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) ni **229,418** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni **33,078**. Aidha, katika kutekeleza sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Hospitali ilitoa **huduma msamaha** kwa jumla ya wagonjwa 90,493 kwa gharama ya **shilingi 6,689,061,150** ikilinganishwa na wagonjwa 18,547 kwa gharama ya shilingi 185,478,000 waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Huduma zilizoongoza kwa kutolewa misamaha ni huduma za kulazwa, kumuona Daktari, maabara na huduma za Afya ya uzazi na mtoto. Hali ya upatikanaji dawa muhimu imefikia asilimia 90 na upatikanaji wa Damu Salama umefikia asilimia 85.

**173. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Hospitali ilifanikiwa kuanzisha **huduma mpya** ya idara ya magonjwa ya damu (hematology) ikiwa ni pamoja na kliniki ya Hemofilia ambapo mpaka sasa kuna wagonjwa 322 wanaoendelea kufanyiwa matibabu. Hatua hii imewezesha wakazi wa Nyanda hizo kupata huduma hiyo ambayo hapo awali walikuwa wanaifuata Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, Hospitali imeendelea na huduma za kibingwa bobezi ambazo ni huduma za mapafu, kifua na njia ya hewa (Pulmonology) ambapo jumla ya wagonjwa 5,162 walihudumiwa; huduma ya magonjwa ya mishipa ya damu na moyo (Cardiology) wagonjwa 29,915; huduma za magonjwa ya ngozi (Dematology) wagonjwa 2,853; na huduma za upasuaji wa kichwa na mishipa ya fahamu (Neuro Surgery) wagonjwa 1,273. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenziwa Jengo la kutolea huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto – Meta na huduma zimeanza kutolewa. Kukamilika kwa jengo hili kutaongeza wigo wa upatikanaji wa huduma hizi katika Kanda ya Nyanda za juu Kusini.

**174. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 4,000 walihudumiwa.

Aidha, katika kuimarika kwa huduma za **tiba utalii**, hospitali ilipokea jumla ya wagonjwa 44 waliopatiwa huduma kutoka nchi za Malawi, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mafunzo** ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake, ambapo jumla ya watumishi 20 wamedhaminiwa na Hospitali katika mafunzo hayo ndani na nje ya nchi.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya ziwa Bugando**

**175. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Rufaa ya Kanda, Bugando imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa kutoka Mikoa nane (8) ya Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Kagera, Mara, Kigoma na Tabora. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi 2023, jumla ya **wagonjwa 334,847** walihudumiwa, ikilinganishwa na **Wagonjwa 291,837** waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) ni **310,618** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni **24,229**. Aidha, Hospitali ilitoa **huduma za msamaha** ambapo jumla ya wagonjwa 9,800 kwa gharama ya **shilingi 2,968,647,399** ikilinganishwa na wagonjwa 548 waliopata msamaha wa matibabu kwa gharama ya shilingi 308,651,412 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Huduma zilizoongoza kwa kutolewa misamaha zilikuwa ni Kujifungua, kusafisha damu, Dawa na mazoezi tiba. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 95 ikilinganishwa na asilimia 93 katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, hali ya upatikanaji wa damu ilikuwa asilimia 94.

**176. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wagonjwa 7,226 wamepatiwa huduma ya matibabu ya saratani, kati ya hao wagonjwa 2,028 walipatiwa tiba ya saratani kwa kutumia dawa (Chemotherapy) na wagonjwa 397 walipatiwa tiba kwa kutumia mionzi (Radiotherapy). Upatikanaji wa huduma hii umepunguza rufaa za wagonjwa wa saratani wa kanda ya

ziwa kwenda Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa zaidi ya asilimia 97. Aidha, Hospitali imeendelea kutoa huduma za Kibingwa kwa wagonjwa 6,422 kati ya hao, upasuaji wa moyo kwa kufungua Kifua 44, upasuaji wa ubongo 86 na upasuaji wa mifupa 5,894, upasuaji wa Fistula 185 na upasuaji wa mdomo sungura 213. Aidha, huduma za kusafisha damu (Renal Dialysis) zimeendelea kuimarika ambapo jumla ya wagonjwa 2,726 walipata huduma hii. Vilevile, huduma za kibingwa za Macho zimetolewa kwa watoto 14,978 na kati yao watoto 827 walifanyiwa upasuaji.

**177. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za Mkoba** ambapo jumla ya wagonjwa 308 walihudumiwa. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mafunzo** ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake, ambapo jumla ya watumishi 44 wamedhaminiwa na Hospitali katika Mafunzo ya Ubingwa na Ubingwa bobezi.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda – KCMC**

**178. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Hospitali ilihudumia jumla ya **wagonjwa 339,945** ikilinganishwa na **Wagonjwa 297,810** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021. Kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) ni **210,434** na wagonjwa wa ndani (IPD) ni **129,511**. Huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zilizotolewa na hospitali ya KCMC kwa kipindi hiki zilikuwa ni (Sikio, Pua na Koo), Upasuaji, Ngozi, na Saratani. Aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi ,2023, Hospitali imetoa huduma kwa wagonjwa wa **msamaha** 6,084 ambapo jumla ya **shilingi 19,189,800,400.00**, zimetumika, kati ya hizo shilingi 15,003,585,600.00 zimetumika kwa wagonjwa wa saratani. Kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 wagonjwa 5,514 walipewa msamaha ambapo jumla ya shilingi 17,089,808,730 zilitumika, kati ya hizo shilingi 9,447,785,700.00 zilitumika kwa wagonjwa wa saratani. Huduma zilizoongoza kutolewa kwa njia ya msamaha zilikuwa ni Saratani, Dawa, Vipimo na Kulazwa. Hali ya upatikanaji wa

dawa ni asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 97 kipindi kama hiki mwaka 2021/22 na hali ya upatikanaji wa damu katika hospitali ni asilimia 93 ya mahitaji.

**179. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** ambapo wagonjwa 873 walifanyiwa kipimo cha MRI, vipimo vya CT Scan wagonjwa 1,429, vipimo vya ultrasound wagonjwa 10,812, vipimo vya X-ray wagonjwa 19,948. Kwa huduma za matibabu wagonjwa 3,455 walifanyiwa upasuaji, matibabu ya Saratani 5,842, upasuaji wa njia ya mkojo 1,677, matibabu ya ngozi 8,763, na matibabu ya macho wagonjwa 14,805. Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wateja 3,384 walipatiwa huduma na kati yao wagonjwa 1,198 walihudumiwa katika huduma za saratani, macho na VVU/UKIMWI katika maeneo ya Rombo, Moshi DC, Marangu na Same. Aidha, Hospitali ilipokea jumla ya wagonjwa 308 waliotoka katika nchi za Kenya, Uganda na Congo na hii ni kutokana na uboreshaji wa huduma uliofanyika katika Hospitali. Vilevile, Hospitali imeendelea kuhakikisha inaboresha **huduma ya mafunzo** ambapo katika kipindi hicho, Wataalamu 64 wapo masomoni katika fani mbalimbali za Kibingwa ndani na nje ya nchi.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato**

**180. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Hospitali imeweza kuhudumia jumla ya **wagonjwa 16,433** ikilinganishwa na **Wagonjwa 5,607** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021. Kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) ni **13,681** na wagonjwa wa ndani (IPD) ni **2,752**. Aidha, Hospitali imetoa **huduma za msamaha** kwa wagonjwa 394 ambapo jumla ya **shilingi 44,355,199** zimetumika ukilinganisha na wagonjwa 181 ambao walihudumiwa kwa msamaha wenye thamani ya shilingi 5,611,220 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Huduma zilizoongoza kutolewa kwa njia ya msamaha zilikuwa ni Radiolojia, Maabara na Upasuaji mkubwa. Aidha, Hospitali

imeanza kutoa Huduma za kibingwa kwa Magonjwa ya wanawake na wajawazito pamoja na magonjwa ya kibingwa ya moyo. Huduma za CT Scan na MRI zimeanza kutolewa ambapo jumla ya wananchi 40 wamepewa huduma hiyo. Hali ya upatikanaji wa damu katika Hospitali ni asilimia 90 ya mahitaji na hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 94 ukilinganisha na asilimia 86 ya upatikanaji kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

**181. Mheshimiwa Spika,** katika kusogeza huduma za kibingwa karibu na wananchi, Hospitali ya Kanda ya Rufaa Chato iliendelea kutoa **huduma za mkoba** katika wilaya ya Kakonko Kigoma ambapo jumla ya wahitaji 233 walipatiwa huduma mbalimbali za kibingwa kulingana na uhitaji. Katika kipindi hicho, hospitali ilifanya **Tiba utalii** ambapo jumla ya wagonjwa 6 kutoka nje ya nchi. Aidha, Hospitali imeendelea kushirikiana na Wataalam mabingwa wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kuhudumia wagonjwa wa moyo katika Hospitali ya Rufaa ya kanda Chato ambapo, jumla ya wagonjwa 514 walihudumiwa kupitia kliniki ya magonjwa ya Moyo. Pamoja na wananchi kupata huduma hizo za kibingwa bobezi karibu na maeneo yao, ushirikiano huu unasaidia kuwapatia ujuzi na uzoefu wataalam waliopo katika Hospital ya Kanda ya Chato.

**182. Mheshimiwa Spika,** katika **huduma za mafunzo** jumla ya Madaktari tisa (9) wamefanikiwa kwenda masomo ya muda mrefu ya kibingwa. Pia watumishi 104 wamefanikiwa kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi kwa mchanganuo ufuatao; watumishi 40 wamepata mafunzo ya utumiaji wa ventilators, watumishi 30 wamepata mafunzo ya EMAT,watumishi 9 wamepata mafunzo ya Echocardiogram, watumishi 2 wamepata mafunzo ya kuchuja/kusafisha damu, watumishi 12 wamepata mafunzo ya kuhudumia wagonjwa wa mlipuko (Ebola), watumishi 2 wamepata mafunzo ya kuhudumia wagonjwa wa mifupa, watumishi 3 wamepata mafunzo ya kuhudumia Watoto wachanga (Neonatal Care), watumishi 6 wamepata mafunzo ya utumiaji wa mashine ya

MRI na CT Scan. Mafunzo hayo elekezi yamewaongezea watumishi ujuzi na ufanisi mkubwa wa kutoa huduma kwa wagonjwa na pia yamewapa motisha katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini - Mtwara**

**183. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Hospitali imehudumia jumla ya **wagonjwa 7,918** ikilinganishwa na **Wagonjwa 336** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2021. Kati yao, wagonjwa wa nje (OPD) ni **7,559** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni **359**. Katika kutekeleza Sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Hospitali imetoa **huduma za msamaha** zenye gharama ya **shilingi 1,689,500** kwa wagonjwa 24. Huduma zilizoongoza kwa kwa kutolewa msamaha ni huduma za dawa, vipimo, na upasuaji. Hali ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali ni asilimia 71 ikilinganishwa na upatikanaji asilimia 54 katika kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Hali ya upatikanaji wa damu katika Hospitali ni asilimia 96 ya mahitaji.

**184. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeanza kutoa **huduma mpya** za uchunguzi kwa kutumia CT Scan na MRI ambapo jumla ya wagonjwa 41 wamepatiwa huduma hiyo. Kuanza kutolewa kwa huduma hizo kumewapunguzia gharama wakazi wa Kanda ya Kusini, kwani hapo awali walilazimika kufuata huduma hizo Dar es Salaam. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo wagojwa 657 walipatiwa huduma ya matibabu ya mifupa na Wagonjwa 567 walipatiwa huduma ya matibabu ya Moyo.

**Hospitali ya CCBRT**

**185. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mashariki – CCBRT imeendelea kutoa huduma mbalimbali za Kibingwa, ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya **wagonjwa 90,577** walihudumiwa ikilinganishwa na **wagonjwa 82,437** waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka

2021/22, kati yao wagonjwa wa nje (OPD) ni **86,723** na wagonjwa wa ndani (IPD) ni **3,854**. Aidha, wagonjwa wenye **ulemevu** waliohudumiwa walikuwa **9,172** ikiwemo ulemavu wa macho, midomo wazi, miguu kifundo na ulemavu mwingine wa viungo, na kuvuja mkojo na haja kubwa kwa wanawake. Katika kipindi hicho, jumla ya wanawake wajawazito waliojifungua ni **413**, kati yao Wanawake **265** sawa na asilimia 64.5 walikuwa **wenye ulemavu**.

**186. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza sera ya kutoa huduma kwa njia ya msamaha na uchangiaji gharama za matibabu kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama hizo, Hospitali imetoa **huduma za msamaha** zenye gharama ya **shilingi 2,973,869,758** kwa wagonjwa 9,711 ikilinganishwa na gharama ya shilingi 1,691,316,934 kwa wagonjwa 10,849 kwa kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Upatikanaji wa dawa ulikuwa asilimia 96 na upatikanaji wa damu salama ulikuwa asilimia 100. Pia huduma za maabara na radiolojia zilipatikana kwa asilimia 100.

**187. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za Kibingwa** ambapo jumla ya wagonjwa 5,994 walifanyiwa upasuaji kati yao wagonjwa 4,041 walikuwa na matatizo ya macho; 240 fistula itokanayo na uzazi; wagonjwa 1,440 upasuaji wa mifupa; wagonjwa 273 walifanyiwa upasuaji wa mdomo sungura, wagonjwa 440 wenye miguu kifundo (Clubfoot) walitibiwa bila kufanyiwa upasuaji kwa kutumia njia ya Ponseti, wagonjwa 147 wenye matatizo ya figo walipata huduma ya dialysis na wagonjwa 653 walipata viungo saidizi (Orthosis 603 na Prosthesis 50). Aidha, Hospitali kupitia kitengo chake cha huduma za utengemao kilichopo Moshi (CCBRT Moshi Rehabilitation Centre) ilihudumia jumla ya wagonjwa 2,075.

**188. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa huduma za mkoba ambapo jumla ya wagonjwa 1,162 walihudumiwa. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa huduma za mafunzo ya

muda mrefu na mfupi kwa watumishi wake, ambapo jumla ya **watumishi 10** wamedhaminiwa na Hospitali katika Mafunzo hayo ndani na nje ya nchi

**Hospitali za Rufaa za Mikoa**

**189. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya **wagonjwa 2,529,971** walihudumiwa katika **Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa zinazomilikiwa na Serikali** ikilinganishwa na wagonjwa 3,985,169 waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa **2,253,991** na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa **275,980**. Aidha, katika kutekeleza Sera ya Afya ya kuhakikisha kuwa huduma za afya zinatolewa kwa makundi maalum, Hospitali za Rufaa zimeweza kutoa **huduma kwa msamaha** kwa wagonjwa 203,041 ikiwa ni asilimia 8 ya wagonjwa wote waliohudumiwa katika ngazi hiyo kwa gharama ya **shilingi 3,048,959,689.**
**Kiambatisho Na .13.**

**190. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuimarisha **upatikanaji wa huduma za Kibingwa** katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ili kufikia adhima ya kutoa huduma za Kibingwa kwa fani 14 (magonjwa ya wanawake na uzazi, magonjwa ya ndani, Afya ya watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo, afya ya macho, magonjwa ya Ngozi, huduma za dharura, utoaji wa dawa za usingizi na ganzi na radiolojia). Kwa kuanzia Serikali imeweka kipaumbele cha kuhakikisha angalau kila Hospitali inatoa huduma tisa (9) za Kibingwa za afya mama na uzazi, huduma za watoto, huduma za upasuaji, huduma za magonjwa ya ndani, huduma za upasuaji wa mifupa, huduma za kinywa na meno, huduma za magonjwa ya dharura na ajali, huduma za uchunguzi wa radiolojia, huduma za utoaji wa dawa za usingizi na ganzi. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Serikali imeweza kuongeza idadi ya Madaktari bingwa kutoka 274 mwaka 2021/22 hadi kufikia Madaktari bingwa 316

Machi 2023. Aidha, Hospitali za Rufaa za Mikoa 8 kati ya 28 zinatoa huduma saba (9) za Kibingwa ikilinganishwa na Hospitali 5 mwaka 2021/22. Kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 14 na Na. 15.**

**191. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za afya ya uzazi, Mama na Mtoto** katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, ambapo jumla ya **akina mama 66,577** walijifungua katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ikilinganishwa na **akina mama 67,908** waliojifungua katika hospitali hizi kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Aidha, katika kipindi hicho vilitokea jumla ya **vifo 213 vya akinamama** vilivyosababishwa na uzazi kwenye Hospitali hizi ikilinganishwa na **vifo 186** vilivyotokea kipindi kama hiki mwaka 2021/22. Kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 16.**

**192. Mheshimiwa Spika,** Hospitali zimeendelea kutoa **huduma za mkoba** ambapo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Hospitali za Rufaa za Mikoa zilitoa huduma za Kibingwa katika fani za magonjwa ya macho, magonjwa ya watoto, magonjwa ya ndani, upasuaji wa kawaida, afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, magonjwa ya kinywa na meno, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya ubongo na mishipa ya fahamu na magonjwa ya masikio, pua na koo. Jumla ya wagonjwa 41,457 walihudumiwa, kati yao 4,076 walifanyiwa upasuaji.

**193. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara iliweza kutekeleza **Huduma za Tiba Mtandao** nchini hivyo kuongeza Huduma na kwa sasa huduma hii imefikia Hospitali 35. Hospitali hizo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali maaalumu za Kitaifa (JKCI, ORCI, MOI) na Hospitali za Kanda (Bugando, Benjamin Mkapa, na Mbeya) na hospitali za Rufaa za Mikoa 21 ambayo ni Bombo-Tanga, Mt. Meru- Arusha, Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere-Musoma- Mara, Simiyu, Shinyanga, Sekou Toure- Mwanza, Bukoba- Kagera, Maweni- Kigoma, Geita, Sumbawanga-

Rukwa, Katavi, Kitete- Tabora, Singida, Iringa, Njombe, Songwe, Songea- Ruvuma, Ligula- Mtwara, Morogoro na Sokoine Lindi. Vilevile Hospitali za Halmashauri za Wilaya za Mafia, Nachingwea, Nyangao- Lindi Vijijini, Kilosa, TurianiMvomero, Nzega na Chato.

**194. Mheshimiwa Spika,** uwekezaji mkubwa wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi kwa Hospitali zilizoko pembezoni mwa nchi umefanyika kupitia Huduma za Tiba Mtandao. Hospitali hizo zimeweza kutoa Huduma za upigaji picha za CT, Digital X-ray n.k na kuweza kutafsiriwa na wataalamu waliopo ngazi ya juu (Teleradiolojia) na vilevile huduma za kuona wagonjwa wengine kwa njia ya mtandao zimeweza kutolewa (Teleconsultation) kwa magonjwa mbalimbali. Huduma hizi zimeweza kunufaisha wananchi takribani 1000 ambapo wameweza kubakia maeneo husika na kupata huduma za kibingwa bila kusafiri umbali mrefu na kuwapunguzia gharama.

**UTAYARI, UDHIBITI NA KUKABILIANA NA MAGONJWA HATARI YA KUAMBUKIZA NA MILIPUKO**

**195. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu na Sekta zingine imeendelea kusimamia, kuratibu na kutekeleza afua za kujiandaa na kukabiliana na magonjwa hatari ya mlipuko yanayoathiri afya ya Jamii ikiwemo UVIKO-19, Ebola, Marburg, Kipindupindu, Homa ya Mgunda. Wizara imetekeleza afua za kujiandaa na kukabiliana na magonjwa hatari ikiwemo kuhuisha **Mpango wa Dharura ya Afya wa Kukabiliana na Majanga** mbalimbali (Health Multi Hazard Emergency Preparedness and Response Plan), Mpango wa Kuzuia na Kujiandaa Kukabiliana na Tishio la Ugonjwa wa Ebola ambao uliripotiwa nchini Uganda, Mkakati wa Dharura na Kushiriki Kukabiliana na Mlipuko wa **Homa ya Mgunda** iliyotokea Mkoani Lindi katika Wilaya ya Ruangwa. Pia, Wizara imefanya tathmini (After Action Review) ya shughuli za kukabiliana na Homa ya Mgunda baada ya ugonjwa huo kuisha. Wizara

imesimamia **uanzishwaji wa vituo viwili (2) vya Operesheni ya Matukio ya Dharura (PHEOCs)** katika Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha na kufikia idadi ya vituo sita (6) na kutoa mafunzo kwa Wataalamu wa vituo hivyo. Aidha, kwa sasa Wizara inakamilisha uanzishwaji wa vituo vipya vitano (5) vya Operesheni ya matukio ya Dharura katika Mikoa ya Songwe, Dodoma, Katavi, Mtwara na Iringa ambapo vifaa vya TEHAMA kwa Mikoa hiyo vimepelekwa kwa ajili ya kufungwa ili kuimarisha ufanisi wa kukabiliana na dharura katika Mikoa hiyo.

**196. Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na janga la **ugonjwa wa UVIKO-19** ambalo limeathiri nchi nyingi Duniani, Wizara imeendelea kuratibu afua za kukabiliana na ugonjwa huu. Idadi ya wagonjwa waliopata ugonjwa wa UVIKO -19 katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 ni watu 2,590 kati yao wanne (4) walifariki. Ufuatiliaji wa wagonjwa wa UVIKO-19 unaendelea nchini kwa kupima wasafiri na watu mbalimbali wenye dalili ili kuwapa huduma mapema na kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza ikiwemo changamoto za upumuaji na kifo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya wasafiri 8,189,248 walikaguliwa ambapo 1,902,837 sawa na asilimia 23.2 ni wasafiri wa nje (International travelers) na 6,286,411 sawa na asilimia 76.8 ni wasafiri wa ndani (domestic travelers). Kati ya wasafiri walioingia nchini, wasafiri 35,604 walichunguzwa uwepo wa maambukizi ya UVIKO 19 kwa kutumia kipimo cha haraka (rapid antigen test) na kati yao, 106 walibainika kuwa na maambukizi na walishauriwa kujitenga katika maeneo waliyofikia ili kuzuia kueneza ugonjwa huo. Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya huduma za matibabu, Kukinga na Kudhibiti Maambukizo (Case management and IPC) kwa watoa Huduma wa Afya **2,253** dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 katika vituo vya kutolea huduma za Afya katika Mikoa yote nchini.

**197. Mheshimiwa Spika,** katika Kuboresha huduma za matibabu dhidi ya magonjwa hatari ya mlipuko, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeimarisha huduma za afya nchini hasa katika kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19, kwa **kuimarisha upatikanaji wa hewa tiba ya Oksijeni** kwa kusimika mitambo mipya 12 ya uzalishaji wa hewa tiba na hivyo kufanya jumla ya mitambo 19. Kusimikwa kwa mitambo hiyo kutapunguza gharama za kununua mtungi mmoja wa Oksijeni kutoka Shilingi 50,000 hadi Shilingi 25,000. Hii italeta pia unafuu kwa wananchi kwenye gharama za kuchangia huduma hiyo. Mitambo hii imesimikwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Dar es Salaa, Mtwara, Mbeya, Dodoma, Geita, Manyara, Ruvuma, Mwanza, Kigoma, Katavi, Songwe, Lindi, Morogoro, Njombe, Simiyu, Mara, Tabora, Rukwa na Shinyanga. Mitambo mingine ipo katika hatua za ununuzi ambapo inatarajiwa kusimikwa pindi itakapowasili. Hii itafanya mitambo hiyo ya Oksijeni kufikia Mitambo 55 katika ngazi ya Taifa, Kanda, Mikoa na Wilaya nchini. Uwepo wa mitambo hii umerahisisha upatikanaji wa hewa tiba hii katika vituo vya kutolea huduma na kupunguza gharama kwa asilimia 50 ya kununua mtungi mmoja wa hewa tiba ya oksijeni. Vilevile, Serikali imenunua na kusambaza mitungi mipya 16,000 katika vituo vya kutolea huduma nchini.

**198. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kuchukua **tahadhari ya Ugonjwa wa Ebola** tangu ugonjwa huo uliporipotiwa nchini Uganda tarehe 20 Septemba 2022, ambapo jumla ya wasafiri 19,561 waliotoka nchini Uganda walichunguzwa afya zao na hakuna msafiri aliyebainika kuwa na ugonjwa wa Ebola. Wizara ilifanya mikutano ya ujirani mwema na nchi ya Uganda, kusambaza vifaa kinga, dawa na kuweka miundombinu ya tahadhari ya tishio la kuingia kwa ugonjwa wa Ebola nchini. Aidha, Wizara iliendesha mafunzo kwa Maafisa Afya 48 katika Mkoa wa Kagera kuhusu usibuaji (Decontamination) na maziko salama (safe and dignified burial) endapo kungetokea kifo kutokana na ugonjwa wa Ebola. Katika kuongeza uwezo wa uchunguzi na uwasilishaji

wa taarifa kwa wakati Wizara ilisambaza vitendea kazi katika Ofisi za Afya mipakani, ambapo ofisi 42 zilipatiwa Laptops 40, Vishikwambi 80, printers 35 pamoja na vifaa 14 vya kisasa vya kupimia joto la mwili (thermoscanners). Aidha vifaa vya kudumu vya kunawia mikono (Mass Hand Washing Facilities) vimejengwa katika mipaka ya Tunduma na Kasumulu ili kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza katika maeneo ya mipakani.

**199. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani imetoa mafunzo maalum kwa watoa huduma za Afya **3,518** jinsi ya kuwahudumia wahisiwa wa magonjwa hatari ya kuambukiza ikiwemo Ebola katika Mikoa iliyopo kwenye hatari zaidi ya Kagera, Arusha, Mbeya, Songwe, Kilimanjaro, Dodoma, Dar es Salaam, Mara, Kigoma, Geita na Mwanza. Ambapo mafunzo yametolewa kwa wataalam wa Sekta mbalimbali zinazoshirikiana kukabiliana na magonjwa hatari ya kuambukiza kutoka ngazi zote nchini na jumla ya wataalam **132** wa mafunzo hayo maalum walihitimu.

**200. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufuatilia na kudhibiti magonjwa mengine ya mlipuko yaliyojitokeza ikiwa ni pamoja na **ugonjwa wa Kipindupindu**. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya visa 144 na vifo 4 vilitolewa taarifa katika Mikoa mitano (5) ambayo ni Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa, Manyara na Ruvuma. Aidha, kumekuwepo na kupungua kwa idadi ya wagonjwa na vifo ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2021/22 ambapo kulikuwa na visa 178 na vifo 5 ikiwa ni kupungua kwa visa hivyo kwa asilimia 19. Wizara imeelekeza nguvu zaidi katika Mikoa ya Kusini mwa nchi inayopakana na nchi jirani zenye mlipuko wa ugonjwa huu ili kuzuia maambukizi kutoka nchi za jirani yasiingie hapa nchini. Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Maji imezindua Mpango Shirikishi wa Taifa wa Kuzuia na Kukabiliana na Kipindupindu kwa kipindi cha

mwaka 2023 hadi 2027 ukiwa na lengo la ushirikiano wa Sekta mbalimbali katika kudhibiti na kupambana na Kipindupindu.

**201. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Ofisi ya Rais-TAMISEMI zimechukua hatua mbalimbali katika **kupambana na ugonjwa wa Kimeta** katika kuimarisha huduma za upimaji wa kimaabara na kuhamasisha uchanjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo ili kudhibiti ugonjwa kwa wanyama. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Mikoa ya Kilimanjaro, Songwe, Arusha na Rukwa imetoa taarifa ambapo jumla ya wagonjwa **270 na vifo vitatu (3)** viliripotiwa. Aidha, kwa milipuko yote hiyo, uchunguzi umefanyika na kuonesha kuwa vifo vilivyotokana na ulaji wa wanyama vimetokana na Ugonjwa wa Kimeta ndio sababu ya kuambukizwa ugonjwa huu. Wizara imeendelea kudhibiti Mlipuko wa **ugonjwa wa homa ya Mgunda** (Leptopirosis) ambao ulitolewa taarifa Mkoani Lindi katika Halmashauri ya Ruangwa mnamo mwezi Julai 2022 na kusababisha uwepo wa wagonjwa **20 na vifo 3.** Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake na Wadau iliweza kudhibiti mlipuko huo ambapo mpaka sasa hakuna visa zaidi vilivyotokea.

**202. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilitoa taarifa kwa umma juu ya uwepo **wa ugonjwa wa Marburg** mnamo tarehe 21 Machi, 2023 katika Wilaya ya Bukoba vijijini, Mkoani Kagera ambapo kulikuwa na visa tisa (9) na vifo sita (6). Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2023, hapakuwepo na mgonjwa mpya aliyethibitika kuwa na maambukizi ya Virusi vya Marburg wala kifo kipya. Kisa cha mwisho cha ugonjwa huu ni mgonjwa aliyeanza kuonesha dalili za ugonjwa wa Marburg tarehe 21 Machi, 2023. Wagonjwa wote 3 waliolazwa walipona na wamethibitishwa na vipimo vya maabara kuwa hawana tena virusi vya Marburg. Hata hivyo mgonjwa 1 kati yao bado anaendelea na matibabu ya changamoto zilizotokana na virusi vya Marburg. Vilevile jumla ya **watu 212** waliotangamana na wagonjwa, walitambuliwa na kufuatiliwa

kuona endapo wangekuwa wamepata maambukizi ili waweze kupata huduma mapema kabla hawajaambukiza wengine. Kati ya hao waliotangamana na wagonjwa hao, ni **watu 2** tu ambao walionyesha dalili na kuthibitika kuwa na maambukizi ambapo **1** alipona na mwingine ni kati ya waliopoteza maisha. Endapo hakutatokea mgonjwa mpya ndani ya siku 42 tangu mgonjwa wa mwisho kuthibitika kutokuwa na maambukizi ya Marburg, ugonjwa huu utatangazwa rasmi kuwa umekwisha nchini.

**203. Mheshimiwa Spika,** katika kutokomeza ugonjwa huu wa Marburg, Wizara kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali iliimarisha afua za kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa homa ya Marburg, ikiwa ni pamoja na kuimarisha upimaji wa sampuli za wagonjwa katika maabara tembezi iliyopo Mkoani Kagera, ufuatiliaji wa tetesi zenye viashiria vya uwepo wa wagonjwa wenye dalili zinazofanana na ugonjwa wa Marburg ili kubaini wagonjwa wapya na kuchukua hatua za kudhibiti mapema. Vilevile Wizara imeimarisha upimaji wa wasafiri katika mipaka yote ya Mkoa wa Kagera ambapo hadi tarehe 31 Machi 2023, jumla ya wasafiri **9,711** walipimwa na kupewa elimu juu ya kujikinga na ugonjwa huu. Afua nyingine ni pamoja na usibuaji wa maeneo mbalimbali ikiwemo vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilivyopokea wagonjwa na wahisiwa vya Ntoma, Ndolage, MFH Polyclinic, Bukoba ELCT, Maruku na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Bukoba. Kazi hii ni endelevu kwa maeneo yote ambayo wagonjwa/wahisiwa walikuwa wanaishi au walipita. Aidha, timu za usibuaji zimefanya usibuaji katika vyombo vya usafiri (ambulance) zilizobeba wagonjwa na wahisiwa, magari yaliyohusika katika mazishi pamoja na kuilinda jamii, kaya zote walizotoka wagonjwa na wahisiwa pia zilifanyiwa usibuaji.

**204. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa Jamii na kuchukua hatua za kuimarisha huduma za maji, usafi wa mazingira na usafi binafsi ili kusaidia jitihada za kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa Marburg katika vituo vilivyotengwa

kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa wa Marburg Mkoani Kagera. Wizara imeujengea uwezo Mkoa kwa kuendesha mafunzo kwa **Maafisa Afya 48** katika Mkoa wa Kagera kuhusu usibuaji (Decontamination) na maziko salama (safe and dignified burial). Mafunzo haya yamesaidia katika kufanya mazishi salama na yenye utu kwa jumla ya **watu 5** waliofariki kwa ugonjwa wa Marburg na kufanya usibuaji wa vituo vya afya vilivyotengwa kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa wa Marburg. Wizara imegawa vifaa vya kunawia mikono katika **maeneo 75** ambayo ni vituo vya kutolea huduma za **afya 19**, masoko **6,** mialo **6**, shule za msingi **15** na shule za sekondari **29** zilizopo katika Halmashauri za Manispaa za Bukoba na Bukoba vijinini ambapo wametoka wagonjwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Mkoa wa Kagera, imeendelea kusimamia udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za afya zinazozalishwa katika vituo vyote vyenye wagonjwa/wahisiwa kwa kuhakikisha zinakusanywa na watalaam waliopewa mafunzo na kuhakikisha zinateketezwa kwa kufuata miongozo na mikakati hii imeleta ufanisi mkubwa katika kudhibiti ugonjwa huo.

**205. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipelekea jumla ya **wataalam 53** Mkoani Kagera kutoka katika Mikoa mbalimbali ili kusaidia kutoa huduma wakati wa mlipuko wa Marburg ambapo **36** kati yao walisaidia kutoa huduma za kawaida katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ili kuchukua nafasi ya watumishi ambao walikuwa wamewekwa karantini kwa siku 21 wakifuatiliwa kulingana na miongozo ya Shirika la Afya Duniani.

**UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA**

**206. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Afya imeendelea kuhimiza na kufuatilia ubora wa huduma mbalimbali za afya zinazotolewa katika ngazi zote nchini. Wizara imeendelea kusisitiza vituo hivyo kuweka mazingira ya huduma kwa mteja (customer care) ambayo ni pamoja na kuweka vibanda au madawati mahususi ya maulizo, kupanga waongozaji

maalum (Niulize Mimi), kuweka vibao/ishara zinazoelekeza maeneo zinapopatikana huduma ndani ya vituo.

**207. Mheshimiwa Spika,** katika kumwezesha zaidi mteja awapo katika maeneo ya kupatiwa huduma; vituo vimeweka mabango yanayoainisha haki na wajibu wa mteja, gharama za huduma, mazingira wezeshi ya upatikanaji huduma mahususi kwa wenye mahitaji maalum, madawati maalum ya jinsia na visanduku ya kutolea pongezi na malalamiko pamoja na namba za simu za viongozi wa vituo ambazo mteja ana uhuru wa kupiga endapo anahitaji msaada. Mfano, kwa baadhi ya Hospitali zetu kubwa uongozi hupata mrejesho kutoka kwa wateja kupitia njia za mitandao kama vile mfumo wa kielektroniki wa e-mrejesho  na njia za kikundi-sogozi cha whatsapp  cha wateja na uongozi wa Hospitali hizo. Pamoja na jitihada zilizofanyika za kuboresha huduma za afya kwa wateja wetu, Wizara inatambua kuwa ubora wa huduma ni suala endelevu na linahitaji miongozo, ushirikiano toka kwa wateja na watoa huduma na tathmini za mara kwa mara.

**208. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea na utaratibu wa kufanya **ukaguzi wa kimatibabu (clinical audit)** na **ukaguzi wa bidhaa za afya (health commodity audit)** ili kubaini hali halisi na maeneo yanayohitaji maboresho kulingana na miongozo na mahitaji ya wananchi.  Aidha, kwa mwaka 2022/23 ukaguzi wa kimatibabu umeonesha ubora wa huduma umeimarika kutoka **asilimia 45** (mwaka 2021/22) hadi **asilimia 58** (mwaka 2022/23) katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa. Wizara imeongeza wigo wa ukaguzi kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa hadi Hospitali za umma na binafsi katika ngazi ya Taifa, Kanda, Maalum na hospitali za Halmashauri.

**209. Mheshimiwa Spika,** kwa kupitia Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watoa huduma kwenye eneo la huduma kwa mteja ikiwa ni pamoja na kuwasisitiza kutoa huduma kwa weledi, lugha za staha na kufariji, kutoa mrejesho kwa mteja, kujali muda wa

mteja na pia kuzingatia miiko na maadili ya taaluma zao. Wizara imetambua na kutoa tuzo kwa watumishi wanaofanya vizuri katika eneo hili na kutoa adhabu kwa watumishi na vituo vinavyofanya vibaya ikiwemo kufuta leseni au usajili wao.

**210. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakiki ubora wa huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi, Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imefundisha jumla ya wajumbe 432 wa Timu za Uendeshaji Afya za Mikoa (RHMTs) na Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri (CHMTs) kuhusu namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki wa kufanyia usimamizi shirikishi katika maeneo yao ya usimamizi. Lengo la mfumo huu ni kurahisisha utendaji na ufuatiliaji wa karibu wa maazimio baada ya usimamizi.

**211. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilifanya ukaguzi wa maeneo ya upimaji VVU katika Mikoa 14 (Songwe, Njombe, Katavi, Mbeya, Rukwa, Shinyanga, Tabora, Mwanza, Mara, Dar es Salaam, Morogoro, Simiyu, Geita, na Kagera) ili kuhakikisha ubora wa huduma za vipimo vya virusi vya UKIMWI (VVU) kwa kipimo cha haraka (HIV Rapid Tests) unazingatiwa. Jumla ya maeneo 1,163 kwenye vituo 702 vya kutolea huduma za afya yalifanyiwa ukaguzi. Maeneo 916 sawa na asilimia 79 yalifikia kiwango cha daraja la 4 (asilimia 90 na zaidi) na hivyo kuwa na sifa ya kupewa cheti cha ubora. Maeneo ambayo hayakufikia daraja la 4 yanaendelea kufanya maboresho kupitia msaada wa kitaalamu kutoka kwenye RHMTs na CHMTs, pamoja na wadau wa utekelezaji kwenye mikoa husika.

**212. Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya jitihada mbalimbali katika kuimarisha ubora wa huduma ikiwemo mafunzo kazini (mentorship) ili kuwajengea uwezo watumishi katika kuzingatia miongozo ya utoaji wa huduma za afya katika ngazi mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya watoa huduma 6,679 wamepatiwa mafunzo kazini ya kuzingatia miongozo ya kukinga na kudhibiti maambukizi. Pamoja na hili, Wizara inaandaa Mwongozo wa

Usalama kwa Mteja (Patient Safety Guideline) kwa lengo la kuimarisha usalama wa huduma kwa wagonjwa.

**213. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa miongozo na viwango vya kukinga na kudhibiti maambukizi na usalama wa huduma kwa mteja. Katika kutekeleza hili, Wizara ilijikita katika afua kuu tatu ambazo ni tathmini ya uwezo wa vituo vya afya katika kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza, kufundisha watumishi wa afya jinsi ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa afua za kukinga na kudhibiti maambukizi, na kuendelea kupambana na usugu wa vimelea dhidi ya dawa. Jumla ya vituo 91 vya kutolea huduma kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi ya afya ya msingi vilifanyiwa tathmini ambapo wastani wa utekelezaji ni asilimia 60 ikiwa ni ongezeko kutoka asilimia 43 mwaka 2021/22. Vilevile, watoa huduma 3,131 walipatiwa mafunzo kazini ya jinsi ya kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa viwango vya kukinga na kudhibiti maambukizi. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha ufuatiliaji wa afua za kukinga na kudhibiti maambukizi kwa kuwajengea uwezo watoa huduma 937 kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara wa namna ya kutumia nyenzo za ufuatiliaji taarifa za viashiria vya kukinga na kudhibiti maambukizi.

**214. Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Serikali za kuimarisha ubora wa huduma zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara pia inakamilisha andiko litakalotoa mwongozo wa utoaji wa huduma bora nchini utakaoakisi ule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) utakaozingatia mila na desturi za kitanzania.

**HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA**

**215. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha **huduma bora za Uuguzi na Ukunga** zinatolewa katika ngazi zote Wizara ilianzisha Idara ya Huduma za Uuguzi na Ukunga kwa lengo la kusimamia ubora wa huduma za uuguzi na ukunga katika ngazi zote za kutolea huduma kwa kuzingatia kuwa huduma

za Afya zinatolewa na kada hii kwa asilimia 80 kwa sasa kuna wauguzi bingwa **267** ambao wamesaidia sana kutoa huduma bobezi na za kibingwa za uuguzi na ukunga. Wizara imetekeleza afua mbalimbali za kuboresha huduma hizi kwa **kufanya mafunzo ya utoaji huduma katika vyumba vya upasuaji** (Theatre Management) na utoaji wa huduma ya msingi ya dharura kwa mama na mtoto mchanga aliyepata changamoto wakati na baada ya kujifungua (Basic Emergency Obstetric and Neonatal Care) ambapo jumla ya wauguzi viongozi **326** walipatiwa mafunzo haya. Aidha, Wizara imeendelea kuhakikisha wateja wanapata huduma bora na kuzifanyia tathmini huduma hizi kwa kuandaa mwongozo unaoelekeza kutoa huduma bora na zenye staha (Respectiful and Compassionate Care and Customer Care) na kutengeneza viashiria vya kumpima muuguzi alivyomhudumia mgonjwa na pia kupata maoni ya mpokea huduma alivyohudumiwa, kwa kipindi hiki tumeshatoa mafunzo haya kwa wauguzi na wakunga wapatao **2,384**. Pia tumeweka kwenye mitaala ya kufundishia kwenye vyuo vikuu vya Uuguzi na Ukunga vya KCMC, Bugando na MUHAS pamoja na kujengea uwezo Wakufunzi 35 ili wanafunzi wanaomaliza shahada ya kwanza ya uuguzi na ukunga wawe wamepata mafunzo haya.

**216. Mheshimiwa spika**, ili kuhakikisha miongozo ya kutoa huduma za Uuguzii na Ukunga inazingatiwa Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa kimatibabu kwa huduma za Uuguzi na Ukunga ambapo hospitali zote za ngazi ya mkoa, kanda, maalum na taifa zilifanyiwa ukaguzi. Aidha hospitalli za Halmashauri kwa mikoa nane (8) pia zilikaguliwa. Kwa hospitali za Rufaa Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa kiwango cha ubora wa huduma za Uuguzi kiliongezeka kutoka asilimia 43 (2021/22) mpaka asilimia 47 (2022/23) na huduma za Ukunga kutoka asilimia 61 (2021/22) mpaka asilimia 66. (2022/23). Aidha, wastani wa kiwango cha ubora wa huduma za Uuguzi kwa Hospitali za Halmashauri ni asilimia 29 na huduma za Ukunga asilimia 63. Viwango hivi bado haviridhishi

pamoja na uwepo wa hali ya kuimarika ubora kwani lengo ni kufikia asilimia 90, hivyo Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi hasa kwa ngazi ya msingi, kujenga uwezo kwa wauguzi na wakunga nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa miongozo.

**217. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za ushauri nasaha upimaji wa VVU na kuanzisha dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati na kutoa rufaa katika ngazi zote kwa kuwatumia wauguzi na wakunga katika ngazi zote (Nurse Initiated Management of AntiRetroviral) mpaka sasa wauguzi na wakunga wapatao 2,880 wamepatiwa mafunzo. Kupitia afua hii huduma hizo zimewafikia wahitaji wote kwa kuwa zinatolewa na wanataaluma hawa ambao wanakuwa vituoni saa 24 katika siku zote 7, Aidha, upimaji wa VVU umeongezeka kutoka asilimia 70 mwaka 2017 hadi asilimia 95 (2022), Uanzishwaji wa dawa umeongezeka kutoka asilimia 39 mwaka 2017 kufikia asilimia 76 mwaka (2022) kwa wagonjwa walioanzishiwa dawa na wauguzi, huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto zimeongezeka kutoka asilimia 39 hadi asilimia 96 mwaka 2022 Afua hii ya NIMART imekuwa nguzo muhimu kufikia malengo ya 95-95-95 kama nilivyoainisha hapo awali katika mwaka 2022.

**RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA**

**218. Mheshimiwa Spika,** pamoja na uboreshaji mkubwa uliofanyika katika eneo la miundombinu ya kutolea huduma za afya kuanzia katika majengo, upatikanaji wa dawa na vifaa vya uchunguzi, Wizara ya afya inatambua kuwa uwepo wa watoa huduma za afya wenye ujuzi na weledi wa kazi ni moja ya nguzo muhimu inayohitajika kwa ajili ya kuwa na mfumo imara na wenye ufanisi kwa ajili ya utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi. Lengo hilo litawezekana iwapo vyuo vya afya vitaendelea kuzalisha wataalam wenye ujuzi na weledi pamoja na kuajiri watumishi wa kutosha katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Wizara kwa kushirikiana

na wadau wa maendeleo itaendelea **kuweka mazingira mazuri na yenye kuvutia kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuandaa mwongozo wa motisha wa kuwabakiza watumishi wa Sekta ya Afya** katika maeneo yao ili kuendelea kutoa huduma za afya kwa wananchi. Pamoja na mwongozo huo, Wizara inawaelekeza waajiri mbalimbali kuweka mazingira mazuri yatakayo wavutia na kuwabakiza watumishi wa Sekta ya Afya kama vile kujenga nyumba za makazi karibu na maeneo ya kutolea huduma, kununua vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuwahudumia watumishi, kutoa posho za masaa ya ziada na za kuitwa kazini (Oncall Allowance) na kuwaendeleza watumishi hao ili wabaki katika maeneo yao kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi.

**Watumishi na Ajira katika Sekta ya Afya**

**219. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2023, Sekta ya Afya ilikuwa na jumla ya **watumishi wa afya wapatao 109,616** ambao ni sawa na **asilimia 50.04** ya watumishi wote **219,061** wanaohitajika katika sekta ya afya kulingana na IKAMA iliyoidhinishwa. Kati ya watumishi hao, watumishi 86,431 sawa na asilimia 78.8 wapo katika ngazi ya msingi na watumishi 23,185 sawa na asilimia 21.2 wanafanya kazi katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa.

**220. Mheshimiwa Spika,** moja ya sababu kubwa inayosababisha upungufu wa watumishi ni pamoja na kasi kubwa ya ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa uchumi isiyoruhusu kuajiriwa kwa watumishi wanaokidhi mahitaji halisi. Sababu nyingine ni pamoja na kuongezeka kwa huduma za kibingwa na kibobezi, upanuzi wa huduma za afya katika ngazi za vituo vya afya kwa kuweka huduma za CEmONC, ongezeko la vyuo vya afya hususani kwa kada za ngazi ya kati. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na TAMISEMI imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuona namna ambavyo changamoto hii

inaweza kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Katika kuziba pengo la watumishi wa afya, Serikali imetoa kibali cha kuajiri jumla ya watumishi wa afya 8,317 ambapo Ofisi ya Rais TAMISEMI imepokea kibali cha kuajiri watumishi 8,070 katika ngazi ya msingi na watumishi 247 katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Kanda na Mikoa.

**221. Mheshimiwa Spika,** hatua nyingine zinazoendelea kuchukuliwa ili kukabiliana na uhaba wa watumishi ni pamoja na; kutekeleza Mwongozo wa ajira za mikataba ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani, kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika Sekta ya Afya kwa kuwashawishi kutumia sehemu ya rasilimali fedha zinazotumika katika kutekeleza programu mbalimbali kugharamia ajira za muda mfupi kwa wataalam wa afya; na kuendelea kufanya uchambuzi wa uzito wa majukumu dhidi ya idadi ya watumishi kwa kila kituo na hatimaye kuwa na uwiano sahihi. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya **wataalamu 8,992** waliajiriwa kwa utaratibu huu ambapo 4,183 waliajiriwa kwa mikataba kupitia mapato ya ndani ya vituo vya kutolea huduma na 4,809 kupitia wadau wa maendeleo.

**Uzalishaji wa wataalam wa afya – Kada za kati**

**222. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya nchini vinakuwa na watumishi wenye ujuzi na weledi. Katika kuhakikisha hilo Wizara imeendelea kusimamia vyuo vilivyopo chini ya Wizara na vyuo binafsi ili kuhakikisha vinazalisha wataalam wenye ujuzi unaotakiwa. Aidha, katika kusimamia uendeshaji wa vyuo ngazi ya kati, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ilifanya udahili wa wanafunzi wapya 37,941 ambayo ni sawa na asilimia 61.9 ya wanafunzi 61,276 walioomba nafasi katika vyuo hivyo. Kati ya wanafunzi 37,941 waliochaguliwa, wanafunzi 4,768 sawa na asilimia 12.6 walichaguliwa kwenye vyuo vya afya vya Serikali na wanafunzi 33,173 sawa na

asilimia 87.4 walichaguliwa kwenye vyuo binafsi na taasisi za dini katika programu mbalimbali.

**Ufadhili wa Masomo**

**223. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufadhili wanafunzi na wataalam wa afya katika kada mbalimbali za kitabibu, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na zinazotolewa na watoa huduma wenye ujuzi wa kutosha. Katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchi, Wizara imeanzisha mkakati mpya uitwao **Samia Health Super Specialization Program** wa kutoa ufadhili kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa utaratibu wa **set.** Utaratibu huu unahusisha kusomesha timu za wataalamu wanaohitajika kwa ajili ya kukamilisha utoaji huduma za kibingwa na bobezi baada ya kuhitimu mafunzo hayo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Serikali imetoa ufadhili wa masomo kwa fani mbalimbali na ngazi tofauti kutegemeana na mahitaji na uwezo wa kifedha. Jumla ya **watumishi 981**, wanaochukua mafunzo ya uzamili katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi walipata ufadhili wa masomo; kati yao 802 ni vyuo vya ndani na 179 ni mafunzo nje ya nchi. Tunamshukuru **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kutoa fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 8** kwa ajili ya mafunzo ya wataalamu bingwa na bobezi nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imetoa ufadhili wa wanafunzi 287 wa fani ya uuguzi na ukunga katika ngazi ya Stashahada.

**224. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa mitaala inayotumika kufundishia katika vyuo inaenda na wakati na inakidhi mahitaji ya kipindi husika, Wizara ya Afya imekuwa ikipitia mitaala hiyo mara kwa mara na kuifanyia marejeo. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 imefanya marejeo ya mitaala ya fani mbalimbali, ambapo mtaala wa kada ya Fiziotherapia umefanyiwa marejeo kwa kuhusisha wataalam mbalimbali wa eneo husika, lakini pia Wizara

inaandaa mitaala ya Astashahada na Stashahada katika fani za Radiolojia; na Tiba Lishe (Clinical Nutrition) ili kuongeza wataalamu hao kwenye utoaji huduma za afya katika kukabiliana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza (NCDs).

**Usimamizi wa mafunzo endelevu (CPD)**

**225. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha mafunzo endelevu (Continuous Professional DevelopmentCPD) kwa watumishi wa Sekta ya Afya yameendelea kutolewa ili kuongeza ujuzi na ubora katika utoaji huduma za afya. Jukumu hili limefanywa kwa kushirikiana na mabaraza ya kitaaluma yanayosimamia mafunzo husika kwa mujibu wa Sheria na Miongozo ya Mabaraza hayo. Aidha, Wizara inatambua changamoto ya uhaba wa watumishi, hivyo ili kupunguza au kuepuka watumishi kuondoka kwenye vituo vyao vya kazi kwa ajili ya kwenda katika mafunzo endelevu (CPD), Wizara imeanzisha mfumo maalumu wa mafunzo kwa njia ya kielektoniki yaani National e-learning Platform. Mfumo huu unatumiwa na watumishi walioko makazini wanaotaka kujiendeleza kupitia moduli za mafunzo zilizopo kwenye mfumo huo. Jumla ya moduli **191** zimeandaliwa na kupakiwa kwenye mfumo kati ya hizo moduli **94** zimeandaliwa na kupakiwa kuanzia mwezi Julai, 2022 had Machi, 2023. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023 watumishi waliotumia mfumo huo kujiendeleza ni **99,952** ambapo watumiaji wapya kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023 ni **6,854**.

**UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA**

**226. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha Watanzania wote wanakuwa na **uhakika** wa kupata huduma za Afya pindi wanapozihitaji bila ya kikwazo cha fedha, Wizara iliwasilisha Bungeni Muswada wenye lengo la kutunga sheria itakayowataka **Watanzania wote kujiunga na Bima ya Afya** ambapo Muswada huo ulisomwa kwa mara ya kwanza mwezi Septemba, 2022 katika Mkutano wa 08 wa Bunge. Aidha, Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya ulipangwa

kusomwa kwa mara ya pili na tatu katika Mkutano wa 09 na 10, hata hivyo haukusomwa kutokana na kuwepo kwa masuala mahsusi yaliyohitaji kufanyiwa kazi na Serikali. Majadiliano ndani ya Serikali yatakapokamilika Muswada huo utawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kusomwa mara ya pili na ya tatu kwa tarehe itakayopangwa. Vilevile, wananchi wanaendelea kuelimishwa kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya ili wahamasike na kujiunga katika mifuko ya bima ya afya iliyopo.

**227. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha mapitio ya **mwongozo wa bei** wa uchangiaji gharama za huduma za Afya katika Vituo vya umma vya utoaji huduma za Afya. Mwongozo huo umeainisha bei za huduma mbalimbali ambazo wananchi wasio na Bima watapaswa kuchangia kupitia utaratibu wa papo kwa papo. Aidha, bei hizo zimejumuisha ngazi zote za utoaji huduma kuanzia katika ngazi ya afya ya Msingi hadi Taifa. Kukamilika kwa mwongozo huo kutawapunguzia wananchi mzigo wa matibabu na kuwepo kwa bei ambazo ni sawa kwa nchi nzima kwa ngazi ya utoaji huduma inayofanana ambapo kutawaondolea adha ya kutojua gharama za matibabu au kutozwa fedha zaidi ya matibabu yaliyotolewa.

**MIRADI YA MAENDELEO**

**228. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara imeendelea na ukamilishaji wa miradi ya maendeleo katika Vituo vya kutolea huduma za Afya. Aidha, katika miradi 209 inayoendelea kutekelezwa kwa awamu mbalimbali, Miradi 29 inatekelezwa kwa fedha za ndani, miradi 150 inatekelezwa kwa kutumia fedha za UVIKO -19 na miradi 7 inatekelezwa kupitia fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo. Kati ya miradi hiyo, miradi 30 inatekelezwa katika Hospitali ya Taifa, Maalumu na Kanda, miradi 142 inatekelezwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, miradi sita (6) inatekelezwa katika vituo maalumu vya kutolea huduma za afya, miradi minne (4) inatekelezwa katika Vyuo vya Afya

pamoja na ujenzi wa Jengo la Wizara katika Mji wa Serikali-Mtumba.

**229. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2023, katika Miradi 29 inayotekelezwa na Fedha za Ndani, miradi minne (4) imekamilika kwa asilimia 100, miradi 10 imefikia asilimia 80 hadi 99, miradi 12 ipo chini ya asilimia 80 huku miradi mitatu (3) utekelezaji wake haujaanza kufanyika. Kwa upande mwingine kati ya miradi 150 inayotekelezwa kupitia fedha za UVIKO-19, miradi 107 imekamilika kwa asilimia 100, miradi 36 imefikia wastani wa asilimia 80 hadi 99 na miradi saba (7) ipo chini ya asilimia 80. Vilevile, miradi 7 inayotekelezwa na Wadau wa Maendeleo, miradi minne (4) imekamilika kwa asilimia 100, miradi mitatu (3) imefikia wastani wa asilimia 80 hadi 99. Taarifa ya kina ya utekelezaji wa miradi hiyo imeambatishwa katika taarifa hii
**Kiambatisho Na. 17**

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**230. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Sura 395 kwa lengo la kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watumishi wa Umma na wategemezi wao. Sheria ya Mfuko imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali ili kuwezesha kupanua wigo wa walengwa kwa kuingiza makundi mbalimbali. Kufuatia marekebisho ya sheria ya Bima ya Afya, Mfuko unajumuisha watumishi katika Sekta ya Umma, wafanyakazi kutoka katika Sekta Binafsi, na makundi mbalimbali katika Sekta zisizo rasmi.

**231. Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Kisheria ya Mfuko ni pamoja na Kuandikisha wanachama, Kukusanya michango na kuitunza, Kusajili watoa huduma na Kufanya malipo kwa watoa huduma za afya. Majukumu mengine ni Kuwekeza

fedha za ziada katika vitega uchumi mbalimbali, kufanya kaguzi kwa waajiri na watoa huduma, Kufanya tathimini ya uhai wa Mfuko na kutoa elimu kwa Umma. Katika Kipindi cha Julai hadi Machi 2023 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulitekeleza yafuatayo;

**232. Mheshimiwa Spika,** kipindi hicho, Mfuko ulikuwa na lengo la kusajili wanachama wapya 536,657 ambapo ulifanikiwa kusajili wanachama wapya 576,509 sawa na asilimia 107 ya lengo ikilinganishwa na asilimia 100 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Idadi hiyo ya wanachama waliosajiliwa, imewezesha Mfuko kuwa na wanachama wachangiaji 1,327,001 na wanufaika 4,921,040 sawa na asilimia 8 ya Watanzania wote. Aidha, mfuko umeendelea kuongeza mtandao wa vituo vya kutolea huduma za afya, ambapo hadi Machi, 2023, ulikuwa umesajili jumla ya vituo 8,965 ikilinganishwa na vituo 8,883 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Vituo hivyo ni vya ngazi na umiliki mbalimbali wa watoa huduma mijini na vijijini ambavyo hutoa huduma za matibabu kwa wanachama na wanufaika wa Mfuko. Kati ya vituo hivi, vituo vya Serikali ni 6,400 sawa na asilimia 71, vituo vya Mashirika ya Dini ni 824 sawa na asilimia 9 na vituo vya watu binafsi ni 1,741 sawa na asilimia 19.

**233. Mheshimiwa Spika,** Mfuko umeendelea kutoa mchango katika uchangiaji wa gharama za matibabu katika Sekta ya Afya ambapo, kwa mwaka 2021/22 Shilingi bilioni 674.25 zililipwa kwa watoa huduma ikilinganishwa na Shilingi bilioni 540.55 mwaka 2020/2021. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, jumla ya Shilingi bilioni 557.82 zililipwa kwa vituo vya kutolea huduma za afya, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 382.14 zilizolipwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Takwimu zinaonesha kuwa, fedha za NHIF kwa sasa zinachangia wastani wa asilimia 80 ya mapato ya vituo vya afya nchini. Aidha, katika kipindi husika, Mfuko umelipa madai kwa wastani wa siku 49 ambazo ni ndani ya matakwa ya Sheria, lengo ni kufikia wastani wa siku 45.

**234. Mheshimiwa Spika,** Mfuko umeanzisha mfumo wa uwasilishaji na uchakataji wa madai kwa njia ya Kielektroniki kwa lengo la kuhakikisha madai ya watoa huduma yanalipwa kwa wakati. Hadi kufikia Machi 2023, jumla ya watoa huduma 180 kati ya 780 wa hospitali ngazi ya Wilaya, Rufaa za Mikoa, Kliniki za Kibingwa, Rufaa Kanda na Rufaa Taifa waliosajiliwa na Mfuko wanaotarajiwa kutumia mfumo huu kwa awamu ya kwanza walikuwa wamejiunga. Aidha, matumizi ya mfumo huu yataongeza ufanisi katika eneo la madai ya watoa huduma na udhibiti wa vitendo vya udanganyifu dhidi ya Mfuko.

**235. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha uboreshaji wa huduma za matibabu nchini, Mfuko unatoa **mikopo nafuu** ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa vituo. Tangu kuanzishwa kwa mpango huo, jumla ya **vituo 399** vilipatiwa mikopo hiyo, ikilinganishwa na vituo 369 vilivyofaidika na utaratibu huu kwa kipindi kama hicho mwaka 2022 ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 40.85** zilitolewa kwa vituo vilivyokidhi vigezo. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi, 2023, Shilingi bilioni 2.85 zilitolewa kwa vituo 20 vilivyokidhi vigezo. Utaratibu huu umesaidia kujenga uwezo wa vituo katika kutoa huduma bora za afya kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

**236. Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kuimarisha uhai na uendelevu wa Mfuko, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya imefanya tathmini ya wanufaika wa huduma zitolewazo kwa kundi la watoto walio chini ya miaka 18, ambao hupata huduma kupitia Mpango ujulikanao kama Toto Afya Kadi. Mpango huu ulianzishwa mwaka 2016 ukiwa na lengo la kusajili angalau asilimia 10 ya watoto milioni 25 waliokuwepo kwa kuzingatia sensa ya watu ya mwaka 2012. Hadi kufikia mwaka 2020/21, Mfuko ulikuwa umesajili watoto 205,796 ambao michango yao ilikuwa ni **shilingi bilioni 5.99** na matumizi yao ni **shilingi bilioni 40.58** sawa na uwiano wa **asilimia 677.** Kulingana na tathmini hiyo, kundi hili limekuwa likipata huduma zaidi katika vituo vinavyomilikiwa na Sekta

Binafsi ikilinganishwa na umma, na kupelekea Mfuko kulipa asilimia 58 ya fedha zote ikilinganishwa na asilimia 22 iliyolipwa kwa Mashirika ya Dini na asilimia 20 kwa vituo vya Serikali, kwa magonjwa kama malaria, kikohozi na homa, ambayo yangeweza kutibiwa katika vituo vya ngazi ya chini.

**237. Mheshimiwa Spika**, kutokana na tathmini hii, ni wazi kuwa kundi hili lina matumizi makubwa na hivyo kutishia uhai na uendelevu wa Mfuko endapo hatua hazitachukuliwa. Hivyo, kuanzia mwezi februari 2023, utaratibu wa kuandikisha kundi hili kwa mtoto mmoja mmoja umesitishwa na msisitizo kuwekwa katika usajili kupitia vifurushi ambavyo vina utaratibu wa kusajili katika ngazi ya familia. Vifurushi hivi vijulikanavyo kama Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya vinatoa fursa kwa familia kusajiliwa kulingana na ukubwa wake pamoja na kipato. Aidha, watoto hawa wanaweza kusajiliwa kupitia shule wanazosoma, lengo ikiwa ni kusajili watoto wengi kwa umoja wao kulingana na misingi na dhana ya bima. **Nitoe rai kwa wananchi wote kutumia fursa hii kwa kuandikisha familia zao mapema na wasisubiri kuugua na ndipo wajiunge, jambo ambalo ni kinyume na dhana ya bima.**

**238. Mheshimiwa Spika,** Mfuko umeendelea kuimarisha mapambano dhidi ya Udanganyifu ambayo kwa kiasi kikubwa hufanywa na baadhi ya watoa huduma wasio waaminifu, wanachama na waajiri. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Aprili 2023, Mfuko ulifanya chunguzi **311** za matukio ya viashiria vya udanganyifu. Kutokana na chunguzi hizo na kupitia taratibu zake za ndani, Mfuko ulibaini madai yasiyo halali ya **shilingi bilioni 9.74** kutoka kwa watoa huduma mbalimbali yaliwasilishwa na kulipwa na Mfuko. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2023, kiasi cha **shilingi bilioni 6.46** tayari kimerejeshwa na kwa kiasi kilichosalia, makato yanaendelea kupitia madai ya vituo husika kwa utaratibu uliopo. Hatua kali zimeendelea kuchukuliwa dhidi ya wale wanaofanya vitendo hivi vya udanganyifu ikiwemo kusitisha mikataba baina ya Mfuko na wamiliki wa vituo pamoja na kuwasilisha majina ya

watumishi katika Bodi zinazosimamia taaluma zao. Hadi kufikia Aprili 2023, Mfuko ulisitisha mikataba na vituo **38** na kuwasilisha watumishi **131** katika mabaraza yao ya kitaaluma kwa hatua zaidi. Nitoe rai kwa watoa huduma wote pamoja na wanachama wa Mfuko, kuacha vitendo vya udanganyifu ili mfuko huu uendelee kuwa endelevu.

**Bohari ya Dawa (MSD)**

**239. Mheshimiwa Spika,** sheria ya Bohari ya Dawa (MSD) ilifanyiwa marekebisho mwaka 2021 na kuongezewa jukumu la uzalishaji. MSD sasa inatekeleza majukumu makuu manne (4); **Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za afya kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na vile vya binafsi** vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya. Katika kutekeleza majukumu hayo, Bohari hufanya ununuzi, utunzaji na usambazaji wa aina **1,500** za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara, ambapo kati ya hizo, **aina 126** ni dawa zinazopatikana kupitia utaratibu wa Miradi Msonge – (Vertical Program) ambazo zinahusu magonjwa ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Malaria, Ukoma na bidhaa za afya za mama na mtoto. Aidha, miongoni mwa hizo, bidhaa za afya **aina 290** zimeainishwa na Wizara ya Afya kuwa ni bidhaa za afya muhimu zaidi na za kipaumbele kwa nchi. Lengo la kuwa na bidhaa za afya muhimu zaidi na za kipaumbele ni kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinapatikana nyakati zote na kuweza kuhudumia vituo vya kutoa huduma za Afya nchini.

**240. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu zaidi 290 katika maghala ya Bohari ya Dawa ilikuwa ni asilimia 59 ikilinganishwa na asilimia 48 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, hali ya upatikanaji wa dawa pekee ni asilimia 75 ikilinganishwa na asilimia 54 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za Mradi Msonge – "Vertical Programs (bidhaa za afya kwa magonjwa ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Ukoma, Malaria na zile za mama na

mtoto) ni asilimia 87 ikilinganishwa na asilimia 80 kwa mwezi Machi 2022.

**241. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake makuu, Wizara kupitia Bohari ya Dawa imesambaza bidhaa za afya za thamani ya **Shilingi bilioni 727.7** kwenye vituo vya kutolea huduma za afya **7,538** kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Machi 2023. Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 19.7** ikilinganishwa na kipindi cha Julai 2021 hadi Machi 2022 ambapo usambazaji wa bidhaa za afya ulikuwa wa thamani ya **Shilingi bilioni 608.1**. Thamani hii inahusisha bidhaa zote za kawaida na zile za miradi msonge zinazotolewa na wadau wa maendeleo.

**242. Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kuanzia mwaka huu wa fedha 2022/23, Bohari ya Dawa imeanza kusambaza dawa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kila baada ya **miezi miwili** yaani mara sita kwa mwaka kutoka usambazaji wa kila baada ya **miezi mitatu** yaani mara nne kwa mwaka.

**Usambazaji huu umefanya vituo vya afya kupelekewa dawa mara kwa mara hivyo kupunguza changamoto za ukosefu wa bidhaa za afya.**

**243. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bohari ya Dawa imenunua na kusambaza bidhaa za Afya (kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya na kuhakikisha vinatoa **huduma ya dharura ya uzazi wa mama na mtoto**Comprehensive Emergency Obstetric and New-born Care - **CEmONC**) aina 256 kati ya 345 zenye thamani ya Shilingi **bilioni 65** ambayo ni sawa na **asilimia 65** ya Shilingi **bilioni 99.6** zilizopokelewa. Usambazaji na usimikaji huo umefanywa kwenye vituo vya Afya **284** ikijumuisha vituo vya afya na Hospitali za Wilaya. **Uwepo wa mashine hizi katika ngazi za vituo ya msingi (PHC), utasaidia kusogeza huduma za vipimo na uchunguzi karibu zaidi na wananchi, ambapo sasa huduma za uchunguzi wa**

**damu (haematolojia na kemia ya mwili) na uchunguzi wa mkojo zitatolewa katika vituo hivyo.**

**244. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bohari ya Dawa imeweza kusambaza jumla ya **mashine 140 mpya za kusafisha damu** katika **Hospitali 14 za Rufaa.** Hadi sasa huduma zimekwishaanza kutolewa katika vituo vitano (5) ambavyo ni;Hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Amana, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa MwanzaSekouToure, na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani (Tumbi). Aidha ukamilishaji wa miundombinu unaendelea katika vituo tisa (9) vilivyobaki ambavyo ni; Hospitali za Rufaa za Temeke, Mawenzi, Morogoro, Ruvuma, Mwananyamala, Mbeya, Lindi, Dodoma na AICC-Arusha. Vilevile Bohari ya dawa imeweza kufunga jumla ya **mashine 2,315 za maabara na usambazaji wa vitendanishi** vyake katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. **Mashine hizi zimesaidia kusogeza huduma kwa wananchi, Kupunguza gharama za uchunguzi, na kuongeza upatikanaji wa huduma kwenye vituo ambavyo awali havikuwa na huduma hizo.**

**245. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Bohari ya Dawa imeanzisha viwanda viwili vya bidhaa za afya. Moja ya kiwanda kinazalisha aina mbili za barakoa; Barakoa Tiba "surgical mask" na Barakoa Maalumu "N95". Kiwanda hiki kipo katika eneo la Keko – Bohari ya Dawa, Dar es Salaam. Barakoa zinazozalishwa katika kiwanda hiki zinakidhi mahitaji ya nchi nzima, zimepunguza bei ya barakoa kutoka **Shilingi 1,600** hadi kufikia **Shilingi 500** kwa barakoa moja na kuokoa kiasi cha **Shilingi bilioni 3** kutokana na uzalishaji kufanyika ndani ya nchi. Kiwanda kingine ni cha mipira ya mikono "gloves" ambacho kinapatikana kijiji cha Idofi mkoani Njombe ambacho kinatarajiwa kuanza uzalishaji mwaka wa fedha 2023/24.

**246. Mheshimiwa Spika,** pamoja na faida za moja kwa moja ambazo wananchi watazipata kwa uwepo wa viwanda hivi hapa nchini, uwepo wa viwanda hivi, utachangia upatikanaji wa ajira. Aidha, kutokana na malighafi zitakazohitajika katika viwanda hivyo, Wizara ya Afya kupitia Bohari ya Dawa imeanza mawasiliano na Wizara na mamlaka mbalimbali ikiwamo Shirika la Maendeleo la Taifa ili kuhimiza uzalishaji wa malighafi zitakazotumika katika viwanda hivi hivyo kuchochea uchumi katika maeneo hayo. Baadhi ya maeneo ambayo yameonekana kuwa na uwezo wa kuzalisha malighafi ya mipira ya mikono Muheza
(Tanga) na Ifakara (Morogoro)

**247. Mheshimiwa Spika,** pamoja na uanzishaji wa viwanda hivyo, Bohari ya Dawa imepata idhini na imeanza taratibu za kuanzisha **Kampuni Tanzu iliyosajiliwa kwa jina MSD Medipharm Manufacturing Company Limited itakayosimamia jukumu la uzalishaji wa bidhaa za Afya kwa ufanisi zaidi.** Uanzishaji wa Kampuni Tanzu utasaidia Bohari ya Dawa kuwa na mfumo madhubuti wa usimamizi wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya kwa kuzingatia misingi ya kibiashara na kuwezesha kujitegemea katika kufanya shughuli za uzalishaji.

**248. Mheshimiwa Spika**, Bohari ya Dawa imeendelea kufanya utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt Samia Suluhu Machi 30, 2022 ya kuifumua na kuboresha utendaji kazi wa MSD. Uboreshaji wa utendaji wa Bohari ya Dawa unahusisha kupitia mfumo mzima kwa kufanya tathmini ya hali ya sasa na kuweka njia bora ya kuifanya taasisi kujiendesha kibiashara na kukidhi matarajio ya wateja na wadau mbalimbali kwa muda mfupi, wa kati na mrefu kupitia Mshauri Muelekezi.

**249. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa maelekezo ya Mh Rais, Bodi mpya ya MSD imeundwa, Mkurugenzi Mkuu ameteuliwa na Menejimenti iliyokuwepo imeondolewa na

sasa hivi inapelekwa Menejimenti nyingine. Utekelezaji huu umeenda sambamba na **kuwaondoa watumishi 39** na **kupeleka watumishi 83 MSD**. Aidha, katika kipindi hiki, watumishi wa Idara ya manunuzi wamejengewa uwezo kupitia Bodi ya Ununuzi na Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma.

**250. Mheshimiwa Spika,** Bohari ya Dawa imeendelea na uboreshaji wa utoaji huduma kwa kuboresha matumizi ya Mifumo ya kielektroniki. Miongoni mwa mifumo iliyotengenezwa ili kuimarisha utendaji ni mifumo inayosimamia Manunuzi (Procurement Digitization), Mifumo ya Uhifadhi na Usambazaji (Warehouse and Inventory Management), Mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa Magari (Fleet Management) na mfumo wa ununuzi wa Bidhaa za Afya kwa nchi za SADC kwa njia ya kielektroni (electronic SADC Pool Procurement). Aidha, Katika kipindi hiki, Bohari ya Dawa imeendelea kuimarisha mifumo yake ya ndani kwa kuongeza mifumo ya usimamizi na utoaji taarifa kwa lengo la kutoa maamuzi kwa viongozi (executive decisions' dashboards) na kuunganisha mifumo ya Bohari ya Dawa na mifumo mingine ya Kisekta kama Mfumo wa Maoteo na Uagizaji Bidhaa za Afya – eLMIS, Mfumo wa Usimamazi wa Vituo vya Afya katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa – FFARS,) kwa lengo la kuimarisha na kurahisisha utoaji huduma kwa wadau mbalimbali ikiwamo vituo vya kutolea huduma za afya.

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**251. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni taasisi iliyoko chini ya Wizara yenye jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kuhakiki ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa zitokanazo na tumbaku. TMDA ilianzishwa ikiwa na lengo la kuongeza tija na ufanisi katika udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kulinda afya ya jamii. Hii ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa

mpango wa Serikali wa kuondoa muingiliano wa majukumu miongoni mwa taasisi za Serikali.

**252. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Mamlaka ilifanya **ukaguzi katika viwanda 123** ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha kuwa, dawa zinatengenezwa kwa kufuata taratibu za utengenezaji bora (GMP) na hivyo kuwalinda watumiaji. Aidha, viwanda 57 vya vifaa tiba na vitendanishi vilikaguliwa ndani na nje ya nchi kujihakikishia kama vigezo vya ubora vimezingatiwa. Aidha, katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa na vipukusi, kati ya maombi 1,251 ya dawa za binadamu yaliyokuwepo katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Mamlaka ilitathmini maombi 860 sawa na asilimia 69 ambapo maombi 516 sawa na asilimia 60 yaliidhinishwa na hivyo kusajiliwa. Idadi ya maombi yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 227 sawa na asilimia 36 ikilinganishwa na maombi 633 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, maombi yaliyoidhinishwa katika kipindi hicho ni ongezeko la maombi 113 ilikinganishwa na maombi 403 yaliyokidhi vigezo katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Vile vile, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 199 ya usajili wa dawa za mifugo ambapo maombi 129 sawa na asilimia 65 yalifanyiwa tathmini na maombi 95 sawa na asilimia 73 yaliidhinishwa baada ya kukidhi vigezo. Katika kipindi hicho, kulikuwa na maombi 379 ya usajili wa maeneo ya biashara zinazohusiana na dawa ambapo maombi 369 sawa na asilimia 99 yalifanyiwa tathmini ambapo 347 sawa na asilimia 94 yalikidhi vigezo vya usajili na hivyo kupewa vibali vya biashara.

**253. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka Mamlaka ilifanya **ukaguzi wa viwanda na maeneo 10,558 ya biashara ya bidhaa zinazohusiana na dawa** ambapo maeneo 8,226 sawa na **asilimia 78** yalikidhi vigezo. Idadi ya maeneo yaliyokaguliwa katika kipindi hiki ni ongezeko la maeneo 3,918 sawa na asilimia 59 ikilinganishwa na maeneo 6,640 yaliyokaguliwa

katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi, kati ya maombi 311 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi maombi 249 sawa na asilimia 80 yalifanyiwa tathmini na jumla ya maombi 155 sawa na asilimia 62 yaliidhinishwa. Idadi ya maombi ya usajili wa maeneo yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 94 sawa na asilimia 34 ikilinganishwa na maombi 275 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, maombi yaliyoidhinishwa katika kipindi hicho ni ongezeko la maombi 73 ilikinganishwa na maombi 274 yaliyokidhi vigezo katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

**254. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha **udhibiti wa bidhaa za tumbaku**, mamlaka ilikagua **maeneo 117** yanayojihusisha na uendeshaji wa biashara ya bidhaa za tumbaku ambapo yote yalikidhi vigezo. Aidha, Mamlaka imeendelea kuhakiki kama bidhaa za tumbaku zinakidhi matakwa ya Sheria ya Dawa na Vifaa tiba Sura 219. Katika kutekeleza hilo, Mamlaka ilikusanya sampuli 19 za bidhaa za tumbaku kwa ajili ya uchunguzi wa ubora kupitia maabara iliyoko Dodoma ambapo sampuli zote 19 zilifaulu.

**255. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka hutekeketeza bidhaa za dawa, vifaa tiba, vipukusi na vitendanishi ambazo hazikidhi vigezo vya ubora, usalama na ufanisi ili kuepusha bidhaa husika zisitumiwe na wananchi. Katika kipindi husika Mamlaka iliteketeza **jumla ya tani 136.61** bidhaa mbalimbali zenye thamani ya takriban Shilingi bilioni 8.40 **na hivyo kuzuia bidhaa duni, bandia na hafifu kuweza kumfikia mwananchi**. Aidha, Mamlaka imeendelea kulinda mipaka ya nchi kwa kuzuia uingiaji wa bidhaa duni, bandia na ambazo hazijasajiliwa kwa kufanya doria na ukaguzi kwa kushirikiana na vyombo vya dola ikiwa ni pamoja na kutoa jumla ya vibali 4,050 vya uingizaji wa bidhaa bora, salama na fanisi kwa ajili ya kulinda afya ya jamii.

**256. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha **utoaji wa elimu kwa umma** na kuboresha huduma kwa wateja, elimu ilitolewa kwa makundi mbalimbali ya wananchi pamoja na kutangaza huduma za Mamlaka kupitia njia tofauti ikiwa ni pamoja na kufanya mihadhara, vipindi na matangazo mafupi ya redio na runinga. Mamlaka pia ilitoa elimu juu ya matumizi sahihi ya bidhaa za dawa, vifaa tiba na tumbaku kwa jumla ya taasisi za elimu 248 (shule na vyuo) zilizopo Mikoa ya Mbeya, Mwanza, Lindi, Mtwara, Songwe, Tanga, Pwani, Iringa, Shinyanga, na Arusha ambapo wanafunzi na Walimu 39,434 walipatiwa elimu juu ya kazi za TMDA na matumizi sahihi ya bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka. Vile vile, jumla ya TMDA School Clubs 44 zilianzishwa katika shule mbalimbali zilizoko katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Mbeya.

**257. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuhamasisha na kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia uwekezaji katika viwanda vya uzalishaji wa bidhaa za tiba ikiwa ni njia mojawapo ya kuimarisha upatikanaji na kujitosheleza katika bidhaa za tiba hapa nchini. Pamoja na kuhamasisha uwekezaji huu, Serikali inafanya kila jitihada ili kuhakikisha inaweka mazingira wezeshi ya kuvilinda viwanda vinavyoanzishwa nchini dhidi ya ushindani na viwanda vya nje. Kufanikiwa kwa jitihada hizi kutasaidia kuendelea kukuza sekta ya viwanda hapa nchini, na kuwavutia wawekezaji zaidi kuja kuwekeza katika eneo la viwanda vya bidhaa za tiba nchini. Lakini pia uwepo wa viwanda hivi hapa nchini utasaidia kukua kwa uchumi na pato la Taifa, kupunguza changamoto ya ajira na utegemezi wa dawa kutoka nje ya nchi.

**258. Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana kwa utekelezaji wa mpango huu ni pamoja na kuongezeka kwa viwanda vya bidhaa za tiba hadi kufikia viwanda 43 mwezi Machi 2023. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika maeneo mengi katika uzalishaji wa bidhaa za tiba, viwanda vya ndani vimefanikiwa katika **uzalishaji wa maji tiba ambapo**

**kwa sasa unajitosheleza kwa asilimia 100.** Katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha inalinda viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa viwanda vya nje, Wizara inaielekeza MSD kununua maji tiba (IV Fluids infusions) zilizozalishwa na viwanda vyetu vya ndani, isipokuwa pale tuu bidhaa tajwa inapotokea haipatikani nchini. Aidha, naielekeza TMDA kusitisha utoaji wa vibali vya uingizaji wa dawa tajwa kupitia mfumo wa usambazaji wa dawa wa Serikali (public supply chain system). Dawa zitakazokuwa zikisambazwa kwenye sekta binafsi (private sector) kupitia maduka ya dawa ya jumla (wholesalers) na reja reja (retailers) yataendelea kuagiza dawa husika kutoka nje ya nchi. Hatua hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 51 (1) (a) cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 ambacho kimeweka masharti ya kusajili dawa kwa manufaa ya nchi (public interest) na ili kulinda viwanda vyetu vya ndani.

**Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)**

**259. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 **Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali** iliendelea kutoa **huduma ya uchunguzi wa Kimaabara wa sampuli** mbalimbali na vielelezo ambapo katika kipindi hicho jumla ya sampuli 99,159 zilipokelewa. Kati ya sampuli hizo, sampuli 96,942 zilifanyiwa uchunguzi sawa na asilimia 97.8 ya sampuli zilizopokelewa ikiwa ni asilimia 123.8 ya lengo la kuchunguza sampuli 78,299. Uchunguzi huo ni sawa na ongezeko la asilimia 16.22 ikilinganishwa na sampuli zilizochunguzwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/22. Aidha, Mamlaka ilisajili wadau 731 wanaojishughulisha na biashara ya kemikali sawa na asilimia 132.9 ya lengo la kusajili wadau 550. Wadau waliosajiliwa waliongezeka kwa asilimia 69.6 ikilinganishwa na Wadau 431 waliosajiliwa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2021/22.

**260. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hichi **Usimamizi wa Kemikali aina ya Sulphur** ulifanyika, ambapo katika kipindi hichi iliruhusu uingizaji wa kemikali ya Sulphur kwa njia ya Kichele, jumla ya tani 890,798 za Sulphur ziliingia nchini ambazo zilichangia kuingiza mapato ya kiasi cha Shilingi 854,728,159.01. Aidha, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa Jengo la Ofisi na Maabara la Mamlaka Dodoma lenye thamani ya Shilingi Bilioni 8.14 ambapo tayari Mkemia Mkuu wa Serikali na baadhi ya viongozi na watendaji wa Mamlaka wameshahamia katika jengo hilo ili kuweza kutoa huduma kwa urahisi nchini. Vilevile, Serikali imeiwezesha Mamlaka kununua mitambo mikubwa mitatu 3 na mitambo midogo 83 na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara vyenye thamani ya Shilingi Bilioni **2**.

**261. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Mamlaka imetoa nafasi za **Mafunzo kwa watumishi** wa mamlaka ambapo, watumishi 24 waliendelea na mafunzo ya muda mrefu, kati ya hao watumishi 22 wanahudhuria mafunzo ndani ya nchi na wawili (2) nje ya nchi. Watumishi 39 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na kati ya hao, watumishi 27 walihudhuria mafunzo ndani ya nchi na 12 nje ya nchi. Aidha, Mamlaka imefanikiwa **kuhuisha Cheti cha Mifumo ya Usimamizi wa Ubora**. Vilevile, **Elimu kwa umma ilitolewa** kwa wadau 4,238 kupitia maonesho mbalimbali kwa lengo la kuwajengea kuhusu namna ya kuzifikia huduma zitolewazo na Mamlaka.

**Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)**

**262. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge **Na.23** ya Mwaka **1979**. Majukumu ya Taasisi yalivyoainishwa na sheria hii ni pamoja na; Kuratibu, kukuza na kuendeleza utafiti wa afya nchini; Kufanya utafiti wa afya ili kupunguza magonjwa yanayosumbua jamii ya Watanzania;

Kufanya utafiti wa tiba asili na tiba mbadala; Kusajili tafiti za afya zinazofanywa nchini; Kuwapa uwezo watafiti wa kitanzania katika kufanya utafiti wa afya; na Kukuza matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya.

**263. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu lake la kuratibu, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa tafiti mbalimbali za afya hapa nchini, Taasisi imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa watafiti mbalimbali kutoka katika Taasisi za tafiti ndani na nje ya nchi, wanataaluma kutoka katika vyuo vikuu na watu wengine wenye nia ya kufanya utafiti katika eneo la afya. Taasisi kupitia Medical Research Coordination Committee imekuwa ikipitia maombi yote yanayowasilishwa, baada ya kuyapitia na kujiridhisha, yale yanayokidhi vigezo hupatiwa kibali (ethical clearance) kwa ajili ya kuanza kufanya tafiti husika. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Taasisi ilipokea **jumla ya maombi 432 ya watafiti ambapo maombi 535 sawa na asilimia 124 yalipatiwa vibali kwa ajili ya kuanza tafiti.** Vibali hivi ni sawa na ongezeko la asilimia 151 ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa mwaka 2021/2022 ambapo Taasisi ilitoa vibali 213.

**264. Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa jukumu la Utafiti, Taasisi imeendelea kufanya tafiti zinazolenga magonjwa ya kuambukiza na yasiyoyakuambukiza, uimarishaji wa mifumo ya afya na pia viashiria vya kijamii na mazingira ya afya pamoja na Tiba asili. Katika kipindi hiki, **Taasisi imeendelea kutekeleza miradi mikubwa na midogo 113** ambayo ni asilimia 94 ya miradi 120 iliyotekelezwa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2021/2022. Hivyo katika mwaka 2022/2023 maeneo yafuatayo yalifanyiwa tafiti ambapo, katika eneo la VVU/UKIMWI (Miradi 11), Malaria (Miradi 17), Kifua kikuu (Miradi 13), Magonjwa yasiyopewa kipaumbele (Miradi 14), Magonjwa yasiyoyakuambukiza (Miradi 5), UVIKO-19 (Miradi 6), Usugu wa dawa (Miradi 4), Afya ya mama na mtoto (Miradi 6), Uimarishaji wa mifumo ya afya (Miradi 7), VVU na magonjwa yasioambukizwa (Miradi 7), VVU na magonjwa

yasiyopewa kipaumbele (Miradi 3), Kifua kikuu na kisukari (Mradi 1), Mahusiano ya hali ya jamii na afya (Miradi 4), Tiba asili (Miradi 2), na Afya Digitali (Miradi 3) na miradi mingineyo 10.

**265. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Tafiti – NIMR, inafanya utafiti katika eneo la Malaria wa kufuatilia hali ya maambukizi ya Malaria nchini kwa kutumia mbinu za vinasaba katika mikoa 13 ya Tanzania Bara (MSMT). Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mabadiliko ya vimelea vya Malaria ili kubaini kama mbinu tunazotumia kupambana na ugonjwa huu zinafanya kazi ipasavyo, kufuatilia ubora na uwezo wa dawa za kutibu ugonjwa wa Malaria na ufanisi wa vipimo vya haraka vya kupima Malaria (mRDTs). Mpaka sasa matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa **tatizo la vimelea vya Malaria kubadilika na kuathiri ufanisi wa kipimo cha mRDT halipo nchini**. Hivo basi vipimo vya mRDT bado vitaendelea kuwa na tija nchini. Aidha, utafiti umeonesha kuwa tatizo la usugu wa vimelea vya Malaria katika maeneo mengi nchini halipo, isipokuwa maeneo machache ya Wilaya za Karagwe na Kyerwa Mkoani Kagera, ambako kulionekana dalili za uwepo wa usugu.

**266. Mheshimiwa Spika,** NIMR imeendelea kufanya majaribio ya dawa mpya zitakazofupisha urefu wa matibabu ya kifua kikuu kutoka miezi sita (6) hadi minne (4). **Matokeo ya awali ya tafiti hizi yameonesha kuwa dawa mpya zina uwezo wa kufupisha urefu wa matibabu toka miezi sita (6) hadi miezi minne (4) kwa wagonjwa wasio na kifua kikuu sugu**. Hata hivyo tafiti zaidi zinaendelea ili kupata mchanganyiko wa dawa ambao una maudhi kidogo kwa wagonjwa. Pia Taasisi imetekeleza utafiti wa kuangalia hali ya afya baada ya matibabu ya kifua kikuu (TB sequel study). **Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa hali ya afya ya mapafu sio nzuri kwa asilimia 70 ya wagonjwa wanaomaliza dawa za kifua kikuu.** Utafiti zaidi unaendelea kuangalia mbinu za kuboresha afya ya mapafu baada ya kumaliza dawa za kifua kikuu.

**267. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imefanya utafiti katika eneo la **Virusi vya ukimwi (VVU):** Utafiti huu ulifanyika kwa watoto ukiwa na lengo la kulinganisha matokeo ya kiafya na wale waliopimwa VVU wiki ya 4 hadi 6 baada ya kuzaliwa kama ilivyo miongozo ya nchi na wale wanaopimwa baada tu ya kuzaliwa. Matokeo yanaonesha kuwa watoto waliopimwa VVU mara tu baada ya kuzaliwa walikuwa na afya bora zaidi baada ya kuzaliwa kuliko wale waliopimwa wiki ya 4 mpaka 6. Pia matokeo pia yanaonyesha kipimo cha viral load kwa mama wajazito wakati wa kujifungua kinawezesha kuwatambua watoto wengi walio kwenye hatari ya kupata maambukizi kutoka kwa mama zao na hivyo kuwezesha kupatiwa kinga sahihi mapema. Matokeo haya yatasaidia kuboresha afya ya mama na mtoto.

**268. Mheshimiwa Spika,** Taasisi kwa kushirikiana na washirika wa kiutafiti imefanya utafiti kuangalia ikiwa dozi moja ya chanjo ya Human Papilloma Virus (HPV) ina ufanisi sawa na dozi mbili au tatu katika kutengeneza kinga dhidi ya wadudu wanaosababisha saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana wa miaka 9 hadi 14. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa dozi moja ya chanjo dhidi ya HPV ina ufanisi kama dozi mbili au tatu. Matokeo haya yatasaidia kupunguza gharama za chanjo dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi. Pia NIMR imefanya utafiti wa kuangalia ukubwa wa tatizo la kisukari kwa wagonjwa wenye VVU na kugundua kuwa tatizo la ugonjwa wa kisukari kwa wenye VVU ni kubwa na imebaini kuwa utoaji wa huduma za magonjwa yasiyoambukizwa kwenye kliniki za wagonjwa wa VVU unaboresha afya za wagonjwa hawa. Matokeo ya tafiti hizi yatatumiwa na wizara pamoja na wadau wengine katika Sekta ya Afya ili kuendelea kuboresha huduma kwa wananchi.

**269. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea kufanya tafiti katika eneo la tiba asili na tiba mbadala. Ambapo dawa nne (4) za tiba asili, ambazo ni NIMREGENIN kwa ajili ya kutibu tezi dume, TANGESHA kwa ajili ya kutibu seli mundu, PERSIVIN kwa

ajili ya kutibu tezi dume na WARBGISTAT kwa ajili ya kutibu magonjwa nyemelezi zinaendelea kufanyiwa uchunguzi wa usalama. Matokeo ya awali ya utafiti huu yameonesha kuwa dawa hizi ni salama katika hatua za majaribio kwa wanyama. Pia NIMR imenunua mashine mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha maabara za uchunguzi wa dawa asili. Taasisi imeendelea kusimika mitambo ya kuzalisha dawa asili katika kiwanda chetu cha kimkakati katika kituo cha Mabibo ili kuongeza upatikanaji wa dawa za asili ambazo zimegunduliwa na Taasisi.

**270. Mheshimiwa Spika,** Tafiti zingine ambazo zinaendelea ni pamoja na **Utafiti wa kuzuia ugonjwa wa kisukari** Afrika: Jaribio Nasibu la awamu ya tatu ya dawa ya Metformin kwa watu walioambukizwa VVU wanaokaribia kupata ugonjwa wa kisukari, na utafiti wa vyakula tiba kwa ajili ya afya ya uzazi: **utafiti wa kutatua mahitaji muhimu ya virutubibisho na madini kabla na wakati wa ujauzito**. Kukamilika kwa tafiti hizi mbili kunaweza kukatoa mwanga wa jinsi ya kukabiliana na tatizo la kisukari kwa ufanisi Zaidi kwa watu wenye maambukizi ya VVU, lakini pia kupunguza adhari za ukosefu wa madini ambayo limekuwa tatizo sugu kwa akina mama wajawazito hapa nchini.

**Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC)**

**271. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) ilianzishwa kupitia Sheria ya Bunge Namba 24 ya Mwaka 1973 ambayo ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria Na. 3 ya mwaka 1995. Lengo kuu la Serikali katika kuanzisha Taasisi ni kuunda chombo mahsusi cha Kitaifa cha kuwaunganisha na kuwaongoza wataalam wa shughuli za ugani na wanasayansi, pamoja na Viongozi wa Kitaifa katika mapambano dhidi ya utapiamlo nchini. Dira ya Taasisi ni kuwa chombo mahiri cha Kitaifa cha kutoa Uongozi wa kimkakati katika mapambano dhidi ya aina zote za utapiamlo nchini.

**272. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Taasisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi yenye lengo la kuchangia katika juhudi za Serikali za kupambana na aina zote za utapiamlo nchini. Mathalani, kwa lengo la kutafuta shuhuda za kisayansi zinazolenga kutafuta majibu ya changamoto za lishe zinazowakabili watu wa jinsia na rika mbalimbali katika jamii na kuimarisha mikakati ya kukabiliana nazo.

**273. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2022 Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya Tafiti, ambapo Katika kipindi hiki Taasisi imefanikiwa kufanya tafiti nne (4) sawa **na asilimia 44.5** ya tafiti tisa (9) zilizopangwa kwa mwaka 2022/23 zikilenga makundi mbalimbali katika jamii ikiwemo watoto wadogo, wanawake na wasichana walio katika umri wa kuzaa. Matokeo ya hizi tafiti yatasaidia kuimarisha afua za mabadiliko ya tabia pamoja na kuboresha bidhaa za lishe zinazotumika na watoto wadogo nchini. Tafiti hizo ni kama zifuatavyo;

(i) Utafiti wa chakula bunifu kilicho tayari kwa matumizi ya watoto wenye utapiamlo wa kadiri katika Mikoa ya Singida na Dodoma "Ready to Use Food". Utafiti huu unalenga kuimarisha matibabu ya utapiamlo wa kadiri katika jamii kwa **kutumia chakula bunifu** kilichotengenezwa kwa kutumia vyakula mbalimbali vilivyopo kwenye maeneo ya jamii husika kikiwa na virutubishi vya kutosha na kwa gharama nafuu. Mategemeo ni kwamba kupitia utaratibu utakaowekwa chakula bunifu kitaweza kupatikana hadi katika ngazi ya Zahanati ambapo wananchi wa kawaida wataweza kukipata kwa urahisi na hivyo kupunguza idadi ya watoto takribani 120,000 wanaohitaji kuhudumiwa na vituo vya afya vya ngazi ya juu kila mwaka. Pia, utaratibu wa kuwawezesha wajasiriamali waliopo katika ngazi za jamii kutengeneza vyakula hivi kwa viwango vyenye ubora vinavyokidhi mahitaji unaangaliwa ili kupanua wigo wa upatikanaji katika jamii.

(ii) Utafiti kubaini mila na desturi zinazohusu ulaji wa vyakula kwa wanawake na wasichana walio katika umri wa kuzaa (miaka 15 hadi 49) katika **Mikoa saba (7) ya Mbeya, Kigoma, Mwanza, Arusha, Singida, Lindi na Dar es Salaam.** Utafiti huu unalenga kutambua miiko inayoambatana na mila potofu kwenye ulaji wa baadhi ya vyakula vinavyopatikana kwenye jamii za Mikoa husika ambayo inachangia sana kuongezeka kwa utapiamlo kwa makundi husika. Utafiti huu utasaidia kuandaa afua zitakazodhibiti mila potofu zilizoko kwenye jamii ambazo zinachangia tatizo la upungufu wa vitamini na madini miongoni mwa wanawake hususan upungufu wa damu kwa wanawake wajawazito ambapo takribani asimilia 28 ya wanawake hudhurika. Matokeo ya utatifi huu pia yanatarajiwa kupunguza matokeo hasi ya ujauzito ikiwemo kujifungua watoto wenye uzito mdogo, njiti au wafu au kupoteza maisha wakati wa kujifungua.

(iii) Utafiti wa **hali ya maambukizi ya minyoo na ugonjwa wa kichocho kwa watoto wenye umri wa miezi 12 hadi miezi 59** katika Mikoa saba (7) ya Tanzania Bara (Dodoma, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Mwanza, Lindi na Pwani). Jumla ya **watoto 1,678** wamepimwa wingi wa damu na maambukizi ya minyoo tumbo. Matokeo ya utafiti huu yataiwezesha Wizara kuimarisha mikakati na uwekezaji katika afua ya nyongeza ya vitamin A na dawa za minyoo tumbo ambayo hufanyika kwa njia ya kampeni kila mwaka. Maboresho haya yataiwezesha nchi kufikia lengo la Shirika la Afya Duniani la kutokomeza madhara yatokanayo na maambukizi ya minyoo ya tumboni na kichocho kwa watoto ifikapo mwaka 2030,

(iv) Tafiti ya **ulaji miongoni mwa wanawake wasio wajawazito** na wasio nyonyesha wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 49 katika **Halmashauri saba (7) za Mkoa wa Mbeya.** Utafiti huu ulihusisha **wanawake 502** ili kubaini aina za ulaji kwa wanawake waliokatika umri wa kuzaa. Kupitia matokeo ya utafiti huu mikakati ya kukabiliana na matokeo hasi ya ujauzito kama vile upungufu wa damu, kujifungua watoto

wenye uzito mdogo, njiti au wafu au kupoteza maisha wakati wa kujifungua yatadhibitiwa.

**274. Mheshimiwa Spika**, Taasisi kupitia maabara yake imeendelea kufanya uchambuzi na kuchakata Sampuli zinazohusu viashiria vya chakula na lishe katika Utafiti wa Taifa wa Afya na Demografia (Tanzania Demographic and Health Survey 2021/22). Katika kipindi hiki sampuli zisizopungua **10,061 zimeshafanyiwa uchambuzi** ambazo ni pamoja na **sampuli 2,091 za mafuta ya kula, sampuli 1,129 za unga wa mahindi, sampuli 1,191 za unga wa ngano, sampuli 4,450 za mkojo**. Uchambuzi huu umelenga kubaini **viwango vya vitamini na madini** ikiwemo madini joto na sampuli 1,200 za "serum folate" ili kupima viwango vya folate. Kazi hii inatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni 2023, na matokea ya utafiti huu yatabainisha viwango vya sasa vya hali ya lishe kwa viashiria vya vitamini na madini kwa nchi nzima. Kupitia matokeo ya utafiti huu Serikali itaweza kuandaa afua zenye tija zaidi za kutatua changamoto za upungufu wa madini na vitamini miongoni mwa jamii.

**275. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki Taasisi imefanya ufuatiliaji kuhusu utekelezaji wa **program ya kuongeza virutubishi kwenye vyakula kupitia viwanda** vikubwa, vya kati na vidogo katika Mikoa mbalimbali nchini. Hadi sasa kuna viwanda vikubwa 57 vinavyotekeleza programu hii; tisa (9) vinaongeza madini joto kwenye chumvi, 13 vinaongeza virutubishi kwenye mafuta ya kula, viwanda kumi (10) kwenye Unga wa ngano na kumi na tatu (13) kwenye unga wa mahindi. Idadi hii ni ongezeko la viwanda 12 ukilinganisha na mwaka 2021/2022. Aidha, hivi sasa kuna jumla ya viwanda vya kati na vidogo 722 ambavyo vinatekeleza programu hii katika Mikoa mbalimbali hapa nchini.

**276. Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha elimu ya lishe kwa umma inawafikiwa **wajasiriamali wasindikaji wa vyakula,** katika kipindi hiki Taasisi imetoa elimu ya **usindikaji wa chakula**

**cha nyongeza** kwa watoto wenye umri wa miezi 6 mpaka 23 ikihusu kutumia mazao lishe, kanuni bora za usindikaji unga wa mahindi na uongezaji virutubishi, pamoja na udhibiti wa sumu kuvu. Jumla ya wajasirimiamali 50 kutoka Halmashauri za Singida Manispaa na Singida Vijijini wamepatiwa. Adha, wasindikaji 20 wa unga wa mahindi kutoka Manispaa ya Dodoma Jiji nao walishiriki katika mafunzo juu ya kanuni bora za usindikaji wa unga wa mahindi pamoja na njia ya kudhibiti sumu kuvu kwa kufanya ukaguzi wa malighafi**.**

**277. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 Taasisi inaendelea pia na jitihada za kuelimisha umma na jamii kupitia vyombo vya habari, mitandao ya kijamii, Tovuti ya Taasisi na Blogu. Katika kipindi hiki wananchi 343,235 walifikiwa kupitia mitandao ya kijamii na tovuti ya Taasisi, Vipindi 75 vya redio na runinga vimeandaliwa na kurushwa, makala 521 zimeweza kuandikiwa na kuchapwa kwenye magazeti mbalimbali ikiwemo makala maalumu ya miaka 61 ya Uhuru, picha habari na posta zenye jumbe za lishe 31 zimesambazwa katika jamii kupitia mitandao ya kijamii, TV na Radio inayoelimisha ulaji wa matunda na mbogamboga imetengezwa na kurushwa kwa muda wa mwezi mmoja katika mikoa mitano (5) na nakala 361 za vitabu, vipeperushi na mabango yalisambazwa kwenye Ofisi za Serikali na mashirika yasiyo kuwa ya Serikali. Pia katika kipindi hiki Taasisi kwa kushirikiana na chama cha walemavu wa macho imetengenezea nyenzo za kufikishia elimu ya lishe kwa watu wenye ulemavu wa macho kwa kufanikiwa kutengeneza vitabu vinne (4) vya kufikishia elimu ya lishe kwa maandishi ya nukta nundu pamoja na redio

**278. Mheshimiwa Spika,** Taasisi pia imetekeleza agizo la **Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuhusu kulifikia kundi la **vijana balehe** alilolitoa wakati wa hafla ya utiaji saini wa mkataba wa lishe na Wakuu wa Mikoa tarehe 30 Septemba, 2022. Katika kipindi hiki, Taasisi iliandaa vipindi vitatu (3) vya runinga ili kutoa elimu ya lishe kwa vijana balehe

700 wakiwemo wasichana 216 na wavulana 484 katika shule za Sekondari Alhasani Mwinyi ya Mkuranga na Bagamoyo zote za Mkoa wa Pwani, na vijana 30 (wasichana 8 na wavulana 22) walio nje ya shule (Bodaboda) katika Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, Taasisi pia imezindua aplikesheni ya kimtandao yenye jumbe za lishe kwa watu wanaoishi na virusi vya ukimwi na kifua kikuu ikiwa na lengo la kuwawezesha mwananchi wa kawaida kufukiwa na elimu ya lishe kupitia simu hanja. Uamuzi huu unalenga kuzidi kuongeza wigo wa wanufaika wa wa elimu ya lishe katika jamii ya Watanzania.

**279. Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha elimu ya lishe kwa umma inawafikia wajasiriamali wasindikaji wa vyakula, katika kipindi hiki Taasisi imetoa elimu ya usindikaji wa chakula cha nyongeza kwa watoto wenye umri wa miezi 6 mpaka 23 ikihusu kutumia mazao lishe, kanuni bora za usindikaji unga wa mahindi na uongezaji virutubishi, pamoja na udhibiti wa sumu kuvu. Jumla ya wajasirimiamali 50 kutoka Halmashauri za Singida Manispaa na Singida Vijijini wamepatiwa elimu hii. Aidha, wasindikaji 20 wa unga wa mahindi kutoka Manispaa ya Dodoma Jiji nao walishiriki katika mafunzo juu ya kanuni bora za usindikaji wa unga wa mahindi pamoja na njia ya kudhibiti sumu kuvu kwa kufanya ukaguzi wa malighafi**.**

**280. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imekamilisha **maandalizi ya mitaala** ya kozi fupi nne (4) za kuimarisha ujuzi (competence based) kwa watoa huduma katika ngazi mbalimbali. Kozi hizo zinahusu; Utoaji wa huduma za lishe wakati wa dharura na maafa; Mahitaji ya Kilishe kwa wagonjwa wa UKIMWI, Uandaaji wa chakula cha nyongeza kwa watoto wadogo na wachanga na Matibabu ya utapiamlo mkali (kuzuia, kubaini mapema na matibabu sahihi). Lengo la Taasisi ni kupanua wigo wa fursa ya elimu ya lishe kwa makundi maalum na kuongeza ujuzi kwa watoa huduma katika ngazi mbalimbali.

**281. Mheshimiwa Spika,** Taasisi kwa kushirikiana na wadau wa lishe nchini ilifanikisha kufanyika kwa Mkutano wa Nane wa

Mwaka wa Wadau wa Lishe uliofanyika Musoma mkoa wa Mara. Mkutano huu kwa mara ya kwanza ulihusisha jamii kama njia mojawapo ya kuongeza ushirikishwaji wa umma katika masuala ya lishe ambapo ulihitimishwa kwa mkutano wa hadhara. Pamoja na mambo mengine mkutano huu ulihusisha shughuli za kijamii ambao viongozi wa Kitaifa pamoja na wawakilishi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa walishiriki kupanda miti ya matunda katika shule ya Msingi Mwisenge ambayo Baba wa Taifa Mwalimu J.K Nyerere alisoma, lakini pia miti mingine ilipandwa katika shule zingine za msingi zinazozunguka eneo hilo. Pamoja na shughuli ya kupanda miti ya matunda, wanafunzi wa shule hizo walipatiwa elimu ya lishe kutoka kwa wataalam ambao walialikwa kushiriki katika mkutano huu. Elimu ya lishe ilitolewa pia kwa umma na jamii kupitia kituo cha Redio.

**E. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MABARAZA NA BODI ZA KITAALUMA.**

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)**

**282. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni mamlaka ya Kisheria, kusimamia Taaluma na wanataaluma wa Uuguzi na Ukunga Tanzania. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga yaani The Nursing and Midwifery Act 2010. Jukumu kuu la Baraza ni kulinda, kuimarisha na kuhifadhi afya ya jamii, usalama na ustawi kupitia usimamizi na udhibiti wa shughuli za mafunzo ya uuguzi na ukunga na utoaji wa huduma, na kuhakikisha jamii inapata huduma bora zenye kiwango na salama. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Jumla ya wauguzi na Wakunga 2,455 wamesajiliwa katika kipindi hiki dhidi ya lengo la kusajili wataalam 4,000 ambayo ni sawa na asilimia 61 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza hadi sasa kufikia 55,945. Aidha kati ya wauguzi na wakunga waliyosajiliwa, wauguzi na wakunga 591 wamepewa usajili wa awali (Provisional registration) na na wanaendelea na mafunzo

katika Vituo 28 zikiwemo Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za Kanda (4) na Hospitali za rufaa za mikoa 23.

**283. Mheshimiwa Spika,** jumla ya Wauguzi na Wakunga 4,865 waliomba na kukidhi sifa za kufanya mtihani kwa ajili ya usajili, Idadi hii ilijumuisha watahiniwa 562 sawa na asilimia 12 wa ngazi ya shahada, watahiniwa 4,049 sawa na asilimia 83 wa ngazi ya stashahada na watahiniwa 253 sawa na asilimia 5 wa ngazi ya astashahada. Watahiniwa waliofaulu walikuwa 2,446 sawa na asilimia 50. Ufaulu kwa ngazi ya elimu ilikuwa kama ifuatavyo; watahimiwa 436 ngazi ya shahada sawa na asilimia 76 walifaulu, watahiniwa 1,842 wa ngazi ya stashahada sawa na asilimia 45 walifaulu na watahiniwa 169 wa ngazi ya astashahada sawa na asilimia 67 pia walifaulu. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya maombi 14 ya kuanzisha mafunzo ya uuguzi na ukunga yalipokelewa. Ukaguzi ulifanyika ili kuona kama vimekidhi viwango vya kitaaluma. Kati ya maombi hayo vyuo 8 vilivyoomba vilikuwa na sifa na kupata kibali cha kuanzisha mafunzo. Vyuo vingine bado vinaendelea na maandalizi. Aidha, kaguzi Uelimishaji na maelekezo ya kuzingatia miongozo yalitolewa kwenye Vituo vya kutolea huduma binafsi za uuguzi na ukunga katika mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Iringa, Mwanza na Kagera.

**284. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki Baraza la Uuguzi na Ukunga lilipokea maombi 5 ya kuanzisha huduma binafsi za Uuguzi na Ukunga katika mikoa ya Mbeya, Geita na Dar es Salaam. Vituo hivyo ni NILAX Nursing home and health rehabilitation Centre, Peter Mobile Nursing na Face Mobile Nursing services vilivyoko Dar es Salaam. Mkoani Mbeya Kituo cha Joyces Nursing and Maternity Homes na Geita Kituo cha Minely Nursing and Maternity Home. Vituo vyote vilikaguliwa na kuonekana kuwa vimekidhi vigezo na hivyo kupewa kibali. Aidha, Vituo 5 vilivyosajiliwa hapo awali vilikosa sifa kwa kutozingatia miongozo na vikafungwa. Vituo hivyo vipo Mikoa ya Mwanza, Kagera na Iringa. Hii inafanya jumla ya Nursing

and Maternity Homes and services zilizosajiliwa na Baraza na kuendesha huduma hadi sasa kufikia 84 kwa nchi nzima.

**285. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hichi, wauguzi na wakunga takribani 33,913 wamefanya mafunzo ya kujiendeleza yaani CPD, kwa njia tofauti tofauti ikiwemo kwa njia ya mtandao, kwa kuhudhuria semina mbalimbali za kujengewa uwezo, na kwa kufanya tafiti mbalimbali. Idadi hii imetokana na kwamba CPD ni takwa la kisheria kabla ya kuhuisha leseni za kutolea huduma. Wauguzi na wakunga wamekidhi kigezo hiki na wamehuisha leseni zao kwa kipindi cha mwaka 2022 hadi 2025. Aidha, jumla ya moduli 73 za mafunzo ya kujiendeleza zilipokelewa, kuhakikiwa ambapo 63 zilikidhi sifa na kupata idhibati. Moduli zimelenga katika eneo la afya ya mama na mtoto, magonjwa yasiyoambukiza, magonjwa yanayoambukiza, utoaji wa ushauri nasaha na mbinu za ufundishaji (Teaching Methodology). Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023 jumla ya mashauri 14 ya tuhuma za uvunjifu wa maadili yalipokelewa. Mashauri kumi na tatu (13) yalifuatiliwa na kutolewa maamuzi kama ifuatavyo: Wauguzi watano (5) waliondolewa kwenye rejesta ya Baraza, Wauguzi wanne (4) walipata karipio kali na wengine walionekana hawana makossa na Shauri moja (1) linaendelea kufuatiliwa.

**Baraza la Madaktari Tanganyika**

**286. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Madaktari limekua likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya wanataaluma 1,601 Wamesajiliwa (Registered), 312 Wameandikishwa (Enlist), 253 Madaktari wa Kigeni waliopewa usajili wa muda (Limited Registration) 1,887 Wameorodheshwa (Enrolled) na 1,053 Watarajali (Provisional Registration) wamesajiliwa katika kipindi hiki, na kufanya jumla ya wanataaluma waliosajiliwa katika kipindi hichi kufikia 5,106.

**287. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilisimamia mtihani wa kabla ya mafunzo ya utarajali ambao ulifanyika tarehe 19 Oktoba 2022. Jumla ya maombi yaliyopokelewa ya kufanya mtihani huo yalikuwa 1,072; ambapo watahiniwa wa Udaktari walikuwa 1,030 na Udaktari wa meno walikuwa 42. Watahiniwa wa Udaktari waliofanya mtihani walikuwa 1,011 na Madaktari wa Meno walikuwa 42. Baada ya mtihani waliruhusiwa kuendelea na mafunzo ya utarajali. Aidha, Baraza lilisimamia mtihani wa baada ya mafunzo ya utarajali ambao ulifanyika tarehe 14 Desemba, 2022. Jumla ya watarajali waliojiandikisha kufanya mtihani walikua 1,391, kati yao waliofanya mtihani walikua watarajali 1,345. Kati ya waliofanya mtihani, 1,310 walikuwa watarajali wa Udaktari, 33 watarajali wa Udaktari wa meno na 2 walikuwa watarajali wa Uafisa technolijia na vifaa Tiba saidizi. Matokeo ya ufaulu wa jumla baada ya Mafunzo ya Utarajali ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini, ambapo wanataaluma 1,130 walifaulu, ambayo ni sawa na asilimia 84 ya watarajali 1,345 waliofanya mtihani.

**288. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Baraza limefanya ukaguzi katika vituo vya Watarajali (Vipya na vilivyopo) ambavyo ni; Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, Simiyu, Hospitali ya Kibosho na Hospitali ya Mt. Joseph – Kilimanjaro, Hospitali ya Agha Khan na Hospitali ya Rabininsia – Dar es Salaam. Baada ya ukaguzi wa hizo Hospitali kuna mapungufu yaliyoonekana hasa kwenye eneo la upasuaji linahitaji kuimarishwa. Hivyo Baraza linaandaa utaratibu wa mafunzo kwa vituo vyote vinavyopokea watarajali ili kuondoa mapungufu hayo.

**289. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2022, Baraza kupitia Kamati ya **Mafunzo endelevu ya kitaaluma(CPD)** imefanya mafunzo ya kuhamasisha Hospitali za Wilaya na za Mikoa kujiandikisha kama vituo vya kutolea mafunzo endelevu katika Kanda tatu zinazojumuisha Mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Manyara, Mwanza, Kagera,

Shinyanga, Tabora, Kigoma, Geita, Mara, Pwani, Dar es salaam na Morogoro, ambapo jumla ya wanataaluma 187 walishiriki kwa kanda zote zilizotembelewa. Mafunzo haya yanapelekea kuongezeka kwa idadi ya Wataalamu wanaofanya mafunzo endelevu na kujipatia pointi za CPD. Aidha, Baraza limefanya vikao vitatu vya uhamasishaji kwa wanataaluma 1873 kwa njia ya mtandao. Aidha, Jumla ya watoa huduma wa mafunzo endelevu (CPD) waliodhinishwa hadi sasa ni 34, na idadi ya kozi zilizoidhinishwa (CPD Activities) hadi sasa ni 291. Vilevile, Baraza limetengeneza kozi tatu za lazima kwa Wanataaluma wote (Mandatory CPD Activities) ambazo ni; Professionalism, Customer care na Medical Ethics.

**290. Mheshimiwa Spika**, Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ambapo jumla ya mashauri 24 yalifunguliwa dhidi ya wataalam waliotuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya taaluma zao. Kati yao, Mashauri saba (7) kutoka mkoani Dar es Salaam; Mawili (2) katika Hospitali ya Muhimbili National Hospital – Mloganzila, Moja (1) Muhimbili National Hospital, Moja (1) Mwananyamala RRH, Mawili (2) Amana RRH na Moja (1) Hitech Sai Health Centre. Mashauri mawili (2) kutoka Mkoani Mtwara katika Hospitali ya Wilaya ya Newala na Kituo cha Afya Likombe, mashauri mawili (2) kutoka Mkoa wa Pwani katika Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo na Tumbi RRH. Aidha, shauri moja (1) kutoka Kigoma kituo cha Afya Ujiji, Tabora shauri moja (1) kutoka Hospitali ya Wilaya ya Kaliua, Shinyanga shauri moja (1) kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-Shinyanga, Mwanza shauri moja(1) Dispensari ya Kirumba - Tanga shauri moja (1) Kerenge Dispensari - Kilimanjaro mashauri mawili (2) Kilema DDH na Siha Hospitali ya Wilaya, Arusha mashauri mawili (2) Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha -Mt. Meru, Ruvuma shauri moja (1) St. Joseph Hospital Peramiho, Mbeya mashauri mawili (2); Hospitali ya Rufaa ya Mkoa -Mbeya na Hospitali ya Wilaya ya Chunya na Songwe katika Kituo cha Afya Isansa. Kulikuwa pia na ufuatiliaji wa tuhuma za utoaji wa huduma mbovu katika Taasisi ya Tiba ya

Mifupa - MOI, ALMC - Arusha, Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Mbeya, Kituo cha Afya Uhai Mbeya na Dr. Shaffiq's Specialised Polyclinic ambapo matokeo ya uchunguzi huu ni kwamba watuhumiwa watatumiwa notisi za kujieleza. Aidha katika Dr. Shaffiq's Specialised Polyclinic maelekezo yalitolewa ya uboreshaji wa huduma za maabara, huduma ya matibabu na huduma ya utoaji dawa.

**Baraza la Famasia**

**291. Mheshimiwa Spika**, Baraza la Famasi ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya, iliyoanzishwa kupitia Kifungu Na. 3 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 kwa lengo la kusimamia taaluma ya wanataaluma wa dawa, utendaji wake ikiwa ni pamoja na usajili na kutoa vibali katika maeneo yanayotoa huduma za dawa na kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa. Baraza la Famasi limekua likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Wafamasia 331 wamesajiliwa, Fundi Dawa Sanifu 1157 wameandikishwa na Fundi Dawa wasaidizi 55 wameorodheshwa katika kipindi hichi na kufikisha jumla ya wanataluma 10,545 ambapo kati ya hao, wafamasia ni 3,357; fundi dawa sanifu ni 6,362; fundi dawa wasaidizi ni 826 wanaotambulika hadi sasa. Idadi hii ni sawa na ongezeko la wanataluma 257 kati ya 1287 waliotarajiwa kusajiliwa kwa ujumla na hivyo kuvuka malengo ya idadi iliyokadiriwa katika kipindi hiki. Aidha, hadi kufikia 30 Machi, 2023 wanataaluma 6,900 (asilimia 65.4) wamehuisha leseni za utendaji utendaji wa taaluma na wafamasia watarajali 346 wamepata usajili wa awali kwa ajiliya mafunzo ya vitendo katika vituo mbalimbali nchini.

**292. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilisimamia mitihani ya usajili kwa kada zote, jumla ya maombi mapya ya mitihani ya usajili yalikuwa ni 3,749 ambapo waliofuzu 2,283 sawa na asilimia 61, kati yao astashahada 266, waliofaulu ni 78 sawa na asilimia 29; stashahada 3,041, waliofaulu 1,833 sawa na asilimia 60 na

shahada 442 waliofaulu 372 sawa na asilimia 84. Aidha, Baraza hadi sasa limetambua vituo 36 vilivyokidhi vigezo na kuidhinishwa kutoa mafunzo kwa watarajali. Utoaji wa idhini ya vyuo vinavyotoa Mafunzo ya Famasi ni mojawapo ya jukumu la baraza. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, jumla ya vyuo 39 viliwasilisha maombi ya kuanzisha kozi ya famasi ngazi ya stashahada (NTA Level 04 – 05) ambapo kati ya hivyo, vyuo 36 vilikidhi vigezo na kuidhinishwa kuanzisha mafunzo ya famasi na hivyo kufanya vyuo vilivyoidhinishwa kutoa mafunzo ya famasi ngazi ya stashahada na shahada, kufikia 89 hadi sasa. Kati ya vyuo 89 vinavyoidhinishwa kutoa mafunzo ya famasi ngazi ya stashahada na shahada, vyuo 23 sawa na asilimia 25.8 vilikaguliwa kwa hatua ya kufuatilia ubora wa mafunzo katika mikoa ya Mwanza, Iringa na Dar es Salaam.

**293. Mheshimiwa Spika,** Baraza kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 limesajili majengo 353 ya kutolea huduma ya afya, ambapo kati ya hizo, famasi za ndani ya Hospitali ni tano (5), famasi za jumla wasio waagizaji dawa nchini 22, rejareja 265, maghala ya kutunzia dawa manne (04), na famasi za jumla na rejareja ni 57 na kufanya jumla ya majengo ya famasi yaliyosajiliwa mpaka sasa kufikia 2,812. Aidha, majengo 67 ya famasi yamefutiwa usajili/kibali cha biashara kutokana na kutoendelea kutoa huduma hizo. Kwa upande wa maduka ya dawa muhimu vibali 2,003 vimetolewa na kufikia jumla ya maduka 15,240 kote nchini. Pia, katika kipindi hiki, Baraza limefanya kaguzi za maduka yanayotoa huduma za dawa katika mikoa nane (8) ya Kagera, Shinyanga, Mara, Geita, Simiyu, Kigoma, Katavi na Dar es Salaam ambapo jumla ya maduka 1,365 yamekaguliwa na maduka 318 sawa na asilimia 23 yalifungwa kutokana na kukosa vibali na wahudumu kukosa sifa za kutoa huduma za kitabibu.

**294. Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanya ukaguzi wa huduma za dawa katika Hospitali nane (08) za Rufaa za

Mikoa na vituo vinne (4) vya kufundishia watarajali ili kuimarisha utendaji wa wanataaluma. Katika Hospitali hizo, Kamati za dawa zimejengewa uwezo wa kutekeleza majukumu yao ili kuhakikisha dawa zinapatikana muda wote. Katika kuhakikisha wanataalama wanajiendeleza huku wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kitaalamu, Baraza liliandaa awamu mbili (2) za mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD) ambapo jumla ya wanataaluma 1,327 sawa na asilimia 12.6 ya wanataaluma wa dawa 10,545 walishiriki mafunzo hayo. Aidha, Baraza limepokea mashauri 33 ya kinidhamu dhidi ya wanataaluma waliokiuka maadili katika maeneo yao ya kazi, malalamiko 25 sawa na asilimia 49 yalithibitika na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

**Baraza la Wataalamu wa Radiolojia**

**295. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wataalamu wa Radiolojia limekua likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Baraza la Wataalamu wa Rediolojia, kupitia vikao viwili vya kisheria lilipitia maombi ya usajili wa Wataalamu wa kada mbalimbali za Rediolojia. Jumla ya Wataalamu 388 kati ya Wataalamu 391 walioomba usajili walipata usajili ambayo ni sawa na asilimia 99 kutokana na kukidhi vigezo. Kati ya hao, usajili wa matazamio walikuwa 207 (Provisional), usajili kamili 171(full Registration) Kujiorodhesha ni 4 (Enrolment), kujiandikisha 6 (Enlisting), na maombi matatu ya usajili wa kudumu (Temporary Registration) yalisubiri kutokana na kukosekana kwa nyaraka muhimu. Aidha, Jumla ya Wataalamu 1,200 walihuisha leseni zao. Aidha, jumla ya Wataalamu 53 waliohitimu mafunzo ya shahada mbalimbali za Rediolojia na kupata usajili wa matazamio (Provisional Registration) walipangiwa katika vituo mbalimbali (Hospitali) kwa ajili ya kufanya mafunzo ya utarajali (Internship)Vituo hivyo ni pamoja na Ocean Road, Taasisi ya MOI, Hospitali ya Benjamini Mkapa, Mloganzila na KCMC.

**296. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilifanikiwa kuongeza kituo kimoja cha utarajali baada ya Ukaguzi shirikishi uliofanyika katika Hospitali ya KCMC idara ya Rediolojia na kujiridhisha kuwa kituo hicho kinakidhi vigezo vya kuwapangia Wataalamu kufanya mafunzo ya Utarajali. Aidha, ukaguzi shirikishi ulifanyika katika Hospitali za Mloganzila, Benjamin Mkapa, Ocean Road na MOI kwa lengo la kuona utendaji wa Watarajali na wasimamizi wa maeneo husika. Changamoto mbalimbali ziliibuliwa na kupatiwa ufumbuzi. Aidha, Wajumbe waliridhishwa na ushirikiano unaotolewa na Uongozi wa idara zote za Rediolojia katika Hospitali husika.

**297. Mheshimiwa Spika,** Mwongozo wa mafunzo endelevu ya Kitaaluma (CPD) upo hatua za awali za maandalizi. Aidha, Jumla ya Wataamu 1280 kati ya Wataalamu 1918 (asilimia 67) waliosajiliwa walipata mafunzo endelevu ya kitaaluma kupitia mikutano ya kisayansi na makongamano yaliyoandaliwa na Baraza kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali na Vyama vya kitaaluma. Aidha, jumla mashauri matatu (3) ya uvunjifu wa miiko na maadili ya taaluma yaliripotiwa ambapo mawili yalijadiliwa kwenye kikao cha kamati ya nidhamu ya Baraza na kutolewa maamuzi; na shauri la tatu limepelekwa mahakamani. Vilevile, Baraza limekuwa likitoa elimu juu ya miiko na maadili kwa wataalamu wake kupitia ukaguzi shirikishi, Mikutano ya Kisayansi na makongamano mbalimbali.

**Baraza la wataalamu wa Macho (Optometria) Tanzania**

**298. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wataalamu wa Optometria limekua likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ya Optometria ya Mwaka 2007 na kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka. Jukumu kuu la baraza ni usimamizi na udhibiti wa wataalamu wa Kada ya Optometria, Kliniki za optometria na wasambazaji wa vifaa na miwani. Kuhahakikisha usajili wa Kliniki zote zinazotoa huduma za Optometria zinasajiliwa na kupatiwa leseni. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, Baraza limetekeleza majukumu yafuatayo;

**299. Mheshimiwa Spika,** jumla ya wataalam 58 wamesajiliwa katika kipindi hiki dhidi ya lengo la kusajili wataalam 105 na hivyo kufikia asilimia 55.2 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa hadi sasa na Baraza kufikia 441. Kati ya Wataalam waliosajiliwa, Wataalam 46 walipatiwa usajili wa awali, usajili wa kudumu ni 368. Aidha, baraza limeanza utaratibu wa kusajili wataalam wake kwa njia ya mfumo wa kielektroniki, ambapo wataalam wote 368 wamesajiliwa kupitia mfumo huo, na wataalam 46 watapata usajili wa kudumu. Aidha, Baraza lilifanya vikao viwili vya baraza na kupitia vikao hivi Baraza lilijadili na kupitisha maombi ya Wataalam wa fani ya Optometria, usajili huo ulikuwa ni wa awali, usajili wa kudumu na leseni na pia maombi ya usajili wa Kliniki za Optometria yalijadiliwa

**300. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilifanya usimamizi shirikishi kwenye Kliniki na vituo vya kusambaza huduma za Optometria katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara na Lindi ambapo jumla ya vituo 46 vilikaguliwa na vituo 27 vilikuwa na changamoto mbalimbali, ambapo baadhi vilishauriwa namna bora ya kuendesha huduma za Optometria, na vingine vilichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Optometria ya mwaka 2007. Katika kipindi hicho, jumla ya wataalam 243 walipewa elimu kuhusu maendelezo ya taaluma (CPD) na namna ya kupata alama za maendelezo ya taaluma ya fani ya Optometria katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, watumishi wa Baraza walijengewa uwezo juu ya matumizi ya mfumo wa Health Facility Registration System (HFRS) na Health Practitioners Registration System (HPRS). Mafanikio ya matumizi ya mifumo hiyo ya kielektroniki imewezesha Baraza kuorodhesha jumla ya wataalam 414 Kwenye rejesta ambapo baraza linategemea kuandaa tovuti itakayohabarisha umma juu ya mambo mbalimbali yanayowahusu wataalam wa Optometria na wajibu wao kwa jamii.

**Baraza la Wataalam wa Maabara ya Afya**

**301. Mheshimiwa Spika,** jukumu kuu la baraza ni kuhakikisha wataalamu wa maabara za Afya wamesajiliwa na kuandikishwa, Wataalamu wa maabara wanafuata miiko na maadili ya taaluma ya Maabara, utekelezaji bora wa usimamizi wa mitaala ya mafunzo ya maabara ya Afya. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 Baraza limetekeleza majukumu yafuatayo; Usajili wa wataalamu wa maabara katika ngazi zote (shahada, stashahada na astashahada); Kuendesha na kusimamia mitihani ya usajili kwa ngazi zote; Kufuatilia mashauri ya uvunjifu wa miiko na maadili ya taaluma; Kusimamia mafunzo ya watarajali wa maabara; Kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vya afya vinavyotoa huduma za maabara; Kufanya ukaguzi wa vyuo vinavyotoa mafunzo ya maabara; Kuimarisha mifumo ya TEHAMA; Kufanya ukaguzi wa maabara kwaajili ya mafunzo ya utarajali; Kutoa leseni za upimaji wa VVU kwa Wataalamu wa Afya wasio wataalamu wa maabara

**302. Mheshimiwa Spika,** jumla ya wataalam wa maabara 2,982 wamesajiliwa katika kipindi hiki dhidi ya lengo la kusajili wataalam 1,890 na hivyo kuvuka lengo na kufikia asilimia 157.7 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa hadi sasa na Baraza kufikia 15,002. Kati ya Wataalam 2,982 waliosajiliwa kipindi hiki, Wataalam 1,754 walipatiwa usajili wa awali (PRP), usajili wa kudumu ni 1,038 (FRP) na usajili wa kuorodheshwa ni 190 (ERP). Katika kipindi hiki, Baraza liliweza kutoa leseni kwa wapimaji wa VVU wasio wataalam wa maabara 2,882 na kufanya jumla ya wapimaji waliopewa leseni na Baraza hadi sasa kufikia 10,780.

**303. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilisimamia mitihani ya usajili kwa ngazi zote (Astashahada, Stashahada na Shahada), jumla ya maombi mapya ya wataalam ya kufanya mitihani ya usajili yalikuwa ni 1,544. Baada ya kupokelewa maombi hayo, Baraza liliwatahini wataalam hao ambapo; Wataalam

wa Astashahada walikuwa 263, waliofaulu ni 88 sawa na asilimia 33.5; Wataalam wa Stashahada walikuwa 985, waliofaulu 543 sawa na asilimia 55 na Wataalam wa Shahada walikuwa 276 waliofaulu 196 sawa na asilimia 71. Baraza limesaili jumla ya watarajali 339, katika vituo 23 vya kutolea mafunzo ya utarajali. Ambao wanatarajia kufanya mitihani ya usajili wa kudumu baada ya kumaliza mafunzo yao ya utarajali. Aidha, baraza lilifanikiwa kuongeza kituo kimoja (1) cha mafunzo ya utarajali mkoani Kigoma na kufanya vituo vya mafunzo ya utarajali kufikia
23.

**304. Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanya ukaguzi katika vyuo viwili vya kati vilivyoomba kuanzisha mafunzo ya Maaabara Mkoani Kigoma katika chuo cha Afya na sayansi shirikishi Devine na Ruvuma katika chuo cha Afya na sayansi shirikishi Litembo. Ambapo matokeo yalikuwa; Katika chuo cha Afya na sayansi shirikishi Devine walipata asilimia 63.61 na waliekezwa kuendelea na udaihili mara baada ya kukamilisha mapufungufu yaliyo bainishwa. Aidha katika chuo cha Afya na sayansi shirikishi Litembo walipata asilimia 36 na hivyo hawakukidhi vigezo vya kudaili wanafunzi wa Maabara. Baraza limefanya kaguzi kwenye Maabara tatu (3) za hospitali za Rufaa za Mikoa ya Kigoma, Katavi na Ruvuma kwaajili ya mafunzo ya watarajali ambapo matokeo yake yalikuwa; Maabara ya Kigoma tu ndio iliyokidhi vigezo vya kupokea watarajali. Aidha maabara mbili (2) walishauriwa kufanyia kazi mapungufu yaliyobainishwa

**305. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilifanya usimamizi shirikishi kwenye Maabara 109 ngazi zote kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2023 katika mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga, hivyo kufikisha Maabara 296 zilizofanyiwa usimamizi shirikishi tangu Baraza la 6 lilipoanza Mwaka 2020. Mapungufu yaliyoonekana yalijadiliwa katika ngazi ya kituo na kuelekezwa kuyafanyia kazi. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, baraza lilifanikisha kuwapatia wataalam wa

Maabara 196 alama za mafunzo endelevu (CPD). Aidha Baraza limeweza kuandaa na kuanza kutumia mwongozo wa mafunzo endelevu (CPD) kwa wataalamu wa Maabara. Aidha taasisi mbili; kituo cha mafunzo ya masafa marefu (E-learning platfform for health) na Chuo kikuu cha Mzumbe zimeidhinishwa kuwa watoaji wa mafunzo endelevu (CPD Provider). Aidha, baraza limeanza kufanya ufuatiliaji wa wataalamu waliopata mafunzo endelevu baada ya kusambaza vitabu vya mafunzo endelevu (CPD logbook). Baraza linaendelea na mchakato wa kukamilisha moduli ya CPD katika mfumo wa usajili wa wataalam (HPRS).

**306. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hichi, Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ambapo jumla ya mashauri matatu (3) yalifunguliwa dhidi ya Wataalam waliotuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya taaluma zao. Wataalamu hao watatu mmoja ni kutoka kituo cha Afya Likombe mkoa wa Mtwara, Manispaa ya Mtwara, mwingine ni kutoka Zahanati ya Nyotanjema, mkoani Mtwara Halmashauri ya Tandahimba na wa tatu ni Kutoka Zahanati ya Ishihimulwa Mkoa wa Tabora Wilaya ya Uyuwi. Wataalam wawili (Kutoka Mtwara) walishutumiwa kugushi vyeti vya taaluma na usajili na mashauri yao yamepelekwa kushughulikiwa na Jeshi la polisi na Mtaalam mmoja (1) kutoka Uyui Tabora, ameshutumiwa kwa kosa la ukiukwaji wa maadili na shauri lake linasubiri maamuzi ya Baraza. Aidha, katika kipindi tajwa Baraza lilipokea matukio mengine manne (4) ya wahisiwa kugushi vyeti vya taaluma ambapo yote manne yapo kwenye uchunguzi wa awali.

**Baraza la Wataalam wa Afya Mazingira**

**307. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wataalam wa Afya Mazingira limekua likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Sura Na. 428. Pamoja na Kanuni za jumla za Usajili "The Environmental Health Practitioners (General) Regulations, 2011" (GN 388 ya 2011) na taratibu kwa kuzingatia mpango

kazi na bajeti ya mwaka 2022/2023. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Baraza ni kusajili Wataalamu wa Afya Mazingira ili kulinda na kusimamia nidhamu na Maadili katika taaluma ya Afya Mazingira.

**308. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Jumla ya Wataalamu wapya waliosajiliwa ni 397 kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa hadi sasa na baraza kufikia 4,135. Ambapo, Usajili kamili walikuwa wataalam 99 (wenye Shahada ya Afya Mazingira na Stashahada ya Afya Mazingira kabla ya Sheria kuanzishwa); Usajili wa Awali ni 209 (Wahitimu wa Shahada ya Afya Mazingira waliopo kwenye mafunzo kwa vitendo); Usajili wa Kuorodheshwa 86 (wenye Diploma ya Sayansi ya Afya Mazingira baada ya Sheria kuanzishwa); Usajili wa kuandikishwa Wataalamu 3 (wenye ngazi ya Cheti kwenye Sayansi ya Afya Mazingira. Aidha, jumla ya Taasisi 19 zinazotoa huduma za Afya Mazingira zimesajiliwa Huduma za Usafishaji 14; Huduma za upuliziaji wa Viuatilifu 3; Huduma za vyoo vya umma 2. Vilevile, Baraza limesaili na kuratibu jumla ya wahitimu 209 wa Shahada ya Sayansi ya Afya Mazingira kwa ajili ya Mafunzo kwa vitendo katika vituo 26.

**309. Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanya ukaguzi katika vyuo viwili (2) ambavyo vimewasilisha maombi ya kuanzisha Stashahada za Sayansi ya Afya Mazingira ambavyo ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na Chuo Kikuu cha Kimataifa Kampala (KIU). Vyuo vyote vilivyokaguliwa havijakidhi viwango na hivyo kutoruhusiwa kuendesha mafunzo kwa ngazi waliyoomba mpaka pale watakapokamilisha vigezo. Pia Baraza limefanya kaguzi sita (6) kwenye vyuo vya mafunzo ya Shahada na Stashahada za Afya Mazingira ambavyo ni Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Ruaha (RUCU) na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS), Kagemu, Ngudu, Mpwapwa, na Muheza ili waweze kuzalisha Wataalamu wenye umahiri utakaowezesha kutoa huduma bora za Afya Mazingira. Baraza limekamilisha rasimu ya

mwisho ya Mwongozo wa Elimu Endelevu (Continiues Proffessional DevelopmentCPD) ili kuweza kuwapatia wanataaluma maarifa na ujuzi mpya katika taaluma kwa lengo la kuweza kujiboresha na kufanya kazi kwa weledi na kuzingatia miiko na maadili ya taaluma. Mwongozo huu utaingizwa kwenye kituo cha mafunzo ya masafa marefu (E-learning platfform for health) pale utakapoaanza kutumika.

**Baraza la tiba asili na tiba mbadala**

**310. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala ni chombo cha kisheria kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria Namba 23 ya Mwaka 2002 yenye lengo la Kusimamia, Kudhibiti na Kuendeleza shughuli za Tiba Asili na Tiba Mbadala nchini. Baraza limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023 jumla ya wataalam (Waganga na Wasaidizi wa tiba asili na tiba mbadala na wauza dawa za asili) 3,604 wamesajiliwa katika kipindi hiki sawa na asilimia 80 ya lengo la kusajili wataalam 4,500 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na baraza hadi sasa kufikia 43,854. Kati ya Wataalam 3,604 waliosajiliwa, Wataalam 3,380 walipatiwa usajili wa awali (temporary registration), usajili wa kudumu (permanent registration) ni 224. Aidha, Baraza lilisajili dawa asilli kundi la pili ambapo hadi Machi, 2023 Baraza limesajili jumla ya dawa asili 79 Na kufanya jumla ya dawa asili zilizosajiliwa hadi sasa kufikia 93. Pia, Baraza limesajili vituo vya tiba asili 22 na kufanya jumla ya vituo 1,375. Vilevile, Baraza linaendelea na utaratibu wa kusajili wataalam wake na vituo vya kutolea huduma kwa njia ya mfumo wa kielektroniki.

**311. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendesha zoezi maalumu la uhamasishaji na utengenezaji wa leseni za Waganga wa tiba asili kwa papo hapo, zoezi hili lilifanyika katika mikoa ya Lindi na Mtwara ili kupunguza changamoto ya Waganga wengi kufanya kazi bila kuwa na leseni, ambapo jumla ya

Waganga 658 na vituo 45 vilisajiliwa. Baraza la Tiba Asili liliendesha zoezi la ukaguzi wa dawa asili katika maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba Jijini Dar es Salaam na maonesho ya wakulima ya Nanenane mkoani Dodoma ili kuhakikisha dawa za asili zinazotolewa kama zinazingatia ubora unaohitajika. Aidha, katika maonesho hayo jumla ya Waganga wa tiba asili 870 walisajiliwa. Baraza la Tiba Asili liliendesha zoezi la ufuatiliaji wa dawa za asili zilizo sokoni katika mkoa wa Morogoro na Dae es Salaam ili kuhakikisha kama zinazingatia ubora unaohitajika kwa ajili ya matumizi ya jamii. Jumla ya sampulii 25 zimepelekwa kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) kwa ajili ya vipimo vya ubora. Matokeo ya vipimo yataliwezesha Baraza kuchukua hatua za kisheria kwa watengenezaji waliokiuka viwango vinavyotarajiwa na kuweka mikakati ya kuendelea kuboresha shughuli za Tiba Asili na Tiba Mbadala nchini. Aidha, katika kipindi hicho dawa asili aina ya Hensha maarufu kama Mkongo iliyokuwa inamilikiwa na kituo cha Nyasosi Traditional Clinic cha Jijini Dar es Salaam ilifutiwa usajili.

**312. Mheshimiwa Spika,** Baraza lina utaratibu wa kupita na kukagua maeneo ya kutengenezea dawa asili zinazoombewa usajili kwa ajili ya kuona na kutoa mapendekezo yatakayowezesha uzalishaji wa dawa asili zenye ubora na salama. Hivyo, Baraza lilikagua maeneo ya kutengenezea dawa yaliyopo Kinyerezi, Kigamboni, Sinza, Temeke na Gongo la mboto. Aidha, katika kipindi hichi Baraza limeshughulika mashauri matatu ya uvunjifu wa maadili ikiwa mawili ni kutokana na kutoa matangazo ya tiba asili bila kibali na moja lipo mahakama ya Wilaya ya Chemba.

**Bodi ya Maabara Binafsi za Afya**

**313. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ina jukumu la kusajili na kusimamia Maabara Binafsi za Afya nchini. Katika kutekeleza hili Bodi inafanya kaguzi kwa

maabara hizo ili kujiridhisha kuwa zinafuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyowekwa katika utoaji sahihi wa huduma za Vipimo. Bodi ya Maabara Binafsi za Afya imesajili jumla ya Maabara Binafsi 3869 ambapo maabara zinazojitegemea (autonomous) ni 1216 na zilizojishikiza kwenye vituo vya afya, Zahanati, Kliniki na Hospitali (Attached) ni 2653. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023 Bodi ya maabara binafsi ilipokea maombi mapya 407, kati ya hayo 216 ilikuwa ni maabara zinazojitegemea na 191 ni maabara zinazojishikiza katika vituo vya huduma za afya. Aidha bodi imeweza kusajili/kuandikisha jumla ya Maabara Binafsi 238, ambapo maabara zinazojitegemea zilikuwa 137 na maabara zinazojishikiza zilikuwa 101.

**314. Mheshimiwa Spika,** Bodi imefanya kaguzi kwenye Mikoa saba (7) ambayo ni Dodoma, Kagera, Kigoma, Singida, Simiyu, Shinyanga na Tabora na kufanikiwa kukagua jumla ya maabara binafsi 528. Matokeo ya kaguzi hizo yanaonyesha kuwa; asilimia 20 ya vituo hawazingatii uhakiki wa ubora wa ndani wa vipimo (IQC), matengenezo kinga kwa mashine za maabara (PPM) na majengo kutokidhi viwango vya ubora. Asilimia 10 zilibainika kukosa watumishi wenye sifa na hivyo kulazimika kutumia matabibu na wahudumu wa afya kufanya vipimo vya maabara. Uwepo wa huduma za kitabibu kwenye maabara zinazojitengemea (Autonomous). Maabara 171 kati ya 528 sawa na asilimia 32 zilibainika kutosajiliwa au kuandikishwa kwa mujibu wa Sheria, asilimia 10 ya wamiliki wa vituo vilivyokaguliwa kutokuwa na akaunti kwenye mfumo wa usajili wa vituo vya kutolea hudma (HFRS).

**315. Mheshimiwa Spika,** kutokanana mapungufu hayo yaliyobainika kwenye ukaguzi, ofisi ya Msajili Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ilichukua hatua zifuatazo ili kuboresha hali ya huduma hususani vipimo vya maabara; ilitoa elimu ya ubora wa huduma za maabara (**Laboratory Quality Management System)** kwa maabara zote zilizokutwa na mapungufu na kuwataka kuanza mara moja kuzingatia kanuni za ubora ikiwa

ni pamoja na kufanya Sampuli za uhakiki Ubora **IQC** na kuzingatia matengenezo kinga kwa mashine zote za maabara **PPM** na kuajili watumishi wenye sifa; ilitoa Ilani ya kusitisha huduma za maabara binafsi kwa muda wa miezi 3 hadi 6 kabla ya kuzifungia maabara ambazo zilikutwa zinatoa huduma bila kuwa na wataalamu wenye sifa, lakini pia zile zilizokuwa zinatoa huduma bila kuzingatia ubora wa vipimo, hatua hii ilichukuliwa ili kuepusha athari kwa wagonjwa; na mwisho, ilielekeza Maabara zote kufuata taratibu za usajili na kusajiliwa ili ziweze kutambuliwa na kusimamiwa na Bodi kwa mujibu wa Sheria hivyo kutoa huduma zenye ubora kwa wagonjwa, hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanajisajili kwenye mfumo wa Health Facility Registry System **HFRS** hadi kufikia mwezi Machi, 2023.

**Bodi ya Hospitali za Watu Binafsi**

**316. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi ina jukumu la msingi la kusajili na kusimamia vituo vyote vya afya binafsi, lakini pia kumshauri Waziri wa Afya kuhusiana na mambo yote yanayogusa vituo vya binafsi nchini. Bodi imeendelea kutekeleza majukumu yake kufuatana na mpango kazi wake. Mpaka kufikia tarehe 30 Machi 2023, Bodi ilikuwa imesajili **jumla ya vituo vya huduma za afya 3,026,** kati ya vituo hivyo vituo vinavyofanya kazi ni 2,917, vilivyofungwa moja kwa moja ni vituo 23 na vituo 83 vimefungwa kwa muda kutokana na sababu mbalimbali. Aidha katika vituo vinavyofanya kazi kuna Hospitali 207, Vituo vya Afya 292, Zahanati 1726, Kliniki 327, Polyclinics 327, Dialysis Clinics 21 na Vituo vya Uchunguzi (Diagnostic centres) 17.

**317. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, **Jumla ya maombi 146 ya Hospitali binafsi yaliyowasilishwa**, maombi 133 yalikuwa maombi ya vituo vipya na maombi 7 yalikuwa ya vituo vinavyoomba kupandishwa daraja ambapo; Hospitali moja (1) mpya inaombewa kuwa ngazi ya Mkoa, Hospitali moja (1)

inaombewa kubadili ngazi kutoka Polyclinic kuwa Hospitali ngazi ya Wilaya, na nyingine moja (1) inaombewa kubadili ngazi kutoka Hospitali ngazi ya Mkoa kuwa ngazi ya Kanda, Kituo cha Afya kuwa Hospitali ngazi ya Wilaya. Pia kuna kituo kimoja kipya kimeomba huduma ya kuchuja damu na Hospitali 2 ngazi ya Mkoa zimeomba kuongeza huduma ya kitengo cha kuchuja damu. Kamati ilichambua kwa kina maombi hayo na kubaini kuwa vituo 39 sawa na asilimia 27 vimekidhi vigezo vya kusajiliwa, na vituo 107 sawa na asilimia 73 havikukidhi vigezo vya kusajiliwa kutokana na mapungufu mbalimbali ambayo wametakiwa kuboresha ndio wapewe usajili.

**318. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hichi, **jumla ya vituo vya huduma 143 vilisajiliwa,** hii ikijumuisha maombi yaliyokuwa yamewasilishwa kabla ya kipindi cha Julai 2022, kati ya vituo hivyo kulikuwa na Kliniki 20, Polyclinics 35, Dialysis clinics 3, Hospitali ngazi ya Mkoa 1, ngazi ya Wilaya 2, kituo cha afya 1 na Zahanati 79. Aidha, jumla ya mashirika 52 yalileta maombi ya kuidhinishwa kusimamia huduma za afya, ambapo mashirika 36 sawa na asilimia 69 yamekidhi vigezo, mashirika 12 sawa na asilimia 23 yalikuwa na mapungufu madogo madogo yanayohitaji marekebisho na mashirika 5 sawa na asilimia 10 hayajakidhi vigezo.

**319. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake na kuhakikisha huduma zinaboreshwa Wizara kupitia bodi ya Hospitali binafsi ilifanya ukaguzi wa vituo vinavyotoa huduma za afya vya binafsi katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Singida na Pwani. **Jumla ya vituo 471 vilikaguliwa** kati ya hivyo kulikuwa na Hospitali 18, Vituo vya afya 39, zahanati 304, Polyclinic 35 na Kliniki 27. Katika ukaguzi wa mikoa hiyo jumla ya vituo 51 huduma zilisitishwa kutokana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhaba mkubwa wa watumishi, miundombinu chakavu na kutozingatia miongozo ya kukinga na kuzuia maambukizi.

**320. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia bodi yake, ilifuatilia malalamiko yaliyowasilishwa kuhusiana na Hospital moja (1) mkoa wa Mwanza, kituo cha Afya kimoja kutoka Tarime Mkoani Mara, Hospitali moja na Kliniki moja ya kibingwa (Specialised Polyclinic), zote kutoka Mkoani Dar es Salaam Malalamiko haya yalifuatiliwa na hatua stahiki zilichukuliwa kutokana na matokeo ya uchunguzi. Hospitali ya Mwanza walitakiwa kuboresha huduma kwa kuajiri Daktari Bingwa wa Watoto, Kituo cha Afya Tarime huduma zilisitishwa ili wafanye maboresho pamoja na kuajiri watumishi wenye sifa, Hospitali ya Dar es Salaam wametakiwa kuajiri watumishi kutosheleza ikama ya kituo cha Afya kwani watumishi waliopo hawakidhi ikama ya Hospitali na Kliniki ya kibingwa (Specialised Polyclinic), iliyopo Dar es Salaam wametakiwa kuongeza vitendea kazi na kuongeza wauguzi.

## F. VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**321. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara ya Afya imejiwekea vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha huduma za afya nchini: -

i. Kuimarisha huduma za Kinga dhidi ya magonjwa ikiwemo huduma za chanjo, huduma za lishe, huduma za usafi na afya mazingira na huduma za afya ngazi ya jamii;

ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya umma katika ngazi zote;

iii. Kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na damu salama katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya;

iv. Kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vya watoto wachanga;

v. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi ili kusogeza huduma hizi karibu na wananchi na kuwapunguzia gharama za kupata matibabu haya nje ya nchi.

vi. Kuimarisha huduma za Afya ya Akili, huduma za utengamao na Tiba Shufaa

vii. Kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatari ya kuambukiza;

viii. Kudhibiti magonjwa ya kuambukiza hususani Malaria, Kifua Kikuu (TB), VVU/UKIMWI na Homa ya ini.

ix. Kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza na kuimarisha huduma za dharura nchini ikiwemo ajali;

x. Kuimarisha upatikaji wa wataalam katika Sekta ya Afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi

xi. Kuendeleza na kusimamia huduma za tiba asili na tiba mbadala nchini

xii. Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu;

xiii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini;

xiv. Kusimamia tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za Afya;

**322. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika mwaka 2023/24, Wizara imekadiria

kutumia kiasi cha **Shilingi 1,234,816,516,000.00** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na uendeshaji wa Ofisi na miradi ya maendeleo.

Baadhi ya shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

1. Katika kuimarisha huduma za Kinga dhidi ya magonjwa ambapo kiasi cha shilingi, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuimarisha utekelezaji wa Afua za Chanjo kwa watoto nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 114,369,238,904.00** kimetengwa. Afua hizo ni:-

a) Kununua, kutunza na kusambaza chanjo kwa gharama ya **Shilingi 87,044,538,781**.

b) Kununua majokofu 1,601 ya mnyororo baridi wa chanjo yenye thamani ya **Shilingi 21,025,327,723**.

c) Kununua magari 102 ya kusambazia chanjo yenye thamani ya **Shilingi 6,299,372,400.** ii. Kuimarisha huduma za lishe kwa kununua na kusimika vinu 300 vya kuongeza virutubisho na kutoa matone ya Vitamin A kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) ili kuboresha huduma za Lishe nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000.00** kimetengwa

iv. Kuimarisha utekelezaji wa afua za usafi na afya mazingira katika jamii na taasisi za umma na binafsi, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

a) Kusimamia uwepo wa miundombinu ya usafi na afya mazingira, (vyoo bora, vifaa vya kunawia mikono) katika jamii na taasisi za umma na binafsi

b) Kuhakikisha mamlaka za Serikali za mitaa zinasimamia sheria ndogo za usafi na afya mazingira katika maeneo ya

makazi na taasisi katika kudhibiti wadudu/wanyama dhurifu na uchafuzi wa mazingira.

c) Kuzuia na kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuambukiza kuingia nchini kwa kuimarishamiundombinu na huduma za afya mipakani

v. Kuanzisha mafunzo maalumu ya miezi sita kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao 5,000 ambao wataajiriwa na kupewa vitendea kazi na kiasi Shilingi 13,500,000,000 kimetengwa

2. Katika kuboresha ubora wa huduma, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

i. Kuanzisha programu ya mabadiliko ya kiutendaji kwa wasimamizi na watoa huduma za afya (**Leadership 4 Health Transfomation Program**) ili kuongeza uwajibikaji, ufanisi na tija katika utoaji wa huduma za afya katika ngazi zote

ii. Kuimarisha utawala bora, uongozi na menejimenti ya usimamizi wa huduma za afya kwa kushirikisha kamati za ulinzi na usalama na viongozi na watendaji wa Serikali katika ngazi zote.

iii. Kufanya kaguzi za mara kwa mara pamoja na kuimarisha usimamizi shirikishi katika vituo vya kutolea huduma za afya

iv. Kuhakikisha utoaji wa huduma za afya unazingatia weledi, maadili na miiko kupitia mabaraza ya kitaaluma na bodi za usajili ikiwemo kuanzisha mfumo wa kuwatambua na kuwapa tuzo wataalam wanaofanya vizuri

v. Kujenga na kukarabati Miundombinu ya kutolea Huduma za afya katika ngazi ya Taifa hadi Hospitali za Rufaa

za Mikoa ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 91,898,000,000.00** kimetengwa. Maeneo yaliyohusika ni pamoja na;

a) Kuendelea na ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda za Chato, Mtwara; na kuanza ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi na Hospitali Maalum ya Taifa ya huduma za Mama na Mtoto katika Mkoa wa Dodoma ambapo jumla ya **Shilingi 29,572,910,244** kimetengwa.

b) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali (4) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa mipya ya Katavi, Geita, Songwe na Simiyu ambapo jumla ya Shilingi bilioni 13 kimetengwa.

c) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali mpya tatu (3) za Rufaa za Mikoa katika Mikoa ya Shinyanga, Singida na Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Mara ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 11 kimetengwa.

d) Kuendelea kukamilisha upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika hospitali Rufaa za Mikoa za Ligula (Mtwara) Kagera, Maweni (Kigoma), Kitete (Tabora), Sekou – Toure (Mwanza) na Mawenzi (Kilimanjaro), Songea (Ruvuma), Manyara, Bombo (Tanga), Mount Meru (Arusha), Sokoine (Lindi), Mbeya, Hospitali ya Ukerewe na uimarishaji wa Hospitali za Rufaa (dharura) ambapo kiasi cha **Shilingi 36,398,000,000** kimetengwa.

e) Kuendelea na ujenzi wa wodi ya wagonjwa binafsi (Private word katika hospitali ya Taifa Muhimbili) ambapo kiasi cha Shilingi 4,500,000,000 kimetengwa.

v. Kuanzisha utaratibu wa kupima utendaji wa timu za uendeshaji wa huduma za afya katika ngazi za Vituo/ Hospitali, Halmashauri (CHMT) na Mikoa (RHMT) katika maeneo ya maoteo ya dawa, upatikanaji wa dawa, huduma za uchunguzi (maabara na Radiolojia) udhibiti wa kuchina na

kuchotora wa dawa, taratibu za kushughulikia malalamiko ya wagonjwa, muda wa kuwahudumia wagonjwa.

vi. Kuunganisha baadhi ya mabaraza ya kitaaluma na kuhamasisha wanataaluma wengi kusajiliwa kwa kupunguza kiwango cha ada za usajili.

vii. Kuhamisha majukumu ya usimamizi wa Maduka ya Dawa kutoka Baraza la Wafamasia na kuhamishia Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba ili Baraza lijikite zaidi katika kusimamia wanataaluma.

viii. Kuimarisha mfumo wa rufaa wa wagonjwa ili kuwezesha Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa kujikita katika kutoa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi.

3. Katika kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za uchunguzi wa magonjwa, yafuatayo yamepewa kipaumbele;

i. Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maabara za uchunguzi wa magonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikiwemo upatikanaji wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara

ii. Kusogeza huduma za radiolojia kwa wananchi kwenye ngazi za afya ya msingi (ununuzi wa Ultrasound na digital Xrays)

iii. Kuratibu na kusimamia mpango wa matengenezo na matengenezo kinga ya vifaa na vifaa tiba ikiwa ni pamoja na kuanzisha karakana, kutoa mafunzo ya mafundi na kununua vifaa na vipuli vya matengenezo

iv. Kusimamia ubora wa huduma kwa kuzingatia miongozo ya ubora kwa maabara zote hadi ngazi ya afya ya msingi ili kupata ithibati

4. Katika kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na damu salama katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya, kiasi cha **Shilingi 205,063,250,000.00** kimetengwa kwa malengo yafuatayo:

i. Kuimarisha uandaaji wa Maoteo ya dawa kutoka katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma kwa kuwasimamia kikamilifu wafamasia wa Halmashauri na mikoa kwa kuweka mfumo wa uwajibikaji na kuhakikisha wanatumia mifumo iliyopo ya maoteo ya dawa na taarifa za wagonjwa.

Nitumie fursa hii kuwaelekeza Wafamasia katika ngazi ya Halmashauri na Mikoa kuandaa na kuwasilisha maoteo sahihi ya dawa na vifaa tiba kabla ya tarehe 31 Januari ya kila mwaka kwa mujibu wa kanuni namba 141 ya kanuni za ununuzi wa umma za mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake.

ii. Kununua, kutunza na kusambaza bidhaa za Afya katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

iii. Kujenga maghala mapya ya kuhifadhia dawa katika mikoa mbalimbali nchini

iv. Kuweka mifumo thabiti ya udhibiti na ukaguzi wa dawa nchini ikiwemo kuimarisha kamati za tiba na dawa (Therapeutic committees) kwa kuzifanyia mapitio na kuzijengea uwezo ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu

v. Kufanya kaguzi za mara kwa mara za hali ya dawa katika vituo ili kudhibiti upotevu na kuzuia kuchina kwa dawa

vi. Kusimamia matumizi sahihi ya miongozo ya matibabu kwa magonjwa (STGs) kwa kuhakikisha watoa huduma za afya wanatumia miongozo hii.

5. Katika kuimarisha ubora wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kiasi cha **Shilingi 16,216,250,000** zimetengwa na kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na;

i. Kusimamia upatikanaji wa huduma bora na salama za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa wakati ikiwemo kufanya uhakiki na kaguzi za mara kwa mara katika vituo vya kutolea huduma ili kuhakikisha huduma zinazotolewa kwa wajawazito na watoto wachanga zinazingatia ubora, weledi, maadili na ziendane na miongozo ya kitaifa.

ii. Kuhakikisha uzingatiwaji wa miongozo ya kutoa huduma za uzazi salama kabla na baada ya kujifungua ikiwemo kuhakikisha wajawazito wanafanyiwa vipimo vyote muhimu hususani wingi wa damu, sukari, Shinikizo la damu (BP), uzito, protein kwenye mkojo na maambukizi mengine wakati wa ujauzito ili kubaini viashiria vya hatari na kuchukua hatua stahiki kwa wakati

iii. Kutoa mafunzo kazini na unasihi (on job training and clinical mentorship) kwa kushirikiana na vyama vya kitaaluma mfano Chama cha Wauguzi Tanzania (TANNA), Chama cha Madaktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake na uzazi (AGOTA) ili kuwaongezea ujuzi na weledi (Skills and competence) wataalam wa ngazi za msingi katika kuwahudumia wajawazito na watoto wachanga. Kupitia mpango huu, wataalam bingwa na bobezi 100 wakiwemo Madaktari bingwa, wauguzi, wakunga, na watoa dawa za usingizi wameandaliwa kutekeleza mpango huu kwa awamu ya kwanza.

iv. Kununua na kusambaza dawa muhimu za uzazi salama ikiwemo dawa Magnesium sulphate (za kuzuia kifafa cha mimba), Oxytocin (dawa za kuzuia mjamzito kutoka damu wakati na baada ya kujifungua), FeFo (kwa ajili ya kuongeza damu) na SP (kwa ajili ya malaria), dawa za uzazi wa mpango, dawa za watoto wa umri wa chini ya miaka 5 kwa

ajili ya kinga za minyoo, dawa za kuongeza damu na dawa za Malaria.

v. Kununua Vifaa Tiba kwa ajili ya Upasuaji kwa wajawazito na kuvisambaza katika vituo 278 vya afya msingi katika mikoa yote.

vi. Kuongeza wodi maalum 100 zenye vifaa vya kutolea huduma za watoto wachanga zikiwemo huduma za Mama Kangaruu (Kangaroo mother care) na huduma za watoto wachanga mahututi (Neonatal Intensive Care Unit-NICU)

vii. Kuongeza vituo vipya 100 vinavyotoa huduma za uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi

viii. Kuongeza vituo vipya 300 vya kutoa huduma rafiki kwa vijana

ix. Kuongeza vituo vipya 16 vinavyotoa huduma jumuishi kwa wahanga wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto

x. Kuendelea na ujenzi wa Hospitali Maalumu ya Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto Dodoma.

6. Katika kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi kiasi cha **shilingi 23,000,000,000.00** kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kuendelea kutoa huduma za matibabu ya ubingwa bobezi katika, Taasisi, Hospitali za Kanda na Maalum pamoja na kuanzisha huduma mpya kulingana na mahitaji;

ii. Kuanzisha programu ya kugharamia huduma za matibabu ya ubingwa bobezi yanayotolewa na Hospitali za ndani ya nchi hususan kupandikiza figo, kupandikiza uloto kwa watoto, kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto na

kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu ambapo kiasi cha **shilingi 5,000,000,000.00** zimetengwa;

iii. Kuimarisha **miundombinu** katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Hospitali maalum ya Kibong'oto na Hospitali za Rufaa za Kanda za KCMC, Bugando, Mbeya na Benjamin Mkapa. Kiasi cha **Shilingi** 10,000,000,000.00 zimetengwa;

iv. Kuwekeza katika vifaa tiba, vifaa vya uchunguzi na vitendanishi vitakavyowezesha utoaji wa huduma za kibingwa bobezi ikiwemo kupandikiza figo, kupandikiza uloto, kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto na kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu ambapo Kiasi cha **Shilingi** 8,000,000,000.00 zimetengwa;

v. Kuimarisha utoaji wa huduma za mkoba na tembezi katika ngazi ya msingi;

vi. Kuimarisha na kuongeza wigo wa ushirikiano na Taasisi/Hospitali za kimataifa zinazotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ikiwemo kupeleka wataalamu katika hospitali hizo na kufanya kambi za pamoja za matibabu;

vii. Kuhakikisha Hospitali na taasisi za ubingwa bobezi zinatekeleza mpango wa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wataalam wao ili kuwaongezea ujuzi na weledi wa kutoa huduma za ubingwa bobezi.

7. Katika kuimarisha huduma za Afya ya Akili, huduma za utengamao na Tiba Shufaa, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja:

i. Kutoa elimu kwa umma kuhusu vihatarishi vya afya ya akili na namna ya kukabiliana navyo;

ii. Kuhakikisha upatikanaji wa wataalamu wa afya ya akili kwa kushirikiana na vyuo vikuu na vyuo vya kati. Kwa mwaka 2023/24 Chuo kikuu cha Afya MUHAS kinaanzisha shahada ya kwanza ya Sayansi ya Saikolojia tiba (Clinical Psychology). Aidha, Vyuo vya kati pia vitaanzisha mafunzo ya wataalam wa afya ya akili ili kusogeza huduma za afya ya akili karibu na jamii;

iii. Kuanzisha kozi maalum za muda mfupi za Afya ya Akili na huduma za utengamao ili kupata wataalam watakaoenda kutoa huduma hizi katika vituo vyetu vya ngazi ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa hadi ngazi ya Afya ya Msingi katika kipindi ambacho tunaandaa watalaam wabobezi katika taaluma hizo;

iv. Kuipandisha hadhi na kuiongezea majukumu Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe na kujenga miundombinu ya kutolea huduma za Afya ya Akili ambapo kiasi cha Shilingi 2,000,000,000.00 kimetengwa;

v. Kuimarisha huduma za Afya ya Akili kwa wagonjwa wa nje wa kuanzia na Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Halmashauri.

vi. Kufanya utambuzi wa vituo vinavyotoa huduma za afya ya akili.

vii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa vya uchunguzi na vifaa tiba kwa ajili ya wagonjwa wa afya ya akili;

viii. Kuhakikisha upatikanaji wa wataalamu wa huduma za utengamao kwa kushirikiana na vyuo vikuu na vyuo vya kati, kipaumbele kikiwa ni kuanzisha mafunzo ya kada za kati katika eneo la huduma za utengamao hususan tiba mazoezi (physiotherapy), tiba kazi (occupational therapy) na Tiba lugha na tiba matamshi (speech therapy);

x. Kuimarisha na kuanzisha huduma za tiba za utengamao (rehabilitative medicine services) hususan kwa watoto katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri

xi. Kuimarisha huduma za utengamao na kuanzisha vituo maalum vya huduma hizo ikiwemo za wagonjwa wa Kiharusi (Stroke centers) ili kuboresha huduma hizo, kuwawezesha kumudu shughuli zao kadri inavyowezekana na kuongeza ubora wa maisha.

xii. Kufanya utambuzi wa vituo vinavyotoa huduma za tiba za utengamao

xiii. Kuimarisha upatikanaji wa viungo saidizi kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa viungo, ikiwa ni pamoja na kuimarisha karakana za kutengeneza viungo hivyo na mafunzo kwa wataalam; na

8. Ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatari ya kuambukiza, kiasi cha **Shilingi 20,750,402,000.00** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza afua zifuatazo:

i. Kuendeleza ujenzi wa vituo vya kuhudumia wagonjwa na wahisiwa wa magonjwa hatari ya kuambukiza (Highly Infectious Disease Treatment Unit) Kisopwa Dar es Salaam na kuanza ujenzi wa kituo katika Mkoa wa Kagera.

ii. Kutoa mafunzo ya wataalam wa Sekta mbalimbali zinazogusa masuala ya afya (one health) ikiwemo kuendesha mafunzo kwa vitendo (simulation exercises) angalau mara mbili kwa mwaka ili kuimarisha uwezo wa nchi katika kujiandaa na kukabiliana na magonjwa hatari ya milipuko

iii. Kuandaa na kuboresha mifumo ya uratibu wa majanga na milipuko ya magonjwa hatari ikiwemo uanzishwaji wa Vituo vya Operesheni ya Matukio ya Dharura (PHEOCs) katika mikoa mitano (5)

iv. Kutoa mafunzo kwa waendeshaji wa vituo vya Operesheni wa Matukio ya Dharura katika ngazi ya mikoa nchini ambapo wataalam wa mikoa mitano itapatiwa mafunzo.

9. Katika Kutekeleza Afua mbalimbali za kudhibiti magonjwa ya kuambukiza hususani Malaria, Kifua Kikuu (TB), VVU/UKIMWI na Homa ya ini, kiasi cha **Shilingi 101,456,809,628.00** kimetengwa. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni:

i. Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria ambapo kiasi cha **Shilingi 25,363,979,112.00** kimetengwa kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa vyandarua vyenye dawa kwenye jamii, ununuzi wa vitendanishi na dawa ili kuwezesha ugunduzi na matibabu ya ugonjwa malaria pamoja na ufuatiliaji wa wagonjwa kwenye maeneo yanayotekeleza afua za kutokomeza malaria.

ii. Utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 16,173,530,473.00** zimetengwa kwa ajili ya uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu kwenye jamii, tiba kinga dhidi ya kifua kikuu kwa WAVIU na watoto chini ya miaka mitano wanaoishi na waliopata maambukizi ya Kifua Kikuu, ununuzi wa vifaa tiba, vitendanishi na dawa, huduma za uchunguzi na matibabu ya kifua kikuu na kifua kikuu sugu.

iii. Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, homa ya ini na magonjwa ya ngono nchini ambapo kiasi cha **Shilingi 59,919,300,043.00** kimetengwa kwa ajili ya manunuzi ya vitendanishi vya kupima VVU, kondomu, dawa kinga na dawa za kufubaza VVU.

10. Ili kudhibiti Magonjwa yasiyo ya kuambukiza pamoja na kuimarisha huduma za dharura nchini ikiwemo ajali, kiasi cha

**Shilingi 22,000,000,000.00** zimetengwa. Maeneo yatayotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kutoa elimu kwa umma kuhusu vichochezi na visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza kama vile tabia bwete, uzito uliokithiri, matumizi ya sukari, chumvi na mafuta kupita kiasi ambavyo vinaweza kusababisha magonjwa ya Kisukari, Shinikizo la Juu la Damu na magonjwa ya moyo

ii. Kuimarisha huduma za uchunguzi ili kuweza kuyatambua mapema magonjwa yasiyoambukiza yaliyopewa kipaumbele

iii. Kuimarisha huduma za utambuzi na matibabu ya magonjwa ya Damu ikiwemo ugonjwa wa selimundu (Sickle Cell) na himofilia (hemophilia) pamoja na kufanya upandikizaji wa uloto (bone marrow transplant) ambapo kipaumbele kitatolewa kwa watoto chini ya umri wa miaka 12.

iv. Kuimarisha upatikanaji wa dawa za kutibu magonjwa yasiyoambukiza ambapo kuanzia Julai 2023, aina mbili (2) za dawa za kutibu shinikizo la juu la damu zitapatikana katika ngazi ya Zahanati na aina tano (5) za dawa hizi zitapatikana katika ngazi ya Vituo vya Afya (Health Center) ambapo awali zilikuwa zinapatikana katika katika ngazi ya Hospitali za Halmashauri

v. Kuimarisha mfumo wa kuwahudumia wagonjwa wa dharura na ajali na kuwasafirisha kutoka kituo kimoja kwenda kingine ili kupata huduma za rufaa. Wizara itatekeleza yafuatayo:

a) Kujenga miundombinu kwa ajili ya vituo vya uratibu wa magari ya wagonjwa (ambulance dispatch centers) katika mikoa 5 ya kimkakati kwa awamu ya kwanza;

b) Kufunga mfumo wa uendeshaji, ufuatiliaji na uratibu wa magari yote ya wagonjwa na uokozi ili kuboresha huduma hizi na kupunguza vifo vinavyozuilika vinavyotokana na kuchelewa kufika kwa magari ya uokozi katika matukio ya ajali na kuwasafirisha majeruhi wa ajali kwenda katika vituo vya tiba;

c) Kuanzisha na kuimarisha mfumo wa kielectroniki wa takwimu za ajali (trauma registries) kwenye idara za dharura nchini ili kuratibu taarifa za kiafya za wahanga wa ajali na kuwezesha mikakati ya kuzuia na kupunguza madhara yanayotokana na ajali;

d) Kuanzisha mafunzo kwa watoa huduma za dharura nje ya hospitali na kuandaa kanuni za usimamizi na uendeshaji. Hii ni pamoja na kuandaa mtaala kwa ajili ya watoa huduma za magari ya wagonjwa (paramedics) kwa kushirikiana na Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu nchini. Kwa awamu ya kwanza, mafunzo yatafanyika kwa watoa huduma 6 kwa kila ambulance wakiwemo wauguzi, maafisa tabibu, madaktari na madereva. Pia mafunzo shirikishi yatafanyika kwa jeshi la polisi, jeshi la zimamoto na uokoaji na wananchi wa kujitolea; na

e) Kuendelea kutoa mafunzo kwa vitendo (mentorship) kwa watoa huduma za EMD kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri ili kuboresha huduma za dharura nchini

11. Katika kuimarisha upatikaji wa wataalam katika Sekta ya Afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi kiasi cha **Shilingi 83,142,000,000.00** kimetengwa. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni:

i. Kuandaa na kuweka mpango wa muda mrefu wa watoa huduma wa afya ili kukidhi mahitaji (human resource planning);

ii. Kutoa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya vya umma na kusimamia ubora wa mafunzo haya katika vyuo vya umma na binafsi;

iii. Kuendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa wataalam wa ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi 649 wanaoendelea na wataalam wapya 450 pamoja na kufadhili mafunzo ya kada za kati za kimkakati ambapo kiasi cha **Shilingi 17,142,000,000.00** kimetengwa;

iv. Kugharamia mafunzo kwa vitendo ya watarajali (Interns) wa kada mbalimbali za Afya wakiwemo Madaktari Wauguzi, Wafamasia, wataalam wa maabara na wataalam wa afya mazingira. Kiasi cha **Shilingi 56,000,000,000.00** kimetengwa;

v. Kukarabati na kujenga majengo mapya katika vyuo vya mafunzo ya Afya vya umma, ambapo kiasi cha **Shilingi 6,000,000,000.00** zimetengwa; na

vi. Kufufua Chuo cha mafunzo endelevu kwa wataalam wa afya walioko kazini (Center for Educational Development in Health-CEDHA), ili kuimarisha weledi, maadili, ujuzi na uongozi katika sekta ya afya. Kiasi cha **Shilingi 4,000,000,000.00** kimetengwa.

12. Katika kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu, ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 2.5** kimetengwa. Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma na kupunguza muda wa wananchi kusubiri kupata huduma za afya. Hatua hii pia itawezesha kudhibiti udanganyifu na upotevu wa rasilimali fedha, dawa na bidhaa zingine za afya;

ii. Kuunganisha mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Afya ili iweze kusomana, kuleta ufanisi na kupunguza usumbufu kwa watoa huduma na wananchi;

iii. Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA katika ngazi zote za kutoa huduma za afya ; na

iv. Kuanzisha kituo cha Taifa cha Umahiri wa masuala ya TEHAMA katika Sekta ya Afya (Center for digital Health).

13. Katika kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kukamilisha Mwongozo wa Taifa wa uchangiaji wa huduma za afya;

ii. Kuimarisha mfuko wa Taifa wa Bima ya afya; iii. Kufanya mapitio ya mahitaji ya rasilimali fedha kwa ajili ya huduma za sekta ya afya (resource tracking studies);

iii. Kutafuta na kuratibu upatikanaji wa fedha za Afya kutoka kwa wadau wa maendeleo ikiwemo kuratibu mfuko wa afya wa pamoja (Health Basket Fund); na v. Kufuatilia rasilimali fedha za afya zinazopelekwa kwa Asasi zisizo za kiserikali kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Wizara inayosimamia Usajili wa Asasi hizo.

14. Katika kuimarishaji shughuli za Tafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu ya Taifa (NIMR), kiasi cha **Shilingi 20,378,969,000** kimetengwa ili kutekeleza afua hii.

**G. SHUKRANI**

**323. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka kwa nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za Afya na Ustawi wa Jamii.

**324. Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Canada (DFATD), Denmark (DANIDA), Ireland (Irish Aid), Uswisi (SDC), Korea Kusini (KOICA) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini hususani afya ya msingi. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za China, Cuba, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali ikiwemo kufadhili miradi mbalimbali inayotekelelezwa na Serikali kwa kushirikia na Mashirika yasiyo ya kiSerikali ili kuboresha huduma za afya nchini.

**325. Mheshimiwa Spika,** nayashukuru pia mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS, UNDP, UNFPA, UN-Women, WHO na IAEA); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); IMF, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); GAVI; PEPFAR; CDC; USAID; PMI; Abbott Fund; DFID; EED; Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF); GIZ; Global Fund (for HIV, TB na Malaria); Bill and Melinda Gates Foundation; Good Samaritan Foundation (GSF); HelpAge International; John Snow Incorporation (JSI); JICA; KfW; Save the Children; World Vision; Benki ya STANBIC; Walter REED; Jhpiego na Delloite

**326. Mheshimiwa Spika,** niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya KiSerikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na Benjamin Mkapa Foundation, AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International,

SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosciation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, Kivulini, WiLDAF, TCRF na FSDT.

**327. Mheshimiwa Spika,** navishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya.

**328. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha utendaji wangu wa kazi, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb.),** Naibu Waziri wa Afya. Aidha, naomba kuwashukuru **Dkt. Seif A. Shekalaghe** Katibu Mkuu na **Dkt Grace Maghembe,** Naibu Katibu Mkuu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Tumaini Nagu**, Mganga Mkuu wa Serikali, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nawashukuru pia Wakurugenzi Wakuu wa Hospitali za Taifa na Kanda ambao ni **Prof. Mohamed Janabi** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Dkt. Respicious L. Boniface** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Dkt Peter Kisenge** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Julius Mwaiselage,** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dkt. Leonard Subi** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dkt. Paul S. Lawala** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Dkt. Alphonce Chandika** (Hospitali ya Benjamin Mkapa), **Dkt. Brian Mawala** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), **Dkt. Fabian A. Massaga** (Hospitali ya Bugando) na **Prof. Geleard Masenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC).

**329. Mheshimiwa Spika,** kipekee naomba kuwashukuru wakurugenzi na wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambazo ni MSD, NHIF, TMDA, NIMR, Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, TFNC pamoja na Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili. Vilevile ninawashukuru Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa Sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa watanzania kujali na kulinda afya zao ikiwemo kwa kuzingatia ulaji wa vyakula unaofaa, kufanya mazoezi ya viungo mara kwa mara na kujiepusha na unywaji wa pombe kupita kiasi. Ni muhimu watanzania wakatambua kuwa Afya ni Mtaji.

**330. Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii pia kuishukuru Familia yangu, upendo wao mkubwa sana kwangu na kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo na kuniombea heri katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa heshma na unyenyevu mkubwa ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Tanga Mjini kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na ya kitaifa. Licha ya majukumu ya kitaifa niliyonayo, nitumie Bunge lako Tukufu kuwahakikishia wana Tanga Mjini kuwa nitaendelea kuwaenzi na kutimiza wajibu wangu wa kuwatumikia bila kuchoka ili kuleta maendeleo ya haraka katika jimbo letu.

## H. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2023/24

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka** 2023/24

**331. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 677,621,168,390.95**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 88,414,775,177.00** zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 111,585,224,823.00** zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, **Shilingi 477,621,168,390.95** zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la **asilimia 9** ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2022/23 ambayo yalikuwa ni kukusanya Shilingi **622,986,024,980.00**.

**332. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2023/24, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 502,951,909,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 41** ya bajeti tengwa, ambapo kiasi cha **Shilingi 354,342,486,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha **Shilingi 148,609,423,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**

**333. Mheshimiwa Spika**, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 732,364,607,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 59** ya bajeti tengwa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi 430,298,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 302,066,607,000.00**

**334. Mheshimiwa Spika**, jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni **Shilingi 1,235,316,516,000.00** ili kuweza kutekeleza malengo iliyojiwekea.

| Na | Matumizi ya Kawaida | % | Miradi ya Maendeleo | % | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 502,951,909,000.00 | 41 | 732,364,607,000.00 | 59 | 1,235,316,516,000.00 |

**335. Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya www.moh.go.tz.

**336. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante kwa kusoma vizuri, na hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wapo Bungeni muda huu. Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya ambao ni Ndugu Ally Jecha Amir, mgonjwa aliyepandikizwa figo katika Hospitali ya Benjamini Mkapa, ameambatana na Ndugu Makia Ibrahim Mussa ambaye ni mke wake alimtolea figo. Hongereni sana. Hayo ndiyo mapenzi hayo. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ni timu ya Madaktari Bingwa wa Huduma za Afya ya Mama na Mtoto kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wakiongozwa na Dkt. Carol Daniel. Hongereni, jukumu mlilopewa ni kubwa, Mungu awatangulie. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, ni wanafunzi 150 na walimu 20 kutoka Shule ya Sekondari Mbabala ya Jijini Dodoma. Karibuni. Wapo wageni 35 ambao ni viongozi na wachezaji kutoka Kaliua *Veteran Sports Club* Mkoani Tabora.

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* anaomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa kesho Jumamosi, tarehe 13 kutakuwa na mechi ya kirafiki ya mpira wa miguu kati ya timu ya mpira wa miguu ya Wabunge na timu ya Mpira wa Kaliua *Veteran.* Mechi hiyo itachezwa uwanja wa Jamhuri saa moja asubuhi, wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Afya na Masuala ya *UKIMWI.*

**MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasoma taarifa hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo. Kwanza kabisa naomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya *UKIMWI* kuhusu Utekelezaji wa Bajeti wa Wizara ya Afya kwa Mwaka Fedha 2022/2023, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kwanza natoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu; utangulizi, utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa mwaka wa fedha 2023/2024, na Maoni na Ushauri na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ilifanyika kwa kuzingatia Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023. Ziara hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi, 2023 katika Mkoa wa Iringa, Mbeya pamoja na Songwe. Taarifa ifuatayo inaeleza miradi iliyotembelewa na kukaguliwa, hali ya utekelezaji na mambo yaliyobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi iliyotembelewa ni pamoja na Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Iringa, mradi wa ukarabati wa jengo la uangalizi maalum kwa maana ya *ICU*, mradi wa jingo la mionzi *(Radiology)*, Ununuzi wa *CT-Scan* na *Digital X-Ray*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri, ujenzi na ukarabati unaoendelea katika Hospitali ya Rufaa ya Iringa, Kamati ilibaini kuwepo na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Hospitali hii. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ufinyu wa eneo la hospitali hali inayoleta ugumu wa kuongeza majengo ya kutolea huduma;

(ii) Ukosefu wa wataalamu wa kutoa huduma za kibingwa za mifupa, njia ya mkojo, masikio na kadhalika;

(iii) Upungufu wa majengo kama jengo la macho, jengo la kutolea huduma za nje *(OPD)* na jengo la kutolea huduma za kuzoeza viungo *(physiotherapy);*

(iv) Wagonjwa wengi kutomudu gharama za matibabu, hali inayopelekea hospitali kutoa misamaha kwa wadaiwa; na

(v) Upungufu wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Kanda, Mbeya (Hospitali ya Wazazi - Meta). Mradi wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya una thamani ya shilingi 12,329,277,541.99. Kamati ilitembelea mradi huu mwezi Machi,2023 mradi ulikuwa umefikia asilimia 99.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza mradi huu wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya kwani itasaidia kuokoa maisha ya wananchi kwa kuwa itahudumia mikoa saba ambayo ni Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Rukwa pamoja na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe unakadiriwa kugharimu zaidi ya shilingi bilioni 9.7. Kamati ilijulishwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 4.5 kimepokelewa, sawa na asilimia 46.7. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni mbili kimepokelewa mwaka wa fedha 2022/2023 ikiwa ni asilimia 100 ya fedha iliyotengwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga hospitali ya rufaa kwa ajili ya mkoa mpya wa Songwe kwani uwepo wa hospitali hiyo utaokoa maisha ya wananchi ambao walikuwa wakipelekwa hospitali

ya rufaa ya kanda Mbeya ambayo ipo umbali wa Kilometa 201.5 kutoka Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati pia ilibaini changamoto ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa mradi huu ambazo ni: -

(i) Mkandarasi SUMA JKT, kutokuwa na nguvu kazi ya kutosha hivyo kufanyika taratibu kinyume na mkataba;

(ii) Fedha kutokupelekwa kwa wakati hali inayosababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi;

(iii) Vifaa vya ujenzi kutopatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya kamati kuwa, changamoto hizi zitatafutiwa ufumbuzi ili mradi huu uweze kutekelezwa kwa kasi inayotarajiwa na kukamilika kwa wakati ili wananchi wa maeneo hayo waanze kunufaika na huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2022/2023. Kufuatia ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na kukaguliwa, kamati imebaini mambo mbalimbali ambayo imeyatolea maoni ili kuleta ufanisi wa utekelezaji. Yafuatayo ni mambo yaliyobainika katika ziara:-

(i) Hali ya Upatikanaji wa Fedha, kamati imebaini kuwa bado hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya miradi si ya kuridhisha. Kwa mfano, katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Songwe, mpaka mwezi Machi, 2023 kamati ilipotembelea mradi huu, fedha zilikuwa zimetolewa kwa asilimia 46.7 tu ilihali muda uliopangwa kukamilika kwa mradi huo ni tarehe

31 Mei, 2023. Ni imani ya kamati kuwa Serikali itatoa fedha hizo kabla mwaka wa fedha 2022/2023 kuisha ili mradi huu na miradi mingine iliyopangwa iweze kutekelezwa kwa wakati na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

(ii) Wakandarasi Kutotekeleza Miradi kwa Ufanisi, kamati imebaini changamoto ya baadhi ya wakandarasi waliopewa kazi za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ndani ya Wizara ya Afya, hususani SUMA JKT wamekuwa hawatekelezi kazi zao kwa wakati. Hali hii inasababisha miradi mingi kutokukamilika kwa wakati uliopangwa jambo linalosababisha ongezeko la gharama za ujenzi. Kamati inasisitiza Serikali ihakikishe wakandarasi ambao hawatekelezi miradi yao ipasavyo wanachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa miradi na kupewa wakandarasi wengine wenye uwezo.

(iii) Upungufu wa Wataalam wa Afya, kumekuwepo na changamoto ya rasilimali watu katika baadhi ya hospitali nchini huku nyingine zikiwa na ziada ya Watumishi. Kamati inaona ipo haja ya Serikali kuweka mizania ya watumishi waliopo katika ajira kwa kuangalia maeneo ambayo yana watumishi wa ziada kuwapeleka kwenye hospitali ambazo hazina wataalam hao au zenye wataalam wachache.

(iv) Uhaba wa vifaa tiba kwenye Hospitali Mpya, Serikali imekuwa ikijenga na kuboresha miundombinu ya hospitali mbalimbali nchini. Hata hivyo, kamati inaona ni vema jukumu hilo likaenda sambamba na ununuzi wa vifaa tiba pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na rasilimali watu ya kutosha kutumia vifaa tiba hivyo ipasavyo ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Maoni na Ushauri Uliotolewa na Kamati mwaka 2022/2023, katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kamati

ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo kumi na moja. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa, Serikali imetekeleza maoni na ushauri wa kamati. Aidha, kwa maeneo ambayo bado haijatekeleza kikamilifu, kamati inaendelea kusisitiza kutoa taarifa hii ikiwemo udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makusanyo na Maduhuli ya fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa hadi mwezi februari 2023, mchanganuo wa makusanyo ni wa kuridhisha kwani asilimia 75 ya lengo la makusanyo yamekusanywa kutoka kwenye hospitali za rufaa za Mikoa, ikifuatiwa na makusanyo ya asilimia 71 kutoka katika Taasisi za Wizara. Kwa upande wa Makao Makuu ya Wizara kiwango cha makusanyo kipo chini kwani makusanyo ni asilimia 48 iilhali ilipaswa kuwa imekusanya angalau asilimia 66 mpaka mwezi Februari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, kamati inaipongeza wizara kwa kufikia kiwango hicho cha makusanyo. Pia, ni imani yetu kamati kuwa, kufikia mwisho wa mwaka fedha yaani Juni, 2023 lengo la makusanyo litafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa Fedha kwa mwaka 2022/2023. Kamati inasisitiza fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu kutolewa kabla ya mwaka wa fedha 2022/2023 kuisha kwani iwapo wizara itapokea fedha kwa mujibu wa mpango kazi, malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa yatafikiwa kwa kipindi kilichobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2023/2024, wizara na hospitali zilizo chini yake zinakadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 225,176,442,530.00. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 113,591,217,707.00 zitakusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya wizara na shilingi bilioni 111,585,224,823.00 kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, Maalum na Kanda. Aidha, taasisi za afya zilizo chini ya wizara zinatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 477,621,168,391.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kamati umebaini ongezeko la asilimia 12.81 ya jumla ya fedha zinazotarajiwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ukilinganisha na kiasi kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2022/2023. Aidha, kwa upande wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka Makao Makuu ya Wizara kuna upungufu wa asilimia 21, makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka hospitali za rufaa za mikoa yameongezeka kwa asilimia 30 na makadirio ya makusanyo ya taasisi yameongezeka kwa asilimia 21 ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inasisitiza Wizara ya Afya kuendelea kusimamia makusanyo na pia Serikali kuhakikisha inakusanya mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Afya (Fungu 52) inaomba kuidhinishiwa shilingi 1,235,316,516,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi 502,951,909,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 732,364,607,000.00 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, shilingi

354,342,486,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 148,609,423,000.00 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha zinazoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo shilingi 430,298,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 302,066,607,000.00 fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kamati umebaini kuwepo kwa ongezeko la shilingi 125,894,794,000.00 sawa na ongezeko la asilimia 11 ya bajeti kwa Fungu 52, kutoka shilingi 1,109,421,722,000.00 mwaka wa fedha 2022/2023 hadi kufikia shilingi 1,235,316,516,000.00 mwaka 2023/2024. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika bajeti inayoombwa ya Matumizi ya Kawaida imepungua kwa asilimia tisa ambapo bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia saba huku matumizi mengineyo *(OC)* ikipungua kwa asilimia 37. Vilevile, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la asilimia 32 kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za miradi ya maendeleo za ndani zimeongezeka kwa asilimia tano na fedha za nje zimeongezeka kwa asilimia 109.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa ongezeko hilo linatokana na ongezezeko la fedha za matumizi mengineyo kwa hospitali maalum kama vile Mirembe na Kibong'oto, hospitali za Kanda ikiwemo hospitali ya Mtwara, Chato pamoja na fedha za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ndani ya nchi na wanafunzi watarajali *(interns)*. Vilevile, kumekuwa na nyongeza ya fedha kwa ajili ya mahitaji ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo katika hospitali za rufaa za mikoa, kanda maalum na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi katika ngazi zote za huduma za afya. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona

umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi yote muhimu katika wizara hii. Ni rai ya Kamati kuwa, fedha zote zitolewazo zitolewe kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha husika

Mheshimiwa Naibu Spika, ulinganisho wa fedha zinazotengwa kwa Wizara ya Afya (Fungu 52) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya uchambuzi wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya kwa miaka mitatu mfululizo, kamati imebaini kuwa katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo bajeti bajeti kwa ajili ya Wizara ya Afya imekuwa ikiongezeka. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 tengeo la bajeti ya Wizara ya Afya linategemea kuongezeka kufikia asilimia 2.8 ya bajeti ya Taifa. Kamati inaipongeza Serikali na kushauri kiasi hiki cha fedha kiendelee kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kuendelea kuboresha Sekta hii muhimu inayogusa moja kwa moja maisha ya Watanzania na maendeleo Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya Afya. Kamati ilifanya tathmini ya bajeti ya sekta ya afya kwa miaka mitatu mfululizo na kubaini kuwepo kwa ongezeko la bajeti jambo linaloashiria kuwa sekta ya afya ni miongoni mwa vipaumbele vya Taifa. Kwa mwaka 2021/2022 zilitengwa shilingi bilioni 2.26 na mwaka fedha 2022/2023 shilingi bilioni 2.149 na mwaka fedha 2023/2024 zimetengwa shilingi 2,435,462,000,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya sekta ya afya kila mwaka ili angalau kufikia kiasi kilichowekwa katika makubaliano ya Abuja ambayo yanataka asilimia 15 ya bajeti ya Taifa itengwe kwa ajili ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa fedha zilizotengwa kwa Sekta ya Afya kwa mwaka 2023/2024**.** Uchambuzi wa kamati umebaini kuwa, katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya sekta ya afya kwa mwaka 2023/2024 kuna maeneo matatu ambayo ndiyo yameongoza kwa kupewa fedha kwa asilimia kubwa. Maeneo hayo ni huduma za tiba asilimia 39, hospitali za wilaya asilimia 34 na huduma za kinga asilimia 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mchanganuo huu, kamati inaona ipo haja ya Serikali kuwekeza zaidi kwenye kugharamia huduma za kinga ili kupunguza uhitaji wa huduma za tiba na hivyo kuwa na jamii yenye afya bora na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya kamati, Baada ya uchambuzi wa bajeti kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/2024 kwa Wizara ya Afya (Fungu 52), sasa naomba kutoa maoni ya kamati, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa vfaa tiba, upatikanaji wa vifaa tiba nchini bado ni changamoto. Kamati inafahamu kuwa kuimarika kwa huduma na upatikanaji wa vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji halisi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini ni moja ya vipaumbele vya Wizara hii. Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa vifaa tiba nchini siyo ya kuridhisha. Hivyo, Kamati inashauri; -

(i) Ujenzi wa miundombinu ya hospitali nchini uende sambamba na ununuzi wa vifaa tiba pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na rasilimali watu ya kutosha kutumia miundombinu hiyo ipasavyo ili kuleta tija kwa jamii.

(ii) Bajeti inayoidhinishwa na Bunge lako tukufu itolewe yote na kwa wakati ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na kuokoa maisha ya watanzania wanaopata huduma katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakandarasi kuchelewesha miradi, kwa kuwa imebainika kuwa wakandarasi waliopewa kazi za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ndani Wizara ya Afya hususani SUMA JKT, wamekuwa hawatekelezi kazi zao kwa wakati kiasi cha kusababisha miradi mingi kutokukamilika kwa muda uliopangwa. Hali hii imesababisha ongezeko la gharama za ujenzi na ucheleweshwaji wa huduma kwa wananchi. Kamati inashauri kwamba, Serikali ihakikishe wakandarasi ambao hawafanyi kazi zao ipasavyo wanachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa miradi na kupewa wakandarasi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba wa rasilimali watu, kwa kuwa imebainika kuwepo kwa changamoto ya rasilimali watu katika hospitali nchini, ni vema sasa Serikali ikaweka sawa mizania ya watumishi waliopo katika ajira kwa kuangalia maeneo ambayo yana watumishi wa ziada kuwapeleka kwenye hospitali ambazo hazina wataalam hao au zenye wataalam wachache ukilinganisha na mahitaji. Vilevile kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya afya Serikali itoe vibali vya ajira ili kuweza kuajiri watumishi wa kutosha kwa hospitali zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ufinyu wa maeneo; kwa kuwa imebainika kwamba, kumekuwepo na ufinyu wa maeneo ukilinganisha na mahitaji ya miundombinu inayotakiwa kuwekwa kwa ajili ya kukidhi uboreshaji wa hospitali za rufaa unaohitajika hususan katika hospitali za rufaa ya Mkoa wa Iringa na hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Mbeya. Kamati inashauri kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kutanua maeneo haya ili kuruhusu kuweka miundombinu wezeshi

pamoja na miradi mingine itakayohitajika kwa ajili ya hospitali hizi kwa miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, misamaha ya matibabu kwa wananchi wasio na uwezo ili kupunguza mzigo wa misamaha ya gharama za tiba ambazo hospitali inatoa kwa wananchi wasio na uwezo, ni wakati sasa kwa Serikali kutenga fungu la msamaha kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa wa ndani ya nchi kama inavyotenga fungu la matibabu ya wagonjwa wanaoenda kutibiwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya afya kwa Watoto, hivi karibuni kumekuwepo na taharuki kubwa kwa wananchi kuhusu kusitishwa kwa bima ya afya kwa watoto maarufu kwa jina la Toto Afya Kadi. Kamati inashauri yafuatavyo: -

(i) Serikali kuangalia namna nzuri ya kushughulikia changamoto hii bila kuleta usumbufu kwa wananchi kwani huduma ya afya ni ya kila Mtanzania.

(ii) Serikali kuona uwezekano wa kuwa na mfuko maalum wa bima ambao utakuwa endelevu katika kusaidia matibabu ya Watoto.

(iii) Wananchi ambao tayari wamekata bima hizi wapewe muda wa kuendelea kutumia kadi zao mpaka pale muda wa kadi utakapoisha. Vilevile kwa wale ambao muda wa kadi umeisha na wanahitaji kuhuisha *(renew)* kadi kwa vifurushi vingine, waweze kupata huduma mara tu baada ya kuhuisha kadi zao badala ya kusubiria kwa muda wa mwezi mmoja kama utaratibu uliopo sasa unavyotaka.

(iv) Ili kuepuka taharuki na sintofahamu kwa wananchi, ni vema Serikali kuzingatia kutoa taarifa za kuonesha nia ikiwa inahitaji kufanya mabadiliko yoyote yanayomgusa mwananchi moja kwa moja kabla ya kuchukuwa hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa yasiyoambukiza, kwa kuwa magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa ni tishio kwa afya za Watanzania. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ufanyike utafiti kubaini ukubwa wa tatizo hili. Aidha, jamii ielimishwe kuhusu vyanzo vya magonjwa hayo na namna ya kuyaepuka hususani kwa kuzingatia mazoezi na lishe. Vilevile kamati inaishauri wizara ishirikishe sekta zingine kwenye mapambano dhidi ya magojwa yasiyoambukiza ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za magonjwa haya mpaka kufikia ngazi ya afya ya msingi (*PHC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa dawa nchini, bado nchi yetu imeendelea kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa dawa. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya dawa ni ndogo na hazikidhi mahitaji. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2021/2022 ziliidhinishwa shilingi bilioni 218 na milioni 100, mwaka wa fedha 2022/2023 ziliidhinishwa bilioni 200 na mwaka wa fedha 2023/2024 zinaombwa kuidhinishwa shilingi bilioni 205.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kamati imebaini moja ya sababu ya changamoto dawa nchini ni Bohari Kuu ya Dawa kukosa mtaji wa kutosha kununua mahitaji yote na badala yake kulazimika kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya. Hivyo, ili kuimarisha upatikanaji wa dawa nchini, Kamata inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali iipatie Bohari Kuu ya Dawa - *MSD* mtaji wa shilingi 592,921,849,776 ili iweze kununua mahitaji yote ya bidhaa za afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinazokaimiishwa kwa ajili ya utolewaji na usambazaji wa dawa zitolewe yote na kwa wakati ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na kuokoa maisha ya watanzania wanaopata huduma katika hospitali zetu; na Serikali itazame upya mifumo ya usambazaji

wa dawa inayotumiwa na *MSD* ili kutatua changamoto zinazotokana na usambazaji. Mifumo ya kielektroniki iwekwe katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kudhibiti upotevu wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa milipuko ya magonjwa, kutokana na milipuko ya magonjwa inayojitokeza mara kwa mara hasa maeneo ya mipakani, Kamati inashauri Serikali ijenge vituo vya magonjwa ya mlipuko hususan maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati mitambo na mashine za kitabibu, Serikali inatumia fedha nyingi kuwekeza kwa kufunga mashine na mitambo mbalimbali katika hospitali nchini. Ni rai ya Kamati kuwa ili mashine na mitambo hiyo inayofungwa katika hospitali nchini iweze kudumu na kufanya kazi kwa muda mrefu ni vema Serikali ikawekeza kwenye matengenezo kinga *(planned preventive maintenace)* kwa kuvifufua vituo vya matengenezo kinga vya kanda vilivyokuwepo ili kuokoa gharama na kuvifanya vifaa tiba vitumike kwa wakati wote na muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya tiba asili na tiba mbadala nchini. Kamati inapongeza wataalam hawa kwa kuwa wabunifu na kuisaidia jamii yetu. Hata hivyo, kumekuwa na utoaji wa huduma hii usiowekewa ubora ili kujua athari hasi zinazotokana na huduma hiyo. Ili kuboresha huduma hizi kwa wananchi, Kamati inashauri Serikali iwatambue watoa huduma hizi za tiba asilia kwa kuwapa ithibati *(accreditation)* ili kuwapa wananchi uhakika *(assurance)* wakati wa kutumia huduma hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuepuka uwepo wa watoa huduma wasio waaminifu Kamati inashauri Wizara iwasajili watoa huduma hawa na kuthibitisha dawa ambazo wanatoa ili kuwa na ubora na usalama kwa watumiaji. Aidha,

Serikali isimamie na kuratibu matangazo ya biashara ya tiba asili na tiba mbadala kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa majengo mapya ya hospitali; kwa kuwa kumekuwepo na changamoto ya kutokutumika kwa baadhi ya majengo ya hospitali hizo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha ujenzi wa hospitali hizi unaenda sambamba na upatikanaji wa vifaa pamoja na watumishi ili majengo hayo yaanze kutoa huduma kwa wananchi na kuwaepusha na kutembea masafa marefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kuhusu usajili wa hospitali za Serikali, Kamati inashauri kuwepo na bodi moja ya usajili wa hospitali za Serikali na binafsi nchini. Hatua hii itaweka ulazima wa hospitali za Serikali kusajiliwa kudhibitiwa na kabla ya kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kiwanda cha Viuadudu Kibaha Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria ikiwa ni pamoja na kutumia bidhaa zilizoidhinishwa na kiwanda cha viuadudu cha kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Hospitali ya *CCBRT,* Kamati inashauri Serikali ikamilishe suala la kulipa mishahara watumishi wa hospitali ya *CCBRT*…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nenda kwenye hitimisho.

**MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Hospitali ya *CCBRT*, miradi ya ukarabati wa vyuo vya afya nchini, ujenzi wa hospitali za mikoa na kanda, madirisha ya wazee, miradi inayotekelezwa kwa ubia kati ya Serikali na wadau kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru Naibu Spika wewe mwenyewe na watumishi wote wa bunge na Wenyeviti wote kwa Utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu *(Mb)* Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel *(Mb)* Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif A. Shekalaghe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Joseph Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati inapokutana nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunamshukuru Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili na ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Hosiana J. Mvunta na Ndg. Victory E. Mrema pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Grace S. Gwivaha kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kiasi cha shilingi 1,235,316,516,000.00 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**12 MEI, 2023**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI WA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu (3) zifuatazo: -

(a) **Sehemu ya Kwanza** - Utangulizi;

(b) **Sehemua ya Pili** - Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

(c) **Sehemu ya Tatu** - Maoni na Ushauri na Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.1 Mambo Yaliyozingatiwa Wakati wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Bunge kufuatilia Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na kushauri ipasavyo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia mambo makuu matatu (3) ambayo ni: -

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu bajeti ya Wizara ya Afya uliotolewa Mwaka wa Fedha 2022/2023;

(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

(iii) Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yanatokana na Kamati kufanya mapitio ya mambo makuu yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya- Fungu 52;

(ii) Hali ya upatikani wa Fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2023;

(iii) Utekelezaji wa malengo yaliyokuwa yamewekwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, uchambuzi huu ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti husika.

### 2.2 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ilifanyika kwa kuzingatia Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023. Ziara hiyo ilifanyika kuanzia tarehe 14 hadi 18 Machi, 2023 katika Mkoa wa Iringa, Mbeya na Songwe. Taarifa ifuatayo inaeleza miradi iliyotembelewa na kukaguliwa, hali ya utekelezaji na mambo yaliyobainika.

#### 2.2.1 Mradi wa Ukarabati wa Jengo la Uangalizi Maalum (ICU)

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kukarabati jengo la uangalizi maalum (ICU) katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Iringa ni kupunguza rufaa za kwenda katika hospitali za rufaa za Kanda na Taifa. Vilevile, kuboresha huduma na kuokoa maisha ya wagonjwa mahtuti katika Mkoa wa Iringa pamoja na Mkoa jirani wa Njombe. Mradi huu umetekelezwa kupitia fedha za UVIKO 19 ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 mradi huu ulitengewa kiasi cha **Shilingi 150,000,000.00.** Fedha hizo zote zimetolewa na mradi umekamilika kwa **asilimia 100**.

### 2.2.2 Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mionzi (Radiology), Ununuzi wa CT-Scan na Digital x-ray

**Mheshimiwa Spika,** Serikali katika kuendelea kuboresha huduma za uchunguzi hususan huduma za mionzi, hospitali ya rufaa ya mkoa wa Iringa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilitengewa kiasi cha **Shilingi 1,791,799,899** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la radiolojia na ununuzi wa mashine ya CT-scan na Digital X-ray. Ujenzi wa jengo la radiolojia uligharimu kiasi cha **Shilingi 272,000,000/=,** na kiasi cha **Shilingi 1,519,799,899/=** kilitumika kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya CT-scan na Digital X-ray. Hadi mwezi Machi, 2023, Kamati ilipotembelea na kukagua mradi huu kiasi chote cha fedha kilikuwa kimetolewa na hivyo mradi umekamilika kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa uliofanyika na unaoendelea kufanyika katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Iringa kwani unalenga kuendelea kusaidia na kuboresha afya za Watanzania, hususan wanaoishi katika Mkoa wa Iringa pamoja na mkoa jirani wa Njombe.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi nzuri inayoendelea katika Hospitali ya Rufaa ya Iringa, kumekuwepo na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya Hospitali hii.

Changamoto hizo ni: -

(i) Ufinyu wa eneo la hospitali hali inayoleta ugumu wa kuongeza majengo ya kutolea huduma;

(ii) Ukosefu wa wataalamu wa kutoa huduma za kibingwa za mifupa, njia ya mkojo, masikio nk;

(iii) Upungufu wa majengo kama jengo la macho, jengo la kutolea huduma za nje (OPD) na jengo la kutolea huduma za kuzoeza viungo (*physiotherapy*);

(iv) Wagonjwa wengi kutomudu gharama za matibabu, hali inayopelekea hospitali kutoa misamaha kwa wadaiwa; na

(v) Upungufu wa watumishi.

### 2.2.3 Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Kanda, Mbeya (Hospitali ya Wazazi - Meta)

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya rufaa ya kanda Mbeya una thamani ya **Shilingi 12,329,277,541.99**. Awali, kiasi cha **Shilingi 9,151,766,914.99** kilitengwa mwaka wa fedha 2021/2022, na baadaye kiasi cha **Shilingi 3,177,510,627.00** kiliongezwa kwa lengo la kukamilisha mradi huo katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 01/05/2019 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30/03/2023 ambapo hadi Kamati ilipotembelea mradi huu mwezi Machi, 2023 mradi ulikuwa umefika **asilimia 99**. Kwa jumla jengo lina uwezo wa kuwa na vitanda 222 vya kulaza wakina mama wajawazito na wanawake wagonjwa wenye changamoto za afya ya uzazi. Aidha, jengo lina vyumba 8 vya madaktari, vyumba 3 vya upasuaji, na vyumba 11 vya kujifungulia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kutekeleza mradi huu wa ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya rufaa ya kanda Mbeya kwani itasaidia kuokoa maisha ya wananchi kwa kuwa itahudumia mikoa saba (7) ambayo ni Iringa, Njombe, Ruvuma, Mbeya, Songwe, Rukwa na Katavi.

### 2.2.4 Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Songwe unakadiriwa kugharimu jumla ya **Shilingi 9,745,114,617.81.** Kamati ilijulishwa kuwa kiasi cha **Shilingi 4,551771,639.20** kimepokelewa sawa na **asilimia 46.7.** Kati ya fedha hizo **Shilingi *2,000,000,000.00*** kimepokelewa mwaka huu wa fedha 2022/2023 ikiwa ni asilimia 100 ya fedha iliyotengwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa katika kiasi hicho kilichopokelewa kiasi cha **Shilingi 1,075,002,743.00** kimetumika sawa na **asilimia 23.6**, na fedha zilizobaki **Shilingi 924,997,257.00** zitaendelea kutumika kununua vifaa vya ujenzi. Aidha, mradi umetekelezwa kwa **asilimia 49** na iwapo fedha zitatolewa kwa wakati, mradi unatarajiwa kukamilika tarehe 31 Mei, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga hospitali ya rufaa kwa ajili ya mkoa mpya wa Songwe kwani uwepo wa hospitali hiyo utaokoa maisha ya wananchi ambao walikuwa wakipelekwa hospitali ya rufaa ya kanda Mbeya ambayo ipo umbali wa Kilometa 201.5 kutoka Mkoa wa Songwe.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilibaini changamoto ambazo ni kikwazo katika utekelezaji wa mradi huu ambazo ni: -

i. Mkandarasi SUMA JKT, kutokuwa na nguvu kazi ya kutosha hivyo kufanyika taratibu kinyume na mkataba;

ii. Fedha kutokutolewa kwa wakati hali inayosababisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi; na

iii. Vifaa vya ujenzi kutopatikana kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, ni matarajio ya Kamati kuwa, changamoto hizi zitatafutiwa ufumbuzi ili mradi huu uweze kutekelezwa kwa kasi inayotarajiwa na kukamilika kwa wakati ili wananchi wa maeneo hayo waanze kunufaika.

### 2.2.5 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na kukaguliwa, Kamati imebaini mambo mbalimbali ambayo imeyatolea maoni ili kuleta ufanisi wa utekelezaji. Yafuatayo ni mambo yaliyobainika katika ziara: -

(i) **Hali ya Upatikanaji wa Fedha**
Kamati imebaini kuwa bado hali ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya miradi si ya kuridhisha. Kwa mfano, katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa wa Songwe, mpaka mwezi Machi, 2023 Kamati ilipotembelea mradi huu, fedha zilikuwa zimetolewa kwa **asilimia 46.7** tu ilhali muda uliopangwa kukamilika kwa mradi ni tarehe 31 Mei, 2023. **Ni imani ya Kamati kuwa Serikali itatoa fedha hizo kabla mwaka wa fedha 2022/2023 kuisha ili mradi huu na miradi mingine iliyopangwa iweze kutekelezwa kwa wakati na kufikia malengo yaliyopangwa.**

(ii) **Wakandarasi Kutotekeleza Miradi kwa Ufanisi**
Kamati imebaini changamoto ya baadhi ya Wakandarasi waliopewa kazi za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ndani ya Wizara ya Afya, hususani SUMA JKT wamekuwa hawatekelezi kazi zao kwa wakati. Hali hii inasababisha miradi mingi kutokukamilika kwa wakati uliopangwa jambo linalosababisha ongezeko la gharama za ujenzi.

**Kamati inasisitiza Serikali ihakikishe Wakandarasi ambao hawatekelezi miradi yao ipasavyo wanachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa miradi na kupewa wakandarasi wengine wenye uwezo.**

(iii) **Upungufu wa Wataalam wa Afya**

Kumekuwepo na changamoto ya rasilimali watu katika baadhi ya hospitali nchini huku nyingine zikiwa na ziada ya Watumishi.

**Kamati inaona ipo haja ya Serikali kuweka mizania ya watumishi waliopo katika ajira kwa kuangalia maeneo ambayo yana watumishi wa ziada kuwapeleka kwenye hospitali ambazo hazina wataalaam hao au zenye wataalam wachache.**

(iv) **Uhaba wa vifaa Tiba kwenye Hospitali Mpya**

Serikali imekuwa ikijenga na kuboresha miundombinu ya hospitali mbalimbali nchini. **Kamati inaona ni vema jukumu hilo likaenda sambamba na ununuzi wa vifaa tiba pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na rasilimali watu ya kutosha kutumia vifaa tiba hivyo ipasavyo ili kutoa huduma bora za afya kwa wananchi.**

(v) **Ufinyu wa eneo**

Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya ufinyu wa maeneo ukilinganisha na mahitaji ya miundombinu inayotakiwa kuwekwa kwa ajili ya kukidhi uboreshaji wa hospitali za rufaa unaohitajika hususan katika hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Iringa na hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Mbeya. **Ni rai ya Kamati kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kutanua maeneo haya ili kuruhusu kuweka miundombinu wezeshi, pamoja na miradi mingine itakayohitajika kwa ajili ya hospitali hizi kwa miaka ijayo. Juhudi za mazungumzo kati ya Wizara ya**

**Afya na Wizara ya Mambo ya Ndani zifikie tamati ili kupata ufumbuzi wa mgogoro wa eneo katika hospitali ya rufaa ya Mkoa Iringa. Vilevile, Wizara ya Afya iangalie uwezekano wa kubomoa baadhi ya majengo madogo madogo ya zamani ili kujenga jengo la ghorofa.**

**2.3 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati Mwaka 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo kumi na moja (11). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa, Serikali imetekeleza maoni na ushauri wa Kamati. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati inaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii ikiwemo udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza.

**2.4 Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia **Fungu 52** katika mwaka wa fedha 2022/2023 ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 622,986,024,980.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 144,260,351,186.00** sawa na **asilimia 23.16** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 85,739,648,814.00** sawa na **asilimia 13.76** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 392,986,024,980.00** sawa na **asilimia 63.08** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara na Hospitali ya Kanda, Maalum na Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa, hadi mwezi Februari 2023, jumla ya **Shilingi 413,888,528,057.50** zilikuwa zimekusanywa, sawa na **asilimia 66.44** ya lengo la

makusanyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya fedha hizo **Shilingi 69,003,441,729.00** sawa na **asilimia 48** zilikusanywa kutoka Wizarani, **Shilingi 64,355,652,438.45** sawa na **asilimia 75** zilikusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 280,529,433,890.5** sawa na **asilimia 71.4** zilikusanywa kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.1

**Kielelezo Na. 1: Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Kipindi cha Mwaka 2022/2023**

| NA | TAASISI | KIASI KILICHOKADIRIWA KUKUSANYWA | KIASI KILICHOKUSANYWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Makao Makuu ya Wizara | 144,260,351,186.00 | 69,003,441,729.00 | 48 |
| 2. | Hospitali za Rufaa za Mikoa | 85,739,648,814.00 | 64,355,652,438.45 | 75 |
| 3. | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 392,986,024,980.00 | 280,529,433,890.5 | 71 |
| **JUMLA** | | **622,986,024,980.00** | **413,888,528,057.50** | **66** |

***Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti (Fungu 52) kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Februari 2023***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi mwezi februari 2023, mchanganuo wa makusanyo ni wa kuridhisha kwani **asilimia 75** ya lengo la makusanyo yamekusanywa kutoka kwenye hospitali za rufaa za Mikoa ikifuatiwa na makusanyo ya **asilimia 71** kutoka katika Taasisi za Wizara. Kwa upande wa Makao Makuu ya Wizara kiwango cha makusanyo kipo chini kwani makusanyo ni **asilimia 48** ilhali ilipaswa kuwa imekusanya angalao **asilimia 66** mpaka mwezi Februari 2023.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, Kamati inaipongeza Wizara kwa kufikia kiwango hicho cha makusanyo. Ni imani ya Kamati kuwa, kufikia mwisho wa mwaka fedha yaani Juni, 2023 lengo la makusanyo litafikiwa.
Vilevile, Kamati imebaini upungufu kwenye ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambao hadi mwezi Februari 2023 ulikuwa **asilimia 66** ikilinganishwa na makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2021/2022 kwa kipindi kama hicho ambapo makusanyo ya maduhuli yalikuwa ni **asilimia 71**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa sababu za upungufu wa makusanyo hayo inatokana na kuondolewa kwa tozo za kupima UVIKO-19.


**2.5 Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2022/2023**
**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti ya mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Afya (Fungu 52) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,109,421,722,000.00** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 554,289,666,000.00** ambazo ni sawa na **asilimia 50** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 555,132,056,000.00** ambazo ni sawa na **asilimia 50** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za matumizi ya kawaida zimejumuisha mishahara ya watumishi **Shilingi 331,566,406,000.00** sawa na **asilimia 60** na matumizi ya kawaida (OC) **Shilingi 221,723,260,000.00** sawa na **asilimia 40** ya bajeti yote ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo ziliidhinishwa **Shilingi 555,132,056,000.00,** kati ya fedha hizo fedha za ndani ni **Shilingi 410,298,000,000.00** sawa na **asilimia 74** ya fedha zote za maendeleo zilizotengwa, na fedha za nje ni **Shilingi 144,834,056,000.00** sawa na **asilimia 26** ya fedha zote za maendeleo zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2023 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya

Shilingi **656,798,247,336.32** sawa na **asilimia 59** ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Afya. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, fedha za matumizi ya kawaida zimetolewa **Shilingi 404,512,004,807.69** sawa na **asilimia 73** ya fedha zote za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa. Fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni **Shilingi 252,286,242,528.68** sawa na **asilimia 49** ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo zilizopokelewa fedha za ndani ni **Shilingi 234,360,798,013** sawa na **asilimia 57** ya fedha zote za ndani za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa. Fedha za nje zimepokelewa **Shilingi 17,925,444,515.13** ambazo ni sawa na **asilimia 12** ya fedha za nje zilizoidhinishwa.

**Kielelezo Na. 2: Mchanganuo wa Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Februari, 2023**




| | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | MISHAHARA | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
|---|---|---|---|---|
| FEDHA ZILIZOIDHINISHWA | 222,723,260,000 | 331,566,406,000 | 410,298,000,000 | 144,834,056,000 |
| FEDHA ZILIZOTOLEWA | 179,994,359,122 | 224,517,645,685 | 234,360,798,013 | 17,925,444,515. |
| ASILIMIA | 81 | 68 | 57 | 12 |

***Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023***

**Mheshimiwa Spika,** hadi Kamati ilipokutana na Wizara mwezi Machi, 2023 kwa ujumla hali ya upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ilikuwa imefikia **asilimia 57**. Kwa upande wa fedha za nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, hali si ya kuridhisha kwani fedha zimetolewa kwa **asilimia 12** tu kiwango ambacho hakiwiani na wastani uliotarajiwa kutolewa. Kamati inasisitiza fedha zote

zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kutolewa kabla ya mwaka wa fedha 2022/2023 kuisha kwani iwapo Wizara itapokea fedha kwa mujibu wa mpango kazi, malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa yatafikiwa kwa kipindi kilichobaki.

### 2.6 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024


**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umezingatia miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja (2023/24), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya (HSSP-V 2020-2025), Mpango Mkakati wa Wizara 2020/2021-2025/2026 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ifuatavyo: -

#### 2.6.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara na hospitali zilizo chini yake zinakadiriwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 225,176,442,530.00**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 113,591,217,707.00** zitakusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara na **Shilingi 111,585,224,823.00** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, Maalum na Kanda. Aidha, Taasisi za afya zilizo chini ya Wizara zinatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 477,621,168,391.00**.

**Kielelezo Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Fungu 52 kwa Mwaka 2023/2024**




***Chanzo: Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2023/2024***

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha Mwaka 2022/2023 na 2023/2024**

| TAASISI | KIASI KILICHOKADIRIWA KUKUSANYWA 2022/2023 | KIASI KILICHOKADIRIWA KUKUSANYWA 2023/2024 | KIASI KILICHO-ONGEZEKA/ KUPUNGUA | ONGEZEKO/ PUNGUZO (ASILIMIA) |
|---|---|---|---|---|
| Makao Makuu ya Wizara | 144,260,351,186.00 | 113,591,217,707.00 | -0,669,133,479.00 | -21.26 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa | 85,739,648,814.00 | 111,585,224,823.00 | 25,845,576, 009.00 | 30.14 |
| Taasisi zilizo chini ya Wizara | 392,986,024,980.00 | 411,621,168,391.00 | 4,635,143,411.00 | 21.54 |
| | **622,986,024,980.00** | **702,797,610,921.00** | **79,811,585,941.00** | **12.81** |

***Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti 2022/2023 & Randama ya (Fungu 52) ya Mwaka 2023***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la **asilimia 12.81** ya jumla ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ukilinganisha na kiasi kilichokadiriwa kukusanywa kwa mwaka 2022/2023. Aidha,

kwa upande wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka Makao Makuu ya Wizara kuna upungufu wa **asilimia 21,** makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka hospitali za rufaa za Mikoa yameongezeka kwa **asilimia 30** na makadirio ya makusanyo ya Taasisi yameongezeka kwa **asilimia 21** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya mwaka 2022/2023.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Wizara ya Afya kuendelea kusimamia makusanyo, na pia Serikali kuhakikisha inakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji wa mapato.

### 2.6.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Afya (Fungu 52) inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 1,235,316,516,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 502,951,909,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 732,364,607,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 354,342,486,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 148,609,423,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha zinazoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo **Shilingi 430,298,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 302,066,607,000.00** fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Kielelezo Na. 5: Fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**




**Chanzo: Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwepo kwa ongezeko la **Shilingi 125,894,794,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 11** ya bajeti kwa Fungu 52 kutoka **Shilingi 1,109,421,722,000.00** mwaka 2022/2023 hadi kufikia **Shilingi 1,235,316,516,000.00** mwaka 2023/2024. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika bajeti inayoombwa ya Matumizi ya Kawaida imepungua kwa **asilimia 9** ambapo bajeti ya mishahara imeongezeka kwa **asilimia 7** huku matumizi mengineyo (OC) ikipungua kwa **asilimia 37.** Vilevile, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuna ongezeko la **asilimia 32** kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za miradi ya maendeleo za ndani zimeongezeka kwa **asilimia 5** na fedha za nje zimeongezeka kwa **asilimia 109**.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa ongezeko hilo linatokana na ongezeko la fedha za matumizi mengineyo kwa hospitali maalum kama vile Mirembe na Kibong'oto, hospitali za Kanda ikiwemo hospitali ya Mtwara, Chato pamoja na

fedha za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi ndani ya nchi na wanafunzi watarajali (interns). Vilevile, kumekuwa na nyongeza ya fedha kwa ajili ya mahitaji ya kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo katika hospitali za rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa; Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba, na vitendanishi katika ngazi zote za huduma za afya.

**Kielelezo Na. 6(a): Ulinganisho wa Bajeti (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**

| MATUMIZI | 2022/2023 | 2023/2024 | ONGEZEKO /UPUNGUFU | % |
|---|---|---|---|---|
| Mishahara | 331,566,406,000.00 | 354,342,486,000.00 | 22,776,080,000.00 | 7 |
| Matumizi Mengineyo | 222,723,260,000.00 | 148,609,423,000.00 | -74,113,837,000.00 | -33 |
| Maendeleo Ndani | 410,298,000,000.00 | 430,298,000,000.00 | 20,000,000,000.00 | 5 |
| Maendeleo Nje | 144,834,056,000.00 | 302, 066, 607,000.00 | 157,232,551,000.00 | 109 |
| **JUMLA** | **1,109,421,722,000.0** | **1,235,316,516,000.00** | **125,894,794,000.00** | **11** |

**Kielelezo Na. 6(b) Ulinganisho wa Bajeti ya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na 2023/2024**




**Chanzo:** ***Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi yote muhimu katika Wizara hii. Ni rai ya Kamati kuwa, fedha zote zitolewe kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha husika.

### 2.7 Ulinganisho wa Fedha zinazotengwa kwa Wizara ya Afya (Fungu 52) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huu wa Kamati umelenga kubaini mwenendo wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa miaka mitatu mfululizo.
Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini yafuatayo: -

**Kielelezo Na. 7: Mwelekeo wa Bajeti inayotengwa kwa Wizara ya Afya (Fungu 52) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa miaka Mitatu**
**(2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024)**

| MWAKA | BAJETI YA TAIFA (MILIONI) | BAJETI WIZARA YA AFYA (MILIONI) | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| **2021/2022** | 37,411,370 | 1,034,133 | 2.7 |
| **2022/2023** | 41,063,915 | 1,109,421 | 2.7 |
| **2023/2024** | 44,388.10 | 1,235,316 | 2.8 |


***Chanzo; Randama za Wizara ya Afya na Taarifa za Mpango wa Maendeleo kwa kwa Mwaka 2021/2022 -2023/204***

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya kwa miaka mitatu mfululizo, Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo bajeti bajeti kwa ajili ya Wizara ya Afya imekuwa ikiongezeka. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 tengeo la bajeti ya Wizara ya Afya limeendelea kuongezeka kufikia **asilimia (2.8%)** ya bajeti Taifa. **Kamati inaipongeza Serikali na kushauri kiasi hiki cha fedha kiendelee kuongezwa mwaka hadi mwaka ili kuendelea kuboresha Sekta hii muhimu inayogusa moja kwa moja maisha ya Watanzania na maendeleo Taifa kwa ujumla.**

## 2.8 Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya Afya

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya tathmini ya bajeti ya sekta ya afya kwa miaka mitatu mfululizo na kubaini kuwepo kwa ongezeko la bajeti jambo linaloashiria kuwa sekta ya afya ni miongoni mwa vipaumbele vya Taifa. Kwa mwaka **2021/2022** zilitengwa **Shilingi 2,261,000,000.00**, mwaka 2022/2023 **Shilingi 2,149,000,000.00** na mwaka 2023/2024 zimetengwa **Shilingi 2,435,462,000,000.00.**

**Kielelezo Na. 8: Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Sekta ya Afya (2021/2022, 2022/2023 na 2023/2024)**




**Chanzo;** ***Taarifa ya Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo (Kitabu cha IV) Wizara ya Fedha na Mipango 2021/22-2023/204***

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuangalia mwenendo huu wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya sekta ya afya nchini inaonesha nia ya Serikali ya kuipa Sekta ya Afya kipaumbele kwa kuzingatia kuwa afya ndio msingi wa maendeleo ya Taifa. **Kamati inaisisitiza Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya sekta ya afya kila mwaka ili angalao kufikia kiasi kilichowekwa katika makubaliano ya Abuja ambayo yanataka asilimia 15 ya bajeti ya Taifa itengwe kwa ajili ya afya.**

## 2.9 Kielelezo Na. 9: Mchanganuo wa Fedha zilizotengwa kwa Sekta ya Afya kwa Mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, katika fedha zilizotengwa kwa ajili ya sekta ya afya kwa mwaka 2023/2024 kuna maeneo matatu ambayo ndiyo yameongoza kwa kupewa fedha kwa asilimia kubwa. Maeneo hayo ni Huduma Tiba **asilimia 39**, Hospitali za Wilaya **asilimia 34** na Huduma za Kinga **asilimia 13** kama inavyooneshwa katika kielelezo namba 9.

**Kielelezo Na. 9: Mchanganuo wa Fedha zilizotengwa kwa Sekta ya Afya kwa Mwaka 2023/2024**

| Na | | Bajeti | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1 | Huduma Tiba | 950,118,000,000 | 39% |
| 2 | Zahanati | 92,843,000,000 | 4% |
| 3 | Hospitali za Wilaya | 821,852,000,000 | 34% |
| 4 | Utawala | 107,596,000,000 | 4% |
| 5 | Vituo vya Afya | 155,094,000,000 | 6% |
| 6 | Huduma za Kinga | 307,958,000,000 | 13% |
| | **Jumla ya Sekta Afya** | **2,435,461,000,000** | **100%** |

**Chanzo;** ***Taarifa ya Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo (Kitabu cha IV) Wizara ya Fedha na Mipango, 2023***

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mchanganuo huu, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kuwekeza zaidi kwenye kugharamia huduma za kinga ili kupunguza uhitaji wa huduma za tiba na hivyo kuwa na jamii yenye afya bora na salama.

## 3.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa bajeti kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2023/2024 kwa Wizara ya Afya (Fungu 52), sasa naomba kutoa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii.

### 3.1 Uhaba wa Vifaa Tiba

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa vifaa tiba nchini bado ni changamoto. Kamati inafahamu kuwa kuimarika kwa huduma na upatikanaji wa vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji halisi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini ni moja ya vipaumbele vya Wizara hii. Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa vifaa tiba nchini siyo ya kuridhisha. Hivyo, Kamati inashauri; -

(i) Ujenzi wa miundombinu ya hospitali nchini uende sambamba na ununuzi wa vifaa tiba pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na rasilimali watu ya kutosha kutumia miundombinu hiyo ipasavyo ili kuleta tija kwa jamii; na

(ii) Bajeti inayoidhinishwa na Bunge lako Tukufu itolewe yote na kwa wakati ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na kuokoa maisha ya watanzania wanaopata huduma katika hospitali zetu;

### 3.2 Wakandarasi Kuchelewesha Miradi

**Mheshimiwa Spika**, kwakuwa imebainika kuwa Wakandarasi waliopewa kazi za ujenzi wa miundombinu mbalimbali ndani Wizara ya Afya hususani SUMA JKT, wamekuwa hawatekelezi kazi zao kwa wakati kiasi cha kusababisha miradi mingi kutokukamilika kwa muda uliopangwa. Hali hii imesababisha

ongezeko la gharama za ujenzi na ucheleweshwaji wa huduma kwa wananchi. Kamati inashauri kwamba, Serikali ihakikishe Wakandarasi ambao hawafanyi kazi zao ipasavyo wanachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa miradi na kupewa Mkandarasi mwingine;

### 3.3 Uhaba wa Rasilimali Watu

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa imebainika kuwepo kwa changamoto ya rasilimali watu katika hospitali nchini; ni vema sasa Serikali ikaweka sawa mizania ya watumishi waliopo katika ajira kwa kuangalia maeneo ambayo yana watumishi wa ziada kuwapeleka kwenye hospitali ambazo hazina wataalam hao au zenye wataalam wachache ukilinganisha na mahitaji; Vilevile, kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya afya Serikali itoe vibali vya ajira ili kuweza kuajiri watumishi wa kutosha kwa Hospitali zote nchini.

### 3.4 Ufinyu wa Maeneo

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa imebainika kwamba, kumekuwepo na ufinyu wa maeneo ukilinganisha na mahitaji ya miundombinu inayotakiwa kuwekwa kwa ajili ya kukidhi uboreshaji wa hospitali za rufaa unaohitajika hususan katika hospitali za rufaa ya Mkoa wa Iringa na hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Mbeya. Kamati inashauri kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kutanua maeneo haya ili kuruhusu kuweka miundombinu wezeshi pamoja na miradi mingine itakayohitajika kwa ajili ya hospitali hizi kwa miaka ijayo.

### 3.5 Misamaha ya Matibabu kwa Wananchi Wasio na Uwezo

**Mheshimiwa Spika**, ili kupunguza mzigo wa misamaha ya gharama za tiba ambazo hospitali inatoa kwa wananchi wasio na uwezo, ni wakati sasa kwa Serikali kutenga fungu la msamaha kwa ajili ya matibabu ya wagonjwa wa ndani ya nchi kama inavyotenga fungu la matibabu ya wagonjwa wanaoenda kutibiwa nje ya nchi.

### 3.6 Bima ya Afya kwa Watoto

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni kumekuwepo na taharuki kubwa kwa wananchi kuhusu kusitishwa kwa bima ya afya kwa watoto maarufu kwa jina la Toto Afya Kadi. Kamati inashauri yafuatavyo: -

(i) Serikali kuangalia namna nzuri ya kushughulikia changamoto hii bila kuleta usumbufu kwa wananchi kwani huduma ya afya ni haki ya kila Mtanzania;

(ii) Serikali kuona uwezekano wa kuwa na mfuko maalum wa bima ambao utakuwa endelevu katika kusaidia matibabu ya watoto;

(iii) Wananchi ambao tayari wamekata bima hizi wapewe muda wa kuendelea kutumia kadi zao mpaka pale muda wa kadi utakapoisha. Vilevile, kwa wale ambao muda wa kadi umeisha na wanahitaji kuhuisha *(renew)* kadi kwa vifurushi vingine, waweze kupata huduma mara tu baada ya kuhuisha kadi zao badala ya kusubiria kwa muda wa mwezi mmoja kama utaratibu uliopo sasa unavyotaka; na

(iv) Ili kuepuka taharuki na sintofahamu kwa wananchi, ni vema Serikali kuzingatia kutoa taarifa za kuonesha nia ikiwa inahitaji kufanya mabadiliko yoyote yanayomgusa mwananchi moja kwa moja kabla ya kuchukuwa hatua yotote.

### 3.7 Magonjwa Yasiyoambukiza

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa magonjwa yasiyoambukiza yamekuwa ni tishio kwa afya za Watanzania. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ufanyike utafiti kubaini ukubwa wa tatizo hili. Aidha, jamii ielimishwe kuhusu vyanzo vya magonjwa hayo na namna ya kuyaepuka hususan kwa kuzingatia mazoezi na lishe. Vilevile, kamati inaishauri Wizara ishirikishe sekta zingine kwenye mapambano dhidi ya

magojwa yasiyoambukiza ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za magonjwa haya mpaka kufikia ngazi ya afya ya msingi (PHC).

**3.8 Hali ya Upatikanaji wa Dawa Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** bado nchi yetu imeendelea kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa Dawa. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya dawa ni ndogo na hazikidhi mahitaji. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2021/2022 ziliidhinishwa **Shilingi 218,100,000,000.00,** 2022/2023 ziliidhinishwa **200,000,000,000.00** na mwaka 2023/2024 zinaombwa kuidhinishwa **Shilingi 205,000,000,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati imebaini moja ya sababu ya changamoto dawa nchini ni Bohari Kuu ya Dawa kukosa mtaji wa kutosha kununua mahitaji yote na badala yake kulazimika kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya. Hivyo, ili kuimarisha upatikanaji wa dawa nchini, Kamata inashauri yafuatayo: -

i. Serikali iipatie Bohari Kuu ya Dawa-MSD mtaji wa **Shilingi 592,921,849,776** ili iweze kununua mahitaji yote ya bidhaa za afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya;

ii. Fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utolewaji na usambazaji wa dawa zitolewe yote na kwa wakati ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa dawa na kuokoa maisha ya watanzania wanaopata huduma katika hospitali zetu; na

iii. Serikali itazame upya mifumo ya usambazaji wa dawa inayotumiwa na *MSD* ili kutatua changamoto zinazotokana na usambazaji. Mifumo ya kielektroniki iwekwe katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kudhibiti upotevu wa dawa.

### 3.9 Milipuko ya Magonjwa

Kutokana na milipuko ya magonjwa inayojitokeza mara kwa mara hasa maeneo ya mipakani, Kamati inashauri Serikali ijenge vituo vya magonjwa ya mlipuko hususan maeneo ya mipakani.

### 3.10 Ukarabati Mitambo na Mashine za Kitabibu

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inatumia fedha nyingi kuwekeza kwa kufunga mashine na mitambo mbalimbali katika hospitali nchini. Ni rai ya Kamati kuwa ili mashine na mitambo hiyo inayofungwa katika hospitali nchini iweze kudumu na kufanya kazi kwa muda mrefu, ni vema Serikali ikawekeza kwenye matengenezo kinga (*planned preventive maintenace)* kwa kuvifufua vituo vya matengenezo kinga vya kanda vilivyokuwepo ili kuokoa gharama na kuvifanya vifaa tiba vitumike na kudumu kwa muda mrefu.

### 3.11 Tiba Asili na Tiba Mbadala Nchini

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya tiba asili na tiba mbadala nchini. Kamati inapongeza wataalam hawa kwa kuwa wabunifu na kuisaidia jamii yetu. Hata hivyo, kumekuwa na utoaji wa huduma hii usiowekewa ubora ili kujua athari hasi zinazotokana na huduma hiyo. Ili kuboresha huduma hizi kwa wananchi, Kamati inashauri Serikali iwatambue watoa huduma hizi za tiba asilia kwa kuwapa ithibati *(Accreditation)* ili kuwapa wananchi uhakika *(Assurance)* wakati wa kutumia huduma hizo.

Aidha, ili kuepuka uwepo wa watoa huduma wasio waaminifu, Kamati inashauri Wizara iwasajili watoa huduma hawa na kuthibitisha dawa ambazo wanatoa ili kuwa na ubora na usalama kwa watumiaji. Aidha, serikali isimamie na kuratibu matangazo ya biashara ya tiba asili na tiba mbadala kwenye vyombo vya habari.

### 3.12 Majengo Mapya ya Hospitali

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kumekuwepo na changamoto ya kutokutumika kwa baadhi ya majengo mapya ya hospitali kutokana na kutokuwa na vitendea kazi pamoja na watumishi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha ujenzi wa hospitali hizi unaenda sambamba na upatikanaji wa vifaa pamoja na watumishi ili majengo hayo yaanze kutoa huduma kwa wananchi na kuwaepusha na kutembea masafa marefu kufata huduma.

### 3.13 Usajili wa Hospitali za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwepo na bodi moja ya usajili wa hospitali za Serikali na binafsi nchini. Hatua hii itaweka ulazima wa hospitali za Serikali kusajiliwa na kukidhi vigezo kabla ya kuanza kutoa huduma.

### 3.14 Kiwanda cha Viuadudu Kibaha

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi kwenye mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria ikiwa ni pamoja na kutumia bidhaa zinayozalishwa na kiwanda cha viuadudu cha kibaha.

### 3.15 Hospitali ya CCBRT

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri Serikali ikamilishe suala la kulipa mishahara watumishi wa hospitali ya CCBRT suala ambalo limechukua muda mrefu hali inayopunguza ufanisi wa hospitali hiyo. Aidha, ni muhimu Serikali kuzingatia masharti ya mikataba inayoingia na hospitali binafsi ili kuepusha mivutano isiyo ya lazima na kuongeza ufanisi wa huduma zinazotolewa.

### 3.16 Miradi ya Ukarabati wa Vyuo vya Afya Nchini

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa vyuo vya afya, Kamati inashauri, miradi hiyo ikamilike kwa wakati, ikiwemo Chuo cha Uuguzi cha Mbozi na Chuo cha Afya Songea.

### 3.17 Ujenzi wa Hospitali za Mikoa na Kanda

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwamba, Serikali ihakikishe inakamilisha ujenzi wa hospitali ambazo zimeanza kujengwa muda mrefu na hazijakamilika ikiwemo hospitali ya Kanda ya Mkoa wa Mtwara.

### 3.18 Madirisha ya Wazee

**Mhesimiwa Spika**, pamoja na kuwa wazee wametengewa madirisha ya kupokelea huduma za afya kwenye hospitali nchini, Kamati inashauri Serikali ihakikishe wazee hao wanapata huduma bora na zinazoridhisha.

### 3.19 Miradi inayotekelezwa kwa Ubia kati ya Serikali na Wadau kutoka Nje ya Nchi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kwa miradi inayotekelezwa kwa ufadhili wa wadau wa maendeleo, ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha inatenga na kutoa fedha kwa wakati ili kuwa na uendelevu wa miradi hiyo.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb)- Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. Seif A. Shekalaghe, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Joseph Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati inapotekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustini Engelbert Ndugulile, (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe hawa wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina wa masuala mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika uandishi wa taarifa hii. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb - **M/MKITI**
3. Mhe. Aysharose Ndaholi Matembe, Mb
4. Mhe. Bernadetha Kasabango Mushashu, Mb
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
6. Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mb
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb
8. Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb
10. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb
11. Mhe. Hassan Haji Kassim, Mb
12. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb
13. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb
15. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb
16. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb
17. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb
18. Mhe. Mussa Omar Salim, Mb
19. Mhe. Seif Salum Seif, Mb
20. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb
21. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati

kutekeleza majukumu yake vyema. Aidha, namshukuru Kaimu Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael L. Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati Ndg. Hosiana J. Mvunta na Ndg. Victory E. Mrema pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Grace S. Gwivaha kwa kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu ikiwemo Taarif hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kiasi cha Shilingi 1,235,316,516,000.00 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**
12 Mei, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, nakushukuru sana mwenyekiti kwa kusoma vizuri sana ansante. Sasa kabla hatujaanza kuchangia Mheshimiwa Waziri pamoja na kazi nzuri mliyoifanya jaribuni kupitia tena gharama za vipimo kwenye hospitali za Serikali, *dialysis*, *MRI*, mishahara analipa Rais, umeme analipa Rais, mitambo ananunua Rais hakuna sababu ngoma ime-*draw* Serikalini na huku uraiani. Wastaafu wazee akina mama watoto uwezo wa kwenda kupima vipimo hivi ni kazi kubwa sana, na ukitazama mfuko wa bima nao unaathirika sababu inabidi ulipe gharama kubwa za vipimo.

Kuna nchi kama India *dialysis* ni dola 28 tu pamoja na vile vifaa vyake. Kwa hiyo jaribuni kwenda kutizama haya mambo ili tupunguze gharama na kumsaidia Mheshimiwa Rais wananchi wake waweze kuwa na mapenzi zaidi.

Kwa hiyo sasa namuita Mheshimiwa Nyongo, jiandae Mheshimiwa Dkt. Mnzava, jiandae Mheshimiwa Mchafu, jiandae Mheshimiwa Mwakasaka.

**MHE. STANSALAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kwanza kabisa ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara hii ya Afya. Kabla sijachangia nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mwenyekiti wa Wabunge wa Afrika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi alivyoaminiwa kuwa Mwenyekiti wa Wabunge wa Kanda ya Afrika kule *IPU*. Basi tumtakie kila la kheri katika safari yake ya kugombea Urais wa Bunge au moja ya Mabunge ya Duniani *(IPU)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa makofi haya Waheshimiwa Wabunge wote wanamuombea uende ukashinde uwe Rais wa wa Wabunge wote duniani, na Inshaalah Mwenyezi Mungu atakubariki na utakuwa Rais wa *IPU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan kwa kipaumbele chake cha kutoa fedha katika sekta ya afya, na kwa kweli tunaona uwekezaji mkubwa ambao anaufanya Rais wetu katika kuwekeza katika sekta hii ya afya na kupeleka huduma kwa wananchi, tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa unayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Kamati ya Afya tumefanya kazi kubwa, tumechambua kwa kina,

tumeangalia kuona ni namna gani Serikali inafanya kazi kwa niaba ya Bunge lako. Tunatambua maadui wakubwa, hatujawasahau; wa kwanza ni maradhi umaskini na ujinga hawa ndio maadui zetu wakubwa katika nchi yetu. Lakini si hivyo tu maadui hawa ni maadui wa Afrika nzima; maradhi ujinga na umaskini ndio maadui wetu wakubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya nyuma viongozi wetu walikaa kule Abuja, walikaa chini wakatafakari wakasema kwamba kila nchi inapoandaa bajeti basi itengwe walau asilimia 15 ya bajeti ya nchi iende ikahudumie masuala ya afya. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza tuna asilimia 2.8 tu ya bajeti yetu tunatenga kwa ajili ya huduma ya afya. Bado tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kwamba tunapeleka huduma za afya kwa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mambo mengi ya kufanya, hakuana anayekataa, lakini mtaji wa kwanza ni afya yako. Kabla hujaenda kutafuta kitumbua au kwenda kutafuta chakula kwa ajili ya watoto wako ni lazima afya yako iwe imara. Ni lazima tuwe na mikakati ya pamoja kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinakuwa ni jambo la kipaumbele; kwa maana ya kwamba kila Mtanzania asiwe na wasiwasi pale anapopata shida ya maradhi yoyote basi aende akapate tiba, tiba ya uhakika na tiba ambayo ni ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Afya yeye na timu yake, Naibu Waziri viongozi alionao katika Wizara ya Afya, Katibu Mkuu wataalamu wetu wakuu wote wa taasisi, hiki kidogo ambacho wanapewa wanakitendea haki kwa kufanya kazi kubwa kwa kuona ni namna gani tupeleke hiki mwanzo na hiki kiwe kipaumbele cha pili. Keki hii ndogo tunayoipata ya taifa wao wanalala hawalali wanapanga ni namna gani Watanzania wapate huduma bora za afya, hongera sana Mheshimiwa Waziri Ummy kwa kazi unayoifanya.

Nakupongeza wewe kwa sababu wakati mwingine umekuwa huogopi kuchukua maamuzi kwa ajili ya Watanzania. Kuna wakati tunakuwa kama hatumuelewi, lakini tuna kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu maradhi ni adui mkubwa ni lazima tuwe na mkakati wa kutenga fedha kwa ajili ya kuwahudumia wananchi. Majuzi tulikuja na mkakati wa kuwa na bima kwa watu wote. Serikali imefanya kazi kubwa kupitia mikataba ya kimataifa, kuna kitu kinaitwa *Universal Health Coverage,* kwamba kila nchi lazima ipeleke Huduma ya Afya kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imefanya kazi kubwa kupitia Serikali yetu. Tumejenga vituo vya afya tumejenga zahanati, hospitali za kanda na hospitali za rufaa. Tumefanya kazi kubwa na sasa hivi ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, kwamba kila Mbunge katika eneo lake kuna vituo vimejengwa, kuna zahanati imejengwa, vituo vya afya vimejengwa na hospitali za wilaya zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni moja ya sehemu ya *universal health coverage* kwa sababu lazima tupeleke matibabu, lazima tupeleke huduma za kinga lazima tupeleke huduma za chanjo, pawe na *parental care* pawe na *dedication;* hizi zote zinaletwa. Changamoto kubwa iliyopo ni kwamba huduma imeshasogezwa kijijini huyu mwananchi anakwenda kulipia vipi huduma katika kituo ambacho ameletewa; na ndio maana tunapiga debe kwamba tuwe na *universal health insurance* kwamba kila mwananchi awe na bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hali iliyopo mfuko wa bima iliyopo ina-*suffocate* kwa upungufu wa fedha. *Toto Afya Card* Mheshimiwa Waziri juzi umeifuta, mimi nilishangaa, lakini tumekuja kukaa Waheshimiwa Wabunge kuona hali halisi hapakuwa na njia, njia iliyopo ni kutafua namna nyingine

mbadala ya kuhakikisha watoto hawa wanapata huduma kwa kupitia huduma za bima; na bima iwe ni kuhakikisha kwamba watoto wanaingia katika *package* za wazazi na shule zetu zihakikishe kwamba watoto wote wawe na bima ya afya. Sasa, tunahakikisha kwa namna gani, lazima tuwe na ushirikiano kati ya wananchi wenyewe na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naishauri Serikali, kwa upande wa Serikali tuanzishe mfuko maalumu kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kupitia bima zao. Tuna asilimia 28 ya Watanzania ni masikini, ni lazima Serikali iwahudumie kwa kuwapatia bima. Lakini Serikali inaingia gharama kubwa ya kuwasafirisha wananchi kwenda nje kwa ajili ya matibabu ya kibingwa. Kuna gharama nyingine kwa ajili ya ubingwa bobezi ndani ya nchi. Lakini bado tuneona hospitali zetu za mikoa na kanda zinatoa misamaha kwa wananchi zaidi ya bilioni 600 wanatoa msamaha kwa mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba tunatoa fedha kwa ajili ya bima kwa wananchi. Suala jingine nataka kutoa ushauri, na kwenye Kamati yetu tumeeleza na Mheshimiwa aliyesoma amesoma vizuri; *MSD* amekuwa ni mtu anayepokea fedha kwenda kununua dawa. Tunaomba tuipatie *MSD* mtataji iliyoomba, inataka bilioni 592 kwa ajili ya kununua dawa. kuna kununua dawa kwenda kujenga maghala pamoja na kuanzisha viwanda vya dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanahitaji bilioni 92 kwa ajili ya kuwawezesha watu binafsi kujenga viwanda ili waweze kuzalisha dawa kwa matumizi ya Watanzania; na si hivyo tu watazalisha dawa hadi kwenda kuuza nje ya nchi. Tunaomba na naomba sana, Wizara ya Fedha mnatusikia, wasikilizeni *MSD.* Msipo wasikiliza tatizo la upungufu wa dawa ambao tunauona kwa wananchi wetu litaendelea kujitokeza. Leo tunaona kabisa kwamba *MSD* anafika sehemu akisema

leo apelike dawa atumie fedha zote anakuwa na upungufu wa zaidi ya bilini 133.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tufanye jambo tuihakikishie kwamba *MSD* anapata mtaji aweze kufanya kazi zake ambazo amepangiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema, kwamba huduma za afya, Wizara ya Afya inafanya vizuri tunaona hospitali za kanda za mikoa zinafanya vizuri, kule chini kwenye hospitali za wilaya, zahanati na vituo vya afya bado tunaona kuna tatizo. Nadhani inafika wakati sasa, aliyeshikilia Sera ya Afya, Mheshimiwa Ummy unafanya kazi vizuri, ushikilie hivyohivyo kutoka hospitali za rufaa tukupe *power* ya kushikiria huduma hii ya afya mpaka kwenye zahanati na Vituo vya Afya uisimamie wewe ili …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili hiyo.

**MHE. STANSALAUS H. NYONGO:** ….wananchi waweze kupata huduma bure bora na safi. Baada ya kusema hayo nami naunga mkono ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Doctor Mnzava, ajiandae Mheshimiwa Hawa, ajiande Mheshimiwa Mwakasaka

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara ya Afya. Kwanza nimshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na

uwekezaji mkubwa ambao ameufanya katika Wizara hii ya Afya kwa kujenga miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba takriban Tanzania nzima, kila wilaya kuna kazi ambayo inaendelea kwa sasa hivi. Kama siyo jengo la *OPD* basi jengo la *MD* kama siyo *wodi* basi ni zahanati; yaani kila sehemu kuna kazi ambayo inaendelea. Kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini nawapaongeza sana sana sana Wizara ya Afya chini ya Mama yetu Ummy Mwalimu pamoja *Doctor* Mollel nadhani Ummy pamoja na Mollel hawalali katika kuhakikisha kwamba Wizara ya Afya inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni shahidi watumishi wa Wizara ya Afya wanafanya kazi nzuri nzuri sana iliyotukuka; kwa nini nasema hivyo? Ukienda kwenye hospitali zetu kwa sasa, kwa mfano mimi nitatolea mfano wa Hospitali ya Benjamin Mkapa; wanafanya kazi nzuri wanahudumia vizuri, yaani wanatibu kwa weledi. Lakini tatizo liliopo kwa sisi Watanzania ambao hatuna bima ya afya ni changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa si muumini sana wa ile bima kwa wote. Sasa hivi kutokana na gharama za matibabu, hasa kwa wagonjwa ambao wana matatizo makubwa kwa kweli bima kwa wote inahitajika. Usipokuwa na fedha ni ngumu sana mgonjwa wako akapata huduma inayostahili. Kweli atapokelewa na atahudumiwa, lakini kuna vipimo ambavyo vinahitajika kuna dawa ambazo zinahitajika, ni lazima uingie mfukoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninawaza je, yule mama wa kijijinim jem yule baba wa kijijini ambaye ni mkulima na hana kipato cha kutosha anapopata matatizo makubwa kwenye familia yake anafanya nini? Ninaomba sana suala la bima kwa wote mlilete mapema Bungeni ili

tuweze kulijadili na kulipitisha kwa sababu ni Watanzania wengi ambao wanahitaji…

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nampa taarifa mzungumzaji kwamba suala la Bima ya Afya ni muhimu. Mimi kwa upande wa Ushetu wakulima wangu wote 800 walijiunga na ushirika wa afya, na wanasisitiza hili suala liletwe Bungeni lipitishwe haraka ili wakulima wa-*enjoy* na ushirika wa afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa hiyo

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa ya kaka yangu Cherehani, ni kweli tuna haja ya kuletewa huo mpango wa bima ya afya kwa wote kwa sababu ni Watanzania wengi sana ambao wanahitaji huduma ni Watanzania wengi sana ambao hawana uwezo wa kwenda hospitali na kulipia matibabu kwa pesa taslimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru tena Serikali kwa kutenga bajeti ya Wizara hii ya Afya na kuweza kuongeza bajeti kutoka bilioni 1.1 mwaka jana ya bajeti inayomalizika na mwaka huu wameweza kutengewa fedha bilioni 1.2 na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tuna haja sana ya kuipitisha Bajeti ya Wizara ya Afya, kwa sababu bila afya hatuwezi kukaa mahali hapa. Bila afya hatuwezi kufanya kitu chochote. Kwa hiyo afya ni msingi lakini kwenye taarifa ya

Wizara ya Afya kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi. Ukiangalia mahitaji ya watumishi katika zahanati zetu Tanzania nzima ni 100,646, waliopo ni 30,625 upungufu ni 70,000 sawa na asilimia 70, upungufu wa watumishi katika zahanati, lakini kwenye vituo vya afya mahitaji ni watumishi 68,204, waliopo ni 25,354, upungufu ni 42,850, sawa na asilimia 73. Kwenye hospitali za wilaya wanaohitajika ni 123,424, waliopo 29,409, upungufu ni asilimia 94,215, sawa na asilimia 76.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina maana gani? Kama kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi kiuhalisia hata huduma hazitakuwa bora. Kwa sababu, kuna kiwango ambacho mtoa huduma za afya anatakiwa ahudumie, kuna viwango ambavyo vimewekwa na Wizara ya Afya. Sasa ukiangalia kwa upungufu huu wa asilimia 70, asilimia 63, asilimia 76 ni uhalisia kwamba watumishi hawa wanafanyakazi kupita kiasi na mtu anapofanyakazi kupita kiasi, matokeo yake atachoka, kwa sababu ni mwanadamu. Matokeo yake ataanza kutoa huduma ambayo sio bora, anaweza akaghafilika, ndio maana unakuta kuna sehemu zingine kuna watumishi ambao wanatoa lugha chafu, sio kwamba amedhamiria kutoa ile lugha chafu ni kwa sababu kazi zimemzidia amechoka, anajikuta anajibu kitu ambacho hakupanga kukijibu. Tunaiomba sana Serikali katika ajira ambazo zinatolewa na Serikali, waangalie sana sana sana Sekta ya Afya, kwa sababu ni sekta ambayo inahusu maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hospitali ya Wilaya ya Kahama, Hospitali ya Wilaya ya Kahama kwa siku inahudumia wagonjwa 450 mpaka 715 *OPD* na tuna watumishi 396. Pamoja na kwamba ni hospitali ya wilaya lakini inafanya kazi kama hospitali ya mkoa na tumekwenda mbali sana, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama wameweza kujenga majengo kwa kutumia fedha za ndani. Wametumia bilioni za kutosha kujenga *OPD*, zaidi ya bilioni

nne, wamejenga kwa fedha za ndani lakini haikutosha wamejenga jengo la uchunguzi wametumia zaidi ya milioni 803. Wamejenga Kituo cha Afya cha Kagongwa cha thamani ya milioni 800 kwa mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali, halmashauri zinapokusanya mapato yake ya ndani zikajenga miundombinu ya afya, tunaomba kwa haraka mtupe *support* kuhakikisha kwamba vifaa tiba vinatolewa. Tuna jengo pale pale la uchunguzi lakini hatuna vifaa tiba, Serikali watusaidie tuweze kupata vifaa tiba ili wananchi wa Wilaya ya Kahama waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kahama haihudumii wakazi wa Kahama pekee yake inahudumia Geita, Kaliua, Urambo, Msalala, Nzega, inahudumia watu wanaopita kutoka Tanzania kwenda Burundi. Kwa maana hiyo basi, kwa sababu Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alikwishatamka kwamba Hospitali ya Wilaya ya Kahama iwe na hadhi ya Hospitali ya Mkoa. Tunaomba Wizara ya Afya, huo mchakato ambao wamekwishauanza ukakamilike ili tuweze kupunguza uzito wa huduma ambayo wale wafanyakazi ambao wako katika ikama ya hospitali ya wilaya waweze kuwa katika ikama ya hospitali ya mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika Wizara ya Afya inafanya kazi kubwa sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Dkt. Mnzava, kengele ya pili hiyo.

**MHE. DKT. CHRISTINA P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, tunaomba watusikilize. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chakoma, wajiandae Mheshimiwa Mwakasaka na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ningependa kuanza kuwapongeza Dkt. Ummy na Dkt. Mollel kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na nikope maneno yake kwamba Mawaziri hawa wako *very loyal* na *very committed* nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nianze kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Rais Samia anaendelea kuboresha na kuimarisha Sekta hii ya Afya Nchini. Hivi tunavyozungumza tayari takribani bilioni 290 zimeshatumika kwa ajili ya kukarabati ama kuboresha hospitali za kanda, hospitali za mikoa na hospitali ya Taifa. Sambamba na hilo Mheshimiwa Rais Samia ameweza kusaidia kupunguza rufaa takribani kwa asilimia 97 za kwenda kutibwa nje ya nchi. Tunampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia tunaona nchi za jirani sasa ni zamu yao kuja Tanzania kufuata matibabu kama ambavyo zamani ilikuwa sisi tunatoka kwenda kufuata matibabu Kenya, India na nchi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimeona Madaktari saba wa Tanzania wakienda Malawi kwa ajili ya kwenda kutoa tiba, lakini pia kufanya uchunguzi pamoja na ukaguzi kwa wagonjwa ambao kimsingi walitakiwa waje kutibiwa Tanzania. Madaktari wetu hawa wakaenda kuwatibia kule kule Malawi. Hongera sana kwa Mama yetu kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nitapenda kumpongeza sana Waziri Ummy na timu yake kwa kuja na wazo la kufikiria sasa Hospitali ya Taifa ya Mirembe kuipandisha hadhi kuwa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili. Napenda sana kuwapongeza

kwa hili, kwani hapo awali hospitali hii ya Mirembe imepewa majina mengi ikiwemo hospitali ya vichaa, jambo ambalo mtu kama unahitaji huduma kwa hospitali ile inakuwa ni changamoto kwa namna vile ilivyokuwa ikiitwa. Kwa hiyo hongera sana kwa Wizara kwa namna ambavyo wameipandisha hadhi na kuweza kuiita Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunaambiwa karibu Watanzania wengi tunazo dalili za magonjwa ya afya ya akili, kucheka kupitiliza tunaambiwa ni dalili ya afya ya akili, kukasirika kupita kiasi, tunaambiwa hizi ni dalili za magonjwa ya afya ya akili, wivu uliokithiri na uliopitiliza tunaambiwa ni dalili ya magonjwa ya afya ya akili, lakini pia uwoga uliopitiliza, zote hizi tunaambiwa ni dalili za magonjwa ya afya ya akili. Kama hivyo ndivyo, mimi nitapenda kuuliza Serikali haya maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, je, Serikali inaifahamu changamoto hii kwa ukubwa gani? Swali la pili ambalo ningependa Waziri Ummy aje atujibu sasa, je, Serikali wamejiandaa vipi sasa kukabiliana na tatizo hili, maana inaonekana karibia kila Mtanzania anayo dalili ya ugonjwa huu wa afya ya akili? Kwa hiyo ningependa kujua mipango na mikakati ambayo wamejipanga nayo na kama wana takwimu sahihi kabisa za wagonjwa hawa na hawa walionyesha dalili za magonjwa ya afya ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili, lilikuwa ni kuhusiana na *Toto Afya Card*, kwa sababu ya muda ningependa Mheshimiwa Waziri achukue ushauri na maoni yaliyotolewa na Kamati hii ya Afya pamoja na Masuala ya UKIMWI, wamelichambua vizuri na wameshauri vyema. Kwa hiyo kwa kutunza muda ningependekeza wachukue ushauri huo uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na *MSD;* amesema vizuri Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii. Niliwahi kuuliza swali hapa ama niliwahi kuchangia hapa kwamba *MSD* sasa hivi kazi yake imekuwa inachukua ama inapokea hela ya Kituo cha Afya Mlandizi, inaenda inanunua dawa ya kituo kingine. *MSD* inapokea hela za Hospitali ya Wilaya ya Kibiti inaenda inanua dawa za Hospitali za Wilaya ya Mkuranga. Kwa maana hiyo imekuwa inachukua hela huku inaenda inanunua dawa kule, wamesema kwamba tuwaongezee mtaji, ifike mahali wapewe mtaji ili waweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la *MSD* ni Bohari ya Madawa, tunatakiwa tuwe na stoo ya madawa pindi zahanati, hospitali ya wilaya ama hospitali ya mkoa inapopeleka mapendekezo ama inapopeleka fedha kwa ajili ya kupatiwa dawa, basi dawa ziwepo *stand by* pamoja na vifaa tiba, lakini tusikuchue hela za dawa za huku na kwenda kununua dawa kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nililokuwa nataka kulizungumzia ni kuhusiana na suala zima la bima ya afya kwa wote. Hili nilishalizungumza na leo narudia tena, Watanzania tumefika mahali tunahitaji bima ya afya kwa wote na hususan kwa upande wa magonjwa yasiyoambukiza. Magonjwa haya yamekuwa yanachukua kiasi kikubwa sana cha bajeti ya Serikali. Kwa hiyo muda umefika, kama suala tunaambiwa 360,000 kwa mwaka ni kubwa, basi tuiangalie tena na tena lakini kwa mwendo huu tunaoenda nao tutawapoteza Watanzania wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakasaka, jiandae Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Afya. Nakushukuru sana. Nianze kwa kupongeza Serikali na hasa kwa jinsi ambavyo imekuwa ikileta fedha nyingi katika eneo hilo la huduma ya afya. Kwa kweli namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaangalia kwa ukaribu afya za wananchi, lakini Mheshimiwa Ummy pamoja na Ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Mollel, nawapongeza kwa kazi nzuri sana wanayoifanya pamoja na timu yao ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa pongezi hizo hizo, sisi Mkoa wa Tabora na hasa Hospitali yetu ya Kitete ambayo ni ya Rufaa na sisi ni miongoni mwa waliopata ile *CT-Scan* ambayo inagharimu karibu shilingi bilioni 1.8. Tunawashukuru sana Wizara na imeshaanza kufanya kazi na inategemewa na wilaya zote kuanzia Kaliua, Nzega, Uyui na sehemu zingine katika eneo hilo, kwa kweli tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze pia Serikali kwa kuweza kuona ule udanganyifu ambao umekuwa ukifanywa na wenzetu wa *NHIF* na zile hatua ambazo wamechukua, Mheshimiwa Ummy na timu yako tunawashukuru, lakini wasiishie hapo. Katika hotuba ya Waziri amekiri bado kwenye zahanati kuna upungufu mkubwa wa dawa. Waangalie kwa nini *MSD* wanaongezewa bajeti na dawa wanapeleka, lakini kwa nini kuendelee kuwa na upungufu kwenye zahanati na hospitali zetu za mikoa na za wilaya nazo zina matatizo ya upungufu wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika yale maduka ambayo Mheshimiwa Ummy kipindi fulani alisema mita 500 na nini, anafuatilia na vitu kama hivyo, maduka haya ya dawa yamejaa dawa siku zote. Ukichunguza sana sio kwamba wale wa maduka ya dawa wote wanaagiza hizo dawa, wanazipata hapa hapa nchini na hatuelewi wanazipataje, wakichunguza mtajua. Nina imani hizo dawa kuna mahali

zinachepuka, badala ya kwenda kwenye hospitali, wanazipata hawa wa maduka binafsi. Umekuwa ni mtindo wa kawaida mwananchi hata kidogo tu anaumwa anaambiwa akachukue dawa kwenye duka la dawa, naomba wafanye uchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo ulilisema hapa kuhusu gharama za mtu wa kawaida kwenda kutibiwa. Wiki iliyopita tu Mheshimiwa Ummy hata akitaka kuona ninayo hapa meseji ya Benjamin Mkapa, *consultation fee* kwa mtu ambaye hana uwezo kabisa, yaani ule ushauri tu 630,000 ninayo hapa. *Consultation fee* narudia yaani ule ushauri tu 630,000 ninayo *bill* yake hapa na imeandikwa ina-*expire within 24 hours*. Ndani ya masaa 24, huyu tena hapati tena hiyo huduma, awe amelipa hiyo 630,000. Sasa anawezaje mtu wa kawaida kupata matibabu. Kwa kweli hicho ni kitu kigumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kwa mara nimekuwa nikisimama kwa ajili ya Hospitali ya Kitete kuhusu upungufu wa Madaktari. Madaktari Bingwa ambao wanahitajika kwa mujibu wa ikama ni 21, lakini tuna Madaktari Bingwa watano tu. Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ni kwamba sita sasa wamekwenda kusoma, kwa ajili ya Udaktari Bingwa lakini bado mashaka yako pale pale. Kwanza hawa sita wote watarudi Hospitali ya Mkoa wa Kitete? Kwa sababu wanaweza ku-*diverge* wakatoka pale wakaenda kwingine, wameshakuwa mabingwa. Madaktari Bingwa wengi wanapenda kufanya kazi katika mikoa ambayo, kwa mfano Dar es Salaam, wamefurika wako wengi ni kwa sababu ya maslahi. Sasa wana mkakati gani kama Wizara kuhakikisha hata hawa ambao wanawasomesha wanarudi kufanya kazi pale kitete ili na sisi tuanze kuona sasa kwamba tunaanza kupata Madaktari Bingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mwenzangu mmoja jana, Mheshimiwa mmoja alikuwa ananiambia kwa nini

huchangii Wizara ya Maji, mbona ni muhimu sana. Nikamwambia nitawapotezea muda wenzangu bure, mimi maji ninayo ya kutosha, kwa hiyo nitachangiaje? Sana sana kule Tabora Mjini sisi tuna maji ya Ziwa Victoria, tunaishukuru sana Serikali na tuna maji *in excess*. Sasa kilichobakiwa ni ile *distribution* na nini, ndio maana nikasema siwezi kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye huduma ya nishati sisi tuko vizuri sana na huduma zingine, kasoro tu Kitete. Ndio maana kila nikiinuka Kitete, Kitete na Tabora Mjini haiitwi Toronto hivi hivi Mheshimiwa Ummy ameshafika mara nyingi. Shida yetu sisi kwenye afya hapa. Naomba atusaidie ile Toronto sasa isiwe mtu anatoka Toronto halafu anaenda kutafuta huduma zingine za afya sehemu nyingine ni eneo tu la Mheshimiwa Ummy, akitusaidia basi atakuwa kwa kweli ametutendea haki sana. Vinginevyo Waziri anafanya kazi nzuri sana, tunamshukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitete hospitali hiyo hiyo ya mkoa, kuna wanaojitolea katika kada mbalimbali wako 91, hao wanajitolea 91 ni watu wengi sana. Sasa tunarudi kule kule kwamba pale watakapotoa ajira wasianze kuwaleta watu ambao wametoka huko, hatukatai kuleta watu wengine, lakini wawape kipaumbele hawa ambao wanajitolea kwa sababu kazi ya uuguzi ni kazi ambayo kwa kweli ni ya kujitolea na kweli wanajitolea, 91 ni wengi sana. Kwa hiyo watakapotoa nafasi zile ambazo wataanza kuajiri naomba waweze kuwakumbuka hawa ambao wanajitolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sera ya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano kwamba wanapewa matibabu bure. Hiki kitu kwenye sera kipo, lakini kiuhalisia sehemu nyingi hakifanyiki. Mwaka mpya nilikwenda kutembelea Hospitali ya Kitete tena nilikuwa na timu pia nilikwenda na baadhi ya viongozi wa Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya kuona wagonjwa lakini na kuweza kutoa vifaa mbalimbali. Tulimkuta

mtoto wa miaka mitano ambaye alikuwa amepataa *referral,* sio tu rufaa lakini pia alikuwa anatakiwa kulipia matibabu. Sasa nikawa namuuliza kwa sababu tuliongoza na Muuguzi Mkuu kwamba imekuaje hawa watoto ambao ni chini ya miaka mitano, sera inasema matibabu ni bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akaniambia kuhusu ugonjwa wake. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye hili suala la watoto wa umri wa miaka mitano wawe wawazi kama kuna magonjwa ambayo hayawi *covered* kwenye hiyo sera ya kwamba matibabu ni bure kwa mtoto wa chini ya miaka mitano, wayaeleze wazi bayana, watu wawe wanafahamu. Vinginevyo wakienda pale akinamama na watoto wao wanajua tu kwamba mtoto wangu kwa sababu yuko chini ya miaka mitano atapewa matibabu bure, anapofika pale anapewa *bill* ya kulipa, inawachanganya sana wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Ummy lingine ni kuhusu suala la udhibiti wa hizo dawa. Kama dawa zinapelekwa kwa mfano hospitali fulani, inajulikana kabisa kwamba *package* ni hii, mnadhibiti vipi hizi dawa? Maana yake tumeona sehemu zingine baadhi ya Manesi siyo wote na baadhi ya watumishi wa hospitali ambao wamekuwa wakikamatwa na hizo dawa wakipeleka kwenye maduka ya madawa binafsi? Hizi dawa wanazitoaje? Udhibiti wa dawa ukoje? Naomba eneo hilo muweze kuliangalia kwa ajili ya kudhibiti upotevu wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia madirisha ya wazee na watu wenye mahitaji maalum. Bado kuna hospitali nyingi hapa nchini ambazo hazina madirisha ya wazee wenye umri mkubwa ambao wanahitaji huduma za afya lakini pia na wale wenye mahitaji maalum kwa mfano, wenzetu ambao wenye ulemavu kwamba waweze kupata huduma hizo haraka kutokana na mahitaji yao ya kimwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mimi kusema haya na kushukuru sana naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Dkt. Alice Kaijage, ajiandae Mheshimiwa Jesca Jonathani.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kujali kabisa tasnia hii ya Afya, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ummy pamoja na Naibu Waziri Mollel pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri njema wanayoendelea kufanya. Kwa kipekee sana niwapongeze watoa huduma wote wa afya Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nianze kwa kuunga mkono hoja asilimia 100. Mnamo Tarehe 05 Februari, 2021 nilisimama katika Bunge lako Tukufu kuzungumzia suala zima la Hospitali ya Mirembe. Nikaelezea ukongwe wake ilikuwa ni mwaka *1993 by then,* nikaelezea miundo duni dhaifu na mikongwe, miundo duni ya watumishi kufanya kazi iliyo dhaifu, nikazungumzia uzito wa kazi wa eneo lile walikuwa wana-*bed state* kama wagonjwa 500 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia walikuwa wanatumia shilingi milioni 280 kwa mwezi. Nikashauri miundombinu irekebishwe japo wana tatizo la akili lakini wanahitaji kuhudumiwa katika sehemu nzuri, nikashauri pia ikiwezekana iwe Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Akili iwe Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuipongeza Serikali sikivu ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan chini ya Waziri Ummy Mwalimu jinsi ambavyo jambo hili limetekelezwa kwa umakini mkubwa sana. Pia ninashauri suala hili pia

liendelee kuzingatiwa na kufikiriwa kwa Hospitali yetu ya Kibong'oto kuwa taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo Tarehe 11 Februari, 2021 nilisimama humu ndani pia kuzungumzia suala zima la matibabu mbalimbali ya aina mbalimbali ikiwepo na mazoezi tiba, kwamba wataalam hawa wako wachache na pia Tanzania nzima Shahada inapatikana Chuo cha *KCMC* tu. Nikashauri ikiwezekana vyuo vingine kama Muhimbili, Bugando, *UDOM* hii taaluma ianzishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sikivu sana ya Mama Samia Suluhu Hassan imekuja na shahada hii ya mazoezi tiba na vitendo mbalimbali vya matibabu katika Chuo cha Muhimbili. Ninaipongeza Serikali ya Mama Samia kuwa sikivu chini ya uongozi wa Waziri wetu Ummy Mwalimu na Watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Serikali imekuwa sikivu sana, leo mimi nakuja na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ina Upanga na Mloganzila. Kwa siku wagonjwa wa nje tu kwenye hospitali hii ni 2,500. Muhimbili wanaona wagonjwa 2,000 kwa siku, Mloganzila 500 na nusu ya wagonjwa hao ni wa msamaha yaani hawana uwezo wa kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sivyo tu, katika wagonjwa wa msamaha tuna wagonjwa ambao ni wafungwa. Hospitali ya Muhimbili peke yake inatumia shilingi milioni 72 kwa mwezi kuhudumia wafungwa, kwa maana ya kumuona Daktari, vipimo na dawa bure. Hospitali ya Muhimbili inatumia shilingi milioni 300 kwa wagonjwa wafungwa waliolazwa. Chai ya asubuhi, chakula cha mchana na jioni kwa mwezi shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, Hospitali ya Muhimbili kwa mwezi kwa umeme na maji shilingi milioni 450

inalipa. Siyo hivyo tu, kuna magonjwa mengi yasiyoambukiza lakini niende kwa matatizo ya figo. Wanaofanya *dialysis* kusafisha damu kwa Muhimbili kwa siku wanafanya *dialysis* kwa wagonjwa 110, Mloganzila 30 na nusu ya hao ni hawana uwezo wa msamaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muhimbili kwa mwezi inasamehe wagonjwa kwa gharama ya shilingi bilion 1.8 mpaka shilingi bilioni mbili msamaha. Nataka kusema nini? Hii Muhimbili magari yake yakiharibika, yakipata ajali, wakienda *TEMESA* wanatozwa fedha nyingi sana walipe. Wakienda ku-*clear* mizigo yao *GPSA* vitendeakazi mbalimbali vitendanishi wanalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwa wafungwa, kwa nini basi Wizara ya Mambo ya Ndani kama inawezekana hiyo bajeti ya kuwatibia wafungwa iletwe Wizara ya Afya au la, watibiwe lakini bili ile ipelekwe Mambo ya Ndani walipe. Hospitali kama Muhimbili ina uwezo gani kwa gharama zote hizo? Bajeti yake haizidi shilingi milioni 400 kwa mwezi kutoka Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna shida bajeti ni ndogo, keki ni ndogo, basi pamoja na hayo yote bajeti inatengwa mwezi Julai tunaipitisha lakini inafika Muhimbili Septemba. Wagonjwa hawangoji kuugua Septemba, wagonjwa wanaumwa kila siku na tukumbuke Muhimbili ni Hospitali ambayo wagonjwa hawapelekwi ambaye ameugua siku mbili labda ana *malaria* au *UTI, infection* ya mkojo ni wagonjwa ambao wameshatibiwa huko wanakuja gharama yao ni ya juu sana. Kwa hiyo, ninasimama hapa kusema leo kwa sababu Serikali imekuwa sikivu sana. Imekuwa sikivu kwa Mirembe na mambo mengine niliyozungumza, leo Muhimbili naomba bajeti itakapopita iende haraka sana na pia iangaliwe kwa jicho la tofauti sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina hayo machache naomba Serikali sikivu ya Mama Samia Suluhu Hassan chini ya Waziri mahiri Ummy Mwalimu waangalie Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa jicho la tofauti sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Profesa Janabi kwa kazi kubwa anayoifanya pale Muhimbili, imebadilika sana. Nilizungumza siku moja humu ndani pawe na *stock center,* naona Mloganzila wametenga, ka hiyo ina maana itakuwa kama Jakaya Kikwete, itakuwa wanapata huduma stahiki, hivyo tuwawezeshe tuwatie moyo, mazingira yawe safi pia wapate vitendeakazi kwa wakati, bajeti ije kwa wakati, wagonjwa hawasubiri muda, wagonjwa wapo kila siku tena wanaumwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo naomba kuunga hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jesca Jonathani, ajiandae Mheshimiwa Mohamed Monni, ajiandae Regina Ndege.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote na mimi nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wake mkubwa kwenye sekta ya afya, akisaidiwa na Waziri wetu Ummy, Waziri makini kabisa na Naibu Waziri Kaka yangu Mollel. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Kamati, nawashukuru sana kwa kuja Iringa na kuona changamoto zilizopo katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa. Tunawashukuru sana kwa ajili ya *Digital X-Ray Scan* na

ukarabati wa lile jengo la *Radiology* ambalo mmetumia zaidi shilingi bilioni moja na milioni mia saba na tisini na moja, tunawashukuru sana pia kwa ukarabati wa *ICU* shilingi milioni 150, tunawashukuru sana. Tunawashukuru pia kwa ajili ya fedha nyingi mlizozileta kwenye hospitali yetu ya Wilaya ya Manispaa ya Iringa ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni moja na milioni milioni mia mbili. Tunawashukuru kwa ajili ya fedha ya Kituo cha Afya Mkimbizi shilingi milioni 500. Tunawashukuru kwa ajili ya fedha katika Kituo cha Afya Ipogoro shilingi milioni 357. Tunawashukuru kwa ajili ya fedha mlizoleta kwenye zahanati zetu, Zahanati ya Mkwawa shilingi milioni 50, Zahanati ya Isakalilo pale shilingi milioni 150, Zahanati ya Nduli shilingi milioni 50, Zahanati ya Ugele shilingi milioni 50. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya changamoto zilizotokea tunaomba muendelee kutuongezea watumishi katika Hospitali yetu ya *Referral* ya Mkoa wa Iringa na pamoja na kwamba mmeshatupatia watumishi wengine karibu 26 lakini bado tuna upungufu. Mmetupatia watumishi 46 kwenye Hospitali yetu ya Wilaya bado tuna upungufu na katika vituo vyetu vya afya kwa mfano Mkimbizi mmetupatia watumishi Saba. Tunawashukuru sana na kwenye zahanati watatu, watatu tunawashukuru tunaomba muongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, Manispaa ya Iringa kwa *geographical location* yake inahudumia siyo Manispaa ya Iringa tu. Tunahudumia Jimbo la Kalenga, tunahudumia Isimani, tunahudumia Kilolo. Kwa sababu watu hawawezi kupita pale Mjini wakaenda kutibiwa Kilolo wakati pale kwenyewe kuna Hospitali. Hawawezi kutoka Kalenga wakapita mjini wakaenda kutibiwa Igodivaa wakati pale kuna hospitali. Hawawezi kutoka Ifunda wakaja kutibiwa huko Igodivaa. Kwa hiyo *location* yetu tunaomba sana mtusaidie. Mtuongezee kituo cha afya Kitilu, mtuongezee kituo cha afya Igumbilo kwa sababu huko ndiko kunakopokea watu kutoka kwenye Majimbo mengine na sisi tupo tayari kwa sababu

kwa mfano Igumbilo pekeyake zahanati inahudumia zaidi ya watu 600. Sasa unaweza kuona mzigo unavyokuwa mkubwa. Kwa hiyo tunaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufinyu wa eneo katika Hospitali ya Mkoa wa Iringa ni changamoto ambayo kamati imesema. Mimi niwaombe rejeeni mapendekezo yetu na *RCC* ya Iringa, kwamba Hospitali ya Wilaya ile ina eneo kubwa sana na wala pale siyo mbali hazifiki hata kilometa Sita. Mnaweza mkaamua *structure* zenu nyingine mkaziweka pale na mkatenga kama mkoa ili tuendelee kupata huduma za *referral* kwenye hospitali yetu ya Mkoa kuliko kufikiria kuihamisha pale Wizara ya Mambo ya Ndani ianweza ikawa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunaomba wataalamu wa mifupa. Mnaona *geographical location* ya Iringa, ipo kati kati pale, barabara kubwa zote zinapita pale, ajali ni nyingi. Kwa hiyo, wote wanategemea kuja pale kwa ukaribu wake. Tunaomba sana wataalam wa mifupa, masikio tupate ili watu wakipata ajali kuliko kuanza kuwakimbiza Benjamin kuwapeleka Muhimbili, na *distance* ni ndefu, basi pale tupate wataalam wa mifupa ili waweze kutusaidia lakini tunawashukuru kwa ajili ya wataalam mliotuletewa wanne kwa ajili ya viungo bandia kwa ajili ya wagonjwa wa ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwashukuru sana pia kwa kuniteua kuwa Balozi wa Afya ya Akili Tanzania. Nakushukuru sana Waziri wa Afya na ninaona jambo hili linaongelewa kwa mapana yake. Sasa katika huo ubalozi naomba basi wale Isanga wanatibu tibasheria, kwa ajili ya wale wenzetu wanaoonekana kule kwenye sheria walipelekwa kimakosa kumbe ni matatizo ya afya ya akili wanapelekwa pale kusaidiwa kutoka Magereza. Wapeni basi hiyo shilingi bilioni moja na milioni 600 walizoomba changamoto ya kibajeti ili waweze kuwahudumia wenzetu

wenye matatizo ya afya ya akili kutoka kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia kwa ajili ya Mirembe kuifanya kuwa Taasisi ya Afya ya Akili Nchini. Ilingane lingane basi sasa na taasisi ya afya. Tumesherehekea mwaka jana miaka 100 pale lakini bado hapaeleweki. Ilingane na taasisi ya afya ya akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kama Balozi nisipoongelea masuala ya afya ya akili nitakuwa sijaitendea haki nafsi yangu mimi mwenyewe. Masuala ya matatizo ya afya ya akili ni makubwa. Ninakushukuru umeweka katika vipaumbele vyako Namba Sita kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utangamano na tiba shufaa. Tunakushukuru sana kwamba umeiingiza lakini ipe uzito unaowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ummy, matatizo ya afya ya akili yanakuletea *cost* kubwa sana kwenye vifaatiba na matibabu. Kama *WHO* wanasema afya ya akili ni kutojitambua, ni kushindwa kupambana na changamoto, ni kushindwa kutoa msaada kwenye jamii, ni kushindwa kufanya kazi kuzalisha kwa faida, hiyo ilitakiwa ipewe kipaumbele cha kwanza. Tukiwapa watu wetu wakawa na uelewa mzuri kwenye akili zao. Kwanza mimi nataka ile *pre copying* kwanza. Kabla hujafikia kutupa dawa za afya ya akili, tujifunze kwanza masuala ya mambo yanayosababisha tukafikia kule kwenye kutumia dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hiii tuifanyaje? Tufanye kampeni maalum. Marekani tangu miaka ya 50 wana mwezi wa kampeni maalum kwa ajili ya masuala ya afya ya akili na wao wanaifanya Mei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi tuchague mwezi maalum ambao tutaongelea masuala ya afya ya akili, tutawaambia

watu wafanye *meditation,* tutawaambia watu mwezi huu nendeni mkafanyiwe *massage,* tutawaambia watu mwezi huu walie wasiolia, tutawaambia watu mwezi huu ni wa kusema matatizo yenu ili watu waseme, watu walie, watu wapate nafasi ya kwenda kufanya *massage,* watu wapate nafasi ya kwenda kutembelea misitu, waende *national parks,* waka-*relax* akili zao. Wakirudi wawe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri haya matatizo ya afya ya akili ndiyo yanakufanya wewe unakuwa na wogonjwa wengi wasio na magonjwa ya kuambukiza hospitali. Unatumia fedha nyingi, kumbe watu wanatakiwa kufanyiwa tu mazoezi, watu wakishachangamana humu kwenye ndoa wakashindana wakidundana ngumi wanakuja kushonwa kwako wewe. Wanapiga *x-ray* mzigo unaongezeka kwako. Watu wakishindwa kufanya maamuzi sahihi wanawasababishia wengine presha. Ndiyo unapata taabu kubwa wengine *veins* zina-*fail* ndiyo tunapata taabu kubwa ya kununua ma-*CT Scan* kumbe mambo mengine yangetibika. Hapa umetuambia umetibu watu milioni 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea na daktari mmoja akasema katika watu 10 wanaoenda hospitali, wagonjwa ni Watatu, Saba wote hawa wameenda kwa sababu tu ya afya ya akili. Mtu tu mke wake kaamua kumletea tatizo kwenye nyumba, mume amefyatuka presha iko juu, anahitaji *CT scan* anahitaji vitu kama hivyo. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunatakiwa sisi tuone kwamba kampeni ya afya ya akili ndiyo kitu cha mwanzo kuliko vitu vingine. Ukija mimi ukaniahidi hapa leo kama Jesca Mbunge, ukaniahidi kwamba chinga wa Iringa tunakwenda kuwaletea shilingi milioni 700 watengenezewe *structure* zao, halafu usipoleta zile fedha mimi umenifanya niwe chizi, na wale machinga wangu wote wamekuwa machizi, hivi hatueleweki afya zetu zimeyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii kampeni ianze kwenye Wizara za wenzio wasiwe *motor behind* kusababisha afya za akili waambie mnanivurugia watu afya zao. Ahadi ziwe zinatekelezeka, mipango itekelezeke ili watu wawe na afya nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, afya ya akili inakwenda kwenye masuala ya imani. Mtu akili ikishashindwa kufika mahali ikaamua jinsi ya kutatua tatizo lake anajipeleka sasa kwenye imani potofu, ndiyo kule wanafikia sasa mtu anaambiwa ukienda ukambaka mzee, ukambaka mtoto, ukambaka dada yako, ukambaka mama yako unapata utajiri. Sasa mwisho wa siku wakibakwa wanakuja kwako Waziri wangu Ummy wanahitaji dawa, wanahitaji huduma za afya, tunaongeza mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo suala hili liweke mwanzo. Kampeni ifanyike kubwa ili watu wetu waelewe kwanza. Katika vitabu vya Mwenyezi Mungu vinasema watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa. Kitu cha kwanza kinachomuangamiza binadamu ni kiuchumi, kisiasa, kinachomuangamiza kwenye jamii ni kukosa maarifa. Kama mtu hana *understanding* ya kwamba kulia ni *deal,* kulia kutaniponya, kwenda *National Parks* kutembea Selous kutaniponya, anafikiri ni anasa peke yake inatupa shida, mtu aelewe kwamba kwenda *National Park* siyo anasa unakwenda kufanya *healing. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenda na watoto wako kuogelea wakati mwingine kutembea na watoto wako porini wakasikia harufu tofuti tofauti, sauti za ndege badala ya sauti za magari peke yake, ile nayo ni *healing* ya kutosha. Wewe kuendelea kusema mimi leo namtoa *outing* mke wako na ukasema leo simtoi mchepuko *outing,* namtoa mke wangu *outing* umemfanyia *healing* akirudi hatakusababishia matatizo ya afya ya akili, lakini watu wanadhani ni anasa.!

Sasa hivi Mabalozi tuko *well empowered,* tunaweza kufundisha watu Mheshimiwa Ummy hapa sasa bajeti ya Balozi iwepo maana yake sasa hata bajeti ya Balozi haipo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mambo haya Mheshimiwa Ummy nimekuwa nayafanya mwenyewe kivyangu, hayawezi kwenda kwenye upana huo. Tengeneza timu sisi twende tukawaambie watu. Tukaongee na vijana wetu, tuwaeleze. Hii tabia ya mtu kujiona eti mimi mwanamke lakini *I am feeling, I am a man* yaani yeye ni mwanamke anajiona ni mwanaume, *no!* hatuangalii jinsia kwa kujihisi, tunaangalia kwa *structure* uliyonayo kwa *physical appearance* yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo tunaongea hapa ushoga, tunaongea sijui usagaji kumbe watu wangekuwa vizuri tu, hana sababu ya kujiona mwanamke mwanaume, mwanaume mwanamke kwa sababu tayari akili yake inge-*sense* tu kwa kiungo nilichonacho mimi ni mwanamme sina sababu ya kujiona mwanamke. Kwa kiungo nilichonacho mimi ni mwanamke, sina sababu ya kujifanya mwanaume.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Balozi.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, ajiandae Mheshimiwa Regina Ndege, ajiandae Mussa Ramadhani Sima.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi walau nichangie kidogo katika Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia afya sote na tuko hapa. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo anaendelea kulihudumia Taifa hili kwa namna ambavyo anatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hakika anafanya kazi kubwa sana. Mimi nafahamu kila Mbunge hapa kwa wakati moja au mwingine ameshawahi kwenda kuomba jambo. Mnafahamu namna ambavyo yuko rahisi na anafikika. Pia nimshukuru Naibu Waziri ni rafiki mzuri wa ndugu zangu wote mlioko hapa na mimi ninaamini wale ambao tunatoka kwenye Majimbo yenye shida nyingi, Majimbo ya Vijijini ambao watu hawana uwezo wa kutibiwa, mara moja au mara mbili tumeenda kwake na ametusaidia. Nichukue nafasi hii pia kumshukuru Katibu Mkuu na Watendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nimshukuru Mtendaji Mkuu wa *MSD*. Tumekuwa na changamoto ya muda mrefu sana huko nyuma. Ninyi ni mashahidi huko vijijini dawa zilikuwa hazifiki lakini kwa sasa kuna *flow* nzuri ya dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri utakuwa ni shahidi Bunge lililopita moja ya ajenda kubwa iliyokuwa hapa ni *MSD,* ndiyo maana kila anayechangia leo, maneno yamekuwa machache kwa sababu dawa zinafika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo la muhimu hapa la kuongea, kwamba kazi ya *MSD* imebaki kupelekewa fedha, kwenda kununua dawa na wale waliopeleka fedha kwenda kuchukua. Sasa hili jambo haliko sawa. Hatuna *option* nyingine, ni lazima *MSD* wapewe fedha. Kama tuna dhamira ya dhati ya kuhakikisha afya za Watanzania zinakuwa imara na kupunguza gharama za Serikali za

kununua dawa, ni lazima fedha iliyoombwa na *MSD* wapewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto, wakati mwingine unaweza kujiuliza maswali, kwamba mbona *MSD* kila mwaka wanapewa fedha, lakini hawana *capital* ya kuagiza dawa wenyewe? Nimejaribu kufuatilia hili jambo nikaona ni kweli kwamba Wabunge wengi wanaweza wakafikiria hilo kwamba wale *MSD* pengine kuna fedha ambayo wanabaki nayo. Ukweli ni kwamba fedha wanayopelekewa ndiyo wanayotumia kwenda kununua dawa, na kafaida kale kadogo pengine ndiyo anakatumia kuendesha ofisi. Sasa ni lazima sasa tuangalie namna bora ya kutoka hapo walipo. Namna bora ni kuhakikisha Wizara ya Fedha imewapa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama tumewahi kufikiria, ni lazima tuamini kwamba katika kitu cha thamani kubwa hapa duniani ni uhai. Ni ukweli kwamba afya ndiyo uhai. Hapa nyuma kumetokea ugonjwa wa Uviko. Ilikuwa ni changamoto kubwa kwa sababu dawa zote tunaagiza huko nje, na viwanda vyetu vilikuwa vimefungwa. Kwa nini hilo halionekani? Maana yake kuna siku tutakosa dawa moja kwa moja, kwa sababu tumeshindwa ku-*empower MSD*. Bawaomba sana Wizara ya Fedha, waangalie kwa upana mkubwa changamoto hii kwa namna ambavyo ilivyo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri tuna mtendaji mzuri wa *MSD* sasa hivi, tunaweza tukamwamini, tukampa fedha, tukaangalia baada ya miaka mitatu, nini kinaendelea? Ila tukiendelea kuwapa fedha ili waagize dawa, wataagiza dawa, watapeleka huko kwenye hospitali, nao hawana kitu, na hawana *Development Plan* ya aina yoyote, maana yake maisha yetu yatakuwa ni hayo. Nawaomba Wizara ya Fedha katika hilo la msingi sana. Pia

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hangamoto kubwa sana na ya kupindukia ya watumishi wa afya. Jimboni kwangu mwaka 2022 tumefungua zahanati nane kwa pamoja, lakini hizo zahanati hazina wahudumu. Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi zinakuja vijijini, nikutolee mfano kwenye hospitali yetu ya wilaya, mmetuletea fedha, tumefunga *X-Ray* mpya, *Ultra-Sound* mpya, mashine ya macho mpya, ya meno mpya, lakini hakuna mtumishi hata mmoja. Maana yake zinachakaa. Mmetuletea mpya, zinachakaa, hakuna chochote kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana, mwenzangu mmoja alisema tunavyoendelea kuweka hii miundombinu ya afya ni lazima tufikirie pia ni namna gani tutapata watumishi wa kwenda kusaidia kwenye vifaa hivi. Haina tija yoyote. Watu wangu pale Chemba wakiona kuna *X-Ray* mpya kweli, kuna *Ultra-Sound,* lakini hakuna chochote kinachoendelea. Mtu akitaka kufanyiwa *Ultra-Sound,* ni lazima aje Dodoma *General*. Namwomba Mheshimiwa Waziri sana katika hilo hebu tusaidie. Naamini sasa kwenye watumishi hawa, ajira mpya zilizotangazwa mtatufikiria zaidi katika Wilaya yetu ya Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kada zote za afya, sisi tuna asilimia ishirini na kitu ya watumishi. Kwa hiyo, unaweza ukaona changamoto kwa ukubwa wake ilivyo kubwa. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwaombeni sana, sana, sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la muhimu, miradi ya afya ambayo inatekelezwa, hii miradi ya *World Bank,*na *Global Funds,* kuna changamoto kidogo ipo. Kwa mfano, kuna jengo la Kata ya Msaada limeanza kujengwa mwaka 2007. Mwaka 2007 hapa wengine walikuwa bado wadogo, mpaka leo halijakamilika na limeishia njiani na watu wanaliona. Kila Mbunge akija, anaambiwa kama unataka tukupe kura, hebu malizia hilo jengo. Sasa kwa nini tunakuwa na mipango ambayo haikamiliki?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Kituo cha Afya Makorongo. Sasa hivi kinatumika na kilifunguliwa na Mheshimiwa Rais wakati huo Jakaya Mrisho Kikwete, hakina *theater,* hakina maabara, hakina mochwari. Kwa nini kiwe nusu? Nawaombeni sana, nimeandika barua mara kadhaa. Nilimwomba Mkurugenzi akaandika, tukaambiwa tulete *BOQ* lakini mpaka leo bado hakijakamilika, wala hakuna fedha yoyote ambayo imekuja kwa ajili ya umaliziaji wa majengo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niishukuru tena Wizara, niwashukuru watendaji, na Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Regina Ndege, jiandae Mheshimiwa Sima.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Afya. Awali ya yote napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoendelea kuboresha sekta hii ya afya ili afya ya wananchi wetu iendelee kuimarika. Nasema haya kwa sababu tumeona ni jinsi gani Mheshimiwa Rais ameendelea kuboresha afya ya wananchi hata kwa kusogeza huduma katika makazi ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, Mheshimiwa Rais ameongeza jitihada ya pekee kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma hapa nchini badala ya kusafiri kwenda nje ya nchi kuendelea kupata huduma za afya. Kwa namna ya pekee nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ummy na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu,

Naibu Katibu Mkuu na Wizara kwa ujumla, kwani wamekuwa washauri wazuri kwa Rais, lakini wameendelea kumsaidia kufanya kazi kwa bidii, kumsaidia Rais ili afya ya wananchi iendelee kuimarika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisipotoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan nitakuwa sijatenda haki. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuletea *CT-Scan* katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Manyara. Kabla hatujaletewa *CT-Scan* katika hospitali yetu, wagonjwa walikuwa wakihangaika kwenda Hospitali ya Benjamin Mkapa, KCMC na wakati mwingine walikuwa wanaenda Muhimbili, lakini hivi sasa huduma inatolewa pale mkoani, wananchi wetu wanapata huduma kwa ukaribu na pia imewapunguzia gharama ya kusafiri umbali mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutujengea jengo la *OPD*. Bahati nzuri alikuja Rais mwenyewe akalizindua jengo lile na sasa hivi linafanya kazi vizuri. Pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutujengea jengo la *Radiology*, na jengo la *ICU* pamoja na damu salama. Hapa naomba sasa, majengo haya ya *ICU* na Damu Salama hayajakamilika. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupelekee pesa pale Mkoani Manyara ili jengo hili liweze kukamilika na liweze kufanya kazi kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia jengo la wagonjwa wa dharura na tayari limeanza kufanya kazi, wagonjwa wanapata huduma. Pia hospitali yetu ya mkoa kulingana na wingi wa watu katika mkoa, hatuna watumishi, waliopo ni wachache sana. Tuna watumishi 250, tunahitaji watumishi wafike 468 ili hospitali hii iweze kutoa huduma vizuri. Tunaposema huduma ya afya inalegea, ni pamoja na kutokuwa na watumishi wa kutosha katika hospitali. Kwa hiyo, mkituongezea watumishi, tunaamini huduma itatolewa vizuri

na wagonjwa wataendelea kupata huduma, itawapunguzia wagonjwa kwenda kutafuta wataalam katika hospitali nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naombe Wizara ituletee daktari bingwa wa magonjwa ya watoto, daktari bingwa wa magonjwa ya mifupa, madaktari bingwa wa macho, daktari bingwa wa usingizi na daktari bingwa wa mionzi. Mheshimiwa Waziri aone ni namna gani tuna upungufu mkubwa kwa sababu hatuna madaktari bingwa katika hospitali yetu. Kwa hiyo, akitupatia hao madaktari, tutakuwa na uhakika kwamba wagonjwa wetu watapata huduma kwa ukaribu na huduma sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, pamoja na kwamba hospitali yetu imeanza toka 2008, tunaishukuru Serikali imeendelea kuleta fedha siku hadi siku. Kila mwaka katika bajeti ya Serikali tumeendelea kuletewa fedha. Naomba, kuna upungufu mkubwa wa wodi. Hatuna wodi ya wanawake, wodi ya wanaume na wodi ya watoto. Ukiwa huna wodi hizo, moja kwa moja ujue kwamba hospitali yetu haijakamilika bado. Kwa hiyo, naiomba Serikali ituletee fedha kwa ajili ya kukamilisha au kujenga hizo wodi ili wagonjwa waweze kuhudumiwa pale na waweze kupata huduma ya malazi kama wagonjwa ambao wanatakiwa kulazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naomba gari kwa ajili ya uendeshaji katika hospitali yetu ya mkoa. Ili kuendelea kutoa huduma hizi katika maeneo mengine, basi ni vyema hospitali ikapata huduma hizi ili huduma za afya zitolewe kwa ukamilifu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusemea hospitali yangu ya mkoa, niende moja kwa moja kwenye changamoto ambayo naiona siyo kwa mkoa wangu tu, bali katika maeneo mengi; suala zima la vifaa. Utakuta katika

maeneo mengi vifaa tiba au vifaa vile vya vipimo vinaharibika, lakini vinachukua muda mrefu kutengenezwa. Mfano, unapoongelea *X-Ray,* inaharibika, na *CT-Scan* inaharibika, lakini haitengezwi. Wagonjwa wanaenda hospitalini hawapati huduma, hawapati vipimo kila akienda anaambiwa kifaa kimeharibika, anaenda wiki inayofuata, kifaa kimeharibika. Kwa hiyo, hii imeleta usumbufu katika maeneo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mifano hai. Kwa mfano, tuna hospitali yetu hapa ya afya ya akili ya Mirembe. Tunapozungumzia hospitali ya magonjwa ya akili, moja kwa moja kifaa kinachoitwa *EEG* ni kifaa muhimu sana katika hospitali, lakini jambo la kushangaza ni miezi karibia sita tunaelekea miezi saba hospitali ile haina kipimo hicho cha *EEG*. Sasa hebu fikiria, mgonjwa anatoka mkoani, analetwa hospitali, hapati kipimo, anatibiwaje? Zaidi tumesema ni hospitali *special* kwa ajili ya magonjwa ya akili. Kwa hiyo naombe Serikali iliangalie hili, kwa sababu tusipoliangalia wagonjwa watalundikwa pale hospitalini, hawapati matibabu na hawapati vipimo sahihi. Kwa hiyo, madaktari watapima kulingana na maelezo, badala ya kupima na kujua tatizo hasa ni nini? Kwa hiyo, naomba sana, vifaa tiba vinapoharibika, ni lazima Serikali ichukue jukumu la haraka sana ili vifaa vile vitengenezwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa tunayoiona ni kwamba, vifaa vile vinashindwa kutengenezwa kwa sababu hatuna wataalam wa kutengeneza vile vifaa katika vituo hivyo. Kwa hiyo, niombe wizara ijipange ni namna gani kuhakikisha wakipeleka vifaa tiba, pale pale kuwe na mtaalam wa kutengeneza vile vifaa pindi vinavyoharibika. Wapo vijana wetu waliomaliza vyuo wamemaliza mafunzo *DIT* wamekaa mtaani. Serikali kwa nini isiwatumie wale vijana wakawepo kwenye vituo au hospitali zetu za *referral* ili kifaa kinapoharibika tu, iwe rahisi kutengenezwa na huduma kuendelea kutolewa kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna changamoto ya ukosefu wa madawa. Pamoja na kwamba Rais amefanya kazi kubwa sana kujenga vituo vingi vya afya, lakini bado madawa kule ni changamoto, hasa maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, naomba Wizara ilichukue hili kuhakikisha kwamba wagonjwa wanapoenda katika vituo vyetu vya afya wanapata madawa muhimu yale ya binadamu ili watu wasipate tena usumbufu mwingi wa kutembea hapa na pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilizungumzie na nilishawahi kulizungumzia hapa Bungeni, ni suala zima la Sera ya Huduma Afya ya Mama na Mtoto. Wamama wajawazito bado wanapata changamoto wanapoenda kujifungua, kwa sababu mama anatakiwa abebe vifaa yenye mwenyewe kama *gloves,* pamba na vitu vingine ambavyo vinahitajika wakati wa kujifungua. katika vituo vyetu vya afya na maeneo mengine, hasa katika jamii zetu za kifugaji na umbali wa kwenda hospitali inawalazimu wale wamama kujinyima baadhi ya vyakula ili mtoto awe mdogo tumboni ili aweze kujifungulia nyumbani badala ya kwenda hospitali. Sasa matokeo yake watajifungua watoto ambao hawana afya na ambao hawajatimiza umri kwa kuwa amekosa virutubisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yanachangiwa na gharama za hospitali. Hizi gharama kuna familia nyingine hawaziwezi kabisa. Kwa hiyo, naomba sera ya afya ikasimamiwe. Sera ya afya ni kwamba mama anapoenda kujifungua, basi apate zile huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwa mtoto mdogo wa umri chini ya miaka mitano, naomba sasa Wizara pia iliangalie hili, kwa sababu wapo watoto wadogo ambao familia zao ni duni pia, wanashindwa kugharamikia matibabu. Kwa hiyo, Serikali ione ni namna gani ya kuendelea kuwahudumia wale watoto kwa kuwapatia

huduma ya afya ili waweze kuishi kama binadamu wengine ambavyo tunaishi kwa sasa. Kwa hiyo, naomba sana Wizara iweze kusimamia sera hii ili Watanzania waendelee kupata huduma hii na afya ya wananchi wetu iendelee kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema. Pia nampongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyoifanya. Sisi Wana-Singida Mjini tumekuwa na kero kubwa ya hospitali ya wilaya, sasa tumepatiwa hospitali ya wilaya. Tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Afya, walikuwa tayari kutuachia majengo ya hospitali ya mkoa ili yaweze kuwa hospitali ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchango wangu nianze kwa rejea ya Mwanafalsafa nguli na mpigania uhuru wa India, Mahatma Gandhi. Aliwahi kusema "*it is health that is real wealth and not pieces of gold or silver.*" Alimanisha nini? Kwa tafsiri isiyo rasmi, afya ndiyo utajiri halisia kuliko kuwa na vipande vya dhahabu ama fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahatma Gandhi alikuwa anamaanisha nini hapa? Unaweza kuwa na kila kitu; na Serikali leo tumewekeza miundombinu ya kutosha kwenye elimu, kwenye afya, na maeneo yote tumewekeza na tumeweka fedha nyingi, lakini tunawahitaji Watanzania wenye afya bora ili waweze kutumia hiyo miundombinu iliyopo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa rejea hii ya Mahatma Gandhi, nataka niangalie maeneo mawili. Moja ni la Mfuko wa Bima ya Afya. Mfuko wa Bima ya Afya siyo siyo taasisi ya kibiashara *(business entity),* mfuko huu unatoa huduma, na kama unatoa huduma, nilitarajia kuiona Serikali inauwekea ruzuku ili uweze kufanya kazi yake vizuri. Leo Watanzania wengi wanasubiri Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Ukiwa na bima, maana yake una *security* ya kuweza kupata huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitoe mifano michache. Kwenye Toto Afya Kadi kwenye taarifa ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri hapa, imeeleza vizuri kwamba katika katika watoto 205,000 waliosajiliwa, wamechangia shilingi bilioni 5.99, wametumia, shilingi bilioni 40. Mfuko huu unaenda kufa. Pia wamesema hapa kwamba kuna huduma za vipimo zinatolewa. Huduma hizi zimekuwa ni za gharama kubwa, hakuna Mtanzania anayeweza ku-*afford*. Anayeumia kwenye hizi huduma, mfuko ndiyo unaenda kuumia kwa sababu ndiyo utakaolipa fidia au utakaolipa hiyo fedha ambayo mtu anahudumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hatuwezi kuchukua vipimo vya India labda shilingi milioni 30, sisi tukaweka Shilingi milioni 15, badala kuangalia uhalisia wa mazingira yetu ili tuweke kiwango ambacho kitamsaidia Mtanzania kupata huduma, na kitausaidia pia huu mfuko uweze kulipwa kwa gharama ambayo inaendana na mazingira yetu tuliojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine muhimu sana ni eneo la dawa. Taarifa ya Kamati imesema vizuri hapa kuhusu *MSD* kwamba wanapaswa kuwekewa fedha ama kukopeshwa fedha zaidi ya shilingi bilioni 500, nakubaliana nao; lakini jambo hapa la kuangalia, kama kuanzia bajeti ya mwaka 2021 tulitenga shilingi bilioni 200, mwaka 2022 shilingi bilioni 200, mwaka huu shilingi bilioni 205, *projection* ya

kutenga hizi fedha za dawa tunaipata wapi? Maoteo ya dawa tunayatoa wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye zahanati zetu huku chini, mtu anayeuza dawa ni *medical attendant*. Ni mhudumu aliyeajiriwa kwa ajili ya kupanga ma-*file* labda kufanya usafi, ndiyo anayetufanyia kazi hii. Nataka nitumie fursa hii kuwapongeza sana *medical attendants* wote, wamefanya kazi kubwa, na wamelibeba Taifa hili, lakini huyu hana taaluma, hawezi kufanya *inventory,* hawezi kutupa *data* halisi za mahitaji ya dawa. Huyu mhudumu anasimamiwa na *DMO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kuajiri wafamasia na wafamasia wasaidizi huku chini ili tupate *data* halisi, tunataka dawa za kiwango gani na dawa gani? Kama leo unatenga shilingi bilioni 200, mahitaji yetu inawezekana ni shilingi bilioni 400. Sasa kama ni shilingi bilioni 400, *ceiling* inatuambia shilingi bilioni 200, kwa nini Serikali kila mwaka tunaweka shilingi bilioni 200? Tuweke walau shilingi bilioni 300 ili matatizo ya uhaba wa dawa yasiwepo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili lina changamoto moja kubwa sana ambayo mimi nadhani mara nyingi nimekuwa nikizungumza, na nilizungumza wakati wa Wizara ya TAMISEMI, wasimamizi wakuu wa eneo hili ni Wizara ya TAMISEMI. Msemaji wa sekta ya afya ni Wizara ya Afya. Unafanya *projection* ya dawa kutoka huku chini, unaenda kumkabishi Wizara ya Afya ili aweze kuleta dawa. Hapo kuna changamoto. Kama upungufu unaendelea, maana yake hapa kuna changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hii kuiondoa ni nyepesi sana. Tunaye *CMO,* Mganga Mkuu wa Serikali; huku chini kuna *RMO*, kuna *DMO*. Hawa watu wawili; *RMO* na *DMO,* wako chini ya TAMISEMI. *CMO* akitoka kule, lazima aripoti kwa Katibu Tawala wa Mkoa, amekuja na jambo

gani? Apokelewe, maana yake atapokea taarifa ambayo wao wameiandaa. Taarifa hii inaweza isiwe halisi, naye hawezi kujiridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushauri hapa, naiomba Serikali, *DMO* hawa ni wataalam; *RMO,* huyu ni mtaalam, hawa sio watawala. Kazi wanazozifanya kule ni za kiutawala zaidi badala ya kufanya kazi za kiutaalam, kwa sababu wao wako chini ya Wizara ya TAMISEMI. Kama tunataka kweli kujali afya za Watanzania na tuondokane na upungufu huu ninaoueleza, maana yake *RMO*, *DMO* wawe chini ya Wizara ya Afya. Wakiwa chini ya Wizara ya Afya, watatusaidia sisi kwenye *projection* yoyote ya dawa na vitu vingine vyote kwenye tiba. Hapa kuna changamoto kubwa sana. Tukishindwa kufanya hivi, basi tutachoweza kufanya *CMO* aanzishe ofisi zake kwenye mkoa ili awe na *authority* ya kuweza kusimamia eneo la tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mwingine mzuri sana. Walifanya vizuri Mheshimiwa Mzee Lukuvi hapa na dada yangu Mheshimiwa Angeline Mabula kwenye Wizara ya Ardhi walipoamua kuwapeleka Makamishna wasaidizi kwenye kila mkoa. Tumepunguza tatizo kubwa la migogoro ya ardhi, na kila mkoa leo unao Kamishna Msaidizi. Bado hata *CAG* tunayemtuma sisi, kule ukienda kuna *National Audit Office,* ziko kule. Kwa nini *CAG* hajafanya kazi na *internal auditor?* Kwa sababu *internal auditor* mwajiri wake anayemsimia ni Mkurugenzi, hawezi kupata *data* halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama huku tumeweza kufanya hivi, kwa nini kwenye afya tusiweze kufanya? Kama *coordination* hii imeshindikana kutupatia taarifa halisi, basi ni vyema tukahakikisha kwamba Mganga Mkuu wa Serikali naye aanzishe ofisi zake kwenye mkoa. Huko kwenye mikoa, anaweza akasimamia vizuri eneo hili la afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia afya ya Watanzania, tunazungumzia jambo la muhimu na jambo la msingi sana. Fedha inayotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa Wizara hii, haitoshi; na kwa kuwa haitoshi, haiwezi kutekeleza majukumu yake kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna hospitali ya wilaya sasa, tumepewa na wenzetu wa Wizara ya Afya. Kwa kweli tunawashukuru sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kidogo kwa sababu ni mchangiaji wa mwisho na Mungu atakubariki sana, kwa kuwa najua kazi hii umeifanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji fedha za ukarabati wa jengo la hospitali ya wilaya Shilingi bilioni moja, na pia tunahitaji fedha nyingine kwa ajili ya kuweka miundombinu mingine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuitakie pia Yanga tarehe 17 waweze kufuzu wacheze vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Mariam Kisangi, sijui kama yupo, na pia ajiandae Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Tecla Ungele, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza mijadala.

Mheshimiwa Mariam Kisangi ameomba udhuru, Mheshimiwa Joseph Mkundi, jiandae Mheshimiwa Tecla Ungele. Mheshimiwa Mkundi hayupo, Mheshimiwa Tecla, Mheshimiwa Reuben, Mheshimiwa Mwantumu Dau. *(Makofi)*

**MHE. MWANTUMU DAU. HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii ya kuwashukuru Mawaziri wangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu wake kwa kufanya kazi nzuri sana. Wanafanya kazi usiku na mchana kupumzika hawajui kupumzika kama kazi iwe tu kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake anazochukua katika Serikali yetu hii ya Muungano jinsi

anavyoifanya kazi kubwa na yeye kwa kila pembe, kwa kila rika anafanya kazi. Kila sekta ukija sekta ya afya hapa hayasemeki sasa hivi, anafanya kazi vizuri, vituo vimeimarika viko vizuri, havina wasiwasi kama vile zamani unaingia kwenye kituo, kituo ukitambua lakini hivi sasa hivi tunashukuru sana kwamba vituo vimeimarika na vinafanya kazi vizuri. Kwa hilo tuhongere kwa sote jamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea pia nishukuru Wizara hii ya Afya ya huku Tanzania, vilevile inafanya kazi vizuri katika nchi yetu hii na hasa inasaidia mpaka na Zanzibar pia inasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe kwamba wizara yako inafanya kazi kutusaidia katika Wizara yetu ya Zanzibar ya Afya kule Mnazi mmoja. Hususani ukija kwenye magonjwa ya moyo, magonjwa ya figo na magonjwa ya kupandikiza pia tunakuja kule yanasadia na wanafanya kambi ya kukaa baina ya madaktari wa kule na madaktari wa huku wanazifanya hizi kazi kwa pamoja kwa mashirikiano ili wale wagonjwa na wao wanajisikia na wanajua wanafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ule muda wa kusema wachukuliwe wagonjwa wapelekwe India au wapelekwe nchi nyingine angalabu sana madaktari wanakuja zao Zanzibar wanawasaidia wagonjwa wa moyo pamoja na figo pamoja na wale ambao wanaopandikizwa kizazi cha kinamama, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea naomba sekta hii isituchoke iwe pamoja na sisi, wawe na mashirikiano na madaktari wetu kwa kila mara, kila wakati wawe wanakwenda kutupa mashirikiano kule kwetu Zanzibar ili kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye mada yangu ya pili kuhusu habari ya saratani. Saratani inatibika tena inatibika sana saratani, zamani ilikuwa ukipata Saratani hofu inakuingia, wasiwasi, mashaka unajua mie hapa tena nishakwenda. Lakini kwa hivi sasa ukiingundua saratani na ukienda uko kwenye Hospitali ya *Ocean Road* ukitibiwa mapema basi unapona na unakuwa mzima. Kama ujaolewa, unaolewa kama hutaki unafanya kazi zako salama salimini kwa hili gonjwa la saratani hivi sasa hivi la kizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa izidi kufanya kazi kuhusu suala hili la saratani, wagongwa wanapotoka kule kwetu Zanzibar wakija huku Bara kuja kutibiwa *Ocea Road* wanatoka kule hali zinakuwa taabani lakini wanakuwa hawajambo na pia kule kuna kitengo mmekiweka nyie cha kwamba wale wagonjwa wakiwa wamepata muda mkubwa huku basi wanakwenda kufanyiwa vipimo pale Mnazi mmoja. Kwa hiyo, nikushukuri kwa hilo pia, mnafanyakazi vizuri si haba tunashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuendelea nazungumzia kuhusu habari ya suala la Afya ya Akili. Suala la afya ya akili haliko kwenye suala la kuwa ndiyo afya ya akili huyu mgonjwa kapata akili, kapelekwa *mentally* au kapelekwa Milembe ahaa afya ya akili inakuja hata mgonjwa wa sukari, shindikizo la damu pia anapata afya ya akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mgonjwa wa sukari akienda akifurahi sana basi kaisha zidisha kila kitu katika kiwiliwili chake, akisema afanye kitu cha ukali kaishazidisha kila kitu wewe unatakiwa uwe *standard* katika kukaa yako na suala hili la ugonjwa wa sukari. Usifurahi sana, usiwe mkali sana wala usiwe na hamaki sana, ukihamaki basi tayari afya ya akili imeshakuingia ujijui, hujitambui saa yeyote unaweza ukapelekwa mentally. Kwa sababu tayari pale ushaichanganya ile sukari na ile afya ya akili kwa hivyo hii

afya ya akili Mheshimiwa Waziri inaingilizana mpaka na magonjwa hayo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ugonjwa huu wa sukari hivi karibuni nilikwenda mie kuhangaika kuhusu dawa za sukari kidogo dawa zilipungua kukawa hakuna kidogo. Kwa hiyo, niombe hizi dawa zinapokuwa tayari basi tuzipate kwa wingi ili zile afya zetu ziimarike na tuweze kufanya kazi ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hivi sasa hivi naunga mkono hoja asilimia mia moja haya niliyoyasema yanatosha na ninashukuru wizara hii ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa ruksa yako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tecla Ungele, jiandae Mheshimiwa Taska Mbogo.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii nami nichangie hoja ya Wizara ya Afya. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunipatia uhai hata sasa hivi niko naendelea na shughuli hii hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wa Afya na Naibu wake Dkt. Molel na timu yote ya Wizara ya Afya hakika mnafanyakazi na tunawaombeeni usiku na mchana Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ya Wizara ya Afya inawezeshwa na Jemedali mwenyewe Mkuu Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa kipaumbele kwa huduma ya afya kwenye nchi yetu hata amewezesha kujenga vituo vya afya, zahanati, hospitali kuanzia ngazi ile kule ya kaya, ngazi ya

msingi hadi ya taifa kwa kweli tuna mshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa zahanati hizi na utoaji wa vifaa tiba kwenye zahanati hizi na hospitali hizi zimefanyika nchi nzima hata sisi watu wa Mkoa wa Lindi tumefaidika ni wanufaika wakubwa wa huduma hizi tunashukuru sana. Hata kule Nachingwea kumejengwa *ICU* nzuri na vifaa tiba vimekwenda na watalam wamekwenda ingawaje bado hawatoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za *ICU* na huduma za *emergency* ni muhimu sana zinavyojengwa kwenye hizi Hospitali zetu za Wilaya kwa sababu jambo hili la kubadilika afya zetu inaweza ikabadilika hata wakati unatembea vizuri hivi lakini hali yako inaweza ikabadilika muda wowote lakini kunavyokuwa na hizi huduma za *emegency* na huduma za *ICU* unaweza maisha yakanusurika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan tunamshukuru sana. Lakini pia kuna huduma bobezi tumeziona kwenye wasilisho la Mheshimiwa Waziri, huduma bobezi hizi zinaboresha na zinatufanya Tanzania tuwe kitovu cha huduma hizi muhimu na pia kufanya nchi yetu iwe tuwe katika eneo lakuwa na *medical tourism*. Ukienda pale *Ocean Road,* ukienda pale Muhimbili, ukienda pale *MOI,* ukienda pale *JKCI* hakika mambo ni mazito yanayofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nijikite kwenye mafunzo, eneo hili la mafunzo naweza niaeleza sana lakini muda hautanitosha kwa sababu ni eneo ambalo limelifanyia kazi kwa zaidi ya miaka 30. Mafunzo ya Afya, mafunzo haya ya afya kwa vyuo vya kati tunaomba mafunzo hayo yaboreswe kwa sababu wahitimu hawa tunaowapata kwenye eneo hili la huduma za afya za kati, mafunzo ya afya ya kati hao ndiyo wanaenda kutumika kwenye zahanati, kwenye vitu vya afya

na ndiko kule kuna mapungufu na ndiyo watu wetu wengi wako kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba katika hili miundombinu ya maeneo yale hasa kwenye vyuo vya Serikali naomba viboreshwe. Kwa mfano kuna jengo pale Nachingwea limeanzishwa lakuendelea kuboresha kile chuo ambacho mafunzo yake yalisitishwa na *NACTE* wakati ule ambayo sasa hivi ni *NACTVET* tunaomba na chuo kile kikamilishwe na jengo lile likamilishwe maana hata sasa wananchi wale wa Nachingwea na Lindi kwa ujumla tunategemea chuo kile ndiyo cha uuguzi pekee cha Serikali kwa Mkoa wa Lindi. Lakini jengo lile limesitishwa, hatujui kinachoendelea kwa kweli wananchi wale wana sintofahamu nini kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hii huduma ninafurahishwa sana leo nilivyosikia yale mafunzo ya *integrated* and *comminated community heathy worker*. Nimefurahi sana Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu alivyosema yale mafunzo yanakuja tena ni *program* ambayo anaileta tena ile itakuwa ni tija kubwa katika jamii yetu kwa sababu wale watakuwa kwenye ngazi ya jamii kule. Wale watashughulika hasa kwenye kutoa ushauri na huduma mbalimbali kuhusu magonjwa yasiyo ambukiza na mambo mengine ambayo yangefanya yawe makubwa zaidi mpaka yakahitajika huduma kubwa zaidi. Hili napongeza wizara, nawapongeza sana Mheshimiwa Ummy Mwalimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huduma za mama na mtoto, huduma hizi za mama na mtoto naomba ziboreshwe mtoto wa chini ya miaka mitano, mama mjamzito bado kuna maeneo mengine Mheshimiwa Waziri bado wamama wale wanahitajika kununua vifaa kwenda kujifungua tafadhali, tafadhali ninaomba suala hili liangaliwe. Kuna maeneo mengine Tanzania kuna shida mtu anakosa hata shilingi 500 sasa mtu huyu atakapoambiwa anunue vifaa hivi, kifaa hiki,

kifaa hiki ili akajifungue hiyo tena itakuwa ni shida na tutazidi kuongezea ule uzito wa tatizo la vifo vya wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote kwa yote ninawapongeza sana Mawaziri hawa na Serikali yote ya Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi wanayofanya kuboresha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Taska, Mheshimiwa Neema, jiandae Mheshimiwa Festo.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Wizara ya Afya kwanza kabisa napenda kupongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi yake nzuri anayoijali kwa kujali Afya ya Watanzania. Mama mjali afya ya Tanzania hiki hakina ubishi kila mtu ameona nchini Tanzania jinsi gani Mheshimiwa Rais alivyoweka pesa nyingi kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Molel wote kwa pamoja wanafanya kazi nzuri sana kuhakikisha kwamba Watanzania wanakuwa na afya nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwakumbushe Watanzania kazi ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya kwenye Wizara ya Afya. Mheshimiwa Rais amehakikisha kwamba Nchini Tanzania kumejengwa zahanati 1,066 kila sehemu katika kipindi cha miaka miwili Mheshimiwa Rais huyu amehakikisha kuna vituo vya afya vimejengwa 234 kwa kipindi tu hiki cha miaka miwili. Mheshimiwa Rais huyu

amehakikisha kuna majengo ya *ICU* yamejengwa takribani 28 nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais huyu amehakikisha kwamba kuna majengo ya dharula maana yake kuna magonjwa yale dharula yamejengwa takribani majengo 80 nchini Tanzania. Huyu Rais anayejali afya za watanzania, huyu Rais anaejali kizazi kinachokuja kwa sababu anataka watanzania wawe na afya njema ili waweze kufanya kazi vizuri na waweze kuendeleza nchi yetu ya Tanzania pongezi ngingi sana kwa Mheshimiwa Rais makofi kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hayo tu leo asubuhi Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha taarifa yake amekuja hapa na madaktari ambao watapita kwenye hospitali zetu kwenda kuwafundisha wale madakta kwenye kila wilaya hili ni jambo ambalo linatendeka kwa mara ya kwanza nchini kwetu Tanzania. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako ni jambo jema wale watakapopita watakwenda kuboresha afya za watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze pia kwa jinsi hospitali yetu ya Benjamini Mkapa inavyofanyakazi wagonjwa wengi wanakuja pale wanatibiwa. Pia kwa lile jambo ambalo Mheshimiwa Ummy alituelezea hapa kuhusu kuweza kuwashughulikia wagonjwa wa Selemundo hilo ni tatizo kwa watanzania wengi. Watanzania wengi wanaumwa huu ugonjwa wa *sickle cell* na watoto wengi wameweza kupoteza maisha kwa ajili ya ugonjwa huu. Kwa hiyo, kuwepo kwa tiba hii nawapongeza sana sana Wizara ya Afya pamoja na watendaji wenu, lakini tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuyatekeleza yote haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona jinsi gani wilaya na mikoa zimepewa *ambulance*, hili halina ubishi. Katika kipindi

cha miaka miwili *ambulance* nyingi zimepelekwa kwenye hospitali zetu, hata kwenye Mkoa wangu wa Katavi, *ambulance* zilipelekwa. Ninapenda kushukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa ajili ya *ambulance* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi ninayo machache ya kuzungumzia kuhusu Mkoa wangu wa Katavi. Kwenye Mkoa wangu wa Katavi tunayo matatizo ya upungufu wa madaktari takribani 17 (*MD)*. Tuna upungufu wa wauguzi 33, pia tuna upungufu wa wataalamu wa maabara takribani 13, tuna upungufu wa wataalamu wa meno. Vilevile tuna upungufu wa wataalamu wa dawa za usingizi. Katika hospitali zetu za wilaya pale tuna upungufu wa vifaa tiba ambavyo vinatakiwa viwepo pale kwenye hospitali yetu ya wilaya. Tuna upungufu mpaka wa vitanda na magodoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niliseme hapa ili muweze kusaidia pale tuweze kupata magodoro pamoja na vitanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mkoa wa Katavi ina madaktari bingwa sita tu, ambapo tuna matatizo katika magonjwa mengine kwenye Mkoa wetu wa Katavi; na mgonjwa anapokuwa na hilo tatizo inabidi apelekwe kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mbeya ambayo ni mbali. Kwa sababu kutoka Mkoani kwangu Katavi mpaka kufika Mbeya kule pana umbali. Kwa hiyo kama inapotokea kuna mgonjwa wa figo anatakiwa kuchujwa damu inabidi apelekwe Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba tuweze kupatiwa hivyo vifaa. Lakini kwenye Mkoa wangu pia wa Katavi tunayo matatizo ya Madaktari Bingwa. Mgonjwa anapoumia, kwa mfano anapovunjika mkono inabidi aende rufaa kama nilivyosema Mbeya au apelekwe Bugando. Lakini tatizo ambalo nimeliona kwenye Mkoa wangu wa Katavi kuna tatizo la kuchangia mafuta kwenye *ambulance,* lakini

kuna tatizo pia la kuchangia fedha ya yule nesi anayemsindikiza mgonjwa. Pia kunakuwa pia na tatizo la kumchangia pesa ya kujikimu…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumuongezea taarifa mama yangu Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalumu kutoka kule Katavi. Jambo hili la kuwataka wagonjwa wachangie mafuta kwenye *ambulance* lipo pia na kwenye Mkoa wetu wa Songwe hususan kwenye Jimbo la Momba. Watu wakiumwa wanataka wachangie mafuta kwenye *ambulance*, sasa, watu wa vijijini wanapata wapi hela ya kuweka mafuta kwenye *ambulance* zaidi ya lita 50? Mheshimiwa Waziri jambo hili anapaswa kulitambua kwenye ngazi za zahanati na vituo vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hiyo unampa aliyezungumza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Nampa taarifa mama yangu wakati yeye anamwambia Mheshimiwa Waziri…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taska.

**MHE. TASKA R MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea taarifa hiyo kwa sababu ndilo suala ambalo nilikuwa ninalizungumzia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia ule umbali wa kutoka pale kwetu Katavi mpaka kufika kule Mbeya kwenye hospitali ya rufaa unamwambia mgonjwa aweke mafuta hiyo

*ambulance*. Kuna familia moja kule kwetu mkoani Katavi ilibidi wauze nyumba ili waweze kumpeleka hiyo mgonjwa kule rufaa Mbeya; lakini wameenda kule wameuza *bill* kubwa lakini pia mgonjwa yule alifariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa ninaomba ufafanuzi; zile *ambulance* ni nani anatakiwa aweke mafuta kwenye ile *ambulance*? Lakini pia yule nesi anakuwa yuko kazini, dereva anakuwa yuko kazini kwa sababu anaendesha ile *ambulance* ambayo ni ya hospitali, sasa inakuwaje anatakiwa alipwe posho zake na mtu ambaye anamuuguza mgonjwa wake? Mheshimiwa Waziri Ummy na Naibu wako najua nyinyi ni wachapakazi wazuri ninaamini kwamba suala hili mmelisikia na mtalishughulikia kwa sababu linafanya mpaka wagonjwa wengine kutoka kwenye ule Mkoa wangu wa Katavi washindwe kwenda kwenye hospitali za rufaa kwa sababu wanakuwa hawana ule uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, tuna mapungufu ya madaktari bingwa, wagonjwa wa ndani, watoto, macho wagonjwa wa akili, mionzi pamoja na mapungufu ya vifaa tiba ni suala ambalo linaukabili Mkoa wetu wa Katavi kwenye vituo vya afya pamoja na zahanati…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango mzuri.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema, jiandae Mheshimiwa Sanga.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kuchangia katika

Wizara yetu hii muhimu sana ya Afya. Nitumie nafasi hii pia kuipongeza Serikali yangu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali inayoongozwa na mama yetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, chini ya dada yetu Ummy pamoja na Mheshimiwa Mollel. Mimi binafsi niseme nina imani kubwa na hawa mawaziri wetu kwa namna ambavyo wamekuwa wakiendelea kutupa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba nawapongeza kwa namna ambavyo nimeweza kuona wameelezea suala la lishe vizuri kwenye taarifa yao. Hii inaonesha kwamba Wizara kama hii wanaona umuhimu wa suala la lishe kwa nchi hii na kuangalia ni namna gani wanakwenda kuisaidia nchi kuweza kuondokana na changamoto za matatizo ya lishe yanayokuwa yanaendelea nchini. Kwa hiyo ninampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kuiona lishe kama ni kitu cha msingi. Nimependa zaidi sana pale walipoweza kuelezea kwamba wataanzisha viwanda vya utengenezaji wa vyakula dawa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni ajabu lakini iliyokweli kuona kwamba Tanzania tunaozalisha karanga, tuna maziwa mengi ya kutosha eti tunaenda kuagiza *plant peanut*, maziwa *F100* na *F75* kuitoka Ufaransa; kweli ilikuwa ni ajabu; lakini naona wameliona hilo na wanakwenda kulifanyia kazi. Na ninaamini hili litaweza kuleta ajira kwa wananchi wetu wa Tanzania kwa sababu karanga ni zetu na maziwa ni ya kwetu. Ninashukuru sana kwa hilo kwa Mheshimiwa Waziri kuweza kuliona

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa na mambo machache, ninadhani yanaweza kuleta tija kwenye Serikali yetu. Wameendelea kutujengea miundombinu mingi sana. Sisi kama Watanzania hususani kutoka Mkoa wa Songwe tunawashukuru na tunajivunia sana yale majengo mazuri

ambayo mmeweza kutujengea katika nchi yetu. Tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wameendela kutoa vifaa tiba vya kisasa vizuri na vingi sana. Kwa hiyo, na hili tunawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu inakuja wapi? Hoja yangu inakuja, ni kwamba majengo na wataalamu waliopo kwenye majengo unakuta haviendani. Haviendani kwa ubora na wala haviendani kwa idadi ya watumishi wanaotakiwa kwenye yale majengo. Kwa hiyo nilikuwa natamani Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku *wind-up* mwishoni atusaidie kutueleza kwamba, ana mpango gani angalau wa kufanya *reshuffling* ya kupeleka wataalamu waliobora kutoka kwenye hospitali zile kongwe ambazo zina wataalamu wazuri Kwenda kwenye hizo hospitali za rufaa mpya ambazo zimeanzishwa, ili majengo na wataalamu watoe huduma iliyobora?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kitu kingine ni kwamba wametusaidia sana kuleta vifaa vingi sana; na nimshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Mollel, mwaka jana mwezi wa pili alitupatia *x-ray* katika Wilaya ya Ileje. Lakini nitoe tu masikitiko yangu leo hii hapa kwamba *x-ray* ile katika Wilaya ya Ileje mpaka leo haifanyi kazi. Nashindwa kuelewa kwamba Serikali kweli Serikali hii inayopambana kutoa fedha nyingi kwa ajili ya vifaa tiba inashindwa kufanya ufuatiliaji na kuhakikisha mitambo hii iweze kufanya kazi kwa wakati? Ile dhamira ya mimi kupambana kuomba *x-ray* mashine katika Wilaya ya Ileje haijaweza kufanikiwa kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unaweza ukaona kwamba kuna wataalamu kule chini ambao wapo na wanafanya kazi na *supervision* wanafanya, na hiyo *supervision* wanazozifanya ipo haja ya wale wataalamu huko chini waangalie kwamba *supervision* zao zinakuwa zina tija

gani? Kwa sababu kama *x-ray* imekuja mwaka jana mwezi wa pili mpaka leo haifanyi kazi; yaani unashindwa kupata picha kwamba wale wataalamu walioko kule chini ina maana hawaoni shida yetu sisi kama Watanzania kwenye eneo lile kwamba tunahitaji *x-ray*? Na kila siku wanakwenda wanachukua posho za hizo *supervision* na *x-ray* bado haifanyi kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo si kwa Ileje tu, Ileje *is just a sample,* lakini nchi nzima yaani kuna maeneo mbalimbali ambayo vifaa vizuri vinapelekwa vya kisasa lakini havifanyi kazi kwa wakati. Lakini pia vifaa hivi vinavyokuwa vinaletwa wataalamu wale wahandisi wa vifaa tiba tunao wanagapi wa kutosha kuweza kutengeneza? Je, hawa wataalamu wa kuweza ku–*operate* hivi vifaa kama nchi tumetengeneza mkakakti gani wa kuwa na wataalamu ambao wataweza ku–*operate* hivi vifaa?

Mheshimiwa Naibu Spika,unashangaa *x-ray* imeletwa unaambiwa mtu wa *radiology* hayupo. Kifaa kimeletwa unaambiwa mtu wa *anesthesia* hayupo. Sasa *you can imagine;* mipango ya ununuzi wa vifaa unaokuwa unaendelea nchini na utengenezaji wa wataalamu ambao wataenda kusaidia vifaa hivyo kufanya kazi hauendi sambamba. Kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Waziri kupitia bajeti hii aje na mkakati ambao utaonesha uwiano wa ununuzi wa vifaa vya kisasa unaoendelea lakini na wale *operators,* wataalamu ambao wameandaliwa kwa ajili ya ununuzi wa hivyo vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kitu kingine, nilitamani kuongelea suala la misamaha. Tumeona hapa, alikuwa naelezea Mheshimiwa Alice kwamba kuna *burden* kubwa ya utoaji wa misamaha kwenye nchi yetu. Kiukweli ukienda kufanya *assessment, critical assessment* misamaha mingi unaweza ukakuta ni *fake*. Yaani watu wanajitengenezea utaratibu wao wa kujipatia kipato ambacho wanaikosesha

Serikali mapato, anapata yeye mfukoni kidogo anaandika misamaha isiyokuwa na tija. Kwa hiyo mimi niombe tu Mheshimiwa Waziri awe na uataratibu wa kufanya *analysis* nzuri ya misamaha iliyotolewa, ukiacha ile ambayo wana mpango wa kuitoa ili tuende sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu sawa tunatoa huduma za afya na watanzania wengi wazee wanakosa huduma kule kisa tu waliopewa misamaha mikubwa ni wengi. Kwa hiyo mimi niombe tu Mheshimiwa Waziri kwenye hili tusaidie, tusaidie sana Dada yetu Ummy kuhakikisha misamaha iwe ile ya kweli, kwa sababu tunaona *burden* iko kwenye *NHIF,* bima yetu ya afya inaelemewa lakini ukienda kufanya *assessment* unakuta na kwenyewe kuna utaratiubu ambao si mzuri ambao unafanyika wa watu kuwahudumia watu ambao hata hawako *registered* na bima, mtu anajipatia chochote kwenye mfuko wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimuombe tu Mheshimiwa Waziri, sisi tunapenda kazi yake anayioifanya, lakini suala la bima ni lazima atusaidie, suala la misamaha ni lazima atusaidie, kwa sababu haiwezekaniki bima mpaka leo eti tunakuwa tunaongelea bima kushindwa kuwahudumia wateja kwamba inaweza ika-*collapse* au ikafanya nini, wakati tuna uhakika waliojiandikisha na bima si wengi kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu spika, baada ya kusema hayo, *I am sorry.* Kuna suala la Tuduma. Tunduma iko mpakani, mpaka ule *you can imagine* tunapokea tu simu kila siku eti *X-Ray* hawana, Tunduma Mpakani, tena ni Halmashauri ya Mji ambayo sasa hivi mmetujengea Hospital nzuri haina *X-Ray* mpaka sasa hivi. Kwa hiyo nikuombe Waziri suala la Tunduma lichukulie kama *emergency* na ukatusaidie tuweze kupata *X-Ray* eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Baada ya kusea hayo naunga mkono hoja, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sanga. Jiandae Mheshimiwa Vita.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa niseme naunga mkono hoja, na nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake ambayo ameitoa leo; ni hotuba ya matumaini. Hata uteuzi wake alipokuwa anateuliwa kwenda Wizara ya Afya watumishi walitabasamu sana wakijua wamepata mtu ambaye walifanya naye kazi lakini kipindi chote amekuwa akionesha uwezo alionao wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza, niseme wazi, kwa Watanzania wafahamu jambo moja, kwamba Mheshimiwa Rais kwenye Wizara ya Afya amefanya vitu vingi sana ambavyo havikuwepo kwa muda wa miaka mingi sana tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Naenda tu kwa takwimu, kwamba, tulikuwa na Mheshimiwa Rais kwa kipindi chake tu kifupi ameongeza *MRI* sita ambazo hazikuwepo nchini, lakini Mheshimiwa Rais ameongeza *CT-Scan* 32, ambazo hazikuwepo kabisa nchini. Lakini wakati huo tayari sasa hivi ameshaanza kununua gari za *ambulance* 727, na tayari gari hizo zimeshaanza kuwasili nchini. Hii yote ni jitihada za Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sekta ya afya na Wizara ya Afya inaweza kutimiza malengo yake na inaweza kutimiza majukumu yake kama ambavyo Watanzania wamekuwa wakitegemea; ukiachana na ujenzi wa miundombinu kwa maana vituo vya afya na hospitali za mikoa. Mheshimiwa Rais kwa kweli anastahili kila heshima ambayo inatakiwa sisi kama Tanzania tumpe

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya jambo kubwa kwenye taifa lolote lile ni suala la afya. Mtaji wa kwanza wa mwanadamu ni afya, si suala la fedha, si suala la nini, ni afya.

Unapoimarisha miundombinu ya afya kwenye taifa lolote umepigania maslahi ya taifa kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa sababu hata ukisoma takwimu na idadi ya vifo vya mama na mtoto vimepungua kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa haya yote ambayo anayafanya; na hata ununuzi wa *digital x-ray* ameshanunua *digital x-ray* 199 na hata Wilaya ya Makete tumepata *digital x-ray* ambayo kitu ambacho sisi Makete hatukuwahi kukitegemea kuwa na *digital x-ray* tungeweza kupata pale Makete.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili, tumeona *emergency* ya hizi *block,* kwa maana *EMD* tayari hata Makete pia zimeshajengwa. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Makete, Mheshimiwa Waziri tunawashukuru sana kwa jinsi ambavyo mnafanya kazi, tunashukuru sana kwa maana ya kwamba Wakurugenzi na Wataalamu wa Wizara ya Afya, kwa kweli sisi kama Wabunge na mimi Mbunge wa Makete wanatupa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo naliomba kwa ajili ya Makete, na wananchi wa Makete wanatusikiliza; ni suala la usambazaji wa dawa na vifaa tiba nchini. Hili ni lazima tuliangalie kwa ukaribu sana. Kwa mfano, mimi nina vituo vya afya takribani vinne vimekamilika, Kituo cha Afya Bulongwa, Kituo cha Afya Kitulo, Kituo cha Afya Mbalache kimeshakamilika, Kituo cha Afya Lukalilo kimeshakamilika, lakini hivi vyote vina changamoto ya kutokuwa na vifaa tiba ili vianze kutoa huduma. Tusingetamani sana vikae muda mrefu kwa sababu vitaanza kuleta taswira ya kwamba majengo yamejengwa lakini huduma haipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea na Mkurugenzi wa *MSD* sasa hivi, na ameniahidi, nimpongeze sana Mkurudenzi wa *MSD,* anafanya kazi kubwa sana, ametuahidi kwamba atatuletea vifaa tiba pale Makete. Kwa

hiyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwenye hili jambo muweze kutusaidia. Jambo langu kubwa lingine Mheshimiwa Waziri kuna hili jambo la wanafunzi ambao wanasoma udaktari; na hapo Mheshimiwa Waziri naomba tusikilizane sana. Tuna wanafunzi ambao wanasomea utabibu, mambo ya utabibu; wanasoma kwa muda wa miaka mitano. Wakishasoma kwa miaka mitano mnawapeleka *internship,* kwa maana wanakuwepo na ile *pre-internship exam*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kunakuwa na changamoto kubwa sana. Watoto hawa wengi ni watoto wa masikini. Amesoma kwa muda mika mitano ameenda kufanya *field*, ametoka kwenye *field* mnampa mtihani huu. Huu mtihani ambao kwa kweli kwenye *syllabus* haupo, ila ninyi miliweka kama sehemu ya kuchujia kama sikosei au mlikuwa mna lengo gani? Lakini hawa watoto wamesoma miaka mitano, na ukisoma kwa takwimu za mwaka 2021/2022 kuna madaktari 200 ambao wamemaliza miaka mitano au wamesomeshwa na Maprofesa wetu hapa nchini, lakini baada ya kufanya mtihani wa pili *internship exam* wamekwama, mmewaondoa kwenye mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *issue* ni moja. Miaka mitano daktari amewekeza kenye kusoma lakini mtihani huo ambao si tu wa chuoni ni mtihani kutoka kwenye Baraza la Madaktari mnaita *MCT*. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri kumbuka hawa ni watoto wa masikini, angalieni utaratibu upya jinsi gani ya kuweza kuwasaidia. Kwa sababu hata rufaa zao ukataji wa rufaa kwa mtu ambaye amefeli hii *pre-internship exam*, mwanafunzi huyu utaratibu wa ukataji rufaa haupo *open*. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, tuna watoto madaktari zaidi ya 200 wamekuwa *disqualified* licha ya kusoma miaka mitano darasani na wamefundishwa na maprofesa wetu hawa, lakini pili wameenda *field* na wamefanya vizuri. Huu mtihani ambao hauna *syllabus* inawezekana ninyi mmeweka ndio mlango wenu wa

kufungulia mtu aweze kupita, lakini sasa umekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa madaktari wetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ambao Taifa linahangaika na upatikanaji wa madaktari kwenye vituo vyetu vya afya na hospitali zetu ninaomba Mheshimiwa Waziri uliangalie jinsi gani ya kuliangalia. Ninajua mlichokuwa mnakiangalia. Kwamba kuna sekta binafsi ambayo imekuwa ikipitisha madaktari ambao wako *disqualified* wanaenda kutusababishia matatizo, lakini tafuteni namna jinsi gani ya kuweza kuwasaidia wanafunzi ambao wamepita Chuo Kikuu cha Muhimbili na Maprofesa ambao tunawaamini waweze wakaende kulisaidia Taifa. Hawa watu 200 ni watu wengi sana, wamesomea miaka mitano, mama ameuza miti ameuza kuni amefanya nini…

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA**: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba, ni muhimu sana tuka-*standardize* Madaktari ambao wametoka kwenye vyuo na sasa wanaenda kugusa mgonjwa kwa sababu, sasa inakuwa utaalam na huduma watakayoitoa inahusu kifo ama uzima wa mteja. Kwa hivyo, ni suala ambalo kama Taifa hatupaswi ku-*compromise* nalo kwa hivyo, pamoja na gharama mtu anayeweza kuingia kwenye *training,* lakini *at the end of the day,* daktari anaenda kugusa mtu na hujui atagusa nani; atakugusa wewe Mbunge, atagusa mkeo ama mtoto, usalama ni muhimu sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante. Taarifa hiyo Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namheshimu sana Mheshimiwa Kigwangalla kwa sababu, hii ni *field* yake na hata mimi mawazo yangu yalikuwa ni hayo kwamba…

**NAIBU SPIKA:** Sasa mwite basi Dkt. Kigwangalla.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. Mawazo yangu nami yanaendana na hayo, kwa sababu huu mtihani ulikuwa una lengo fulani ambalo Waziri analifahamu, lakini umekuja ku-*include* hata vijana ambao wako *qualified* na wamesomeshwa na Madaktari wetu. Kwa hiyo, naomba kama ni mchakato uweze kuangaliwa ni jinsi gani ya kuweza kudhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika jambo ambalo hatuwezi ku-*compromise* ni suala la afya na uhai wa mwanadamu. Hili pia nipitie hapohapo, kati ya jambo ambalo Mheshimiwa Waziri anatakiwa aliangalie sana ni maslahi ya Madaktari kwenye Taifa letu. Namwomba sana kati ya watu ambao tunaweza tukawa tunazungumza sasa hivi kwa sababu, tuna afya njema, toka hapa nenda Benjamin Mkapa, Muhimbili, sijui hospitali gani ya Mkoa, Rufaa, Bugando, Madaktari wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa *24 hours.* Naomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie maslahi ya Madaktari kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hapa tumeshiba tunaona ni jambo rahisi, lakini ukienda kwenye mazingira ambayo wanafanya kazi ni mazingira magumu. Takwimu zinaonesha mwaka huu tu 2022/2023, wagonjwa milioni 35 wamepitia kwenye mikono ya Madaktari wetu. Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu sana na siamini kama Serikali inaweza ku-*compromise* kwenye kuboresha maslahi ya Madaktari wetu kwenye Taifa letu kwa sababu, sisi wote jeuri yetu ni afya.

Wabunge, Mawaziri na watu wengine kama wakulima jeuri yao yote ni afya. Kwa hiyo, naomba sana Waziri aangalie suala la maslahi ya Madaktari kwenye Taifa letu wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda kwenye vyumba vya watoto njiti na hili pia niweze kusaidia, Hospitali yetu ya Benjamin Mkapa ina changamoto ya mashine ya *oxygen* kwa ajili ya watoto njiti. Namuomba Mheshimiwa Waziri, hili waweze kulifanyia kazi, mashine za *oxygen* pale zimepungua na nimeshuhudia kwa macho yangu. Ni vyema sana wakiweza kusaidia Hospitali ya Benjamin Mkapa wakaongezewa mashine kwa ajili ya *oxygen* kwa ajili ya watoto wetu njiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini nasema wazi kabisa Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri, Mheshimiwa Mollel anafanya kazi nzuri, lakini *the master of all these* ni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameenda kuifanya Sekta ya Afya ionekane ni moja kati ya sekta muhimu kwenye Taifa letu na ameweza kutusaidia kwenye mambo mengi sana. Mungu ambariki sana Mheshimiwa Waziri, achape kazi, sisi wadogo zake tuko nyuma na Mungu amsaidie sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Vita, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Florence na Mheshimiwa Getere.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu kwetu kwa afya zetu na kwa wananchi wetu wa Tanzania. Naomba nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Tumeshuhudia wakiwa mstari wa mbele katika mambo mbalimbali na magonjwa mbalimbali ya mlipuko yanapotokea na wanajitahidi chini ya uongozi wao kuzima magonjwa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais katika kipindi hiki cha mwaka 2022/2023, tumeweza kupata zaidi ya bilioni tano na milioni 318 katika kujenga miundombinu ya hospitali zetu katika Wilaya ya Namtumbo. Hospitali ya Wilaya tulipata bilioni mbili na milioni mia tatu, tumejenga majengo, wodi ya akinamama na akinababa, tumejenga Hospitali ya meno na macho, lakini tumejenga jengo la mama ngojea, tumejenga na *mortuary* pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mama ngojea ni muhimu sana sisi kwetu kwa sababu, jiografia ya Namtumbo, Kijiji cha mwisho kinafika kilometa 254, kwa hiyo, kuna akinamama wanaopata *complications* kutoka katika hospitali wanapata rufaa kuja pale wengine kwa ajili ya kungojea kusubiri kujifungua, basi Serikali imewajengea jengo la mama ngojea, wanasubiri wakiwa palepale. Kwa hiyo, hii ni kazi nzuri sana waliyoifanya na inawasaidia sana mama zetu wale ambao wakifika pale wanakuwa bado hawajawa-*admitted,* lakini wanakuwa katika jengo lile la mama ngojea. Kwa hiyo, dharura yoyote inapotokea wanatibiwa, kwa hiyo, tunashukuru sana Wizara na Serikali kwa eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili Serikali wametujengea vituo vya afya vilivyokamilika. Kilichokamilika kimoja cha Mtakanini, lakini tuna vituo vya afya viwili viko mwishoni tulipata bilioni moja, Kituo cha Afya cha Ligela milioni 500 na Kituo cha Afya cha Magazini milioni 500 ambayo tuko katika hatua za mwisho kabisa. Pia Serikali ilitugawia fedha za kukamilisha zahanati nane, tulipata milioni 400; kila zahanati milioni 50 na tumekamilisha Zahanati ya Namali, Uramboni nayo iko mbioni kukamilika, Nahimba pia iko mwishoni, Kilangalanga iko mwishoni kukamilika, Misufini iko tayari na inatoa huduma, lakini Kumbara iko mwishoni kukamilika, Nahoro nayo ipo mwishoni, Luhangano nayo iko mwishoni kukamilika na Muhangazi iko mwishoni kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo ila tuna mapungufu ambayo pia, naomba niiombe Wizara kwamba, Kituo chetu cha Afya cha Mtakanini kina upungufu bado wa wodi mbili, wodi ya akinamama na wodi ya akinababa ya kulaza wagonjwa, lakini pia tuna upungufu wa wataalam wa usingizi, hatuna mtaalamu wa usingizi pale, alkini pia hata Hospitali ya Wilaya pia ina upungufu wa mtaalam wa usingizi, lakini ikama ya watumishi katika Hospitali ya Wilaya haijatimia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru Kituo cha Afya cha Mtakanini walitupatia watumishi 11 na walifika wameripoti na wanaendelea na kazi, lakini bado tuna upungufu wa mtumishi wa usingizi. Hospitali ya Wilaya nayo ina upungufu wa vitendeakazi vingine kama *standby generator* kwa ajili ya mtu akiwa anafanyiwa *operation* na dawa zile ambazo zinahitaji kuwekwa kwenye majokofu umeme unapokatika, hatuna *standby generator* katika Hospitali ya Wilaya na vituo vyetu pia havina *standby generator.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya pia ina upungufu wa vitanda, baada ya majengo mengi kujengwa bado tuna upungufu wa vitanda. Kwa hiyo, tunaomba sana Wizara ituangalie kwenye hili, watumishi, lakini pia baadhi ya vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tunaambiwa hela zimepelekwa *MSD,* lakini kuna kuchelewa kufika kwa vifaa tiba na dawa pamoja na kwamba, tulipata vifaa tiba vya milioni 758, tunaishukuru sana Serikali, vifaa tiba vya milioni 758 tumeshavipokea, lakini kuchelewa kwa vifaa tiba vingine nayo inatuchosha, lakini tunawashukuru sana. Nawashukuru sana Waziri wakati wote na Naibu Waziri nikiwafikia, basi huwa wananisikiliza na wananitatulia tatizo langu, kwa hiyo, nawashukuru sana, waendelee hivyohivyo na kwa kusema kweli wameiweza Wizara yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna upungufu pia wa wataalam wa meno na vifaa vyake. Kwa sababu, tuna jengo jipya la huduma hii ya meno kwa hiyo, hatuna vifaa vyake, lakini tuna upungufu pia wa *ultra sound* katika Kituo cha Afya cha Mtakanini kwa hiyo, tunaomba sana. Hivi vituo vya afya vingine viwili vilivyobakia ambavyo viko mwishoni tunaamini kabisa wakati wowote vitakamilika na watatupatia vifaa tiba. Tunaomba sana ili majengo yasikae muda mrefu, tungeweza kuanza kupata vifaa tiba sasa hivi yanapokamilika kwa sababu, yameshaisha, wako kwenye *final touches,* kwa hiyo, vile vifaa tiba vingeanza kupelekwa sasa hivi, ili wakimaliza kabisa, basi huduma inapatikana. Tunawashukuru sana kwa yote ambayo wanatutendea sisi Namtumbo katika kipindi hiki, asanteni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Florence, jiandae Mheshimiwa Getere.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Afya. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo amejipambanua kuendelea kuboresha huduma za afya. Wenzangu wameshasema, tumeona jinsi ambavyo amekwenda kuboresha huduma za afya kwa kuongeza vituo vya kutolea afya. Tumepata hospitali nyingi, tumepata vituo vya afya, zote hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba afya za Watanzania zinakwenda kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata sisi kule Muhambwe tumepata vituo vya afya viwili ambavyo vimeshakwisha kabisa katika Kata ya Kibondo Mjini na Kata ya Kunyambo na sasa hivi tunaendelea na ujenzi wa Kituo cha Afya katika

Kata ya Rugongwe, ili kuendelea kuboresha afya za wananchi wa Muhambwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi. Wamejituma na wamejipambanua kuhakikisha kwamba, wanafikisha huduma na hasa huduma bora ambazo ndio wananchi wanazitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amekuwa akisema kila siku kwamba, si bora huduma, hapana, anachotaka ni huduma bora. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kujua kwamba, wananchi sasa wanahitaji huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo imepeleka vifaa kila mahali. Wenzangu wameshasema, sasa ni jukumu letu sisi kuendelea kuvisimamia vile vifaa kule ambako tumeletewa ili viweze kutoa huduma inayostahiki kwa kuvitunza, ili viweze kutoa huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia lengo la Wizara na nikaona katika vipaumbele vyao wameweka kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto ya uzazi na mimi nitajielekeza hapo. Nimeona pia kwenye takwimu vifo vya mama na mtoto vimepungua kwa asilimia nne, niwapongeze sana Wizara kwa jitihada hizi za kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa sababu, wote tunafahamu kwamba, afya ya jamii yoyote inapimwa kwa kupunguza vifo vya mama na mtoto. Kama kuna vifo vingi vya mama na mtoto, basi jamii hiyo haina afya iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee bado tuna mikoa ambayo haifanyi vizuri sana, ukiwemo Mkoa wangu wa Kigoma. Tumeona hapa kuna vifo 900.  Katika hivi vifo 982

Mkoa wangu wa Kigoma una vifo 102, *accumulative* ni vifo vingi japo hatujazidi kwingine, lakini kwa vifo hivi bado akinamama wanakufa katika Mkoa wa Kigoma. Wilaya yangu ya Kibondo tumepata vifo 12 kwa mwaka huo 2023 kwa hiyo, ina maana tuna kifo cha mama mmoja kila mwezi. Bado hali hii haikubaliki kwa wananchi wa Muhambwe, bado tunahitaji jicho la pekee. Mheshimiwa Waziri Ummy anaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mkoa wa Kigoma tumejipambanua na tumekuja na Kauli Mbiu inasema Kigoma Safi ya Kijani Bila Vifo vya Mama na Mtoto Inawezekana. Sisi peke yetu hatutaweza, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atuangalie kwa jicho la pekee hasa kwa watumishi. Tunafahamu ziko changamoto nyingi zinazosababisha haya, Mheshimiwa Rais ameshaleta vifaa, ameleta majengo, sasa watumishi bado ni tatizo. Tuna uhaba, upungufu wa watumishi kwa asilimia sabini na kitu, ni ukweli usiopingika kwamba, hawawezi kukabiliana na vizazi hivi ambavyo viko vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu 12 wamekufa katika vizazi hai 17 elfu kwa hiyo, unaweza ukaona ile *burden* tuliyonayo. Tuna *burden* ya wazazi wanaojifungua wengi kwa hiyo, tunaomba Mkoa wa Kigoma kipekee tupewe kipaumbele hasa kwa hawa watumishi ambao wanategemea kuajiriwa, ili waje kutia nguvu katika haya mapambano ambayo kipekee sisi wenyewe tumeyaanza. Nichukue nafasi hii kumpongeza *RMO* Jesca, kwa kweli ni mwanamama anajituma anafanya kazi. Tunaamini kabisa wakituwezesha watumishi basi, tutatoka huko tuliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopinga kwamba, bado tumeona kwenye taarifa ya Wizara ukurasa wa 66 wameonesha ni jinsi gani halmashauri na zahanati, kliniki zina *burden* kubwa ya wagonjwa wa *OPD*. Amesema wameongezeka kutoka asilimia 16 hadi 22 na tukiangalia

katika lile jedwali hospitali za rufaa zinachangia asilimia 5.5 ya wagonjwa wa nje, tunaita *OPD*. Hospitali za rufaa asilimia 6.6, lakini hospitali za halmashauri asilimia 22.8 na zahanati zinachangia asilimia 39, hii ina maana gani sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunahitaji kuelekeza huduma nyingi sana kule kwenye Halmashauri zetu kwa sababu, ndiko ambako wale wagonjwa wataweza kupatikana na wakipata huduma nzuri, basi tutapunguza hata wale wagonjwa wa kuwapeleka kwenye *referral*. Maana Dkt. Mzuri wa kwanza au nesi mzuri wa kwanza ni yule anayemwona mgonjwa mara ya kwanza na akaweza kutoa *diagnosis* iliyo sahihi na akaweza kutoa matibabu yaliyo sahihi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba, halmashauri zetu, zahanati zetu na hivi vituo vya afya bado vinahitaji wahudumu wa afya na huduma bora kwa sababu ndiko wagonjwa wengi ambako wanaanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inawezekana kwa sababu, nimpongeze kwa hii program ya Samia Tuvushe Salama, ina maana wataalam hawa 100 wafike kule kwenye zahanati zetu, wafike kule kwenye kliniki zetu, wakafanye hizo *mentorship* na *coaching* ili tuweze kupata ujuzi ulio bora na weledi kwa watumishi wetu wa afya ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi wetu kule kwenye halmashauri zetu na kwenye zahanati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemwona Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ameeleza vizuri jinsi gani ya kuboresha maslahi ya watumishi wa afya, motisha itaenda kuchangia kuleta huduma bora kwa watumishi. Ni ukweli usiopingika kwamba, bado hakuna ulinganifu wa mishahara na motisha kwa watumishi wa afya kwenye hospitali za *referral* na hospitali za halmashauri. Kama tunaenda kupeleka watumishi kwenye halmashauri zetu na kwenye zahanati, lakini bado maslahi yao yako chini, basi tutashindwa kuwashikilia kule kwenye zahanati zetu kwa

sababu, wote tumeshuhudia ajira zikitangazwa Muhimbili watu wanaomba kutoka kwenye halmashauri zetu wanakwenda Muhimbili. Ajira zikitangazwa huku kwenye hizi taasisi watumishi wanahama, wanahama kwa sababu Daktari Bingwa wa akinamama aliyepo kwenye Hospitali ya Kibondo na Daktari Bingwa yuleyule aliyeko kwenye Hospitali ya Muhimbili mishahara ni tofauti, motisha ni tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatutaleta ulinganifu wa hizi motisha za watumishi wa afya kwenye hospitali za *referral* na hospitali zetu za halmashauri, tutawapeleka hawa watumishi kwenye zahanati zetu na hawatakaa maana kila mtumishi anatafuta *green pastures.* Kama anatafuta *green pastures,* hawezi kukaa kusubiri mwongozo ambao kwa kweli mwongozo huu umeongelewa miaka mingi. Tuliambiwa unapitiwa ulinganifu, zile zahanati na *dispensary* na hospitali za *referral,* ni miaka mingi. Tunaiomba Serikali, sasa ni muda muafaka, kwa sababu Serikali imeshawekeza kwenye zahanati na vituo vya afya, basi na maslahi ya watumishi wa halmashauri yaboreshwe ili yaweze kulingana na hospitali nyingine humu nchini. Imewezekana kwenye taasisi nyingi, kilimo walikuwa na shida hiyo, *I mean* mifugo walikuwa na shida hiyo, lakini waliweza kuweka ulinganifu na watumishi wameweza kukaa mahali pale, kwa hiyo, hili linawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwa haya magari ya *ambulance* yaliyoletwa. Tumeona Serikali inavyopambana kupunguza vifo vya mama na mtoto na kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Waziri amejipambanua kabisa akinamama sasa wameongezeka kwenda hospitalini. Tumeona akinamama walioenda hospitali mara moja asilimia 96, walioenda mara nne asilimia 86, ambao wameenda chini ya mimba ya wiki 12 ndio wchache asilimia 36. Hii ina maana gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana akinamama wengi wanakwenda hospitali. Sasa akinamama tunawa-miss wapi?

Tunawa-*miss* sana pale kwenye huduma ya kwenda kujifungua. Tumeona jinsi *M-Mama* imeanza juzi na inafanya vizuri sana. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, hawa watumishi wa afya ya jamii ambao tumeamua kuwasomesha na kuwawezesha tuwaweke kwenye mitaa yetu, hawa ndio waweze kujua mzazi yuko wapi na *ambulance* inaenda saa ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia *ambulance* zikikaa hospitali kusubiri *referral.* Kama tuna *ambulance* nne kila halmashauri, kwa nini zipaki hospitali zisiwahudumie hawa akinamama wajawazito ili waweze kuwahi hospitali? Kwa nini zipaki kusubiri mgonjwa mahututi na wakati mwingine hayupo? Ndio maana unakuta hizi *ambulance* saa nyingine zinafanya kazi ambazo hazikukusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri hawa watumishi wa ngazi ya jamii tuwatumie vizuri kwenye jamii zetu kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa maana kwamba, waweze kuwa na *coordination,* huyu mama anapata uchungu saa ngapi, anategemea kujifungua saa ngapi, gari la *ambulance* liko wapi, ili limuwahishe hospitali ili aweze kupata huduma za afya. Hapa tutakwenda kupunguza vifo vya mama na mtoto kwa sababu, *ambulance* tunazo, *ambulance* haibebi mgonjwa kila wakati, tukifanya *coordination* nzuri hii inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Waziri kwa jinsi alivyoona kwamba, sasa alete huduma ya ujuzi wa uongozi. Ni ukweli usiopingika kwamba, tunakuwa Madaktari hospitali na Manesi, tunajiongoza wenyewe hakuna kiongozi hospitalini. Kwa hiyo, naamini kabisa hii kozi ambayo ameamua kuileta ya *leadership…*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Florence. Kengele ya pili.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere, wajiandae Mheshimiwa Tunza na Mheshimiwa Reuben.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya Afya. Cha kwanza niwashukuru tu Waziri wa Wizara ya Afya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wataalam wote wa Wizara ya afya. Kimsingi kwenye upande wetu wa afya kwa ngazi za juu wanajitahidi sana kufanya vizuri, wanafanya kazi nzuri na Mheshimiwa Ummy kwa kweli, ni zawadi tu ya kukupa mfanyakazi bora wa kufanya kazi za umma hatujakupa, lakini anafanya kazi vizuri sana. Hana mbambamba, yuko *straight* kwenye jambo hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo yananitatiza hapa naomba niyaseme tu. Hivi kweli toka tumepata uhuru tunashughulika na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Hivi kweli toka tumepata uhuru wakati wa Nyerere, zahanati zilikuwa chache sana na vituo vya afya vichache sana na kwenye Wilaya tunapata hospitali chache, lakini huduma zilikuwa zinapatikana. Hivi kweli nchi yetu leo tunapeleka mabilioni ya hela kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na mikoa, lakini hakuna huduma, hakuna huduma kwenye zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli nchi yetu leo tunapeleka mabilioni ya hela kujenga zahanati, kujenga vituo vya afya, kujenga hospitali za Wilaya na Mikoa, hakuna huduma. Hakuna huduma kwenye zahanati, hakuna! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda pale Bunda, juzi nilikuwa natembelea hospitali moja ya Bukama mpya tumejenga ina Nesi mmoja. Huyo ndiyo alete dawa, atibu, afanye nini. Ni mwanadamu yule, anaweza kupata tatizo. Ukienda zahanati ya Matimero, kamejengwa kabanda watu wanazalia, wanazaa nje, ukienga Kambubu ni hivyo hivyo. Zahanati za Tanzania – sijui kuhusu maeneo mengine – lakini kwenye Jimbo langu hali ni mbaya kuliko kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafanyaje, tunajenga majengo mpaka lini, yaani tunafanyaje kwa mfano? Kwa nini tusiamue hizi tulizonazo tukubaliane kupeleka wahudumu wa afya na wataalamu wa afya kwenye maeneo haya. Kwa nini tunajenga majengo makubwa? Nenda Hospitali ya Wilaya ya Bunda, jengo la kwangu, bilioni 35 iko pale, sijawahi kuona hospitali ya Wilaya rufaa inaenda kituo cha afya, sijawahi kuona ndiyo Bunda hiyo tunaiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani mtu akienda hospitali ya Wilaya hapati dawa anakwenda kituo cha afya Ikizu ndiyo anapata dawa. Ikizu hiyo ni hospitali ya zamani ya mwaka 1959, imechoka. Kwa nini tusikubali, kwani sisi ni wafungwa wa mfumo wa *D by D? Devolution by Decentralization* sisi ni wafungwa? kwamba lazima tufanye hivi? Hivi kweli TAMISEMI kweli, ishughulike na ajira tunalia hapa, ishughulike na majengo tunalia hapa, ishughulike na *TARURA* tunalia hapa, ishughulike na kila kitu TAMISEMI?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusikubali tusijaribu maisha ya Watanzania hiyo Wizara ya Afya ichukue mfumo wote kutoka juu mpaka chini, kwa nini? Kwa nini tunajaribu maisha ya Watanzania, kwa nini watu wanakufa tunaona hadharani. Kwa nini watoto wetu wanakufa mtaani? Tuwaache Watanzania tuwatibu wapate akili, waweze kujigharamia wenyewe kwenye umaskini wao na ujinga wao waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba kwa vyovyote vile itakavyokuwa Wabunge tukubali tuombe inavyowezekana, mbona tumeomba maji imewezekana, tumeomba kilimo imewezekana, kwa nini leo tunashindwa kuomba afya zetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunataka kutibu watu wetu kwa bima ya afya kwa wote, hivi kweli tutaipeleka bima ya afya kwa hali hiyo? Yaani Waziri anayeiamuri *MSD* atoe dawa ni mwingine na Waziri anayepokea dawa ni mwingine, haiwezekani. Madaktari wa zahanati, vituo vya afya na Wilaya wametuma hela kuja *MSD* kununua dawa, hela zinakuja *MSD* kununua dawa, dawa hazitoki, ni maneno tu. Nani atasema sasa huyu *MSD* atoe dawa? Tukubaliane kwamba jamani afya za Watanzania tusichezee, kama tumejenga zahanati zimefika mwisho tuongeze watumishi, hospitali na dawa watu watibiwe, shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna sera ya Taifa inalinda watoto, miaka mitano utakwenda utoe 54,000 utatibiwa, iko wapi? Watoto wanakufa nani anapokea? Hakuna kitu. Kwa hiyo, niombe kwenye hili jambo kwamba sasa tuna hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Mgeta cha kwangu pale tumejenga karibu milioni 500 lakini sasa nenda *mortuary* imejengwa 2018 haina jokofu mpaka leo, vifaa kuna *ultrasound* hakuna wataalam, tulijenga tulisema vile vituo vya afya vya zamani cha kwangu kilipewa milioni 400, tukaambiwa kwamba kuna milioni 700. Milioni 400 ya majengo, milioni 300 ya vifaatiba hakuna. Ni shida. Nani aamuru? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubali kwamba sasa Wizara hii tusiweke afya za Watanzania kwenye mashaka, tuiweke iwe moja. Haya mambo ya *D by D* tuyaache, kwani nani anakufa, si dini tu, mradi ukubali mambo ya dini utaishi

maisha yako marefu. Uwe Muislam utaishi, uwe Mkristo utaishi, hata ukiwa Mlokole, mradi tu uache dhambi. Sasa kwa nini tusikubali ili hospitali hizi zitoe matibabu, afya zetu ziende hii Wizara ichukue Wizara yote, ikope mikopo ya kutosha ilete kwetu hapa tufanye kazi. Kwa hiyo naomba hiyo inaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ummy, juzi nilikuwa India nikawa naongea na watu wa Apollo. Apollo ziko nyingi India. Sasa nikawauliza hivi ninyi mnafanyaje? Wakasema huku kwetu Waziri yeyote wa Serikali, hizi Apollo unazoziona ni za Serikali lakini ana uwezo wa kuja hapa akaangalia kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri wakati tumekaa pale tunasubiri Waziri anafika pale. Dawa ni *cheap,* bei ndogo sana India dawa. Sisi kwetu hapa kila mtu ana bei yake, wala Waziri husogei, wala husemi. Tuna bei elekezi ya maji, bei elekezi ya mafuta, bei elekezi ya dawa hakuna, wewe kunywa tu ufe, hakuna! Hakuna bei elekezi! Tuna bei elekezi ya kila kitu lakini siyo dawa. Wewe nenda unavyotaka fanya unavyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakaniambia bwana ninyi Watanzania afya zenu mnaweka siasa. Tusifiane hapa humu ndani lakini kwenye afya watu wanakufa, tusifiane nenda kwenye mstari utaendaje, utasemaje? Unakwenda kituo cha afya mtu mmoja utasema nini sasa, haiwezekani. Kwa hiyo ombi langu ni kwamba Wizara hii iwe moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ummy nilipokuwa India niliuliza hivi mashine hizi za saratani ninyi mnafanyaje, wakatuambia iko mashine inaitwa *PET-CT Scanner,* ninyi watalaam akina Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla mnaijua, ambayo imefungwa *Ocean Road* toka 2021 mpaka leo haijafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo ukiiweka ikikamilika maana yake ukimwingiza mgonjwa yeyote mwenye saratani na magonjwa yoyote ya moyo inasoma moja kwa moja bila kuleta ujanja. Kwenye nchi zetu nasikia hapa Afrika Mashariki ni sisi tu tumenunua hapa ni bilioni 14. Sasa nikajiuliza bilioni 14 ndiyo nini? Kwa nini tusinunue ile mashine ikawepo Benjamin Mkapa, Wabunge tuko hapa ndiyo Bunge linaishi, ndiyo Mji Mkuu wa Serikali, ukimpeleka Mbunge pale mpaka umpeleke aende kupiga mionzi Dar es Salaam. Kwa nini tusinunue bilioni 14 ikakaa hapa, tukanunua Mwanza, tukanunua kwenye kanda, bilioni 14 *PET- CT Scanner* zikakaa pale zikatusaidia. Mionzi yenyewe mpaka uende kupigwa *Ocean Road,* hakuna Mwanza, tuna Hospitali ya Mkoa Mara imekaa pale Mheshimiwa Ummy, si uende uitembelee uione ina hali mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unatibu tu wagonjwa, jamani hivi hospitali ya Mkoa wa Mara imekuwa tena kama *clinic?* Maneno gani haya, imekuwa kama zahanati! Sasa Mkoa wa Baba wa Taifa mmeufanyaje? Jamani, mbona hali mbaya. Mama Maria badala ya kutibiwa pale Mkoani analetwa mpaka Dar es Salaam, mambo gani haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niombe hii *PET-CT Scanner* ifanye kazi lakini muilete Benjamin Mkapa, iende Mwanza, Mara, kila mahali iweze kufanya kazi, vinginevyo ndugu zangu mimi niwaombe hata ningeongea nini kama hii Waziri hatuwezi kuiunganisha tunapoteza muda. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Tunza, jiandae Mheshimiwa Reuben.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii jioni ya leo kuchangia katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *MSD* wanaomba wapatiwe mtaji wa bilioni 593, bilioni 592.9, hiyo ndiyo tunasema bilioni 593. Mimi sina shida, hata mimi naunga mkono wapatiwe ili waweze kutekeleza majukumu yao, maana yake watakuwa wamejipima, wame-*discuss* wakaona wakipatiwa hii fedha wataweza kutekeleza majukumu yao vizuri. Shida yangu kubwa, wakati ule wa taarifa za Kamati tuliona ripoti ya CAG inaeleza dawa nyingi zinafika vituoni zikikaribia kuisha muda wake *(ku-expire)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati *MSD* wanaomba kuongezewa fedha na Bunge hili na Kamati imeongea maana yake tunaunga mkono, hata mimi naunga mkono, lakini na wao *MSD* wanapaswa wajitathmini, wanapaswa wafanye kazi yao kwa weledi. Wanapaswa wawe waaminifu, wapeleke dawa huko zinakohitajika katika Mikoa yetu na Halmashauri zetu wakati zina muda mrefu kabla ya kufikia muda wa ukomo wa matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanaumwa katika hospitali, wanaumwa majumbani wanashindwa kwenda hospitali lakini unaambiwa dawa zinateketezwa. Kwa hali ya kawaida hilo jambo halifurahishi. Kwa hiyo, wakati Bunge linataka kusema *MSD* ipewe fedha na watumishi wa *MSD* nao wajione wana jukumu na wana dhamana waliyoibeba kwa nchi yetu hii ya Tanzania, hilo jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kule kwetu Mtwara tunasumbuliwa sana na ugonjwa wa Malaria, hilo linajulikana. Miongoni mwa Mikoa ambayo ni hatarishi kwa ugonjwa wa Malaria, kuna mmbu wengi sana ni pamoja na Mikoa ya Mtwara na Lindi. Sasa naomba niiulize Serikali, kama Zanzibar imeweza kudhibiti mmbu na kudhibiti Malaria, huku

Tanzania Bara ni kitu gani kinashindikana? Katika hali ya kawaida tunasema kinga ni bora kuliko tiba, sasa hivi tungekuwa tujadili zaidi kukinga kuliko tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunacho kiwanda pale kila siku nikichangia Wizara hii ya Afya naongelea kile kiwanda chetu cha Kibaha. Kila siku ukikisikia kina-*underperform,* kwa nini kina-*underperform* wakati matatizo bado ni makubwa? Sisi watu wa Mtwara giza likianza kuingia mmbu wanang'ata utasema wana meno. Sasa Serikali ione namna. Hapo Zanzibar ukienda kuna unafuu wa hali ya juu na Mheshimiwa Waziri unajua, kwa nini huku Tanzania Bara na hii yote ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Zanzibar wamefanya miujiza gani iwezekane na huku Tanzania bara kinashindikana kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naiomba na kuiomba Serikali iangalie jambo hili, maisha ya watu yanateketea sana kwa ugonjwa huu wa Malaria. fedha za Serikali, za walipakodi, zinatumika sana kwa sababu ya ugonjwa huu wa Malaria. Tujitahidi sana kuweka kinga kuliko kusubiri tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine la mfumo. Bado hii mifumo katika hospitali zetu inasumbua. Unajua ukimwona mtu ametoka nyumbani amefika hospitali anaumwa na Mtanzania ukimwona amekwenda hospitali walio wengi maana yake ameshindwa, yaani anaumwa. Anachotamani yeye akifika hospitali atibiwe arudi nyumbaji. Unafika hospitali unaambiwa cheti hawawezi kukata kwa sababu mfumo haufanyi kazi, sijui *network* iko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri hili katika Hospitali yetu ya Mkoa Ligula pale Mtwara linatokea, ingawa ndiyo hivyo mkiwasiliana na wahusika wanasema tunaandika pembeni tutakuja kuingiza na vitu kama hivyo. Kwa hiyo mimi nafikiri kuandaliwe utaratibu, mgojwa akifika atibiwe hayo

mengine ya mfumo mnayajua ninyi. Mimi nikiumwa nahitaji nitibiwe, sihitaji kuambiwa habari za mfumo kutokufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali yetu ya Kanda ya Kusini, wananchi wa Kanda ya Kusini, ukiwemo Mkoa wa Mtwara, tunashukuru hospitali ipo, imefunguliwa. Lakini hospitali ile bado inahitaji iendelee kutengewa fedha na fedha zitolewe. Kuna ujenzi ule wa awamu ya pili, bilioni mbili bado hazijapelekwa, tunaomba zipelekwe. Pia hakuna *ambulance,* Hospitali ya Kanda ya Kusini haina *ambulance,* hakuna gari la Mkurugenzi, naye yupo tu, yaani ndiyo ile tunasema anaazima azima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia karibia asilimia 80 ya watumishi wanaohitajika katika Hospitali ile ya Kanda ya Kusini hawapo. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ione umuhimu, sisi tunafurahi na tunapenda wananchi wa Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara tukitaka kwenda Dar basi tuende kwa mambo mengine siyo kwenda kutibiwa, tukitaka kwenda kutibiwa tuende tukatibiwe katika Hospitali yetu ya Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ambayo sasa hivi ipo bado kuna changamoto ambapo tunaomba Mheshimiwa Waziri, tunaiomba Serikali iangalie kwa jicho la upekee hospitali ile ya Kanda ya Kusini ili sisi tusilazimike. Unapokwenda Dar es Salaam wakati unaumwa bado unafikiria huduma zingine za malazi na chakula ambazo ni ghali ukiwa nje ya mji wako. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ichukulie jambo hilo kwa uzito wake na kwa umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la mwisho jioni ya leo nataka niiombe Serikali ukikaa ukisoma kwenye mitandao mingi, unakuta watu wanapostiwa wanaumwa magonjwa makubwa makubwa yakiwa katika *stages* za mwisho sana.

Mtu utaona anaumwa *cancer,* anaumwa ugonjwa gani, unajiuliza huyu mtu imekuaje alikaa nyumbani mpaka amefikia *stage* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali – sielewi labda ni elimu kwamba Watanzania hatuna ule uelewa zaidi wa kwenda hospitali, sielewi. Naiomba Serikali itilie mkazo, kwa sababu kila sehemu kuna watumishi wa Serikali, waone wanawashauri vipi wananchi. Mwananchi yeyote anapopata tatizo la kiafya sehemu ya kwanza iwe hospitali, tusikae tukasubiri hali imekuwa mbaya ndiyo unakwenda hospitali, hata kutibiwa inakuwa ni vigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nashukuru sana, *MSD* wawe makini wananchi wanaumwa na wanahitaji dawa, hatutaki kuona dawa zinachomwa kwamba zime-*expire*. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni hii ni wanafunzi 139 na walimu Wanne kutoka Shule ya Sekondari Umonga ya Jijini Dodoma, karibuni kwenye Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Reuben, ajiandae Mheshimiwa Iddi Kassim.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara yetu muhimu ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika maeneo ambayo Serikali ya CCM imefanya mapinduzi makubwa ni eneo hili la afya. Mapinduzi haya yaliyofanyika ya kuleta miundombinu vikiwemo vituo vya afya, zahanati, Hospitali za Rufaa za Kanda, Mikoa yamesababisha tuwe na changamoto. Kwa hiyo, wajibu wetu sisi ni kuishauri Serikali hii namna ya kutatua

changamoto hizi ili mafanikio haya ambayo tumeyapata yasigeuke kuwa laana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitaongelea jambo moja tu ili kuishauri Serikali, jambo la dawa. Mwaka jana nilisimama hapa nikazungumzia kuhusu *MSD*, ninaipongeza sana Serikali kwamba ilichukua hatua thabiti na bado inaonesha dhamira ya kuleta mabadiliko kwenye Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pale *MSD* nataka leo tupaangazie upande wa pili, tuuache ule wa *MSD* tuangazie upande wa pili wa mfumo wetu wa dawa. *MSD* pana miradi Minne ya kununua dawa. Mradi wa kwanza ni ununuzi wa vifaa na vifaatiba vya huduma za dharura, mradi wa pili ni ule wa mapambano dhidi ya *Covid-19*, mradi wa tatu ni utekelezaji wa mradi wa mfuko wa dunia na mradi wa Nne ambao ndiyo mimi leo nataka kuuzungumzia ni ule wa fedha zinazolipwa kutoka kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hivi hospitali zetu kwa maana ya Madaktari wetu wa Wilaya, Halmashauri zetu zinapoweka oda kununua dawa *MSD* uzoefu unaonesha kwamba wakiweka oda ya dawa 10 *MSD* wanapata Nne, Sita hawazipati. Uzoefu unaonesha kwamba wakitoa oda ya dawa 100 pale *MSD* wanapata dawa 40, 60 hawazipati, huo ni uzoefu na ndiyo takwimu zilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa upo mwongozo kwamba zile dawa ambazo Halmashauri zetu zikiweka oda *MSD,* dawa ikikosekana mwongozo unawataka wataalamu wetu na hospitali zetu zikanunue dawa kwa *prime vendors* (washitiri). Sasa hili la washitiri ndiyo mimi nataka tulijadili. Mimi hili la washitiri naliona ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tatizo kwa sababu gani, kwanza nitoe takwimu Halmashauri ya Handeni Mjini mwaka 2021/2022 *MSD* tulinunua dawa za milioni 40 tu, lakini kwa

washitiri tulipeleka milioni 60. Mwaka huu wa fedha mpaka *as of 31st March MSD* tumepeleka milioni 55 kununua dawa lakini kwa washitiri tumepeleka milioni 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo kusema nini? Fedha zetu nyingi za dawa kwenye Halmashauri zetu zinakwenda kwa washitiri. Kwa hiyo, tusipopaboresha hapa kwenye huu mfumo wa washitiri hili tatizo la ukosefu wa dawa tutaendelea kuwa nalo la ukosefu wa dawa.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ni tatizo kwa washitiri?

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa msemaji anaongea vizuri sana. Tatizo lililopo *MSD* hana fedha ya kununua dawa na kuzihifadhi ili anapopata oda kutoka kwenye Halmashauri aweze ku-*deliver on time*. Halmashauri wanapomkuta *MSD* hana dawa inawabidi waende wakanunue kwa mshitiri na ndiyo maana tumeomba katika taarifa *MSD* apewe mtaji awe na dawa ili huyu anapopata *order* apelike palepale. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Reuben uanipokea taarifa?

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwanamapinduzi, lazima tufanye mapinduzi. Washitiri ni tatizo, na matatizo nayaeleza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wakienda kununua dawa kwa mshitiri, bei wanayotuuzia washitiri ni kubwa kuliko ambavyo tungenunua *MSD*. Ni kubwa! *Last time* nilitaja *figures* hapa watu wakashangaa, kwa habari ya kidonge cha shilingi milioni nne kununuliwa kwa shilingi milioni 200 na kitu. Leo sitaji *figures,* nasema tu kwa ujumla, kwamba, tukienda kununua kwa washitiri, bei tunayonunua ni kubwa kuliko ambayo tungenunua *MSD,* la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tatizo kubwa ni kwamba, wale washitiri bei wanazotuuzia ni kubwa kuliko za *wholesellers* wetu wanaopatikana hapa nchini. Ni kana kwamba haitoshi, hata uki-*order* leo dawa, au kifaa tiba kinaweza kikamaliza mwaka hakijaletwa. Hii siyo sawa. Tuondokane na hii habari ya washitiri. Sasa wenzetu wa Wizara ya Afya wanayo mawazo, wanafikiri kwamba, badala ya kuweka mshitiri mmoja kwenye Mkoa mzima, waweke hata wanne. Hiyo haiwezi kuwa *solution* namna mlivyofikiria, kwa sababu nyie mnataka wawepo wanne, lakini wa-*specialize* kwamba huyu awe analeta hivi, huyu alete hivi, huyu alete hivi. Hapo hapatakuwa na ushindani. Kama bado mna *idea* ya kuwa na washitiri, ruhusuni wawepo washitiri washindanishe bei ili tusiwe tunalanguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaongea hivi kwa sababu Mheshimiwa Rais anapeleka fedha nyingi sana. Sikilizeni niwaambie, bajeti ambayo *MSD* wanaihitaji ni kama shilingi bilioni 592 tu, lakini miezi sita tu iliyopita *MSD* wamefanya manunuzi ya zaidi ya shilingi bilioni 257. Hizi zinazonunuliwa na *MSD* zikiwa *managed* vizuri, na hizi tunazonunua Halmashauri, zikiwa *managed* vizuri, dawa zinatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika ni kwamba tunanunua bei mara tatu mara nne ya bei halisi. Haitakiwi kuwa hivi, kwa sababu tukifanya hivyo, wananchi wa wa Kwedizandu watapata lini dawa? Wananchi wa Kwalwala, Kwasindi, Kwabaya; haya majina ninayoyataja siyo ya Kongo,

ni ya Handeni Mjini msiojua. Wananchi wa Kwedi, kule kwa Magono, hawawezi kupata dawa tukiwa na mpango huu. Kwa hiyo, twendeni tukafanye mapinduzi kwenye huu mfumo wa washitiri tuuangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mheshimiwa Waziri namwamini sana, ni mchapa kazi mzuri, ana wasaidizi wazuri, ana wataalam wazuri wamemzunguka, twendeni tukakae chini, tufikirie namna ya kuisaidia *MSD*. Hii habari ya kukosa dawa wakati tuna fedha, kwa sababu dawa inapoagizwa, ikachelewa kuja kwa miezi tisa, kwa mwaka wakati fedha tunazo, huu ni umasikini mkubwa kabisa wa namna ya kuyatazama mambo. Hivi, huwa najiuliza kila siku, kama magari yanaweza yakaletwa Dar es Salaam, tukawa na *bounded warehouse,* yako hapo yamekaa, inashindikana nini kwa dawa tukawa na *bounded warehouse* za dawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, asije mtu akachukulia kwamba habari ya *bounded warehouse,* naongelea *godown*, dawa zina utaratibu wake wa kutunza, ndiyo naongelea hivyo. Hayo maeneo ya kuhifadhi dawa, kwa nini tusiongee na wazalishaji, *order* tunazijua, maoteo ya vituo vyetu vya afya yote tunayajua. Tena katika eneo ambalo mnatakiwa mkaboreshe ni namna ya maoteo ya dawa yanavyofanyika, haya ndiyo yanayopelekea dawa zichomwe. Tunaagiza zaidi ya tunavyotumia, tuna-*spend* fedha nyingi zaidi ya tunavyotumia. Kwa ujumla kinachofanyika hapa ni *mismanagement. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wetu msaidieni Waziri wetu, isije ikafika mahali tukisimama hapa ionekane tunaisema Serikali, tunawasema watu; tunawasema nyie wataalam, tunashindwaje kuji-*organize?* Fedha zinapoteapotea tu, tumelipa huku, tumelipa huku, nyingine zimechomwa, haiwezi kuwa nchi ya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nahoji tena, kwa nini tusiwe na *bounded warehouses* za dawa na za vifaa tiba, kwamba mzalishaji akizalisha Urusi aje ahifadhi hapa Tanzania, mzalishaji akizalisha Ujerumani, aje ahifadhi hapa Tanzania ili *MSD* iki-*place order* saa mbili asubuhi, saa saba mchana dawa zimeshafika. Nini kinashindikana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Iddi Kassim, jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami leo kuchangia. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, hasa kwenye sekta hii ya afya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, nampongeza pia Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Niseme tu kwamba, kwa kweli Waziri ana Naibu Waziri ambaye ni mchapakazi sana. Mimi nitakuwa ni mfano wa Wabunge ambao nimeshuhudia kazi kubwa ambayo anaifanya Naibu Waziri. Hafanyi yeye, ni kwa sababu Waziri anamtuma. Kwa hiyo, ni mtiifu kwake, anatii maelekezo yake na anakuja kutusaidia kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya kazi ya ziara na Mheshimiwa Dkt. Mollel kwenye Jimbo la Msalala tukizungukia vituo vya afya na zahanati mpaka saa nne za usiku, na wakati huo tunafanya ziara hiyo toka asubuhi mpaka jioni alikuwa hajala, anakula korosho na maji. Ni huyu anajali afya za Watanzania, na hata sisi Wabunge anatusikiliza na kutufanyia kazi kubwa kwenye maeneo yetu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Katibu Mkuu na Naibu wake, dada yangu Grace, naye pia anafanya kazi kubwa sana. Nimekuwa nikikutana naye mara kwa mara akihangaika kutembelea miundombinu ya afya katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, nampongeza Mheshimiwa Daktari Mama Samia Suluhu Hassan kwa wema wake wa kututendea sisi Watanzania katika sekta hii ya afya. Katika Jimbo la Msalala mimi naweza nikawa ni Mbunge ambaye nimepata bahati sana ya kupata fedha nyingi ambazo zinaenda kwenye vituo vya afya, kwenye zahanati, na ununuzi wa vifaa tiba kwenye maeneo hayo. Mama Samia Suluhu Hassan ametoa fedha, tumejenga, tumemaliza kituo cha afya na Mheshimiwa Dkt. Mollel nafikiri alifika baada ya kutumwa na Waziri, akakitembelea Kituo cha Afya Isaka, kimekamilika, kimeanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hivyo, tumekamilisha Kituo cha Afya Mwalugulu kinatoa huduma, tumekamilisha Kituo cha Afya Bulige kinaendelea kwenye ukamilishaji, Segese na chenyewe kipo kwenye hatua ya mwisho, Mwalugulu tayari, kwa hiyo, utaona zaidi ya vituo vinne vya afya vyote vinakamilika. Niendelee kuwapongeza sana wadau wakubwa, Barrick ambao kimsingi wameunga jitihada za Mheshimiwa Rais katika kukamilisha zahanati mbalimbali. Wametupatia fedha, tumeweza kukamilisha zahanati 34 kwa mpigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika Jimbo la Msalala tuna vijiji 92 na tunavyozungumza hivi, matarajio yetu mpaka sasa tumebakiza maboma zaidi ya kumi na kitu tukamilishe idadi ya kila Kijiji kuwa na zahanati; na vituo vya afya vinane. Hapa tunapozungumza Mheshimiwa Waziri tunapata fedha nyingine, mmetuletea tena, tunaenda kuanza ujenzi wa vituo vya afya Kata ya Mwanase na Kata ya Busangi. Kwa hiyo, utaona zaidi ya zahanati 92 kwenye vijiji

hivyo, utaona vituo vya afya vinaenda kuwa zaidi ya kumi, na pia kuna hospitali ya Wilaya ambayo na yenyewe tayari imekamilika, na niwapongeze sana. Nampongeza Mama Samia Suluhu Hassan, tayari ametuletea fedha kiasi cha Shilingi milioni 700 tunaendelea kumalizia majengo ya mama na mtoto, mmetuletea fedha tumejenga *ICU,* na mmetuletea vifaa vya *ICU* kwenye maeneo hayo. Kimsingi, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan katika Jimbo la Msalala, tunamwahidi 2025 kura zake nyingi za kutosha kabisa tutampigia kwa sababu katika sekta ya afya ameonesha ni namna gani anatujali Wana-Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi, kwa kuwa tumepata zahanati zote, tumepata Vituo vya Afya, lakini namshukuru pia Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, ametupatia fedha za kununua vifaa tiba zaidi ya Shilingi milioni 600. Tayari kwenye maeneo haya, tumepeleka baadhi ya vifaa tiba, lakini bado havitoshi. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii, chonde chonde, tunazo zahanati zimekamilika na hivi sasa bahati mbaya nyingine zimeanza kuota nyasi baada ya kukosa vifaa tiba. Fedha mliyotupatia ni kidogo sana, tumejaribu kuweka kwenye zahanati zaidi ya nne tu, lakini bado kuna zahanati zaidi ya 24 hazina vifaa tiba. Siyo vifaa tiba tu, hata watumishi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Jimbo la Msalala, kuna upungufu mkubwa sana wa watumishi kwenye kada ya afya. Utaona kwa sasa tuna watumishi Zaidi ya 264, lakini tuna upungufu wa watumishi zaidi ya 500. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie ili tuweze kupata watumishi, kwa sababu tumekamilisha maboma ya zahanati kwenye kila Kijiji, lakini changamoto iliyopo sasa hivi ni vifaa tiba na watumishi ambao wataenda kutusaidia katika kuhakikisha kwamba tunazifungua zahanati hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposema kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri alifika na amezishuhudia zahanati

hizo kwa macho yake zipo, na sasa kwa wananchi kila siku wanaenda kufanya kazi ya usafi kwenye maeneo yale wakisubiri vifaa tiba na watumishi. Mbali na hilo, nashukuru sana wadau wetu wa Barrick na Serikali, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu, na namna gani anaweza kukabiliana na upungufu wa watumishi, tayari ametupatia fedha, shilingi milioni 400, tumejenga Chuo cha Afya. Hicho Chuo cha Afya sasa kinaenda kukamilika. Namwomba Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mollel amefika alipomtuma, amekiona ni chuo cha kisasa, ni chuo kizuri. Sasa niwaomba waende kukifungua chuo hicho ili tuweze kusaidia upungufu wa watumishi kwenye maeneo yetu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri, wametujali mno. Mheshimiwa Naibu Waziri nakupongeza mno, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan nakupongeza mno kwenye sekta ya afya. Niseme tu kwamba kumekuwa na changamoto, na hii siyo kubwa sana lakini ichukulieni kwa uzito wake. Amezungumza hapa Mbunge mwenzangu, kwenye baadhi ya vituo vya afya, kuna maduka ambayo yameanzishwa mle ndani. Ninapozungumzia maduka haya, nahusisha suala zima la dawa. Kumekuwa na maduka kwenye vituo vya afya, lakini maduka haya bado hayajaunganishwa na huduma hii ya *NHIF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa utakuta maduka haya bado usajili wake ni tofauti na zahanati ni tofauti. Mtu mwenye kadi ya *NHIF* anapoenda pale hapewi huduma kwenye duka lile kwa sababu bado halijaunganishwa. Hivyo hivyo maduka haya kwa sababu tumeyafungua kimkakati kuweza kuhakikisha dawa zinapatikana kwenye maeneo yale, tuwape uhuru wa kuweza kufanya biashara. Wanapouza, wanapata fedha zile kwenda kwa mshitiri kama alivyozungumza hapa Mbunge

mwenzangu hapa Mheshimiwa Reuben, bado kuna changamoto kubwa sana ya hawa washitiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mtoe vibali vya kwenye maduka haya yaweze kununua dawa kwa haraka zaidi kwa sababu fedha tunazo kwenye baadhi ya maeneo ya zahanati, lakini changamoto, wanapopeleka fedha zile aidha *MSD* au kwa mshitiri, dawa zinapokosekana, fedha zile zinabaki kule na wananchi wanaendelea kuumia. Toeni vibali, *process* hizi ni mpaka mtu atoke hapa aende mpaka kwa *RAS* Mkoani, wapate kibali ndiyo waje waanze kufanya utaratibu wa kununua dawa. Sasa naomba hebu toeni utaratibu wa namna gani maduka haya ambayo yamo kwenye vituo vya afya hivi, ili yanapotaka dawa yaweze kwenda kununua maeneo yoyote yanapohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, naomba tuweke mfumo mzuri kwenye vituo vyetu vya afya vya ukusanyaji mapato. Fedha nyingi zinapotea. Vile vile namwomba sana Mheshimiwa Waziri waone ni namna gani basi wanaweza kuviwezesha hivi vituo vya afya au zahanati viweze kuwa na vibali vya kuajiri kwa mkataba. Leo hii tunapozungumza hapa, ni kwamba ukiangalia Hospitali ya Bugarama kuna changamoto kubwa sana ya watumishi kwenye maeneo yale. Leo tumepatiwa fedha na Mgodi ya Bulyanhulu pale tumeweza kununua *machine* moja ya *x-ray* na *utra-sound.* Hata Mdhibiti Mkuu wa Serikali amezungumza, vifaa vile tumevinunua muda mrefu, tumevitunza pale, havina watumishi, havina wataalam wa kuviendesha, vimekaa pale. Naomba sana tuleteeni wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, wametuletea fedha nyingine tumenunua *digital x-ray* kwenye Kituo cha Afya cha Isaka, lakini bado na penyewe hatuna mtumishi. Sasa vifaa vya kisasa tunavyovileta kule, kama hatutatua changamoto ya ungufu wa wataalam kwenye maeneo yale, maana yake vifaa hivi

vitakaa kwa muda mrefu na vitaharibika. Kwa hiyo, nawaomba sana, tuleteeni wataalam kwenye maeneo yale ili wananchi wetu sasa waweze kupata huduma kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuzungumzia habari ya *ambulance* kwa sababu mmeshatuahidi kwamba kila Jimbo tutapata *ambulance*. Kiu yetu ilikuwa ni *ambulance*. Kwa hiyo, ninaamini kabisa *ambulance* zikija, mimi Mbunge wa Msalala ndio nitapewa kipaumbele namba moja, ili nije nipokee *ambulance* hiyo ikafanye kazi kwenye maeneo yetu hayo ili kuhakikisha kazi kubwa kwenye huduma ya afya inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia la mwisho mtusaidie. Tunapozungumza habari ya huduma zinazotolewa kwenye vituo vyetu vya afya na zahanati, bado huduma haziridhishi kwenye maeneo yale, Mheshimiwa Dkt. Mollel aliona.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, endeleeni kuchapa kazi, tunawaamini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, jiandae Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Awali ya yote nishukuru na kuipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa sana ya kuleta fedha za maendeleo ambazo zimekuja kwenye eneo la Wilaya ya Tanganyika. Naishukuru sana Serikali kupitia Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha nyingi za maendeleo. Tumejengewa

Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika, tunavyo vituo vya afya visivyopungua saba, na vipo vingine viwili vinajengwa. Hayo ni mafanikio makubwa sana kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Tunaipongeza Serikali, na tunawapongeza Mheshimiwa Waziri, na Naibu Waziri. Wote walishafika kwenye maeneo ya Wilaya hiyo ya Tanganyika na kwenye hospitali ya wilaya na baadhi ya vituo vya afya. Tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie sana uhaba wa watumishi. Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika ni miongoni mwa Wilaya ambayo imejengewa hospitali nzuri ya kisasa, lakini kwa bahati mbaya hospitali hii haina watumishi kabisa. Ina watumishi wachache na huduma ambazo zinatolewa kwa sasa ni kama vile hadhi ya zahanati. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Mheshimiwa Waziri atuletee watumishi ambao watakuja kufanya kazi ili hadhi ya majengo yaliyojengwa, na Mheshimiwa Waziri ni shahidi, amefika kwenye eneo lile. Mheshimiwa Rais alimsifia kwa kujenga hospitali nzuri na ya kisasa, na mandhari yenyewe ilikuwa ya kuvutia sana. Sasa zile sifa ambazo ulipewa Mheshimiwa Waziri, kazifanyie kazi ulete watumishi. Vile vile Naibu Waziri amefika hapo, ameleta fedha za vitendea kazi na aliwaahidi wananchi kwenye eneo lile ili kufanya maboresho makubwa kwenye Hospitali ya Wilaya. Naomba sana, Mheshimiwa Waziri nendeni mkalete wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika ina watumishi 20 tu. Kwa hiyo mkija kuangalia hadhi ya hospitali iliyojengwa ni tofauti na vitendea kazi kwa maana ya rasilimali watu. Namwomba Mheshimiwa Waziri, pelekeni watumishi kwenye vituo vya afya ambavyo vimejengwa. Tunavyo vituo vya afya vya Karema, Mheshimiwa Waziri umefika pale. Tunavyo vituo vya afya vya Kasekese, Kituo cha afya cha Mwese, Kituo cha Afya cha Mishamo, tunavyo Vituo vya Afya Nyagala, hivyo vyote havina watumishi. Naomba sana kwenye eneo hili mlifanyie

kazi na mtusaidie ili wananchi waangalie huduma iliyoletwa na Serikali iendane na mazingira halisia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Hospitali ya Wilaya tumeletewa *x-ray* ya kisasa kabisa, nzuri, lakini kwa bahati mbaya hata kutuletea wataalam wa mionzi imeshindikana. Kwa hiyo, huduma hiyo haipo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri alikuja, aliona hali halisi, lakini vifaa tiba vilivyoletwa, kuna upungufu, wale wataalam wa Tume ya Mionzi wameshindwa kufika kwenye eneo hilo. Naomba Wizara ishughulikie ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliahidiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri vifaa tiba, alileta vyenye thamani ya shilingi milioni 270, zikabaki kama shilingi milioni 230 ili hospitali ile iweze kufanya kazi, mpaka sasa bado vifaa hivyo havijakamilika. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba mtuletee hivyo vifaa tiba, sambamba na watumishi ili wataalam wetu waweze kutoa huduma. Tunao watumishi wachache ambao wanajitahidi sana kufanya kazi nzuri ya kuwatumikia wananchi. Kwa bahati mbaya idadi ya wanaohitaji huduma ni kubwa. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Serikali iangalie tatizo lililopo kwenye Wilaya ya Tanganyika na ukiangalia ni mazingira ambayo ni Wilaya iliyoko pembezoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ilijenga kwa nguvu za wananchi hospitali teule eneo la Ikola kule Tarafa ya Karema na ilijengwa mahususi kwa sababu katika ukanda wa ziwa kuna mlipuko wa magonjwa ya dharura ambayo huwa yanajitokeza, na ukiangalia tumepakana na nchi jirani ya *DRC* ambapo kuna milipuko ya mara kwa mara ya magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa bahati mbaya pamoja na jitihada ambazo zilizofanywa na Serikali kupitia halmashauri ya wilaya, bado hatuna hata mtumishi mmoja na kuifanya hospitali ile iliyojengwa kuwa kama eneo ambalo ni mazalia ya popo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri utakapopata fursa ya kuja Mkoa wa Katavi, tembelea kwenye eneo hilo uangalie jitihada ambazo zimefanywa na nguvu za wananchi namkaona jinsi walivyojipanga. Tusiangalie tu pale ambapo magonjwa yanapokuja kwenye mlipuko ndio tunakuja kuangalia jitihada za kutatua wakati wenzetu walishafanya jitihada za awali. Niombe na niishauri Serikali wafanye jitihada za dharura kuja kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo ahadi za viongozi ambazo zimetolewa kwenye Wilaya ya Tanganyika. Mheshimiwa Waziri, alifika kwenye eneo la Kata ya Katuma alituahidi kumalizia Kituo cha Afya cha Katuma. Niombe Mheshimiwa Waziri, ahadi yako uikamilishe na wananchi walishatumia nguvu zao na wametumia fedha za mfuko wa hewa ya ukaa kama chanzo cha awali cha kujenga kituo chao cha afya. Kwa hiyo, kilichobaki sasa tunasubiri fedha zile ambazo ziliahidiwa na Serikali ziweze kwenda kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ahadi nyingine zilizotolewa na ukiangalia mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ilivyo ni *ambulance* ambazo ziliahidiwa mbele ya Makamu wa Rais. Tunaomba ahadi ile iweze kutolewa. Ukiangalia jiografia ilivyo tumetembea na Mheshimiwa Waziri anaijua vizuri Wilaya ya Tanganyika jinsi ilivyo. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba *ambulance* kama tatu hivi kwa ajili ya vituo vya afya cha Kalema, Kituo cha Afya cha Mishamo, Kituo cha Afya cha Mwese. Sambamba na

*ambulance* ambazo zitahitajika kwenye hospitali ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie eneo la Bima ya Afya, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, wamepata fedha za hewa ya ukaa ambazo waliziingiza kwenye vijiji nane ili wapate huduma ya bima ya afya. Kwa bahati mbaya na masikitiko makubwa sana, pamoja na kuweka fedha nyingi na Mheshimiwa Waziri ndiye aliyekuja kuzindua kwenye eneo hilo, bado huduma ile iliyokusudiwa haipo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nikuombe ufuatilie jambo hili uone ni kitu gani ambacho nakizungumzia kwa sababu ninaelewa ninachokisema wewe unakifahamu tulishiriki wote lile zoezi. Huduma haipo, wananchi wamelipa fedha na huduma ya afya haipo kabisa kiasi kwamba sisi wawakilishi tunaonekana kama tumeshirikiana na Serikali kuwaibia wananchi kwa sababu hawapati hiyo huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana, naamini haya yote ambayo tumeyazungumzia kama Wabunge, Serikali ikiyachukua ikayafanyia kazi itawasaidia sana wananchi wa eneo la Wilaya ya Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumzie hospitali ya Mkoa, hospitali yetu ya mkoa…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na ndio mwisho wako huo.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kapinga, jiandae Mheshimiwa Mkundi, jiandae Mheshimiwa Mwambe, jiandae Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii ya Afya. Awali ya yote niungane na wenangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kumpongeza sana Naibu wake, lakini kuipongeza wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, wanafanya kazi kweli kweli. Hakuna asiyejua ndani ya nyumba hii kwamba watu hawa ukiwaambia neno wanakukimbilia, ukiwapa changamoto wanaisikiliza na kuitatua lakini ukiwaita kwenye jimbo lako wanakuja. Leo niwaombe, najua hamjafika Jimbo la Mbinga vijijini, kwa hiyo, niwaombe sana kupitia nafasi hii, tukimaliza hotuba hii au baada ya Bunge hili basi mpate nafasi mfike Mbinga vijijini. Karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana na nitoe shukrani kwa Serikali hii ya Awamu ya Sita, imefanya kazi kubwa katika jimbo langu. Nitoe shukrani kwa shilingi milioni 400 kwa ukarabati wa Kituo cha Afya Mapera. Sio hivyo tu, hivi karibuni wametoa milioni 350 vifaa tiba, kituo hiki cha afya sasa hivi kiko *full full*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepewa ahadi kupitia mradi wa *Global Fund* kwamba naenda kupata *ambulance*. Kwa hiyo, kwa kweli tunashukuru sana. Tukijumlisha na ile ya *COVID* maana yake tunakwenda kuwa na *ambulance* hizi mbili. Ahsanteni sana Serikali hii ya Awamu ya Sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi, tumejenga sasa hivi na kukamilisha vituo vya afya, Muungano, Matili na Mkumbi lakini pia kuna kituo cha Afya Magagula kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama, niombe sana tupeleke maeneo haya vifaa tiba lakini na madaktari wakafanye upasuaji katika maeneo haya. Kwa sababu Jimbo la Mheshimiwa Jenista Mhagama na la kwangu yako Jirani. Kwa hiyo, hata wananchi wanaingilia na wanalima kule

upande wa Msonga na Magagula yenyewe. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri, kama ulivyofanya hapa juu fanya pia na pale kupeleka hivi vifaa tiba ili wananchi hawa wapate huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo langu la pili, utoaji wa huduma na huduma hizi za kibingwa. Kama nilivyosema hapo awali, nchi yetu sasa hivi kila mahala kuna majengo mazuri ya kutolea huduma hizi za afya. Tuna zahanati, tuna vituo vya afya, tuna hospitali za wilaya na tuna hospitali za rufaa kwa maana za mikoa na hizi za kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwa ninaumizwa sana na ninasikitika sana pale wananchi wetu wanaposema siendi hospitali hii naenda hospitali fulani. Hapa niwe *specific,* kwa kule kwetu sisi sasa hivi habari ya mjini ni Ikonda iko Makete. Sasa mwananchi anakuja hana hela anaomba nauli ya kwenda Makate. Unamwelekeza kwa nini usiende hapa hospitali ya wilaya hii? Hakuelewi. Kwa nini usiende usiende pale mkoani kuna hospitali pale General? Hakuelewi anakwambia huduma nzuri zinatoa? Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwa kweli niwapongeze kwanza madaktari wetu wanafanya kazi nzuri katika mazingira haya tuliyokuwa nayo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nikuombe hebu tutafute majibu na utujibu hapa ni majibu gani yatakayowafanya wananchi waliopo huko wakaacha vituo vya afya na hospitali zilizopo maeneo haya waende sasa kwa mfano nilivyosema Ikonda? Sisemi kwa nia mbaya kwamba naichukia Ikonda, hapana naomba mnielewe sana. Hoja yangu tumejenga, tuna vituo vya afya vizuri na majengo mazuri na tuna madaktari maeneo haya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, niombe utupe maelezo mazuri namna gani wananchi wetu hawa wataviamini hivi vituo na kupata huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ni utoaji wa fedha za dawa. Upo ucheleweshaji mkubwa sana wa utoaji wa fedha hizi za dawa na hasa pale kituo kinaposajiliwa. Inachukua muda mrefu sana kituo kikisajiliwa kuingia kwenye mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano katika halmashauri yangu, kuna vituo vimesajiliwa muda mrefu vimechukua miezi mitano mpaka sita kuingia kwenye mfumo. kwa hiyo, niombe Waziri tubadilishe huu utaratibu, kwa sababu sasa hivi Serikali inasomana kwa nini ichukue muda mrefu? Tumesajili labda zahanati, tumesajili kituo cha afya, tumesajili hospitali lakini inachukua miezi mitano mpaka sita kituo hiki kuingia kwenye mfumo. Hawa watu wanafanyaje kazi? Sasa wanaanza kuwa omba omba, wanakwenda kituo fulani wanaomba, wanaenda kituo fulani wanaomba dawa. Hii inaleta shida hata kwenye kile kituo wanachoomba dawa. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, tutafute namna ya kurahisisha mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia fedha hizi za *basket fund,* hapa naomba tuwe na utaratibu mzuri. fedha hizi nadhani zinatoka Wizara ya Afya zinakwenda TAMISEMI halafu ndio zinakwenda eneo la kutolea huduma, lakini zinachukua pia muda mrefu sana. Sasa tatizo hapa sijui wapi wanapocheleweshaji kati ya Wizara ya Afya au TAMISEMI? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitolee mfano, fedha za mwezi wa saba katika halimashauri yangu, yaani *quoter* ya kwanza na ya pili zimekuja kutoka Desemba mwishoni. Sasa maana yake kazi yake zinakwenda kufanyiwa Januari. Hapa kutakuwa na ucheleweshaji wa mambo mengi yaliyopangwa kwenye ule mpango. Hata hivyo, tunasababisha hoja kwa hawa watu wa halmashauri. Kwa sababu, kwa nini hawakutekeleza huu mradi kwa wakati husika? Kwa hiyo, niombe sana kama ni Wizara ya Afya na

mimi siamini, lakini pia siamini pia kule kwa Mama yangu Kairuki kama ndiko wanakochelewesha. Sasa niombe mkae mzungumze ni wapi hizi fedha zinacheleweshwa? Lakini tuzitoe kwa wakati zikafanye ile miradi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama nilivyosema pale awali, tumejenga vituo vya afya na vituo hivi vya kutolea hudma za afya ni vingi sana. Iko shida mpaka sasa *sealing* inayotumika ni ile ile ya miaka mitano. Maana yake ni nini? Kama eneo limejengwa sasa hivi vituo vya afya vitano au zahanati tano mpaka kumi, zahanati hizi zinatumia bajeti ile ile ya miaka mitano iliyopita. Hii inapelekea watu hawa kupata mgao mdogo tofauti na uhalisia uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu tupeleke hizi dawa, tupeleke hizi fedha kulingana na hali halisi iliyopo kwenye mazingira hayo. Tunajua na mnajua kwamba Serikali sasa hivi inafanya kazi, kila siku tunajenga, kila siku tunasajili basi tunaposajili tuingize kwenye mfumo na *sealing* isomeke na dawa ziende kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu yalikuwa haya naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi, jiandae Mheshimiwa Mwambe, jiandae Mheshimiwa Mwambe, jiandae Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunipa fursa hii ya kuendelea kuvuta pumzi hii ya bure. Nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa sana anayoifanya kwenye maeneo yote yanayohusu huduma za jamii kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Ukerewe ni wanufaika wakubwa sana wa mapenzi mema ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nikupongeze Mheshimiwa Waziri,Dada yangu Ummy, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara. Mheshimiwa Ummy na Naibu Waziri, ninyi ni watu wema sana, ni watu wasikivu, ni watu wafuatiliaji lakini zaidi ni watendaji wazuri na watendaji bora sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui nini nitawalipa lakini Mwenyezi Mungu atawalipeni. Hamna baya kwangu na ninaamini hamna baya kwa wananchi wa Ukerewe, hasa kwa mapenzi mema mliyonayo na mipango mliyonayo kwa wananchi wa ukerewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukerewe nimekuwa ninasema kila wakati tuna changamoto nyingi lakini huduma za afya ni moja kati ya changamoto zinazotusibu sana wananchi wa Ukerewe. Nishukuru kwa miaka michache hii kuna jitihada kubwa za kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. Tumeongeza zahanati, tumeongeza vituo vya afya, Serikali imetuletea pesa tumejenga kituo cha afya cha Ilugwa. Mwaka 2022 tumepata pesa tunaendelea na ujenzi wa kituo cha afya cha Murutilima lakini pamoja na zahanati nyingi zinazoendelea, tumejenga Kituo cha Afya cha Igala, yote ni mema.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yangu kwako Mheshimiwa Waziri, pamoja na changamoto tulizonazo lakini niombe sana vituo hivi tulivyovijenga bado havina vifaa. Niwaombe sana mtusaidie vituo hivi vitatu vya afya vipate vifaa. Lakini zahanati ambazo tumejenga kwa kushirikiana na wananchi, zahanati zaidi ya sita, vilevile, tupate vifaa ili zianze kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, pale Bwise mmetuletea pesa tumekamilisha ujenzi wa kituo cha afya kikubwa sana ambacho tumekipandisha kuwa Hospitali ya

Wilaya na Kituo cha Afya cha Muliti, bado vituo hivi havina majokofu kwa ajili ya kutunzia miili ya wenzetu walioaga dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea kwa mfano pale Muliti hata pale Ukara, ikitokea mwenzetu kaaga dunia inabidi tusafirishe kupeleka hospitali ya wilaya kumhifadhi halafu ndio taratibu nyingine ziendelee. Ni mateso kwa wananchi wetu, mtusaidie ili tuweze kuboresha kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tuna changamoto ya watumishi. Mheshimiwa Waziri, nishauri sijui kama itawezekana lakini ni jambo jema. Sisi pale Ukerewe kwa sababu za kijiografia wanakuja watumishi lakini muda mfupi wanaondoka kwa sababu mbalimbali. Mnaonaje mkianzisha chuo cha uuguzi na uganga pale Ukerewe? Ili kupitia Chuo kile wanafunzi wakiwa wanapata mafunzo yao pale wakiwa wanatumia muda wao wa mafunzo kufanya mazoezi kwenye zahanati, hospitali na vituo vyetu vya afya, inawezekana ikasaidia sana kupunguza changamoto ya watumishi tuliyonayo kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri na wizara kwa ujumla, tulileta kilio kwenu kuonesha changamoto tulizonazo kwenye visiwa vya ukerewe hasa tunapopata wagonjwa wa dharura wanaohitaji rufaa kwenda kupata huduma kwenye hospitali ya mkoa. Mlitusikiliza mkaridhia kujenga hospitali ya rufaa kwa ngazi ya mkoa kwenye Visiwa vya Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo jema sana ninashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Ukerewe. Lakini niwapongeze sana kwa changamoto zilizojitokeza namna mlivyotusaidia kuzishughulikia mpaka hapa tulipo leo. Mheshimiwa Waziri, ulinipa jukumu la kutafuta eneo ili tuendelee na ujenzi wa hospitali yetu ile ya rufaa ngazi ya

Mkoa. Nikuhakikishie tayari kwa kushirikiana na viongozi wenzangu tumekwisha kamilisha mchakato huo eneo limepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe baada ya bajeti yako kupitishwa, ninaimani wala sina shaka tutaipitisha, twende ukerewe, ukajiridhishe na eneo lile ili kazi iendelee. Hautakuwa na baya kwa wananchi wa Ukerewe, hautakuwa na baya kwangu na kama nilivyosema wema wenu Mwenyezi Mungu atawalipeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yote bado tuna changamoto ya madawa, kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya bado shida kubwa sana ni upatikanaji wa madawa. Wamesema wenzangu waliotangulia kuchangia, kwenye eneo la *MSD* ambao tunatarajia kwamba wawe waokozi wetu kwenye eneo la madawa, bado kuna shida kubwa sana kwamba hawana mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, ili kuweza kuondokana na hili na Kamati yetu inayohusika na masuala ya Afya wametoa pendekezo, Mheshimiwa Waziri, niombe sana tuwawezeshe *MSD*. *MSD* wakipata uwezo kwa mfano kwa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati, wakipata fedha hizi bilioni 500 ninaamini matatizo makubwa tunayokutana nayo sasa kwenye upatikanaji wa huduma za afya hasa kwenye eneo la madawa inawezekana tukaondokana nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa hiyo, niungane na waliopendekeza hasa Kamati, tuwape mtaji *MSD*, tukiwapa mtaji *MSD* haya matatizo tunayokutana nayo inawezekana yakaondoka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mheshimiwa Waziri, pamoja na kazi kubwa sna mnayofanya na pamoja na kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais, bado kuna shida hasa

kwenye sera yetu ya afya kwenye utoaji wa huduma za afya kwenye kundi la wazee, lakini na watoto wachanga chini ya miaka mitano. Bado kuna tatizokubwa!  Kuna kila sababu ya Mheshimiwa Waziri kupitia shida iko wapi? Kwenye eneo la watoto wachanga, kinamama wajawazito lakini vilevile kwenye kundi la wazee. Ili changamoto zilizopo basi tuzifanyie marekebisho ili sera yetu tuitekeleze kikamilifu na watu wetu waweze kupata huduma ile inayotarajiwa. Kama tutaweza kuboresha eneo hili hata changamoto tunazozipata katika ku-*initiate* hili suala la Bima ya Afya kwa watu wote inawezekana tukaondokana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliona nichangie kwenye maeneo hayo; lakini nimalizie kwa kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yako yete kwa kweli mnafanya kazi kubwa sana. Mmetembelea Ukerewe mmetutia moyo na changamoto tulizokuwa nazo mmezifanyia kazi, na niwaombe muendelee kuzifanya kazi. Zaidi ya yote niendelee kuwashukuru sana na kuendelea kuwakaribisha Jimboni Ukerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe, ajiandae Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na wengine wote kwanza kukushukuru wewe mwenyewe lakini kwa namna ya pekee kabisa kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameamua kuipa nguvu sasa sekta ya afya. Niwapongeze sana pia Mawaziri, kwa maana ya Mheshimiwa Waziri Ummy pamoja na Naibu Waziri, watendaji wote wa Wizara ya Afya kuanzia wale wa juu kabisa mpaka wa chini ambao tuko nao kule vijijini kwa kazi kubwa wanazozifanya bila kuchoka usiku na mchana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze kwa namna ya pekee Mawaziri hawa wanavyoshirikiana. Siku zote katika kazi zao ukimkosa Mheshimiwa Ummy ukimpata Mheshimiwa Mollel pale atatatua jambo lako kama ambavyo Mheshimiwa Ummy angeweza kulitatua, kwa hiyo niendelee kuwapongeza kwenye hili. Pamoja na hayo mimi ni mjumbe wa Kamati ya Afya na masuala ya UKIMWI. Tumeongea mengi sana kule ndani na nisingependa niyalete hapa kwa sababu tumeyaleta kwenye taarifa yetu na tulishakubaliana. lakini nina mchongo wangu wa ziada kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kutoa pole sana kwa familia ya Mzee wetu Benard Membe kwa msiba mkubwa uliotokea huko. Wananchi wote wa Jimbo la Mtama, Mbunge wa Mtama pamoja na wananchi wa Chiponda kule Londo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo ningependa nishauri ili tuweze kuyafanya marekebisho ili Mheshimiwa Waziri waendee kutoa huduma zaidi kama ambavyo sasa hivi wanatoa huduma bora, lakini tunataka huduma bora zaidi kwenye Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa, hasa ukiangalia *tone* za Waheshimiwa Wabunge hapa ndani kuna haja kubwa sana kati ya wizara ya Elimu, Wizara ya Afya pamoja na TAMISEMI mkae na kuanza ku-*define* upya mipaka yenu ya kazi. Jambo hili limekuwa linatuchanganya sisi pamoja na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopata nafasi wanaongea Habari za zahanati ambazo ni huduma za afya za msingi chini kabisa, kitu ambacho naamini na nyinyi mna-*level* yenu. Kwa hiyo tunachanganya kati ya majukumu ya TAMISEMI, majukumu ya Wizara ya Afya lakini pamoja na majukumu ya Wizara ya

Elimu. Kwa hiyo niombe kabisa tafuta nafasi mtusaidie ku-*define* hii, na ikiwezekana sasa tuweke mstari ulionyooka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano ambao uko wazi kabisa, ninyi kwenu mnamiliki *CMO,* kwa maana *Chief Medical Officer,* lakini *Chief Medical Officer* hana mamlaka ya moja kwa moja kwa *RMO. RMO* naye hana mamlaka ya moja kwa moja kwa *DMO*. Nafikiri ananielewa Mheshimiwa Waziri; jambo ambalo linaleta mkanganyiko mkubwa, wakati ninyi Wizara ya afya mnatakiwa mfanye kazi kama Jeshi. Amri ikitoka juu kwa maana ya *CMO* iende mpaka chini kabisa kwa sababu ninyi ndio mnaoshughulikia masuala ya milipuko ya magonjwa pamoja na mengine. kwa hiyo niwaombe mkae na ku-*define* vizuri jambo hili ili *CMO* tumpe mamlaka lakini pia *CMO* awamiliki madaktari wenzie kwenye kada mbalimbali kushuka huko chini badala ya kuacha mfumo kama ambavyo uko sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tulikokuwa kwenye Kamati tulishauri suala la *CCBRT* pamoja na suala la Ndanda Hospitali; kwa maana ya wale madaktari wa *CCBRT* kuhakikisha wanapata mishahara yao kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutoa huduma kwa watoto wenye mapungufu lakini pamoja na masuala ya ujumla ya ulemavu ikiwa ni pamoja na huduma za macho. Kwa hiyo wanastahili kupewa mishahara ili kuwapunguzia mzigo na kupunguza gharama kwenye eneo hili. Sawasawa na ilivyokuwa kwa Ndanda Hospitali, sasa hivi wameondolewa *basket fund* lakini wakati Hospitali yetu ya Kanda ya Mkoa wa Kusini inakua sehemu ambayo tunategemea sana kupata huduma ni Hospitali ya Ndanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tuone namna ambavyo tunaweza tukawarudishia *basket fund* au kutafuta namna yoyote ya kuwawezesha waweze kugharamia huduma waweze kutoa huduma ya mama na mtoto kwenye

eneo hili kwa gharama nafuu kwa sababu sasa hvi yamekuwa malalamiko makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo jingine ni suala la Mfuko wa Bima ya Afya. Bima ya Afya sasa hivi inasuasua, lakini tukumbuke kwamba hawahawa Bima ya Afya ndio ambao walitoa fedha zao wakapeleka kuchangia kwenye ujenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa pamoja na Muhimbili. Kwa hiyo tuone namna Serikali itakavyolipa madeni haya ili mfuko huu uweze kujiendesha wenyewe kwa sababu sasa hivi hawafanyi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo jingine nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ukaangalie taratibu au namna ya kufanya ili mifumo iwe inasomana. Sasa hivi kumekuwa na shida kubwa sana ya huduma za afya. Kwa mfano mgonjwa akitoka Hospitali ya Kanda ya Mtwara akatakiwa kuja kutibiwa Muhimbili Dar es salaam, atakapoleta kadi yake ya afya ikiwa ndani ya masaa 24 itaonekana kwamba imetumika; lakini hata vipimo alivyovifanya Mtwara, Hospitali ya Muhimbili Dar es salaam italazimika kuvirudia tena, kama ilivyo *CT scan* na vipimo vingine, kitu ambacho kinaongeza gharama kubwa sana. Ni bora hawa watu wenye kadi ya afya wanaweza kujigharamia, lakini watu wanaotumia *cash* ndani ya muda mfupi anarudia vipimo vilevile mara mbili ama mara tatu kutegemea na hospitali aliyokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jambo jingine ambalo nataka kushauri, Tanzania sasa tumeendelea sana kwenye masuala ya afya; tuanzishe kitengo cha *medical legal,* kwa maana ya kutaka kusimamia taaluma ya madaktari. Siyo siri kwamba maslahi ya madaktari siyo mazuri sana, na ninaomba Wizara yako iboreshe. Kwa mfano sasa hivi wanapata asilimia 40 ya mgonjwa anayemhudumia akitokea kwenye Bima ya Afya, na ndiyo maana madaktari wanakuwa wanaamua wakati mwingine kufanya tiba ambayo si sahihi. Unaweza kukuta mama anauwezo wa ku-*push* mwenyewe lakini wanajua

akiwa hospitalini akimchaji akimwambia kwamba inatakiwa afanyiwe *scissor* ya milioni moja na laki tano tuseme atapata pale pesa na yeye asilimia 40 ya hiyo pesa ili aweze kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi kuna madaktari wanaohamisha wagonjwa kutoka kwenye hospitali kubwa na kuwapeleka kwenye hospitali ndogo ambazo haziwezi kutoa huduma nzuri. Na Mheshimiwa Waziri mimi nitakuletea jina la daktari ambaye ninamfahamu amemuumiza ndugu yangu. Alimtoa Hospitali ya *Regency* akampeleka Hospitali ya Kinondoni, amefanyiwa *operation* na sasa hivi nakueleza ameridiwa kufanyiwa *operation* ya *appendix* kwa mara ya tatu kwa sababu daktari wa kwanza hakufanya majukumu yake sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa watu kama hawa ambao wanaangalia zaidi kuhusu pesa badala ya kutoa huduma ndio ambao tunasema tuunde hii *medical legal* ili mwisho wa siku huyu naye awe na wajibu wa kushitakiwa kama alivyo mharifu mwingine yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua nia ya madaktari ni kutoa huduma, na nia yao hasa ni kuokoa maisha ya mgonjwa; lakini daktari anpofikia kwamba anataka sasa kuanza na kufanya biashara kwenye mwili wa mgonjwa kwa kumtoa hospitali kubwa anampeleka kichochoroni kwenda kumpa huduma ambayo haistahiki na baadaye mgonjwa yule anatolewa akiwa mahututi kwenye hospitali ya kichochoroni na kurudishwa tena kwenye hospitali kubwa, hili jambo halikubaliki. Tuyaangalie, tuwaongezee maslahi yao ili waweze kuacha kitu kingine

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine, tunazo *polyclinics* nyingi sana zimezuka sasa hivi. Kunakuwa na *emergency* zinazotokea mitaani, tunaruhusu watu wa *polyclinics* waweze kusajiriwa na *NHIF* ili kuwaza kuzuia ajali kwa kupata huduma hapo wakati mwingine ama vifo

vinavyotokea mitaani. Kwa hiyo tuyaone haya na tuone namna ya kuyasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama ambavyo nimesema tangu mwanzo, kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Afya, kwa hiyo kwa vyovyote vile mchango wangu sehemu kubwa nilitoa nilipokuwa ndani ya Kamati. Nataka tu kuyasisitiza haya machache, tufanye *definition* upya ya kuona mstari mzima kutoka Wizara ya Afya, Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie pia huo uwezekano wa kuwa na *medical legal* kwa ajili ya kuwasimamia madkatari ambo wanafanya vitu vya ovyo kwenye fani yao kama ilivyo kwa wengine; na ikiwezekana hata kabla ya kupata leseni nyingine madaktari hawa tukawapa *record tracks* zao za utendaji wao mzuri huko badala ya kufanya kwa uzoefu tunawapa leseni kila wanapofikia msimu wa ku-*renew* leseni wakati watu pengine wanayaacha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jingine kubwa tuone namna ya kuhakikisha sasa Mfuko wa Bima ya Afya unawezeshwa kwa kulipa madeni yake; madeni yaliyoko Mhimbili, Benjamini Mkapa, na ninaamini pia madeni yaliyoko Bugando; tuhakiishe tunawalipa ili waweze kujiendesha wenyewe, kwa sabau mara nyingi mfuko wa afya tumekuwa tunaona wandaiwa na watu wengi tu huko chini wanashindwa kutoa huduma nzuri na kisingizio kinakuwa kwamba wao hawajapewa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nisisitize kuhusu kuwapa stahiki zao *CCBRT,* kama ambavyo tumeongea kwenye Kamati

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi zake nzuri. Kama ambavyo nimesema, mimi ni mjumbe wa kamati kwa hiyo kwa

vyovyote vile mchango wangu nilitoa kule ndani lakini nilitaka nikukumbushe hayo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kwenye majimbo yetu tunaona kuna vituo vya afya. Ukifika Jimbo la Ndanda sasa muda si mrefu tutapata huduma katika maeneo ya Lukuredi, Mpajani, Chilolo, Ndanda yenyewe na Ndanda na maeneo mengi. Kwa hiyo kwa vyovyote vile nikushukuru na kukupongeza, na ninakutakia kila la kheri kwenye utendaji wako. Na nikuhakikishie kwamba kwa sura ninazoziona za Waheshimiwa Wabunge hapa bajeti yako itapita tena kwa kishindo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi niliyopewa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kyombo, jiandae Mheshimiwa Manyinyi, jiandae Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ambayo inagusa Maisha yetu. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dct. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuiimarisha Wizara hii. Pia tunaona kazi nzuri ambayo inafanyika katika ujenzi wa hospitali za rufaa za mikoa ambazo ziko chini ya Wizara, na kazi kwa kweli imeboreshwa baada ya kuwa chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, dada yangu Mheshimiwa Ummy, kazi unaifanya nzuri pamoja na Naibu Waziri wako Mheshimiwa Dkt. Mollel, mnajitahidi sana, nafikiri pongezi nyingi mmezipata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Hatupongezi kwa ajili ya kufurahisha; kazi ukiwa unafanya tunakuambia na kama mambo hayaendi vizuri pia tuna kushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua viongozi hawa hawafanikishi bila kuwa na wasaidizi wao wa chini; Katibu Mkuu Kaka yetu Seif, Naibu Katibu Mkuu Grace Maghembe (Dkt.). Pia Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu na madaktari wote, naona jopo limekamilika. Nikiangalia Wakurugenzi wako hapa, naona akina Dkt. Subi, akina Dkt. Chandika, wapo wote, Prof. Lugajo, wote wapo. Kwa hiyo unayo timu nzuri ambayo inaweza kuleta mageuzi makubwa katika Wizara yako, na wengine ambao sikuwataja lakini nawaona hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajikita katika maeneo kama manne, na eneo la kwanza nataka kushauri kwenye suala la *NHIF*. Tunajua Serikali ilichukua jukumu la kuboresha au kuona ni jinsi gani ya kusimamaia Mfuko wa *NHIF,* na ikaondoa *form 2C*. *Form 2C* ni fomu ambayo mgonjwa akikosa dawa katika kituo alichoenda kuandikiwa basi anapata fursa ya kuipata sehemu nyingine kwa utaratibu ambao Serikali iliuweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo jema kwa Serikali, lakini mimi wasiwasi wangu, na sintofahamu yangu ni kuangalia maandalizi gani mazuri yaliyofanyika ili kitu hiki kisiathiri mfumo wa matibabu; na madaktari wapo hapa, niliowataja na ambao sikuwataja, wanajua *basic practice* ya *medicine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, anapoenda mgonjwa kwa daktari akaandikiwa dawa inatakiwa apate dawa ile ile. *Unless* daktari abadilishe ile dawa, lakini akilenga zaidi katika matumizi ya dawa hii kumsaidia mgonjwa, asilenge katika upatikanaji wa dawa iliyoko stoo ili apewe mgonjwa; suala ambalo leo ndio linalofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa kweli hilo suala linaniuma kama mtaalamu wa dawa ilhali nikijua wanaosimamia sera hii na upande huu ni madaktari ambao

ni wabobezi, na ni wazuri, wanajua umuhimu wa mgonjwa kuandikiwa dawa fulani akaipata dawa hiyo ambayo daktari mwenyewe amemuandikia inamsaidia kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuishii kwenye *form 2C,* kupata ukakosa dawa stahiki, tunaenda na wale ambao ni watoa huduma wa kusaidia pale Serikali inapokuwa haijafikisha mkono wake. *Pharmacy* za watu binafsi ambazo zinatoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tumeenda mbali, ikaonekana kwamba zile *pharmacy* ambazo ziko nje ya hospitali, kwamba zinauza dawa za wizi hazitakiwi kuwepo. Mheshimiwa Waziri mimi nakupenda sana, najua unachapa kazi, lakini mpaka leo hizo *pharmacy* hazina vibali; tulizinyima vibali. Sasa sijajua *intention* ni nini; kwamba tunataka zi-*phase out* au tunataka kuzifuta. Lakini ni kosa gani limefanywa na hizo *pharmacy*?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nirejee tena, madaktari hawa tunaowaona sura, mimi nimesomea Muhimbili na hawa wote ni *colleagues,* tunajua jinsi ambavyo wamefaidi zile *pharmacy* zilizoko pale nje kupata dawa nje na ile ambayo inatakiwa labada kutoka nchi kama vile Ujerumani na *Egypt*. Yote hii inasaidia Serikali, pale ambapo inakuwa haijafikisha huduma Serikali yetu inaendelea kuonekana kwamba inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, niseme katika eneo hilo…

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze mwenzangu, anachangia vizuri sana na *input* yake ni muhimu sana na ina hoja. Lakini natataka tu nimpe taarifa kwamba, kwenye hilo eneo la *form 2C,* kwenye fedha ambazo zimeokolewa na Bima ya Afya, bilioni 115, asilimia 80 zinatokana na *form 2C*. kuna watumishi ambao wamekamatwa wako mahakamani sasa hivi, na kuna maduka ya dawa ambayo sasa hivi yamefungiwa, yamenyang'anywa bima na wengine wako mahakamani yanatokana na *form 2C*. Kwa hiyo *form 2C* ndicho kichochoro chenyewe. Jana tu, wiki mbili zilizopita tulikuwa pale kutokana na *form 2C*, tuliokoa milioni 600, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naipokea taarifa, maana hapa tunajenga, wala hatubomoi. Serikali pale ambapo inaweza kusimamia vizuri rasilimali za Serikali isimamie vizuri. Mimi nilitaka kushauri, kama kweli inaonekana kuna *pharmacy* ambayo imeshiriki kuiba dawa za Serikali, *penal code* zipo. Ukienda *section 302* unaweza kumpeleka na ukamfunga zaidi ya miaka saba. Ambacho hatujakiona, ambacho Serikali imetuonesha ni kwamba kuna mtua ambaye ameshapelekwa mahakamani amefungwa kwa sababu amekutwa na dawa za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya kama hayaonekani hatuwezi kusema kwamba hayafanyiki. Lakini kama Serikali inachukua hatua sisi tunawapongeza sana, hakuna ambaye ana kipingamizi na hatua mnazozichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi niachosema ni kuhusu maandalizi mazuri ya mazingira. Leo mgonjwa akienda, watu wanatibiwa hapa, kwenye hospitali yetu nzuri kwa Dkt. Chandika, lakini ukienda pale dawa ukakosa

unaishia kuambiwa bwana tafuta utaratibu unaowezekana. Sasa, ni suala ambalo mimi nafikiri ushauri muuchukue Dkt. Mollel yaani usiendeleze taarifa ili tuweze kuboresha kuona sasa ni namna gani ambayo tunaweza kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni suala la bei, nafikiri Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi, nimekuletea vipimo ambavyo kipimo hicho kwa *cash* ni shilingi laki mbili lakini ukienda kwa Bima ni milioni moja. Vipo kwa *evidence* na kwa kuonesha wazi. Tukasema tuboreshe katika maeneo hayo. Fedha zinapotea kwa Bima ya Afya lakini na sisi wenyewe tumeweka bei ambazo si za soko. Kwa hiyo haya yote yakiboreshwa mimi nafikiri tunaweza kukaa vizuri na Serikali yetu ikaendelea kutoa huduma kwa wananchi kama tulivyoahidi kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili niongee suala la *MSD*. Mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, alichukua hatua kuiboresha chini ya Wizara ambayo ni Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wanaendelea kusimamia. Lakini kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri amesema Menejimenti bado; Menejimenti ndiyo inasaidia; hata kama Mtendaji Mkuu yupo, hata kama bodi ipo, iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nishauri, Mheshimiwa Waziri pale ambapo tumechelewa kidogo basi kimbiza hiyo Menejimenti ikamilike. Lakini na Wakurugenzi wako wote wa *MSD* wote wanakaimu. Sasa unapokaimu maana yake maamuzi ya kufanya pale huwezi kuyafanya kwa kujiamini. Hata kama mtu anataka kumshauri Mkurugenzi Mkuu wa *MSD* atakuwa anasita kwa sababu hajui kwamba kiti alichokikalia ni cha kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pamoja na suala ambalo limejadiliwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kwamba waongezewe *MSD* mtaji. Tunachotaka kuona ni ni kwamba

dawa zinafika kwenye zahanati na vituo vya afya pamoja na hospitali, ili sasa *MSD* ionekane kwamba inafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niishauri Wizara kuhusiana na masuala ya majukumu makubwa ya Wizara, ambayo ni Kinga na Tiba. Suala la Wizara pamoja na kututibu lakini lazima kinga iwe ni bora zaidi. Katika eneo hilo kuna suala ambalo Mheshimiwa Waziri analijua. Tuna suala la kemikali ambazo zinatumika katika jamii kwa mfumo wa vipodozi, kuna zinazotumika kwa mfumo wa chakula; lakini zimeachwa zinaendelea kuzagaa katika soko letu, na mwisho wa siku anayeathirika ni Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi juzi nilikuwa naangalia taarifa ya Habari *ya RPC* Mwanza, watu saba wamekula chakula ugali na furu, wawili wakafariki saba wako hoi; lakini dalili anasema wametapika. Hizo zote ni dalili ambazo kwa daktari anajua kwa hiyo ni *mycotoxin,* ni sumu kuvu. Sasa, sumu kuvu unapoiacha ikadhibitiwa na watu ambao hawana taaluma ya udaktari sioni kama tunaisaidia nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi bado nimuombe Mheshimiwa Waziri mimi, nay eye ni mwanzilishi wa hili suala; bidhaa hizo mbili za chakula na vipodozi sisemi ziende wapi wala wapi lakini zirudi katika Wizara yake inaweza ikawa kinga kwa wananchi ili waweze kuzi-*manage* vizuri. Lakini anapoacha bidhaa huria vipodozi, dada zangu mtanisamehe, kuna vitu vingine ambavyo tunatumia kama wataalamu lazima tuseme ukweli, kwamba kesho na kesho kutwa tunapata Kansa ya Ngozi, tunaanza kuwa na magonjwa ambayo ni *hormonal imbalance* kwa sababu ya kutumia vitu ambavyo havitakiwi. Sasa ni nani ambaye anaweza kusimamia hili suala likaenda vizuri ni Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Wizara ijitahidi katika eneo hilo, na najua Mheshimiwa Waziri analifahamu

basi aendelee kushauri kule kukubwa ili aweze kusikilizwa mpaka hili liweze kufanyika. Baada ya kusema hayo kuna la mwisho, Mheshimiwa Waziri umekuja Mkoa wa Kagera umetutembelea umeona jinsi tulivyo changanyikana na Uganda na…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niombe basi na sisi Mkoa wa Kagera tuweze kupata hospitali ya rufaa ya mkoa yenye hadhi ya mkoa ule ili tunapokuwa jirani na Uganda, Rundi na Rwanda tuweze kuwa na…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, muda wako umekwisha.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, jiandae Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara ya Afya. Nampongeza Waziri, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu kwa namna alivyoweza kutupatia fedha za kutosha. Zahanati tumeweza kupata fedha za kutosha, hatuna shida huko, vituo vya afya tumepata fedha za kutosha, lakini kubwa zaidi namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa namna nilivyoweza kumwomba ile hospitali yetu ya mkoa ili iwe hospitali ya manispaa na hivi sasa tayari ile hospitali ni ya kwetu kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wa Jimbo langu la Musoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru sana kwa huduma ya hospitali yetu ya rufaa sasa, ile ya Kwangwa kwa huduma inazozitoa. Kwa hiyo leo maana yake ni kwamba tunaanzia kule kwenye kata, tunaenda wilayani na hatimaye kwa yale magonjwa ambayo yanashindikana basi tunaweza kwenda kwenye hospitali yetu ya rufaa, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli leo sina mambo mengi, ya kwangu namwomba Mheshimiwa Waziri machache tu tena yote ni mepesi ambayo naamini kwamba hata utekelezaji wake wala hautamsumbua sana. Moja, tunashukuru kwamba wameweza kutuletea *CT scan* pale kwenye Hospitali yetu ya Kwangwa, lakini kwa bahati mbaya sana sasa yapata miezi isiyopungua mitatu haijafungwa. Kwa hiyo sasa maana yake ni kwamba watu wetu wanapata tabu, lakini tayari Serikali ilishaweka fedha mashine iko pale. Kwa hiyo, tunaomba kwa haraka kabisa hiyo huduma iweze kupatikana kama huduma zingine zinavyopatikana leo pale, watu wetu walikuwa wa kusafishwa figo walikuwa wanasafiri leo mambo yote yanaishia pale. Habari ya mifupa watu walikuwa wanasafiri leo hizo huduma zote zinapatikana pale kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ndio maana nimesema nampa Waziri yale mepesi mepesi. Baada ya kuwa vifaa vingi vimefungwa pale, ile *transformer* iliyoko pale ni ndogo. Sasa vifaa vingi vinashindwa kufanya kazi. Sasa tukisema vifaa vingi vinashindwa kufanya kazi, maana yake ni kwamba kuna watu wanaendelea kukosa huduma kwa sababu ya shida ya umeme na tatizo ni *transformer* iliyoko pale ni ndogo. Hilo nalo naamini kwa Waziri wala si suala kubwa, alishughulikiwe mara moja kwa maana ya aidha azungumze na Waziri mwenzake Mheshimiwa January atupatie *transformer* kubwa, basi kama vipi waweze kununua ili tuweze kupata huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo kwetu ni la muhimu sana, ambalo na lenyewe nalo liko kwenye uwezo wa Waziri. Mji wetu wa Musoma kama nilivyokwisha sema ni mji ambao uko pembezoni. Kwa hiyo lazima tuwe na mikakati ya kuufanya mji ule ukue. Sasa liko suala ambalo mimi binafsi toka ile hospitali inajengwa pale nilianza kuomba kwamba angalau iweze kuwa sehemu ya chuo kikuu kwa ajili ya kufundisha wauguzi pamoja na Madaktari. Baada ya kuwa nimeliomba hilo Serikali imeendelea kuchelewa, lakini bahati nzuri tumekuja kivingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu chetu sasa cha Mwalimu Nyerere kimeleta ombi pale kwamba lile eneo la hospitali yetu ya Kwangwa kwa sababu ni kubwa watukatie pale hekari 20 ili tuweze kujenga pale Tawi la Chuo Kikuu ambacho kitakuwa kinatutolea wataalam kwa ajili ya magonjwa mbalimbali. Kwa hiyo naamini hilo ni suala ambalo liko kwenye uwezo wa Waziri. Akishalitolea hilo uamuzi, basi mara moja kile chuo kikuu kitajengwa pale na Mji wetu wa Musoma na wenyewe nao sasa utakuwa miongoni mwa miji mizuri iliyoko hapa kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni ushauri, Mheshimiwa Waziri sisi wote hapa tumezaliwa na wazazi na kwa sababu tumezaliwa na wazazi, wale wazazi wetu sasa wameshakuwa watu wazima wanahitaji huduma zetu na hata ukiangalia katika nchi zingine zimeelekeza zaidi katika afya au kwenye kuwatunza wazazi. Sasa sisi tulikuja na sera nzuri kwamba wazazi wale ambao wana umri zaidi ya miaka 60 waweze kutibiwa bure. Mpaka sasa wazazi wetu wengi wanataabika, maana akienda mara aombwe kitambulisho hiki, akipeleka hicho kitambulisho mara anaambiwa hizi dawa hazipo. Kwa hiyo wanapata shida sana. Kwa hiyo, ombi langu la kwanza ni kwamba, kama kuna watu tunahitaji kuwapa bima ya afya ni pamoja na wazazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe tu Waziri kwamba katika yote hilo ujitahidi ulifanyie sana kazi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali, wajiandae Mheshimiwa Leah na Mheshimiwa Neema.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye Wizara hii ya Afya.

Kwanza nipende kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi ambazo amekua akizitoa hasa katika upande wa afya na Wizara zingine, lakini hasa kwenye Wizara hii ya Afya, ameleta mapinduzi makubwa sana. Tunaweza kuona kwa muda mfupi, tumeweza kununua mashine za *MRI* na zimeweza kusambazwa baadhi ya hospitali na hospitali zingine zitapatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mapinduzi makubwa ambapo hapo awali mashine hizi za *MRI* ulikuwa ukizipata katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na ilikuwa inabidi upate ratiba ya hospitali, kwamba kama Mgonjwa atatoka Igunga Choma Chankola anaenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, atafika pale hatoenda kupata moja kwa moja kipimo cha *MRI,* itabidi apangiwe muda, inawezekana baada ya mwezi mmoja au miezi miwili ndio aweze kupata kipimo hicho. Wakati akisubiria maana yake huyu mgonjwa amesafiri, amepanga *guest,* lakini pia hata hiyo huduma kuja kuipata

inategemea kama Mwenyezi Mungu amemjalia kupata huo uhai wa kufika huo mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwepo kwa mashine za *MRI* kuongezeka katika kanda mbalimbali inapunguza kufanya watu wetu kusafiri kwenda katika Jiji la Dar es Salaam lakini inapunguza usumbufu wa kulipa katika *hotels,* lakini pia inapunguza usumbufu wa kusubiri kwa muda mrefu. Tunapongeza sana juu ya jitahada hizi kubwa ambazo Serikali imezifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kwamba Mheshimiwa Waziri Ummy anafanya kazi nzuri pamoja na Naibu wake, kazi zao ni nzuri sana na ndio maana unaweza kuona karibu Wabunge wote wanawapongeza kwa sababu ya namna ambavyo wanaweza kufanya kazi zao. Niwaombe tu na kuwakumbusha kwamba Mkoa wa Tabora ni mkoa mkubwa sana kijiografia, lakini sio tu mkoa mkubwa kijiografia, idadi ya watu pia ni mkoa wa tatu baada ya Dar es Salaam, Mwanza inafuata Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri sijaona mashine ya *MRI* akitupa pale katika Hospitali ya Tabora. Napenda kumwomba Mheshimiwa Waziri katika *wind up* yake ahakikishe basi anatupa matumaini kwamba ni lini Hospitali ya Tabora tutapata mashine ya *MRI* na ukitambua Tabora iko katika Ukanda wa Magharibi. Inategemewa na Mikoa ya Katavi, Kigoma na wakati fulani Singida. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri azingatie Hospitali yetu ya Kitete pale kuweza kuipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza kwa maboresho ambayo wamendelea kuyafanya kwenye hospitali za wilaya. Kupeleka fedha hospitali mbalimbali hata sisi pale Igunga wametuletea fedha kwa ajili ya Jengo la *ICU,* lakini na fedha ambazo wametupatia milioni 900 kwa ajili ya kuboresha hospitali yetu. Tunawapongeza sana na ambalo

napenda kuzungumza ni kwamba nawapongeza kwa fedha walizotupa za vituo vya afya, tulipokea sisi milioni 500 kwa Kituo kipya cha Afya cha Ziba na milioni 150 kwa ajili ya ununuzi wa madawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, niombe hii inawezekana wanashikirikiana na watafutaji wa fedha, wanashirikiana pamoja na watu wa TAMISEMI. Waendelee kutafuta fedha tuendelee kujenga vituo vya afya, mahitaji ni makubwa, Mkoa wa Tabora ni mkubwa, Jimbo letu pia la Manonga ni kubwa. Tunahitaji tupate hizo fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda kusema vituo, zahanati, hawa wagonjwa wanaokwenda kwenye hospitali kubwa hizi wanasababishwa na kutokupata huduma kwa wakati katika zahanati au vituo vya afya. Kwa hiyo wanatumia madawa ya kienyeji, wanapokuja kujua wana tatizo ugonjwa umekua mkubwa inawasababisha kwenda kwenye hospitali kubwa za Muhimbili. Waboreshe au tumalizie maboma yaliyopo kwenye zahanati itasaidia kupunguza idadi ya wagonjwa kuja kwenye hospitali kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumza ni masuala mazima ya upungufu wa watumishi. Tumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi na hii inasababishwa ni kwamba wanaomaliza wengi wametoka vyuo vikuu, hawa wa kwenye kwenda kwenye hizi zahanati wakati mwingine ni changamoto kwa sababu ya *level* ambayo wamefikia. Tunahitaji tuwekeze katika vyuo vya kati, kwanza vyuo vya kati ada zao ni ndogo, lakini pia hata kama tukiwakopesha ni rahisi kulipika. Kwa hiyo niombe sana Serikali iangalie suala hili la kuwekeza katika hawa watu wa *rural medical officers,* tupewe fedha nyingi sana kwa kuwakopesha na hawa wote tuwachukue twende kuwaajiri kwenye zahanati zetu. Tutaondoa tatizo la watumishi katika *level* za chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, Mheshimiwa Waziri kuna huu ugonjwa *UTI* ni changamoto sana. Kila ukienda hospitalini ukipimwa unaambiwa una *UTI* yaani hapo hapo *UTI,* hivi hii haina kuotesha kwamba nikae siku moja angalau niweze kujua na kama iko hivo je, hakuna chanjo? Tuweze kupata chanjo ya huu ugonjwa wa *UTI*, athari kubwa ziko kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sasa kuzungumzia maboma yaliyojengwa kwa muda mrefu. Tutafute fedha tuyakamilishe. Majengo ya maboma haya yamekaa zaidi ya miaka saba au miaka nane…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, lakini mwisho niwapongeze wananchi Yanga kwa kazi nzuri wanayofanya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hayo ulikua unasemaje? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Leah, jiandae Neema.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyopo mbele yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa namna anavyofikika kirahisi pamoja na Naibu wake, lakini naomba nitoe *case study* ndogo kwa Mheshimiwa Waziri Ummy pamoja na Mheshimiwa Angellah Kairuki kupitia Fedha za Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO–19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, walipatiwa fedha bilioni 69.1 kwa ajili ya kununua magari *ambulance* na magari ya kusambazia dawa, chanzo lakini walipoona bei ya *supplier* ni kubwa waliamua kufanya mazungumzo na *UNICEF*. Kwa hiyo, wakaweza kununua magari haya moja kwa moja kwa mzalishaji. Bei waliyopewa na mzabuni ilikuwa milioni 144.3 kwa ajili ya *basic ambulance* na gari la chanjo milioni 163, lakini badala yake walinunua *ambulance* kwa milioni 99 na la chanjo wakanunua milioni 162. Kwa hiyo waliokoa fedha taslimu bilioni 13.2 na hivyo wakaongeza magari kutoka 503 hadi 663. Kukawa na ongezeko la magari 160 na magari hayo 160 yana uwezo wa kusambazwa katika halmashauri zote zilizopo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hapa tunalo la kujifunza, tuendelee kuangalia Sheria zetu za Manunuzi, tuiruhusu Serikali au taasisi kunapokuwa na manunuzi makubwa wanunue moja kwa moja kwa mzalishaji. Tutaokoa fedha nyingi ambazo zitafanya kazi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivyo hivyo naomba nijielekeze…

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hilo analolizungumza Mheshimiwa Mbunge ni sahihi kabisa na lilifanyika chini ya *GPSA* na Wizara ya Afya wakaamua kumuacha *GPSA* na kuenda kununua hayo magari na kuokoa zaidi ya bilioni kumi na kitu ambazo zimetajwa. Kwa hiyo ule msimamo wa Mheshimiwa Rais ni kweli *GPSA* lazima waondoke kwa sababu walitaka kuiangamiza Wizara ya Afya

kwenye ununuzi wa magari. Ahsante sana na hongera kwa mchangiaji. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ummy haya ndio nataka uandike kwenye taarifa yako uyaseme. Haya Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, naunga mkono hoja kabisa kabisa yapo manunuzi makubwa yanafanywa tunaendelea kupoteza fedha kwa kupitia watu wa kati badala ya kwenda moja kwa moja kwa mzalishaji. Suala hili pia lipo upande wa manunuzi wa madawa, tuiruhusu *MSD* kunapokuwa na manunuzi makubwa waende moja kwa moja kwa mzalishaji na haya yafanywe, sheria iletwe hapa tuweze kufanya mabadiliko ya sheria. Niombe sheria upande wa madawa isilingane na vifaa vingine kutokana na umuhimu uliopo kwa dawa za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kabisa *MSD* ina changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na sisi Kamati ya Bajeti mwaka jana tulipendekeza unapoanza mwaka wa fedha wakopeshwe bilioni 150 na Benki Kuu ili wanunue madawa. Hospitali zinapohitaji dawa *MSD* wakutwe wanazo, sio hospitali zinapohitaji dawa ndio *MSD* waende wakanunue. Suala hili halijatekelezwa lakini naunga mkono maombi yao ya kuomba bilioni 592 kuweza kufanya maboresho *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba hizo fedha zina mgawanyo, uwekezaji, ujenzi wa maghala pamoja na usambazaji wa madawa kwenye *item* ya madawa, naomba kutoa ushauri mnapoenda kufanya maboresho, lakini maboresho haya bila kuziba mianya ya uvujaji wa dawa, bado katika jambo hili watakuwa hawajafanya kitu chochote. Niwaombe katika fedha walizoomba wameweke kipengele cha udhibiti cha TEHAMA,

kuwepo na mfumo katika upokeaji na utoaji wa dawa hadi kwa mgonjwa ili tuweze kujifunga wapi dawa zinapotelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mfano kwa Hospitali yetu ya Taifa ya Benjamin William Mkapa, inayo mfumo mzuri wa utoaji wa dawa. Naomba na hospitali za mkoa nazo basi zijifunze kupitia Benjamini Mkapa na hapo tunaweza tukajua wapi dawa zinavuja, wapi dawa zilipotelea, lakini pia wataalam wetu wa hospitali hawana weledi wa kutosha katika matumizi ya mfumo na hii inapelekea fomu nyingi kuweza kukataliwa Bima ya Afya. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Neema.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii muhimu ya hotuba ya bajeti ya Wizara ya Afya. Niungane na Wabunge wenzangu kuipongeza sana Wizara inayoongozwa na dada yangu mahiri kabisa Mheshimiwa Waziri Odo Ummy Mwalimu, lakini pia na Naibu Waziri Dkt. Mollel na viongozi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kusisitiza kwamba kwenye Wizara hii ya Afya pamoja na kufanya tiba, lazima tuwekeze jitihada za maksudi kabisa kwenye kinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi za Wizara nikiri wazi nimesikitika kwamba katika hotuba nzima ya Mheshimiwa Waziri na baada ya kusikiliza hotuba pia nimeipitia, sijasikia akigusia jambo lolote linalohusiana na suala zima la usalama wa chakula. Nasema usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*. Mara kadhaa ndani ya hili Bunge tumekuwa tukisisitiza suala la usalama wa chakula ni dhamana ya uhai na maisha na afya ya Watanzania. Hatuwezi kuendelea kuweka maisha ya Watanzania rehani kwa kuruhusu suala la kudhibiti usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* iendelee kuwa chini ya *TBS* kwa maana ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri *TBS* ina *conflict of interest*. Huwezi ukawa wewe ndio unatoa vibali kwa wafanyabiashara, halafu wewe ndio unaangalia udhibiti wa usalama wa chakula kwa maana ya *food safety*. Mheshimiwa Waziri ni shahidi pamoja na Naibu Waziri, hili jambo nimelisemea mara nyingi hata nikiwa kwenye Kamati ya Huduma ya Maendeleo ya Jamii iliyokuwa Huduma ya Maendeleo ya jamii na hata ndani ya Bunge lako Tukufu. Tukifanya rejea kwenye *hansard* tutakuta kuna kauli ya Serikali kupitia Wizara ya Afya ambayo iliahidi kwamba Serikali inafanyia kazi jambo la kuhamisha mamlaka ya masuala ya usalama wa chakula, kutoka kwenye *TBS* na kuja kwenye Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa, pamoja na pongezi na jitihada kubwa za Sekta hii ya Afya kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa ya kansa, kumekuwa na ongezeko kubwa na magonjwa yasiombukiza ambayo hayaeleweki, ambayo mengi yao yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na ulaji wa vyakula ambavyo havina ubora wa usalama wa chakula. Ikiwa tunaweza kukidhi vigezo vya usalama wa chakula ili tupate soko la nje. Kwa mfano soko la *EU,* tunashindwa vipi kulinda na kukidhi na kuweka vigezo vya

kulinda uhai wa soko la ndani ambalo ni zaidi ya wananchi milioni 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala naongea kwa uchungu mkubwa kwa sababu tunaendelea kuweka maisha ya Watanzania rehani, wakati tunaweza kudhibiti ikiwa tu tutarudisha mamlaka ya udhibiti ya usalama wa chakula yarudi chini ya Wizara ya Afya, ambao kimsingi ndiyo awna dhamana ya kuhakikisha uhai wetu unaendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana viongozi wa Hospitali zetu za *KCMC*, Bugando, Muhimbili, *JKCI*, *Ocean Road*, hapa Benjamini Mkapa, lakini naamini hata na wao watakubaliana nami, suala la usalama wa chakula limekuwa likiendelea kutotiliwa mkazo na maanani wakati linaendelea kutuwekea Watanzania hatarani. Haiwezekani tukaendelea kuruhusu suala la usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* libaki chini ya *TBS* ambao kimsingi mimi binafsi ninao ushahidi dhahiri na nimeshasema hapa Bungeni. Kuna ndugu yangu aliwahi kuagiza bajaji, bajaji zile zilikwenda kufanyiwa ukaguzi na wahitimu wa *food science*, kwa nini? Kwa sababu pale *TBS* hawana kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anafanya kazi kubwa sana, nimwombe sana atulinde Watanzania, tunaingiza vyakula hapa nchini, nani anaangalia usalama wa vyakula vinavyoingia. Tunazalisha chakula hapa nchini, nani anaangalia usalama wa chakula tunachokula? Nani anaangalia machinjioni usalama wa chakula, nani anaangalia mbogamboga na vyakula vinavyokuja sokoni iwapo *chemical residue* yake ipo vipi, lakini tunafanya hivyo kwa soko la nje, kwa nini tunashindwa kufanya hivyo kwa soko la ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana wale wananchi wa nje wana haki zaidi kuliko sisi Watanzania zaidi ya milioni 60.

Pamoja na kwamba dada yangu nampenda sana, niweke wazi nisipopata kauli ya Serikali inayoridhisha kuhusu nini Serikali inakwenda kufanya kuhusu suala zima la kuhakikisha usalama wa chakula kwa maana ya *food safety* linarudishwa kwenye Wizara ya Afya, naondoka na shilingi ya mshahara wa Waziri mpaka kieleweke.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na wachangiaji wote wamekwisha. Niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri. Nakupongeza Waziri wa Afya kwa bilioni zaidi ya 13 ambazo zingeweza kuliwa na matokeo yake mmeongeza magari mengine. Huo ndio utumishi uliotukuka na wale wote walioshiriki kuokoa pesa hizi, basi tunawapongeza sana na haya matatizo yapo kwenye *procurement* na hasa kwenye halmashauri zetu. Hupewi kazi mpaka cha juu kiongezwe na *quality* ya kazi inakuwa mbovu sababu pesa nyingi zinapigwa juu kwa juu. Kwa hiyo, niombe tu wahusika mzifanyie kazi, kuhakikisha pesa za umma zinafanya kazi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.42 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 15 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*